

24 APRILI, 2013

## BUNGE LA TANZANIA

---

### MAJADILIANO YA BUNGE

---

### MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Kumi na Mbili - Tarehe 24 Aprili, 2013**

*(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani :-

#### **NAIBU WAZIRI WA MAJI:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Maji kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

#### **MHE. AMINA N. MAKILAGI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI):-**

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 na maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

24 APRILI, 2013

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Makilagi ambaye pia ni Katibu Mkuu wa Umoja wa Kinamama wa CCM Tanzania. Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani. Namwona Mheshimiwa Cecilia Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESO (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA MAJI):-**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Maji Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 95

**Serikali Kushindwa Kulipa Madai Mbalimbali ya Wafanyakazi**

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA (K.n.y. MHE. DAVID E. SILINDE)** aliuliza:-

Miongoni mwa malalamiko makubwa ya wafanyakazi kwa Serikali ni kushindwa kulipa malimbikizo yao ya mishahara, likizo pamoja na makato mengine.

(a) Je, ni lini Serikali itayashughulikia matatizo haya na kuwalipa wafanyakazi stahili zao?

(b) Je, kwa nini Serikali imekuwa ikipuuza malalamiko ya wafanyakazi hao na kuyafanya yaonekane sio ya msingi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA aljibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa David E. Silinde, Mbunge wa Mbozi Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali imekuwa ikilipa madai ya malimbikizo ya mshahara ya watumishi wa Umma kulingana na uwezo wake ambapo katika mwaka wa fedha 2011/2012, Serikali iillipa madai ya malimbikizo ya mshahara kwa watumishi 54,010 yenye jumla ya shilingi 72,351,994,390.92/-.

Aidha katika mwaka wa fedha 2012/2013 Serikali imeendelea kulipa madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi wa umma hadi kufikia Machi, 2013 jumla ya madai ya watumishi wa umma 11,820 kati ya watumishi 52,039 wameliipwa malimbikizo ya mishahara na kiasi cha shilingi 12,603,190,834/- kimetumika.

Malipo ya malimbikizo ya watumishi 27,245 yenye thamani ya shilingi 16,089,986,605/- yalikuwa yameshahakikiwa na yanashubiri kufanyiwa malipo kutegemeana na upatikanaji wa fedha. Madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi 12,974 lenye thamani ya shilingi 12,588,847,207/- yalikuwa kwenye hatua ya uhakiki kabla ya kuingizwa kwenye mfumo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuepuka tatizo la malimbikizo ya mshahara vilevile Serikali inatekeleza mikakati mbalimbali iliyojivekea kama ifuatavyo:-

(i) Serikali imeanza kutumia Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mshahara (*Human Capital Management Information System (HCMIS)*) katika kushughulikia mishahara ya watumishi wa umma pale mwajiri alipo ili kuepuka ucheleweshaji.

(ii) Kutekelezwa kwa Waraka wa Katibu Mkuu Kiongozi Na.1 wa mwaka 2009 kuhusu udhibiti na ongozeko la madeni ya Serikali kwa watumishi wa Umma, Waraka wa Katibu Mkuu Kiongozi Na.1 wa mwaka 2010 kuhusu uwajibikaji katika kusimamia rasilimali watu Waraka wa Katibu Mkuu Utumishi Na. 1 wa mwaka 2011 kuhusu kuimarisha usimamizi wa rasilimali watu Waraka wa Hazina Na. 2 wa mwaka 2010 kuhusu uwajibikaji na udhibiti katika usimamizi wa malipo ya mishahara.

24 APRILI, 2013

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hatua hizi nilizozitaja hapo juu sio kweli kwamba Serikali imekuwa ikipuuza malalamiko ya wafanyakazi kwa kuwa kwa nyakati mbalimbali ikipokea, huhakiki na kulipa madai ya malimbikizo ya mshahara na matumizi mengineyo. (*Makofi*)

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa Serikali imekiri kwamba imeanza kulipa madeni ya wafanyakazi wakiwemo walimu kuanzia mwaka 2011/2012 lakini kutokana na taarifa tulizo nazo ni kweli kwamba kuanzia mwaka 2011 kushuka chini bado kuna watumishi hususan walimu ambao wana malimbikizo ya mishahara yao na stahili zao hususan Chama cha Walimu ambacho kimetoa taarifa kwamba mpaka sasa hivi kinaidai Serikali jumla ya shilingi bilioni 27.

Je, ni lini Serikali italipa malimbikizo ya watumishi hawa hususan walimu ili elimu yetu iendelee kuwa endelevu na bora?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, katika Bajeti ya mwaka jana tulipitisha hapa fedha za kuwalipa walimu ambao watafanya kazi katika mazingira magumu jumla ya shillingi 500,000/-. Lakini mpaka sasa hivi kuna malalamiko makubwa ya walimu hususan ni vijijiini wanaofanya kazi katika mazingira hayo magumu kwamba zile fedha hazijalipwa mpaka sasa hivi na kwa taarifa tulizo nazo ni kwamba zile fedha zilitoka kwa wafadhili na Wizara imetumia katika shughuli nyingine.

Je, ni utaratibu gani uliotumika kwa Wizara kubadilisha matumizi ya fedha hizo bila kwanza kuleta hapa Bungeni? Ahsante sana.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA ELIMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, moja ni kwamba Julai, 2011 wakati Chama cha Walimu kilipotangaza kwamba kinaidai Serikali shilingi bilioni 29, ilikuwa inajumuisha malimbikizo ya madeni yote mpaka kipindi hicho.

Lakini Serikali ilifanya hatua ya kukaa nao pamoja baada ya kutangaza hivyo, ikaamua kuhakiki pamoja na CWT na ikagundulika kwamba sio bilioni 29, waliyokuwa wanasema bali ni shilingi bilioni 52. Serikali ikatenga fedha hizo ikaanza kuzilipa awamu kwa awamu lakini kwa njia uharaka kwa sababu ilipangwa mishahara ilipwe na Hazina na fedha zisizokuwa za mishahara italipwa na TAMISEMI pamoja na Wizara ya Elimu. Mpaka Januari mwaka huu 2013 deni lile la bilioni 52 pesa zote zimekwishalipwa na hakuna pesa ambayo haijalipwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nina hakika kwamba kuanzia pale tulipokubaliana hivyo madeni yaliendelea kujijenga lakini tuko katika mkakati kama alivyosema, alitangulia kujibu swalii hili kwamba tuko katika mkakati wa kuhakikisha kwamba tunadhibiti na haturudii tena kurundikana na madeni hayo kwa miaka ijayo ili tuwaondoshee adha walimu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hili la pili linalohusu shilingi 500,000/- zile za mazingira magumu ambazo tumepewa na wahisani; tulipewa fedha hizo kwa mwaka mmoja na kwa walimu tu. Wakati zinaandalisha kulipwa ikazuka mgogoro kwamba wale wanaoripoti mwaka juzi ule ndiyo wanalipwa posho zile za kuingia katika mazingira magumu.

Lakini Walimu waliokuwepo nao wakadai kwamba sisi je, ambao tupo tayari hapa posho zetu ziko wapi. Lakini katika mazingira tuliyonayo kuna watumishi wengi tu kwenye Wilaya hizo kama waganga na kadhalika ambao wakaja juu nao.

Serikali ikalazimika ku-*hold* na kuzungumza na mhisani ili zitumike zile pesa kwa namna nyingine ya kuwafaa walimu hawa kuliko kuwapa posho ambayo tayari imeshaingia katika mgogoro. (*Makof!*)

24 APRILI, 2013

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Kwa mujibu wa Katiba kifungu cha 20 (1) na (4) suala la wafanyakazi kuwa wanachama wa chama chochote cha wafanyakazi ni suala la hiari. Sasa hivi karibuni kuna kesi moja pale manispaa ya Kigoma Ujiji ya walimu kuendelea kukatwa asilimia mbili na Chama cha Walimu.

Tatizo liliopo ni mwajiri kukataa kuondoa yale makato na kesi ilishaisha Mahakamani. Suala hili halipo Mahakamani kama Mheshimiwa Naibu Waziri alivyoeleza.

Je, Waziri yupo tayari kuweza kusimamia suala hili ili kuhakikisha kwamba walimu wa Manispaa ya Kigoma Ujiji ambao wameshaomba kujiondoa na shauri lilihakwisha Mahakamani ili makato yao haya ya asilimia mbili yaweze kusimama mara moja ili wizi huu au tatizo hilli la Chama cha Walimu kuendelea kuwakata pesa zao ambazo wao hawako hiari iweze kukoma?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Machali, swali la msingi linahusu malimbikizo ya mishahara lakini namwona Mheshimiwa Waziri Kazi na Ajira.

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Chama cha Wafanyakazi ni chama cha hiari na tunaomba wafanyakazi wote wajue hivyo. Kwa hiyo, walimo kama wafanyakazi wengine kuingia *CWT*lazima waingie kwa hiari kwa kujaza fomu na kwa kujaza fomu nyingine ambayo inaruhusu makato.

Lakini tatizo la walimu ni kwamba katika Sheria hiyo wanapokuwa wafanyakazi wanapoingia kwenye chama na ni zaidi ya asilimia 50 kuna kitu kinaitwa Wakala wa kusaidia mazungumzo na mwajiri kwa chama husika. Kwa hiyo, walimu kinachowakumba ni hicho.

24 APRILI, 2013

Lakini tumeshaagiza vyama vyote vituletee taarifa ni wafanyakazi wangapi wanaowakata na ni wafanyakazi wangapi wanaokatwa hiyo ada ya uwakala. Chama cha Walimu wametuambia by June, 2013 watakuwa wametuletea hiyo taarifa na tumewaagiza pia watoe elimu kwa wafanyakazi wao kabla hawajawakata hiyo ada ya uwakala.

Na. 96

### **Tatizo la Ulipaji wa Mafao ya Wastaifu**

**MHE. SAID AMOUR ARFI** aliluliza:-

Kumekuwepo na tatizo sugu la kulipa mafao ya wastaifu na mirathi kwa waliokuwa watumishi wa umma.

Je, ni sababu zipi zinazopelekea Serikali isilipe stahiki hizo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mbunge wa Mpanda Mjini, kama ifuatavyo:-

Mhehsimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa inalipa stahiki za wastaifu na warithi wa mirathi kwa wakati pale nyaraka na kumbukumbu kamilifu zinapofikishwa Hazina.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu kubwa inayosababisha malipo tajwa kuchelewa ni baadhi ya waajiri kutokamilisha taarifa za waajiriwa wao na kuziwasilisha Hazina ndani ya majalada husika kwa wakati ili Hazina waweze kulipa madai husika.

Aidha, taratibu zinamtaka kila mstaifu au mrithi kuhakiki taarifa zao kwenye mifuko ya pensheni kila baada ya miezi sita (6) na asiyehakiki malipo yake husitishwa hadi atakapofika kuhakiki.

24 APRILI, 2013

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wastaafu ambao walilipwa kwa mkupua huko nyuma na kurejeshwa kwenye *payroll* ya Serikali hivi karibuni, ucheleweshaji umekuwa unatokana kwa wastaafu hao kutokamilisha nyaraka na kuziwasilisha Hazina kwa wakati.

Aidha, kwa upande wa malipo ya mirathi kumekuwepo na matatizo kwa baadhi ya warithi/wasimamizi wa mirathi ama kutoelewa taratibu au migongano ndani ya familia hali inayosababisha malipo kuchelewa. Mfano kuna madai yalifishwa Hazina baada ya miaka saba tangu kifo cha mtumishi kutokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Fedha kwa kutambua tatizo hili imekuwa ikitoa elimu kwa wadau na waajiri kwa njia mbalimbali ikiwemo vipindi vyta redio, runinga na semina mbalimbali za kikanda. Aidha, Hazina kupitia maonyesho ya sabasaba, nane nane na wiki ya Utumishi wa Umma imekuwa ikitoa elimu hii kwenye mabanda yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inapenda kutoa wito kwa wastaafu na wasimamizi/warithi wa mirathi kuhakikisha wanahakiki taarifa zao kila baada ya miezi sita ili kuepusha tatizo la kufutwa/kuchelewesha malipo yap.

Aidha Ofisi za Hazina Ndogo zilizopo kila Mkoa zina Afisa anayeratibu masuala ya wastaafu na mirathi, hivyo ni vema wananchi wakazitumia ofisi hizi badala ya kusafiri hadi Dar es Salaam. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na maelezo marefu sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakin kimsingi anasema kwamba wastaafu na waarithi wa mirathi wanalipwa kwa wakati. Naomba tu unisaidie Mheshimiwa Naibu Waziri ni kwamba nimeandikiwa SMS na yatima wanasema kwamba watanikumbuka kwa kutokuwasimamia kulipwa mafao yao ya mirathi ya marehemu Peter Mtindo aliyefariki tangu mwaka 2003 na akawasilisha nyaraka zake mwaka 2005 na akafuatilia ofisi

ya *TDS* mwaka 2009 akakuta jarada limepotea, likatumwa *temporally file* mwaka 2010 na mpaka leo mwaka 2013 hawajaliwa na wewe unasema wanalipwa kwa wakati. Kama mnawadhulumu watu hawa mseme na kama Serikali itakuwa tayari kuwalipa sasa pamoja na riba kutokana na kuwacheleweshea malipo yao. Hilo swali la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili wastaaifu wengi hawalipwi fedha zao kwa wakati na hasa mifuko wa *PSPF* unachelewesha kulipa mafao ya wastaaifu kwa wakati, aidha kwa sababu ya ukata ulioko *PSPF*.

Je, Serikali imeshalipa madeni inayodaiwa kwenye mifuko hii ya hifadhi ya Jamii?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):**

Mheshimiwa Nailbu Spika, kwanza naomba kukuhakikishia wewe pamoja na Wabunge wote kwamba Serikali ama Hazina inapopata nyaraka zote halali kwa wakati, basi *within seven days* tunalipa mafao hayo. Sikatai *that is the policy that we have*, sikatai kuna mtatizo baadhi ya *communication flow* baina ya wale wanaofanya hiyo kazi na wale wanaokwenda kudai mafao yao, sikatai hiyo ipo kwa sababu wale wote ni binadamu lakini ni *policy* yetu kulipa *within seven days*.

Mheshimiwa Arfi umesema hiyo *special case* lakini ninaomba mimi kama Naibu Waziri nипатие hiso nyaraka nizifuatilie na ninakuhakikishia kuwa kama hakuna matatizo yoyote basi huyo ama hao mayatima watalipwa mali yao kama kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haioko hapa kumdhulumu mtu yoyote. Lakini suala la pili kuhusiana na mifuko ninadhani hiyo ni ripoti ya *CAG* imetokana na ripoti ya *CAG definitely* tutakuja kujibu, tutatoa maelezo kutokana na majibu ambayo sisi kama Serikali tutalipa ku-*respond*hiyo ripiti ya *CAG*. Suala la mwanzo ninamwomba Mheshimiwa Arfi nипатие hiso document na tutakwenda kuzifuatilia, tatizo hasa liko wapi ahsante sana.

24 APRILI, 2013

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wapo walimu wastaafu wa Singida Mjini ambaao walifanya kazi kwa Mkataba kwa miaka miwili na ambaao nimepiga kelele sana hapa Bungeni, sasa hivi wamelipwa walimu saba kati ya nane amebakia Mwalimu Manase Mboga.

Je, huyu mwalimu Manase Mboga atalipwa lini stahili zake maana hata afya yake imedhoofu asije akafa kama wengine walivyokufa bila kupata mafao yao?

**MHE. SAADA MKUYA SALUM (NAIBU WAZIRI WA FEDHA):** Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana kuwa labda kulikuwa na matatizo ya taarifa kutokana na huyu mawalimu lakini ninaomba nipatiwe hizo nyaraka *again* twende tukafuatilie ni kwa nini hasa mwalimu huyu naye hajalipwa akama ambavyo wenzie walivyolipwa. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ninashukuru sana, sasa tuhame hapa katika Wizara ya Fedha na mimi niwaambie tu Wizara ya Fedha kuwa kila Mbunge wa Jimbo hapa ana orodha ya wastaafu ambaao hawajalipwa miaka. Kwa hiyo, ni jambo la kulitazama kipeke yake kabisa. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi Mheshimiwa Silvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini.

Na. 97

**Gereza la Mkuza – Kibaha Mjini  
Kuboreshwa**

**MHE. SILVESTRY F. KOKA** aliuliza:-

Gereza la Mkuza lililopo Kibaha Mjini lilijengwa mwaka 1995/1996 likiwa na uwezo wa kuchukua mahabusu 45 tu lakini sasa hivi linachukua mahabusu 150 likiwa na uhaba wa nyumba za askari na pia hospitali iliyopo inahudumia wafanyakazi na wananchi na hivyo haitoshelezi mahitaji.

24 APRILI, 2013

(a) Je, Serikali haioni kuna haja ya kulifanya Gereza kuwa la Mkoa na kupewa vifaa vya kutosha?

(b) Je, ni Serikali itajenga majengo na ofisi muhimu zinazokosekana katika Gereza hilo?

### **NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mmabo ya Ndani ya Nchi ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Silvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote ninaomba nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kuwa katika Muundo wa magereza nchini hakuna daraja la Gereza la Mkoa. Magereza yamegawanyika katika makundi manne ambayo ni Magereza ya kati (*Central Prisons*), Magereza makubwa ya wazi (*Open Farm Prisons*), Magereza ya Wilaya (*District Prisons*) na Kambi ya Magereza (*Prisons Camps*). Kwa kuzingatia maelezo hayo ni wazi kuwa Gereza la Mkuza haliwezi kufanywa Gereza la Mkoa.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, Gereza la Mkuza linakosa majengo ya msingi kama vile jengo la utawala wa Zahanati ya nje ambayo ujenzi haujakamilika. Hata hivyo Serikali itaendelea na mpango wake wa kujenga majengo ya magereza katika Magereza yote nchini kote likiwamo Gereza la Mkuza na kutoa vifaa kadiri hali ya fedha itakavyoruhusu.

**MHE. SILVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Gereza hili linahifadhi Mahabusu na Wafungwa zaidi ya mara mbili ya uwezo wake ambapo liliengwa na kwa kuwa sasa Mahabusu hawa ambaao ni wananchi ambaao bado hawajapatikana na hatia wanakaa katika hali ngumu na hususani wakati wa jua na mvua kama hivi sasa. Kwa kuwa Gereza hili limezungushiwa miti na senyenge mithili ya boma la mbuzi au ng'ombe

24 APRILI, 2013

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Mahabusu hawa na Wafungwa hawa kwa jithada za haraka wanapata mahali salama pa kukaa ili utaratibu mzima na stahili zao zote ziweze kupatikana kwa mujibu wa Sheria?

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, pale kwenye Gereza hili kuna Zahanati ambayo kimsingi inawahudumia Wafungwa, Watumishi pamoja na Wananchi, lakini majengo ya Zahanati hii ni duni kupita kiasi na hata vifaa ni duni sana.

Je, Serikali sasa kwa utaratibu huo huo Gereza limekwishafanya utaratibu wa kujitolea na kuanza kuandaa ujenzi wa Zahanati mpya?

Je, Serikali sasa ina mpango gani wa haraka kuhakikisha Zahanati hii inaboreshwa ili Wafungwa hawa pamoja na wananchi wa jirani waweze kupata huduma kutoka Zahanati hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kuhusu uhifadhi wa Mahabusu hivi karibuni mwaka jana na mwaka huu Wizara kwa niaba ya Serikali imejenga mabweni mawili pale na kila bweni lina uwezo wa kuchukua Mahabusu 50. Mabweni haya kilichobakia ni kazi ndogo ya kupiga plasta na kuweka meshi kwa ajili ya kuongeza usalama au uhakika wa kutokutoroka kwa watu hawa. Ni lengo la Serikali na Wizara kuhakikisha kuwa kazi hii ambayo iko hatua kubwa sana inakamilika ili hawa Mahabusu wapate hifadhi stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Zahanati kwanza ninaomba niwapongeze wananchi na Mkuu wa Gereza hili kwa kujitolea siyo tu kwa ujenzi wa Zahanati lakini pia kuna nyumba tunaita za ubunifu pale nyumba nne wamejitlea, na ni wajibu wetu sasa Serikali kuhakikisha kuwa tunaungana nao mkono ili kuikamilisha zahanati hii haraka iwezekanavyo. Pamoja na kusema hivyo ni lazima tukiri kuwa Bajeti ni ndogo na Magereza yenye matatizo ni mengi nchini lakini tutaliangalia Gereza la Mkuza kama hali ya hewa itakavyoruhusu. (*Makof!*)

24 APRILI, 2013

Na. 98

### **Uzalishaji wa Gesi Nchini**

**MHE. RITA E. KABATI** aliuliza:-

Nchi yetu imeanza kuzalisha gesi kwa wingi:-

(a) Je, gesi hiyo inazalishwa kiasi gani?

(b) Je, ni kiasi gani cha gesi kinafika Ubungo kwenye mitambo kutoka huko inakozalishwa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE.GEORGE B.SIMBACHAWENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya futi za ujazo zipatazo milioni 105 zinazalishwa *Mnazi Bay* na Songosongo kwa siku, ambapo futi za ujazo milioni 103 zinazalishwa Kisiwani Songo Songo na futi za ujazo milioni 2 zinazalishwa *Mnazi Bay* Mtwara.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wastani futi za ujazo milioni 100 hadi 203 za gesi zinafika Ubungo kwenye kituo cha kupokelea gesi (*receiving station*) kila siku kwa ajili ya matumizi ya kuzalisha umeme, matumizi ya viwandani, hotelini, majumbani na magari. Kati ya hizo kiasi cha futi za ujazo milioni 90 zinatumika kuzalisha umeme katika mitambo na kufua umeme wa *SONGAS* na *TANESCO* iliyopo Ubungo na Tegeta. Kiasi cha futi za ujazo milioni 10 hadi 13 ni kwa ajili ya matumizi mengine yaliyotajwa hapo juu.

**MHE. RITA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakumbuka Kamati ya Nishati na Madini iliunda Kamati ndogo kwa ajili ya kuchunguza mapunjo ya mauzo ya gesi ya dola milioni 21 kutoka katika kampuni ya *Pan African*.

24 APRILI, 2013

Je, malipo hayo yalishalipwa na Serikali?

(c) Serikali imejipanga vipi kuwaelimisha wananchi ili kusitokee tatizo kama lililotokea Mtwara katika maeneo mengine ambako kumegundulika dalili ya madini ya gesi au madini mengine?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE.GEORGE**

**B.SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa Kamati ilipoundwa ya Nishati na Madini ile ndogo iliweza kugundua kuwa kulikuwa na mapunjo na hivyo kuagiza Serikali iweze kuzirejesha hizi fedha. Lakini pia ni kweli kuwa *Pan Africa* wanaidai *TANESCO* pesa nyngi pengine kuliko hata ambazo tunawadai na katika hali hiyo tunachokifanya pale ni kama tunalipana maana tunadaiana na ile ni biashara endelevu na hivyo tunakatana humo kwa humo lakini itafika wakati ambapo na sisi tutakapokuwa hatudaiwi basi deni lile litakuwa limekwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hawa ni wadau ambaao tunafanya nao biashara na wao wameweka uwekezaji ni lazima tuheshimu uwekezaji huku tukiamini kuwa tunapaswa kulinda rasilimali za Taifa ili tusiweze kupunjwa.

Suala la elimu kwa rasilimali kama ilivyotokea kule Mtwara ni kweli kuwa Mtwara kumetokea hali ambayo ilipelekeea kuhitajika sana kuelimishwa kwa wananchi na niseme tu kuwa mwalimu wa kwanza katika jambo hili amekuwa ni Mheshimiwa Rais ambaye ameweza kutoa elimu katika hotuba zake, lakini pia Makamu wa Rais amesema jambo hili, Waziri Mkuu amesema jambo hili, Waziri wangu Professor Muhongo amesema jambo hili na mimi nimesema lakini pia viongozi mbalimbali wamelisemea jambo hili. (*Makof!*)

Nichukue nafasi hii kuwaomba sana wote ambaao tunajua umuhimu wa ku *share* rasilimali za Taifa letu tushirikiane katika kutoa elimu pale tunapoona kuna haja ya kufanya hivyo na siyo kutumia mwanya huo pengine kwa faida binafsi na faida ya muda mfupi na hasa kwa sisi

wanasiasa. Ninasema hivi kwa sababu kwa kiasi kikubwa sasa kule Mtwara hali imetulia wananchi wameelewa basi iweb ni jukumu la wananchi wote wale tunaoelewa na hasa wanasiasa kutoa elimu na siyo kusema hatujatoa elimu, sote tutoe elimu kwasababu ni jukumu letu kama viongozi.

**MHE. RITA L. MLAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa nchi yetu imepata bahati ya kupata gesi nyingi namna hiyo ambayo inaweza kutusaidia kwa uchumi wa nchi yetu kama kujenga viwanda, umeme na mambo mengine mengi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutokuiua kabisa hii gesi ili iweke *reserve* kama nchi za wenzetu kwa miaka mingi ijayo ili tuweze kuitumia na tuuze bidhaa tutakazozipata kwa ajili ya kutumia gesi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE.GEORGE B.SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na madini ninapenda kujibu swalii nyongeza la Mheshimiwa Rita Mlaki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wake ni mzuri na unawezekana tu pale kama una resource hiyo kwa kiasi kidogo lakini kiasi tulichonacho tulichogundua na tunachotarajiwa kuwa nacho baada ya kujenga miundombinu ni kiasi kikubwa ambacho kw hakika tunaweza kutumia kwa haya yote anayoyasema ya kuzalisha umeme, viwanda na kila kitu nabado tukauza nje. Lakini tukubaliane kuwa tunapoingia katika uzalishaji, utafiti na utafutaji wa rasilimali hii ziko gharama kubwa za mitaji kutoka nje ambazo tunashirikiana kama wadau muhimu wa kawaida katika uchumi wa kileo wa Dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, katika makubaliano hayo kuuza nje pia ni eneo muhimu sana kwa sababu na wao wanahitaji kurejesha rasilimali ile kwa uchumi wetu na kwa kiasi cha uchumi wetu hatuwezi kuwarejeshea fedha ile kwa muda huo ambao tumekubaliana, nirudie kusema kuwa rasilimali hii ni nyingi na inaweza kufanya haya yote lakini pia tukaweza kuuza nje.

24 APRILI, 2013

Na. 99

**Mradi wa Kuvuta Umeme Kutoka  
Manyoni Kwenda Nkonko**

**MHE.CAPT. JOHN Z. CHILIGATI** aliuliza:-

Licha ya kazi nzuri inayofanywa na Shirika la kusambaza Umeme Vijijini (*REA*)bado kuna tataizo la kupeleka Umeme Vijijini katika Wilaya ya Manyoni hasa katika Tarafa ya Nkonko ambako hakuna hata kijiji kimoja chenye umeme:-

Je, ni lini *REA* itaananza mradi wa kuvuta umeme kutoka Manyoni Mjini kwenda Nkonko hadi kijiji cha Sanza?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE.GEORGE B. SIMBACHAWENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Capt. John Zefania Chiligati, Kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa kuvuta umeme kutoka Manyoni Mjini kwenda Nkonko hadi Kijiji cha Sanza pamoja na vijiji vya Chikola,Chidamsulu, Heka,Mwitikiala, Sasilo, Chikombo, Mpola, Ntumbi, Iseke, Igwamadete na Ntope umejumuishwa katika Mpango kabambe wa kiusambaza umeme vijijini Awamu ya pili chini ya uwezeshaji wa Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*). Zabuni ya kuwapata wakandarasi wa kazi hizi ilitangazwa mwezi Desemba, 2012 na kufunguliwa mwezi Machi, 2013 na wakati wowote atateuliwa Mkandarasi wa kujenga mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi za mradi huu zitajumuisha: (i) Ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa Kv 33 yenye urefu wa Km 156,(ii) Ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa Volti 400 yenye urefu wa Km 26,(iii) Ufungaji wa *transfoma tano(5)* za *KVA 25*; sita (6) za *KVA 50* na moja (1) ya *KVA100*,na (iv)Kuunganisha wateja wa awali wapatao 650.

Gharama za kazi hizi ni shilingi bilioni 6.1 na zinatarajiwa kutekelezwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri na yanayotia moyo wananchi wa Tarafa ya Nkonko lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwanza, katika orodha ya vijiji vitakavyonufaika na mradi huu Kijiji cha Itetema hakimo na nguzo zinapita hapo hapo katika Kijiji hicho lakini vilevile umeme ukishafika pale Sanza ambako ndiko Makao Makuu ya Kata na Vijiji viwili vya Kata hiyo Kijiji cha Kiteho na Ikasi viko kilomita kama nane kutoka Makao Makuu ya Kata navyo havimo.

Je, Waziri anasemaje kuhusu Vijiji hivi?

Hivi sasa *REA* wanamalizia mradi wa kusambaza umeme kutoka Manyoni Mjini mpaka Kijiji cha Kintingu Vijiji vingi katika mradi huo umeme umekwisha waka lakini nguzo katika vijiji hivyo hivyo hazijasambazwa kulingana na Mkataba jinsi ulivyo, na wananchi ambapo nguzo hazijafika wameshalipia *REA* wanasema wameishiwa na fedha.

Kwa hiyo, wametukatisha tamaa ninaomba Waziri au Wizara inasemaje kuhusu vile vijiji ambavyo nguzo hazijafika na wananchi wameshalipa lakini umeme hawajapatiwa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE.GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika orodha niliyoitaja na pengine katika orodha zingine zozote zile za miradi iliyoko katika Majimbo ya Waheshimiwa Wabunge, inawezekana tukataja kijiji cha mbele hapa vya katikati tusivitaje. Ninataka kuwahakikisha kuwa hilo siyo tatizo hata kidogo kwa sababu kama tulivyosema *formula* yetu kuu ni kwamba umeme hauruki kijiji sasa. Lakini pale ambapo umeme umepita juu tunakuja na mradi kwa ajili ya kushusha ambao utakuwa unahuishisha *transforma* na *electrification* kidogo.

24 APRIL, 2013

Kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa kama kijiji hiki cha Itetema kiko katikati *formula* yetu inasema haturuki.

Hili suala la maana ni kama masuala matatu kuna suala la Sanza ambalo anasema ni kilomita nane kutoka mradi unapoishia, inapotokea kuwa ni kilomita nane na pakawa kiuchumi tunapaona panafaa na kwamba mradi ule umeishia nyuma kidogo hapa kuna ni tatizo. Kwa sababu ni ama unasema unaongeza kazi ya ziada ama inakuwa vinginevyo vyo vyote vile.

Lakini miradi hii tumejaribu kuweka *provision* katika mikataba yetu na wakandarasi kwamba tutahakikisha kuwa tuna *renegotiate* kila mara kulingana na hali ya mazingira inavyokwenda. Kwa hiyo, katika Sheria yetu ya manunuzi pia kuna *allowance* ya 15% ya *extension*. Kwa hiyo, *we can play within* tukaona tunaweza tukafanya nini lakini hii siyo *fomula* kuu, *formula* inasema ni ile inasema kijiji kiwe katikati.

Lakini la pili ni lile la mradi wa Manyoni - Kitinku ambapo umeme umewaka lakini bado maeneo mengine hayajafikiwa, tutawasiliana na Mbunge tuone namna bora ya kufanya jambo hilo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zitto usubiri kidogo tumalizane na Manyoni, Mheshimiwa Lwanji swali fupi sana na Mheshimiwa Zitto utafuata.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Naibu Spika ahsante sana. Ili kutoa umeme kutoka Manyoni Mjini kwenda Chikola au Nkonko kuna vijiji njiani, kijiji cha Kashangu, Kijiji cha Idondyandole na Kijiji cha Jeje ambavyo havikutajwa katika orodha ya hivyo vijiji ambavyo umeme unapita. Je, Serikali inasemaje kuhusu hili?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba kama vijiji

hivyo visto katikati na kinachotajwa kipelekewa umeme kipo mwisho na umeme utatokea Manyoni, ni dhahiri kwamba *formula* tulioiweka ni kwamba haturuki nitafanya kazi, kwa hivyo nimwondoe wasiwasi Mbunge kwamba kijiji cha Kashangu, Idodyandole na Jeje vitakuwa katikati kwa hivyo havitarukwa na vyenyewe vitapewa umeme.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, toka mwaka 2011 Serikali imekuwa ikipanga bajeti kwa ajili ya miradi wa umeme vijijini, vijiji 16 katika Jimbo la Kigoma Kaskazini lakini mpaka sasa miradi hiyo bado hajifanyika.

Lakini hali ni hiyo hiyo kwa Majimbo mengi sana ya uchaguzi. Hali halisi ya miradi ya umeme Vijijini (*REA*) ikoje mpaka hivi sasa, ili tuweze kupata uhakika ni namna gani tunaweza kwenda kuwaambia wananchi, kwa sababu kila wakati tunaenda kuwaambia wananchi kuhusu miradi na haitokelezwi, hali ikoje kihalisia kwa miradi yote ya *REA* hapa nchini.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tangu mwaka 2011 tumekuwa na miradi ya *REA* na hapa tulikuwa na *REA Phase I* na tumetekeleza katika baadhi ya maeneo, lakini kwa sasa tumekuja na mpango mkubwa ambao tumeukaza kutokana na Bajeti yetu ya mwaka jana tulipitisha vijiji vile. Niseme tu tuna vijiji vya Mheshimiwa Mbunge Kaskazini visto na tuna orodha kubwa sana ya vijiji vingi zaidi ya 1200 kwa nchi nzima. Vijihi vidi dhamira ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni kuhakikisha kwamba inapeleka umeme katika vijiji vyote hivi vikiwemo vijiji 16 vya Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningemwomba Mbunge siyo tu nikuletee pia na wewe uje tuweze ku-share kwa sababu tumefikia hatua ya mbele sana ambayo bado zile *documents* bado zipo kwenye *process* ya *procurement*. Kwa hiyo, nikuhakikishie kwamba tukionana utaweza kuviona na nitakuonesha usiwe na mashaka. (*Makofii*)

24 APRILI, 2013

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge natambua mna maswali mengi sana kwenye eneo hili la umeme, lakini tuendelee na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii.

Na. 100

**Uwiano wa Mitaala ya Tanzania Zanzibar  
na Tanzania Bara**

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA** aliuliza:-

Wanafunzi wa Tanzania Zanzibar hufanya mtihani wa Kidato cha Nne ulio sawa na ule wa Tanzania Bara licha tofauti ya baadhi ya sehemu ya mitaala iliyopo baina ya sehemu hizo mbili za Muungano:-

- (a) Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu uwiano na ushirikiano wa mitaala hiyo?
- (b) Je, Serikali haioni kuwa ndiyo utofauti wa mitaala hiyo unawaathiri sana wanafunzi wa Tanzania Zanzibar na kuwa ndiyo sababu ya kufeli katika mitihani yao?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**  
alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mbunge wa Chwaka, lenye sehemu a na b kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hakuna tofauti ya mtaala wa elimu ya sekondari kati ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar, kwa msingi huu, kwa kuwa, mtaala ni mmoja wanafunzi wa elimu ya sekondari wa pande hizi mbili za Muungano hufanya mtihani wa kidato cha Nne ulio sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la ushirikiano Baraza la Mitihani Tanzania limekuwa likiwahusisha walimu wa sekondari wa pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano katika masuala ya kutunga mitihani, kufanya *moderation*, kusahihisha mitihani na kuwianisha alama za ufaulu (*standardization*).

Aidha, Baraza la Mitihani limekuwa likishirikiana na Taasisi ya elimu Tanzania Bara pamoja na taasisi ya elimu Tanzania Zanzibar katika shughuli zote za uandaaji na uboreshaji wa mitaala kama vile kushiriki katika kuboresha mihtasari ya masomo (*syllabus*) na mikutano mbalimbali ya paneli za masomo mbalimbali ya sekondari.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, taarifa iliyopo ya uhakika ni kwamba baada ya walimu wa Zanzibar kusahihisha mitihani na kumaliza hurejea nyumbani, na sehemu iliyosalia hadi matokeo hushirikishwa sehemu moja ya Muungano ikiwa kama wapo watu pale ni kama ajira. Je, hili utathibitishia vipi wananchi wa Zanzibar kuhusu taarifa hii.

Kama hili uliolieleza ni kweli Je, ni kwa kiwango gani ushirikishi wa watu wa Zanzibar?

#### **NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:**

Mheshimiwa Naibu Spika, si kweli kwamba baada ya kusahihisha mitihani walimu wa Zanzibar wanaondoka wote kurudi majumbani na baadaye upande mmoja ndiyo wanashiriki katika kumalizia kazi ile. Kwa sababu hata katika Bodi ya Baraza la Mitihani ambapo Kamishana wa Zanzibar ni Mjumbe, Mkurugenzi wa Mitihani Zanzibar ni Mjumbe, Mkurugenzi wa Mitaala na mwakilishi kutoka huo Kikuu Cha Serikali ya Zanzibar vile vile ni mjumbe. Hawa wote huwa wanakuwepo kuanzia mwanzo wa kazi mpaka mwisho wa kazi. Ndiyo maana tunasema Baraza la Mitihani lina Bodi na hao ndiyo huwa wanatangaza hata matokeo. Kwa hiyo ushirikishwaji ni kwa pande zote mbili kwa pamoja.

24 APRILI, 2013

**NAIBU SPIKA:** Swali hili linaendelea kututhibitishia kwamba mitaala ipo, Mheshimiwa Ndugulile swali la mwisho la nyongeza.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Naibu Spika nashukuru kwa kunipatia fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, mitaala huanzia katika sera ya elimu na kwa muda mrefu Wizara ya Elimu imekuwa inalifanya kazi suala la sera ya elimu.

Je, ni lini sera hii ya elimu itawekwa hadharani na kuanza kutumika nchini?

Swali la Pili;..

**NAIBU SPIKA:** Ni swali moja tu Mheshimiwa. Waziri wa Elimu kwa kifupi sana.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwa sababu suala la elimu ni suala muhimu sana na ni la uhai wa Taifa, Serikali imechukua muda mrefu kulifanya kazi kwa umakini sana. Imeshaletwa Bungeni mara mbili na hivi sasa Bunge lako limepanga kufanya mapitio ya Sera hiyo mpya tarehe 19 Mei, 2013 ndiyo tarehe ambayo tumepewaa.

Kwa hiyo tutakuja tena mara ya tatu katika Bunge hili Tukufu, kwa njia ya semina ili baada ya hapo ipelekwe kwenye Baraza la Mwaziri iweze kuwa Sera rasmi na tutaanza kuandaa mitaala mipyaa badala ya ile ya 2005.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Lakini kabla sijaauliza swali langu hili sisi wengine ni waumini wa utulivu naomba Serikali yetu iwe makini na mambo yanayoendelea huko Liwale ili isije ikawa chachu ya kutuletea vurugu kama iliyotokea Mtwara.  
*(Makof)*

24 APRILI, 2013

Na. 101

### **Nafasi za Masomo Nje ya Nchi kwa Vijana**

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA** aliuliza:-

Kwa miaka mingi vijana wa Tanzania wamekuwa wakipata nafasi za masomo nje ya nchi:-

(a) Je, ni vijana wangapi wamepata nafasi za masomo nje ya nchi kuanzia mwaka 2010-2012?

(b) Je, ni vijana wangapi kutoka Tanzania Zanzibar wamepata elimu hiyo kwa kipindi hicho?

(c) Je, ni nchi ngani vijana hao walienda kusoma?

### **NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi naomba kujibu swali la Mhehsimiwa Khalifa Suleiman Kahalifa Mbunge wa Gando, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya mwaka 2010 hadi mwaka 2012 vijana wa Kitanzania waliopata nafasi ya masomo nje ya nchi ni 342.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, *scholarship* zinazotolewa na nchi rafiki zinashindaniwa kwa kutumia vigezo vya kitaaluma, umri na uraia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa vile kinachozingatiwa zaidi ni kigezo cha kitaaluma, mwombaji ye yote anayetimiza kigezo hicho anayo haki ya kunufaika na *scholarship* bila kujali anatokea sehemu gani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Aidha, kutokana na mwingiliano wa wananchi wa pande mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inakuwa vigumu kutofautisha sehemu ya Jamhuri alipotokea mwombaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusisitiza kuwa, nafasi za masomo zinazotolewa kwa ajili ya wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwamba wote wanashindanishwa kwa vigezo vyta kitaaluma na si vinginevyo.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2010 hadi mwaka 2012, nchi ambazo zimekuwa zikitupatia nafasi za masomo nje ya nchi ni Cuba, Algeria, Urusi, Msumbiji, Serbia, Uingereza, Misri, Korea Kusini, Macedonia, Uturuki, China, Ujerumani na Oman. (*Makofii*)

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na nimeyasikia vizuri majibu ya Naibu Waziri.

Kwa kadiri ya ufahamu wangu *component* hii ya elimu ya juu ni *issue* ya Muungano na ni utamaduni wetu tokea tumeanzisha Muungano katika masuala mazito kama haya Zanzibar huwa inatengewa asilimia fulani katika masuala ya *scholarship* na hili si jambo geni. Sasa nashtuka ninaposikia hii au kwa sababu upande wa pili watu wamesoma sana?

Kwanza; nataka kujua ni sababu ipi iliyopelekea ule mpango wa zamani wa kuweka asilimi fulani kutoka Zanzibar ukaondoshwa?

Kwa sababu hali hii inaweza ikapelekea watu wa upande mmoja tu wakapata nafasi zote hizo wakaenda. Je ikitokea hali kama hii kama mwanafunzi hata mmoja hakupata fursa kama hii, upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano inawapa raha jambo kama hili? Kama haliwapi raha.

Je, ni lini watarekebisha basi hali hii?

### **WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:**

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kuhusu kutengewa nafasi kwa ajili ya wananchi wa Tanzania Zanzibar. Hatujawa na utaratibu huo wa tengeo kwa nafasi za *scholarship* kwa vijana wa Tanzania Zanzibar na wale wa Bara, tuna tengeo katika maeneo mengine kwa mfano ajira katika sekta zile za kimuungano lakini kwenye elimu hasa *scholarship* hatujawahi kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye *scholarship* kuna Kamati maalum ambayo kila zinapokuja *scholarship* Kamati hii ambayo inajumuisha Maafisa wa Bara na Maafisa wa Zanzibar kuweza kukaa pamoja na kuamua nani aende. Lakini pia nafasi hizo wakati mwingine hatuzipati zote.

Kwa mfano *Commonwealth* imetoa nafasi 12 mwaka juzi wamekwenda sita tu kwa sababu inaenda kwa vigezo. Mnapowapeleka wale watu mnasema hawa ndiyo watu wetu tunataka wapewe *scholarship* kama hawatimizi vigezo vile vya kimataifa wanaweza wasiwachukue wote.

Kwa hivyo siyo suala la tengeo ni suala la *qualification*. Kwamba kama ana-*qualify* anaenda, ni kitu ambacho kinatuma lakini hatuna uwezo nacho kwa sababu hili ni jambo ambalo linatoka kwa wahisani na wana vigezo vyao vya kuchukua wanafunzi ambao wanawachukua hatuna jambo jingine. Lile ambalo litakuwa la *mkururo* tutakuwa tunahakikisha kwamba Kamati hii ambayo inahusu Zanzibar pamoja na Tanzania Bara ndiyo inafanya maamuzi siyo Tanzania Bara peke yake inafanya maamuzi ya *scholarship* hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kama wanafunzi wa Zanzibar wote watakosa nafasi ya *scholarship* inawapendezesha hili upande wa Bara, nasema hapana. Sisi hatufurahi kama vile ambavyo Watanzania wote hawawezi wakafurahi kama itatokea katika *scholarship* wanafunzi wa Zanzibar hawakupata nafasi.

24 APRILI, 2013

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, kwa sababu ya muda Waheshimiwa Wabunge mtaona muda wetu ni mdogo na nina maswali matatu, naomba tuhamie Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, swali la Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi.

Na. 102

### **Vyama vya Ushirika Mbeya**

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE (K.n.y. MHE. GODFREY W. ZAMBI)** aliuliza:-

Vyama vya Ushirika vya *MBOCU, KYERUCU* na *MICU* vilivyoko katika Mkoa wa Mbeya vimekufa na vingine havifanyi kazi sawa sawa:-

(a) Je, Vyama hivyo vilikuwa na madeni kiasi gani ambayo vililipiwa na Serikali?

(b) Je, mali za Vyama hivyo kama maghala, samani na kadhalika, zinamilikiwa na nani?

### **NAIBU WAZIRI, KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyama vya Ushirika vya *MBOCU, KYERUCU* na *MICU* vilivyoko katika Mkoa wa Mbeya havijafa, vinafanya kazi japokuwa baadhi ni dhaifu kutokana na kujigawa kiwilaya na hivyo kupunguza nguvu za umoja wao. Chama cha Ushirika cha *KYERUCU* kilijigawa na kuanzishwa vyama viwili vya *KYECU* Wilaya ya Kyela na RUCU Wilaya ya Rungwe.

Mkoa wa Mbeya kwa sasa una Vyama Vikuu vya Ushirika sita ambavyo ni Mbeya lleje *Cooperative Union (MICU)* cha Wilaya za Mbeya na lleje, Isanza *Iyula Cooperative Union (ISAYULA)* na Mbozi *Cooperative Union (MBOCU)* vya Wilaya ya Mbozi, Rungwe *Cooperative Union (RUCU)* cha Wilaya ya Rungwe, Kyela *Cooperative Union (KYECU)* cha Wilaya ya Kyela na Chunya, *Tobacco Growers Cooperative Union (CHUTCU)* cha Wilaya ya Chunya. Vyama vya *MICU, MBOCU, ISAYULA, RUCU na KYECU* ni miongoni mwa Vyama vya ushirika 38 vilivyoahakikiwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali na kuonekana vilikuwa na madeni ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, sasa naomba kujibu swali kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Vyama vya *MICU, MBOCU, ISAYULA, RUCU na KYECU* vilikuwa na madeni ya shilingi 886,048,314 yaliyohakikiwa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali CAG na kati ya madeni hayo yaliyolipwa mpaka sasa ni shilingi 714,005,044 na madeni ya shilingi 172,043,270 hayajalipwa. Ulipaji wa madeni yaliyobaki utafanyika kulingana na upatikanaji wa rasilimali fedha. Mchanganuo wa madeni hayo ni kama ifuatavyo.

*MICU* deni lake lilikuwa 349,417,595 limelipwa lote, *MBOCU* deni lake lilikuwa milioni 50.6 kiasi kilicholipwa ni milioni 8.9 kimebaki shilingi 41,660,039, *ISAYULA* deni lilikuwa shilingi milioni 36 zimelipwa milioni 32. *RUCU* deni milioni 245 zimelipwa milioni 178 imebaki milioni 67 na *KYECU* deni ni milioni 204 imelipwa milioni 144 limebaki milioni 59.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa vyama hivyo bado vinafanya kazi na mali za vyama hivyo bado zinamilikiwa na wanaushirika wenye. (*Makofii*)

24 APRILI, 2013

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Naibu Spika ahsante sana. Kwa kuwa Vyama au Ushirika imara ndiyo njia pekee ya kuweza kumkomboa mwananchi kutokana na kunyonywa, na kwa kuwa llani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi inasitisiza kuimarisha vyama vya ushirika.

Je, Serikali ina makakati gani wa dhati kuhakikisha kwamba vyama hivi vya ushirika vinaimarishwa kwa manufaa ya wanaushirika wenyewe na wananchi kwa ujumla?

Pamoja na kwamba Naibu Waziri amejibu swali hili kwamba vyama vinafanyakazi lakini ukweli havifanyi kazi.

Je, ni vipi vyama hivi vitafufuliwa ili viweze kufanya kazi yake vizuri?

**NAIBU SPIKA:** Majibu mafupi sana Naibu Waziri.

### **NAIBU WAZIRI, KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:**

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba ushirika ni nguzo muhimu sana ya ukombozi wa mkulima pale unapofanyakazi vizuri. Nguzo kuu ya ushirika ni uzalishaji ndiyo pale vyama hivi vinapopata nguvu kadiri vinavyozalisha kwa wingi na vyenyewe vinakuwa na nguvu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo jambo la kwanza ambalo tutafanya ni kuhakikisha kwamba kwa yale mazao ambayo ushirika ule umejikita Serikali itatoa msukumo zaidi ili vyama vile viwe na uzalishaji mkubwa zaidi.

Lakini kwa upande wa pili kama tulivyosema jana wakati wa kuhitimisha Bajeti ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ni lazima sheria mpya inayokuja ya Ushirika iwe na mifumo mikali zaidi ya usimamizi na adhabu kali ili kuondoa matatizo ya wizi na ubadhilifu ndani ya vyama vya ushirika. (*Makof!*)

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Napenda kwanza, kutoa masikitiko yangu juu ya tukio lillotokea usiku wa jana katika Wilaya ya Liwale, Wakulima wa korosho wameghadhabika sana. Kulikuwa kuna mapambano makali kati yao na Askari na hatimaye wameweza kuchoma baadhi ya nyumba za Viongozi, moto.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sababu hii inatokana na ukweli kwamba, waliahidiwa wangelipwa mauzo ya korosho kiasi cha 1,200/=.

Awamu ya kwanza wakalipwa 600/=, lakini awamu ya pili wamelipwa kiasi cha 200/=, kwa maana hiyo jumla wamelipwa kiasi cha 800/=. Sasa wakulima hawa wanadai ile tofauti ya kiasi cha 400/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimezungumza na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, amenieleza kwamba, bei ya korosho imekuwa ikienda ikibadilika. Sasa ninaomba Serikali, inipatie majibu ni namna gani inaweza ikafidia hiki kiasi cha 400/=, ili mkulima aweze kulipwa kile kiasi chake cha 1,200/=? (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Zainab Kawawa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hili tukio la Liwale jana ni tukio la kusikitisha sana. Kwa sababu, kusema kweli, hii tabia ya wananchi kuchukua Sheria mkononi na kwenda kuchoma nyumba za viongozi ni lazima tukubaliane kuna vitu vimejificha humo ambavyo sio tatizo la zao la korosho. Kwa sababu, Serikali, imeshatoa tamko kwamba, tunakwenda tukibaini matatizo ya korosho yaliyotokea kwa misimu miwili. (*Makofii*)

24 APRILI, 2013

Mheshimiwa Naibu Spika, na ni lazima nikwambie, kote ambako tunalima korosho pamoja na Jimbo langu la Mkuranga, matatizo yallyosababisha korosho kutokuuzwa yanatofautiana. Kuna kwingine kuna matatizo ya Vyama vya Ushirika, kwingine kuna matatizo ya wanunuzi.

Kwa hiyo, tumesema kwamba, Serikali, tutakwenda kote ambako kuna zao la korosho na kuna matatizo, tutapitia, tutakutana na wananchi na tutajua tatizo ni nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maeneo mengine tatizo limetokana na huko huko kwenye vyama vya ushirika. Sasa inawezekana hao hao Viongozi wa Vyama vya Ushirika ndio wanahimiza watu kuchoma nyumba, ili kufunika madhambi yao.

Mheshimiwa Nailbu Spika, lakini nasema kwa kuwa, sitaki kuweka dhana hiyo ya tatizo ni nini, nimesema Serikali, itakwenda huko kubaini tatizo ni nini na italipatia ufumbuzi tatizo hili.

Sasa kwa hawa waliochoma nyumba, basi wataonana na Mheshimiwa Emmanuel Nchimbi, maana sasa hili ni tatizo lingine sio tatizo la Wizara ya Kilimo. (*Makofii*)

Na. 103

#### **Tatizo la Ukame na Fursa za Umwagiliaji Katika Wilaya ya Bahi**

**MHE. MWIGULU L. M. MADELU (K.n.y. MHE. OMARY A. BADWELL)** aliuliza:-

Wilaya ya Bahi, yeye ukame mkubwa imekuwa ikitazimika kuomba chakula Serikali Kuu kila mwaka, ili kukidhi mahitaji ya wananchi. Zipo fursa nyingi zitakazowezesha kilimo cha umwagiliaji katika Wilaya hiyo na kutoa tija kwa wananchi.

Je, Serikali iko tayari kufanya utafiti katika Wilaya hiyo, ili kubaini sababu za ukame na pia kuzibaini fursa zilizopo katika sekta ya umwagiliaji ili kuondoa tatizo la njaa katika Wilaya hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA  
alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omary Ahmad Badwell, Mbunge wa Bahi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali, inatambua kuwa Wilaya ya Bahi, ipo katika ukanda wa maeneo kame, ambapo tabia ya maeneo hayo ni pamoja na kuwa na mvua kubwa za muda mfupi na zenye mtawanyiko usloaminika, *unpredictable*. Wastani wa mvua katika Wilaya ni milimeta 600 kwa mwaka, kiwango ambacho kwa ujumla hakikidhi mahitaji ya maji kuzalisha aina nyingi za mazao, isipokuwa yale yanayostahimili ukame.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watafiti wengi, kikiwemo Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam kupitia Taasisi yake ya Tathmini ya Rasilimali (*Institute of Resource Assessment - (IRA)*, walifanya uchambuzi wa kitaalam kuhusu mwenendo wa mvua unavyoathiri kilimo katika maeneo kame, ikiwemo ya Mkoa wa Dodoma kwa kipindi kati ya miaka ya 1980 – 1997. Utafiti huo ulibaini kuwa, katika maeneo haya, ukame wa siku 10 hadi 40 mfululizo ndani ya msimu wa mvua ni hali tarajiwu. Aidha, mabadiliko ya Tabianchi yamesababisha tatizo la ukame na mafuriko kuwa kubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya hii ina historia ya kukumbwa na uhaba wa chakula karibu kila mwaka na hivyo, kulazimika kuomba msaada wa chakula. Hii ni kutokana na kiwango cha ukame katika Wilaya hii, kama nilivyosema. Hali hii inaonesha wazi umuhimu wa kuwa na mikakati ya kuwawezesha wakulima kuzalisha katika mazingira haya ya ukame.

24 APRILI, 2013

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali, imeanza kutumia fursa zilizopo ambazo ni pamoja na kuvuna maji ya mvua kwa hizi siku 40 zinazonyesha na ya mafuriko, ili kuimarisha uzalishaji wa mazao ya chakula katika Wilaya ya Bahi, kuititia Programu ya Kuendeleza Kilimo katika Maeneo Kame (*Special Development Programme for Marginal Areas - SDPMA*).

Aidha, kuititia Programu ya *ASDP*, hususan Mfuko wa Uendelezaji Kilimo cha Umwagiliaji Ngazi ya Wilaya, (*D/DF*), Serikali, ilioa jumla ya shilingi billioni 3.2 ambazo zimetumika kuboresha mifumo ya umwagiliaji ya Skimu za Mtitaa, Chikopelo, Chali, Bahi Sokoni, Bahi Makulu, Mtazamo, Matajira na Kongogo. Uboreshaji huu uliwezesha kuongeza tija ya zao la mpunga kufikia tani 6 kwa hekta katika baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kushirikiana na wananchi wa Wilaya ya Bahi, kutenga fedha kadiri Bajeti itakavyoruhusu, ili kukamilisha miradi ya umwagiliaji, kujenga miundombinu ya kuvuna maji na ya kutumia maji ya ardhini. Hivyo kuimarisha uzalishaji wa chakula katika Wilaya hiyo. (*Makofii*)

**MHE. MWIGULU L. M. MADELU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana namshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la mafuriko na kuvuna maji ni zaidi ya kuvuna maji tu kwa ajili ya umwagiliaji, bali maji yale yakitawanyika husababisha mimea pamoja na mashamba yote kupelekwa na mafuriko. Maeneo mengine yanayofanana na hili yako mengi tu kama ilivyo kwa Igunga, Kidaru, Ndago na Mtoa.

Je, Serikali, inaweza ikasema sasa kwamba, italiondoa suala hili la mabwawa kutoka Halmashauri ambazo haziwezi zikachimba mabwawa na badala yake wakaweka Wizarani ambako kuna fedha, ili kuweza kuvuna maji maeneo hayo ambayo yana mafuriko na kuepusha mimea kuharibiwa na mafuriko?

24 APRILI, 2013

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Afande Mwigulu Mchemba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hili tatizo la kuvuna maji na mafuriko, Serikali, inapeleka pesa kwenye Wilaya, kwenye Halmashauri, kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya umwagiliaji kama tulivyosema kupitia *DIDF*.

Ni utaratibu ambao kupitia mfumo wa kupeleka pesa kwenye ngazi ya chini *D – by – D*, tumeuanza katika ngazi nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kupeleka pesa, tunapeleka na taaluma. Kwa hiyo, mimi nadhani tatizo hapa haliko zaidi sana kwenye suala la fedha kuwa kwenye *Central Government* kwa sababu, pesa nydingi iko huko huko chini. Tatizo nakubaliana na Mheshimiwa Mwigulu Mchemba kwamba, kwenye maeneo ambayo kuna mafuriko tutengeneze miundombinu ya umwagiliaji ambayo, inakabiliana na mafuriko hayo kuweza kufanya *water harvesting* kwa mana ya kuvuna maji hayo na kuyahifadhi kwa ajili, ya matumizi ya wakulima pale ambapo yatahitajika msimu wa mvua ukimalizika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimekubali ushauri wake, tutalifanyia kazi.

Na. 104

**Usafirishaji wa Mazao ya Samaki  
(Mwaka 2005 – 2012)**

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR (K.n.y. MHE. HAMAD RASHID MOHAMED)** aliuliza:-

(a) Je, katika kipindi cha mwaka 2005 – 2012, Tanzania imesafirisha tani ngapi za mazao ya samaki kutoka Bahari Kuu na Maji Baridi (Maziwa)?

24 APRILI, 2013

(b) Je, ni meli ngapi za uvuvi wa Bahari Kuu, zilipewa leseni na zilisafirisha tani ngapi za samaki kwa thamani ya kiasi gani?

(c) Je, Serikali, imepata mapato kiasi gani na kwa kutoza kodi za aina gani?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI  
alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, Mbunge wa Wawi, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2005 – 2012, Tanzania imesafirisha jumla ya tani 371,317.8 za samaki na mazao ya uvuvi ambapo tani 17,954.5 ni kutoka maji chumvi na tani 353,362.7 kutoka maji baridi.

Ziwa Viktoria likiwa limetoa tani 339,893.1, Ziwa Tanganyika tani 11,418.8, Ziwa Nyasa tani 110.9 na maeneo ya maji madogo tani 1,939.9 pamoja na samaki hai 301,839. Jumla ya fedha iliyopatikana kutokana na ushuru kwa mauzo ni 54,495,683,615.73/= . Kati ya hizo 5,528,438,590.96/= kutoka maji chumvi na 48,967,245,025.77/= kutoka maji baridi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya mwaka 2009, wakati Mamlaka ya Uvuvu Bahari Kuu (*Deep Sea Fishing Authority*) kuanzishwa, Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar, zilikuwa zinatoa leseni kila mmoja kwa ajili ya uvuvi katika Bahari Kuu.

Kati ya mwaka 2005 – 2009, Tanzania Bara ilitoa jumla ya leseni 274 kwa ajili ya uvuvi katika Bahari Kuu. Baada ya kuanzishwa Mamlaka hiyo, kati ya mwaka 2010 – 2012 jumla ya leseni 124 zilitolewa. Hivyo kwa kipindi cha mwaka 2005 – 2012 jumla ya meli 398 zilipewa leseni za uvuvi wa Bahari Kuu. (*Makof!*)

Aidha, meli zote 398 zilizopewa leseni zilivua jumla ya tani 40,081.8 za samaki ambazo zilisafirishwa na kuuzwa nje ya nchi. Thamani ya samaki waliosafirishwa ni vigumu kufahamika, kwani bei ya samaki hutegemea aina ya samaki, uchakataji wake, aina ya uhifadhi wake na nchi walikouzwa; taarifa ambayo hatunazo kama Wizara.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2005 – 2012 Serikali, imepata jumla ya Dola za Kimarekani 7,780,908 kutokana na ada ya leseni sawa na 12,605,070,960/=, kwa *rate* ya sasa. Ada hizi zilizotozwa kwa viwango vya dola za Marekani 35,000 kwa mwaka kwa *Purse Seine* na dola 32,000 kwa *Longline* kwa mwaka.

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nitakuwa na maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; kwa kuwa, kuna tofauti kubwa ya mapato baina ya uvuvi wa maji baridi na uvuvi wa maji bahari, yaani bilioni 49 na bilioni 5.

Je, Serikali, iko tayari kuboresha sekta ya uvuvi wa maji ya bahari? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili. Je, Serikali, ina mikakati gani ya kuwawezesha wavuvi wadogowadogo kwa kuwapatia zana za kisasa, ili waweze kwenda kwa wakati, japokuwa kwa njia ya mkopo nafuu?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

24 APRIL, 2013

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na ye ye kwamba, tofauti ya mapato ni kubwa. Ukiona katika Ziwa Viktoria tu lenyewe, zaidi ya 70% ya mapato yote imetoka Ziwa Viktoria na hii ni kwa sababu, miundombinu iliwezekana kuboreshwa katika eneo hilo na soko la uhakika la Ulaya limekuwepo.

Tutaboresha na tayari mikakati imeanza kuhakikisha kwamba, miundombinu hasa ya bandari ya uvuvi pia, itajengwa katika eneo la Bahari Kuu, ili meli zinapokuja ziwe na mahali pa kutua, kuweka nanga, kupewa leseni na baada ya uvuvi ziweze pia kurudi na kuhakikiwa kuhakikisha kwamba, wanachovua ni halisi. Ni kiasi ambacho wameidhinishiwa kuvua. Na kwa njia hii nina uhakika kwamba, mapato yatakuwa na yataongezeka kwa sababu, Bahari kuu ndio ina uwezo zaidi kiuvuvi kuliko maji ya baridi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, tayari tumejipanga kama Serikali, na kama nilivyosema mara nyininge tena hapa, tayari Benki ya Rasilimali, imeweka dirisha la mkopo ambalo limeanza kukopesha wavuvi. Wengine wamekopeshwa zana, wengine mitaji, ili waweze kuwa na uwezo na kuongeza uwezo waweze kuvuna kwa ufanisi zaidi na kujinufaisha wenyewe na kutunufaisha sisi kama nchi kwa kuongezewa uwezo. (*Makof*)

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina swali moja dogo la nyongeza. Ni kwa nini, tunawaachia wenzetu wa Malawi wanavua uvuvi wa kisasa na sisi tunawaangalia tu? Au kwa vile lile Ziwa si letu, kama Malawi wanavyodai? (*Makof/Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Hiyo sehemu ya mwisho nimeifuta kabisa, Ziwa ni letu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

### **NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvu, naomba nijibu swalii la Mheshimiwa Capt. Damian Komba, kama ifuatavyo:-

(i) Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kupitia Bunge lako Tukufu, naomba tu niseme kwa uhakika kwamba, Ziwa Nyasa ni ziwa tunaloshirikiana na nchi ya Malawi. Sehemu ya Tanzania ambayo ipo kwenye ziwa hilo ni ya kwetu na itaendelea kuwa ya kwetu daima. (*Makofî*)

(ii) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini Wamalawi wanavua kwa kutumia vyombo nya kisasa; nadhani niseme tu kwamba, jibu linafanana na nililotoa katika jibu langu la msingi kwamba, tutajaribu kuwajengea watu wetu uwezo. Naomba Mheshimiwa Capt. Damian Komba atuvumilie.

Lakini pia nitumie Bunge lako Tukufu, kuwambia wenzetu wanaokaa kando ya ziwa hilo na wao wajikusanye, waanzishe *SACCOS*, waweze kupata mikopo na kwa njia ya mikopo hiyo, kwa uhakika na wao watakuwa na vyombo nya kisasa na teknolojia ya kisasa itakayowawezesha kuvua vizuri zaidi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yameisha na muda wetu kwa kweli, umepita. Niwashauri tu Waheshimiwa Mawaziri, majibu ya maandishi kwa baadhi ya Wizara yanakuwa ni marefu sana. Tujitahidi kuyaangalia, ule utangulizi sio wa lazima sana, ili kupunguza, kuufanya muda wetu uweze kutosha.

Naomba nimirage mgeni ambaye yuko kwenye *Galleryya* Spika na yeche ni Mheshimiwa Waziri Mkuu Mstaafu, Mheshimiwa Frederick Sumaye. Karibu sana Mheshimiwa Sumaye, kwa niaba ya Bunge hili, tunaomba tukukaribishe tena katika eneo hili ambalo umekuwa Mbunge mwenzetu kwa miaka mingi. Tutakukumbuka sana kwa ajili ya ujenzi wa Ukumbi huu, ambao tunautumia sasa kama Bunge, pamoja na mambo mengine mengi. (*Makofî*)

24 APRILI, 2013

Matangazo mawili, ia Mheshimiwa Zitto Kabwe, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali, (PAC) anawaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane Ukumbi Namba 231, Jengo la Utawala, saa 5.00. Kamati ya Hesabu za Serikali saa 5.00 wakutane Jengo la Utwala kwa kikao maalum.

Mheshimiwa Anna Magreth Abdallah, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, anawaomba Wajumbe wa Kamati hiyo, wakutane Ukumbi wa Msekwa C, Saa 7.00 mchana. Kamati ya Ulinzi na Usalama, ikutane Msekwa C, na tangazo hili limeletwa na Mheshimiwa Anna Magreth Abdallah, Ukumbi wa Msekwa.

Baada ya Matangazo hayo, Katibu?

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Liko tangazo la tatu, nimelipata sasahivi. Mheshimiwa Idd Azzan, Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club*, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge mnaopenda kushiriki mchezo wa Kikapu (*Basket Ball*), mnatakiwa kuanza mazoezi kesho tarehe 25 Aprili, katika Uwanja wa Jamhuri kuanzia saa 12.00 asubuhi.

Mazoezi haya ni kwa ajili ya kijiandaa kwa mechizijazo, chini ya Kocha Mheshimiwa Injinia Ramo Makani; wale wanaopenda *Basket Ball*. (*Makofi*)

Mwongozo? Mko wangapi? Wawili eeh? Asiongezeke mtu sasa hapo. Mheshimiwa Capt. John Komba pia? *Ok*, Mheshimiwa Machali. *Ok*, anza Mheshimiwa Machali.

## **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Ninasimama kuomba Mwongozo wako Kuhusu Utaratibu, kwa mujibu wa Kanuni ya 68 (1) pamoja na ile ya 68 (7).

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nimeuliza swali la nyongeza, alisimama Mheshimiwa sana Mama yangu Waziri wa Kazi na Ajira na kulieleza Bunge lako kwamba Walimu wanakatwa ile 2% hata wale ambao siyo wanachama kwa sababu ya Sheria ya *The Employment and Labour Relations Act* ya 2004. Naomba niweke record kwamba ni kwa mujibu wa Sheria ya *The Trade Union Act* ya mwaka 1998, kifungu kile cha 55 pamoja na kifungu cha 56(1),(2),(3). Vifungu vyote hivi ukiangalia vinakiuka Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo ndiyo sheria mama, kifungu kidogo cha kwanza na kifungu kidogo cha nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda, naomba nisinukuu, niishauri Serikali iende ikarejee Sheria hii na vifungu hivi ambavyo vinakiuka huu utaratibu na mara moja waweze kuhakikisha kwamba wanawasaidia Walimu wa Manispaa ya Kigoma UJiji ambao wameomba kujitoa kwenye Chama cha Walimu na wameweza kushinda kesi yao ili kusudi suala hili liweze kuharakishwa kwa sababu kuwakata fedha ni kinyume cha Katiba yetu kama ambavyo nimeeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Mwongozo wako kuhusiana na taarifa ambayo ilitolewa na Mheshimiwa Waziri ambayo inakiuka matakwa ya Katiba yetu kama ambavyo nimefafanua nini kifanyike.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Machali, kwa kweli ulichofanya ni kutimiza wajibu wako wa Kikatiba wa kuishauri Serikali na umefanya hivyo, umetoa ushauri mzuri tu kwa Serikali. Kwa hiyo, Serikali imepokea ushauri huo itautazama na kwa sababu hizi Wizara zinakuja huko mbele, tutafikia mahali pa kulijadili jambo hilo vizuri, Mheshimiwa Mpina!

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Maswali na Majibu tarehe 16 April, 2013 hapa Bungeni wakati nikiuliza swali la nyongeza katika swali

24 APRILI, 2013

namba 47 la Mheshimiwa Thuwayba Idrisa Muhammed kuhusu Deni la Taifa, nilieleza kuwa moja ya sababu ambayo inasababisha Deni la Taifa kuongezeka ni pamoja na Serikali kuwa na matumizi makubwa kuliko uwezo wa mapato yetu ya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha wakati akijibu swali langu alisema, kwa namna yoyote ile hatukopi fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida, tunakopa fedha kwa ajili ya kulipia miradi ya maendeleo na akanitaka mimi nihakikishe takwimu zangu kama zipo sawasawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kukuhakikishia kwamba takwimu zangu zipo sawasawa na leo nimekuja na kitabu cha hotuba ya Waziri wa Fedha cha mwaka 2012/2013 ambapo mapato yetu ya ndani yalikuwa shilingi trilioni 9.1 wakati matumizi yetu ya kawaida yalikuwa shilingi trilioni 10.6 na hapo kulikuwa na *gap* la shilingi trilioni 1.5. Misaada kama misaada tuliyopata ilikuwa ni shilingi bilioni 878.4 tu. Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba *gap* lilitlobaki lilitfidiwa na fedha za mikopo na kwamba hata hiyo shilingi trilioni 9.1, shilingi trilioni 2.2 nazo tulizipeleka kwenye maendeleo kwa hiyo ukitoa pale unaweza ukaona *gap* la matumizi ya kawaida kulipiwa na mapato ya ndani inaongezeka kuwa kubwa zaidi. Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba matumizi yetu ya kawaida ni makubwa kuliko hata uwezo wa mapato yetu ya ndani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi naomba Mwongozo wako kama majibu ya Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Saada M. Salum aliyoyatoa siku hiyo yanakidhi masharti yaliyowekwa na Kanuni ya 46(1). Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru Mheshimiwa Mpina, nipokee Mwongozo huo, nitatoa maelezo yangu baadaye, naomba tuendelee.

24 APRIL, 2013

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2013/2014 - Wizara ya Maji

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji iliowasilishwa hapa Bungeni kuhusu Wizara ya Maji, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Profesa Peter Mahamudu Msolla, Mbunge wa Kilolo, kwa kupokea na kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2012/2013 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu kwa mwaka 2013/2014, kisha kutoa maoni na ushauri muhimu uliozingatiwa wakati wa utayarishaji wa Bajeti ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii, kuwapongeza Wenyejiti na Makamu Wenyejiti wapya wa Kamati mbalimbali za Kudumu za Bunge walioeteuliwa hivi karibuni. Ni matumaini yangu kuwa tutaendelea kushirikiana nao katika kutekeleza majukumu yetu kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu, kwa hotuba yake ambayo imetoa mwelekeo wa utekelezaji wa bajeti na kazi za Serikali kwa mwaka 2013/2014. Nawapongeza pia, Mawaziri wenzangu wote walionitangulia kuwasilisha hoja za Wizara zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu ilipokea kwa mshtuko mkubwa taarifa ya kifo cha ghafla cha Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mbunge wa Chambani kilichotokea

wakati wa vikao vya Kamati za Kudumu za Bunge. Nachukua nafasi hii kutoa pole kwako wewe Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako Tukufu, familia ya marehemu, ndugu na wananchi wa Jimbo la Chambani kwa msiba huo mkubwa. Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi. Amin.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya sekta ya maji nchini. Wizara yangu katika kutekeleza majukumu yake, inazingatia maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Tanzania Awamu ya Pili (MKUKUTA II), Malengo ya Milenia, Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na ahadi za Serikali. Katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu itaendelea kutekeleza majukumu yake kulingana na Sera ya Maji ya mwaka 2002; Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Maji; Sheria za Maji na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (*WSDP*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu inasimamia Sekta ya Maji ambayo imegawanywa katika sekta ndogo kuu tatu, ambazo ni Rasilimali za Maji, Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini na Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Miji ni. Hadi sasa hali halisi ya Sekta ya Maji ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, rasilimali za maji. Nchi yetu inakadiriwa kuwa na rasilimali za maji juu ya ardhi zinazofaa kutumika kwa matumizi mbalimbali (*annual renewable surface water resources*) ya kiasi cha wastani wa kilomita za ujazo 89 kwa mwaka. Aidha, inakadiriwa kuwa hifadhi ya rasilimali za maji chini ya ardhi ni kilomita za ujazo 40. Hata hivyo, kutohana na tofauti ya hali ya hewa na jiolojia; mtawanyiko na upatikanaji wa rasilimali hizo nchini hauko sawa katika maeneo yote. Kiasi cha maji kilichopo kwa sasa kwa kila mtu ni wastani wa lita milioni 2.02 kwa mwaka lakini kutohana na ongezeko la watu, ifikapo mwaka 2025 kiwango hicho kinatarajiwa kupungua hadi lita milioni 1.5. Hivyo, inatulazimu kuchukua hatua madhubuti za kuhifadhi maji katika maeneo mbalimbali ya nchi na kuboresha matumizi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengi ya nchi yetu yameendelea kuwa na uhaba wa maji kwa matumizi yaliyokusudiwa kutokana na maji hayo kutokuwa na ubora unaokubalika, uharibifu wa mazingira na athari za mabadiliko ya tabianchi. Sababu nyine ni pamoja na gharama kubwa za ujenzi wa miundombinu ya kuhifadhi rasilimali za maji, matumizi ya maji yasiyozingatia ufanisi, uchafuzi wa vyanzo vya maji unaosababishwa na shughuli za kibinadamu na kasi kubwa ya ongezeko la watu. Hivyo, ni muhimu tuchukue hatua za kuhifadhi vyanzo vyetu vya maji ili kunusuru rasilimali hiyo. Jukumu hili ni letu sote kuanzia ngazi za jamii, Wilaya, Mkoa na Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Februari mwaka 2013, hali ya upatikanaji wa maji haikuwa nzuri kutokana na uhaba wa mvua za vuli katika maeneo mengi nchini. Kwa ujumla, hali hiyo ilisababisha kiasi cha maji katika mabwawa, mito na Maziwa kupungua ikilinganishwa na mwaka uliopita. Katika Bonde la Ruvuma na Pwani ya Kusini, kiasi cha mvua katika kipindi hicho kilikuwa ni milimita 550 kwa upande wa magharibi wa bonde (Songea) na kwa upande wa mashariki wa bonde (Mtwara) ni milimita 800; ikilinganishwa na kiasi cha mvua cha kawaida cha milimita 1,000. Aidha, hali ya maji katika Bonde la Mto Pangani kwa ujumla haikuwa nzuri kutokana na mvua kunyesha chini ya wastani. Hadi kufikia tarehe 10 April, 2013 kina cha maji katika bwawa la Nyumba ya Mungu kilikuwa mita 682.53 juu ya usawa wa bahari.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya upatikanaji wa maji katika Bonde la Mto Rufiji kwa mwaka 2012/2013 haikuwa ya kuridhisha. Hadi kufikia tarehe 14 Machi, 2013 kina cha maji katika Bwawa la Mtera kilikuwa mita 688.66 juu ya usawa wa bahari. Aidha, hali ya maji katika mabwawa yaliyopo katika Bonde la Ziwa Tanganyika hadi Februari 2013 haikuwa ya kuridhisha ambapo kumekuwa na kushuka kwa kina cha maji katika mabwawa ya Kazima na Igombe yanayohudumia Manispaa ya Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya upatikanaji maji katika mito ya Bonde la Wami/Ruvu imeendelea kupungua

24 APRILI, 2013

kutokana na mvua kunyesha chini ya wastani. Hadi kufikia mwezi Februari 2013, wingi wa maji katika mito mingi ulipungua ikilinganishwa na mwaka 2012. Hali hiyo ilisababisha kina cha maji katika Bwawa la Mindu kupungua na kuathiri upatikanaji wa maji katika Manispaa ya Morogoro. Bonde pekee ambalo kwa ujumla wingi wa maji ulationgezeka ni Bonde la Ziwa Victoria. Hata hivyo, katika baadhi ya maeneo kwenye Bonde hilo kulikuwa na upungufu. Hadi kufikia mwezi Februari 2013, kiasi cha maji kwenye Mto Kagera kiliendelea kupungua lakini hali ilikuwa tofauti kwa Mto Mara na Mto Simiyu ambapo kulikuwa na ongezeko la maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mvua za masika zilizoanza kunyesha mwezi Machi, 2013 katika maeneo mengi nchini zinaelekea kuleta ahueni ya hali ya upatikanaji wa maji iwapo zitaendelea hadi mwishoni mwa mwezi Mei kama illivyo kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, huduma za maji Vijijini. Sera ya Maji ya mwaka 2002 inalenga katika kuhakikisha kuwa, wananchi Vijijini wanapata huduma ya maji safi na salama umbali usiozidi mita 400 kutoka kwenye makazi yao. Katika kufikia lengo hilo la Sera, Serikali kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo, Serikali za Mitaa, Wananchi na wadau wengine inaendelea kuboresha huduma za maji Vijijini kwa kujenga miradi mipyua, kupanua na kukarabati miundombinu ya maji. Miradi ya maji Vijijini huteklezwa na Halmashauri kwa kuwashirikisha wananchi wa Vijiji husika na sekta binafsi. Sekretariati za Mikoa husimamia na kutoa ushauri wa kiufundi. Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI huratibu utekelezaji ambapo Wizara ya Maji hutafuta fedha na kuandaa miongozo ya utekelzaji na kutoa ushauri wa kitaalam.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za utekelezaji wa miradi ya maji Vijijini kutoka Serikali Kuu hutumwa kwenye Halmashauri kwa kutumia fomula inayozingatia kigezo cha kiwango cha upatikanaji wa huduma ya maji, wingi wa watu na aina ya teknolojia inayotumika katika Halmashauri hizo. Halmashauri zenye kiwango kidogo cha huduma ya maji

Vijijiini hupatiwa fedha nyingi zaidi kuliko zile zenye kiwango kikubwa. Lengo ni kuondoa tofauti ya viwango vya upatikanaji wa huduma ya maji Vijijiini mionganii mwa Halmashauri (*equity*).

Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada zinazofanyika katika uboreshaji wa miradi ya maji kuititia vyanzo hivyo vya fedha zimeongeza huduma ya maji kwa wananchi waishio Vijijiini kutoka watu milioni 16.3 mwezi Desemba 2005 hadi kufikia watu milioni 20.6 mwezi Desemba 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, huduma ya maji Miji ni inasimamiwa na kutekelezwa na Mamlaka za majisafi na usafi mazingira katika Miji Mikuu ya Mikoa, Mamlaka katika ngazi za Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Kitaifa ya Maji. Katika kuimarisha usimamizi, Mamlaka hizo zimegawanywa katika Madaraja ya A, B na C kulingana na uwezo wa kila Mamlaka kujitegemea. Mamlaka za Miji Mikuu ya Mikoa zimegawanyika kama ifuatavyo; Mamlaka 13 za Arusha, Dodoma, Iringa, Mbeya, Morogoro, Moshi, Mtwara, Mwanza, Shinyanga, Tabora, Tanga, Songea na Musoma zipo daraja 'A'. Katika daraja hilo, Mamlaka zina uwezo wa kulipia gharama zote za uendeshaji na matengenezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka za daraja 'B' zipo nne, ambazo ni Bukoba, Kigoma, Singida na Sumbawanga. Mamlaka hizo zinapata ruzuku ya kulipia asilimia 50 ya gharama za umeme wa kuendesha mitambo. Mamlaka zilizo kwenye daraja 'C' ni Babati na Lindi ambazo bado zinapata ruzuku ya mishahara ya wafanyakazi wake pamoja na kulipia gharama za umeme wa kuendesha mitambo. Serikali imekamilisha kuunda Bodi za Mamlaka za Miji Mikuu ya Mikoa mipya. Miji hiyo ni Mpanda, Njombe, Geita na Bariadi ambayo kwa kuanzia itakuwa daraja C.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Mamlaka zote za ngazi ya Wilaya, Miji Midogo na miradi saba ya kitaifa nazo zipo katika daraja C. Wizara imeendelea kuzijengea uwezo Mamlaka hizo ili ziweze kuijendesha kibiashara na kuwashumia wateja wake kwa ufanisi. Katika kuboresha

huduma za majisafi na usafi wa mazingira Miji ni, Serikali imeendelea na ujenzi, ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya majisafi katika Miji Mikuu ya Mikoa, Miji Mikuu Ya Wilaya, Miji Midogo na miradi ya kitaifa ya maji. Kwa wastani, hali ya huduma ya maji katika Miji Mikuu ya Mikoa, Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na maeneo yanayohudumiwa na miradi ya kitaifa ya maji imeendelea kuimarika mwaka 2012/2013 kulinganisha na miaka ya nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma ya Majisafi katika Miji Mikuu ya Mikoa hali ya utoaji wa huduma ya majisafi kwa wakazi wa Miji Mikuu ya Mikoa kwa Mamlaka za daraja A isipokuwa Jiji la Dar es Salaam ni asilimia 89 hadi Desemba 2012 na kwa Mamlaka za daraja B na C wastani wa maeneo yanayopata maji ni asilimia 83. Iliyokuwa Miji Mikuu ya Wilaya za Njombe, Mpanda, Geita na Bariadi kwa sasa ni Miji Mikuu ya Mikoa. Hivyo, hali ya upatikanaji maji katika Miji hiyo ni wastani wa asilimia 53.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa majisafi kwa Mamlaka zote 19 za Miji Mikuu ya Mikoa uliongezeka kutoka wastani wa lita milioni 330.99 kwa siku kwa mwezi Machi 2012 hadi kufikia wastani wa lita milioni 341.77 kwa siku mwezi Machi 2013. Ongezeko hili limetokana na ukarabati wa miundombinu ya maji iliyokamilika na inayoendelea katika Miji Mikuu ya Mikoa mbalimbali nchini, hususan Miji ya Mbeya na Iringa. Ufungaji wa dira za maji kwenye Miji Mikuu ya Mikoa 19 umeongezeka kutoka dira 264,090 mwezi Machi 2012 hadi kufikia dira 280,832 mwezi Machi 2013. Ongezeko hilo limefanya idadi ya wateja waliofungiwa dira katika Miji hiyo kufika wastani wa asilimia 93. Aidha, upotevu wa maji umepungua na kufikia wastani wa asilimia 36. Lengo ni kupunguza upotevu huo hadi kufikia wastani wa asilimia 20 (kiwango kinachokubalika kimataifa) ifikapo mwaka 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, makusanyo ya maduhuli yatokanayo na mauzo ya maji katika Mamlaka za Miji Mikuu ya Mikoa 19 kwa mwezi yameongezeka kutoka shilingi bilioni 4.45 mwezi Machi, 2012 hadi kufikia shilingi bilioni 5.53 mwezi

Machi, 2013, sawa na ongezeko la asilimia 24. Kuongezeka kwa maduhuli kunaziwezesha Mamlaka za Maji kuboresha huduma zinazotolewa ikiwa ni pamoja na kuwekeza katika miundombinu mipyä kwenye maeneo ambayo hayajafikiwa na mitandao ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za majisafi katika Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na miradi ya Kitaifa. Hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa wakazi wa Miji Mikuu ya Wilaya na Miji Midogo ilikuwa asilimia 53 katika mwaka 2011/2012. Katika Miji hiyo kuna wateja 97,718 na asilimia 57 ya wateja hao wamefungiwa dira za maji. Kwa miradi ya kitaifa wateja ni 11,405 na kati yao asilimia 54 wamefungiwa dira za maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za majisafi katika Jiji la Dar es Salaam. Kwa upande wa Jiji la Dar es Salaam na Miji ya Kibaha na Bagamoyo, huduma ya maji hutolewa na Shirika la Usambazaji Maji Jijini Dar es Salaam (*DAWASCO*). Huduma ya maji katika Jiji hilo, inatolewa kwa mgawo kutokana na uwezo wa mitambo iliyopo na ongezeko kubwa la wakazi katika Jiji. Idadi ya wakazi wanaopata huduma ya maji katika Jiji la Dar es Salaam, Kibaha na Bagamoyo ni asilimia 68. Kati ya hao, asilimia 55 wanapata huduma ya maji kutoka kwenye mtandao wa mabomba na wanaobaki wanapata huduma ya maji kutoka kwenye visima, magati na huduma ya magari (*water bowsers*).

Mheshimiwa Naibu Spika, uwezo uliopo wa mitambo ya kuzalisha maji kwa Jiji la Dar es Salaam ni lita milioni 300 kwa siku. Hadi kufikia mwezi Desemba, 2012, uzalishaji wa maji ulikuwa ni wastani wa lita milioni 260 kwa siku. Upungufu huu unatokana na tatizo la kukatika mara kwa mara kwa umeme kwenye mitambo ya kuzalisha maji pamoja na matengenezo ya mitambo na mabomba yanayovuja kutokana na uchakavu. Mahitaji ya maji kwa Jiji la Dar es Salaam hivi sasa ni lita milioni 450 kwa siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, upotevu wa maji bado umekuwa ni changamoto kubwa kutokana na uvujaji,

uchakavu wa miundombinu, wizi wa maji na uharibifu wakati wa ukarabati wa barabara na kusababisha kuharibu miundombinu ya maji. Hadi mwezi Desemba 2012, upotevu wa maji ulikuwa ni asilimia 53.75. Lengo ni kufikia asilimia 30 ifikapo mwezi Juni 2014. Kati ya mwezi Machi na Aprili 2013, jumla ya watu 94 wamekamatwa kwa kujihusisha na wizi wa maji; na kesi 82 za matukio ya wizi wa maji zimefunguliwa Mahakamani. *DAWASCO* imeanza kusajili magari yanayosambaza maji kwa lengo la kutekeleza kanuni za udhibiti wa biashara ya maji yanayosambazwa na magari na visima. Hatua hiyo itasaidia kudhibiti wizi wa maji, usalama wa maji na bei za maji yanayosambazwa kwa magari hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma ya uondoaji wa Majitaka Mijini. Idadi ya wakazi wa Miji ni wanaopata huduma ya mfumo wa uondoaji majitaka ni ndogo ukillinganisha na mahitaji, hivyo mifumo hiyo inahitaji kupanuliwa. Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira ambazo zina mifumo ya majitaka ni za Miji ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Mbeya, Morogoro, Moshi, Mwanza, Tabora, Tanga na Songea. Serikali ina mpango wa kuweka miundombinu ya uondoaji wa majitaka kwa Miji ya Musoma na Bukoba. Katika Miji mingine ambayo haina mitandao ya majitaka, mfumo unaotumika kuhifadhi majitaka ni makaro yaliyoko majumbani na magari yanayobeba majitaka na kuyamwaga katika maeneo maalum yaliyotengwa kwa ajili ya kuhifadhi na kutibu majitaka. Kukosekana kwa mitandao ya mabomba ya majitaka katika Miji hiyo kumetokana na kutokuwa na uwekezaji mpya katika kipindi hicho. Uwekezaji wa miundombinu ya majitaka utaanza katika awamu ya pili ya Programu ya Maendeleo ya Maji inayotarajiwa kuanza mwaka 2014/2015. Hadi kufikia mwezi Desemba 2012, jumla ya wateja wa majitaka Miji ni wamefikia 21,680 kutoka wateja 20,773 mwezi Machi 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya 2012/2013 na mpango wa bajeti kwa mwaka 2013/2014. Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka 2012/2013 na malengo ya mwaka 2013/2014 kwa Sekta ya Maji

katika maeneo ya rasilimali za maji, huduma ya maji na usafi wa mazingira Vijijini, huduma ya maji na usafi wa mazingira Miji ni na masuala mtambuka umeainishwa kama ifuatavyo:-

Mheshimwa Naibu Spika, kwanza, rasilimali za maji. Majukumu ya Wizara yangu katika kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji ni pamoja na kuchunguza na kutathmini rasilimali za maji nchini; kuimarisha usimamizi wa rasilimali za maji; kuimarisha Bodi za Maji za Mabonde ili zisimamie kikamilifu rasilimali hizo. Kazi nyingine ni kuandaa mipango shirikishi ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji na kuwezesha ujenzi wa miundombinu ya kipaumbele, yakiwemo mabwawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji. Katika kusimamia mwenendo wa rasilimali za maji nchini, Wizara yangu imeendelea kuimarisha vituo vya kufuattilia wingi na ubora wa rasilimali za maji juu na chini ya ardhi ili kuboresha upatikanaji wa takwimu na taarifa sahihi na kwa wakati. Takwimu na taarifa hizi husaidia kutambua hali ya maji kwa nyakati tofauti kwenye maeneo mbalimbali hapa nchini, hivyo kuwezesha kufanyika kwa maamuzi sahihi ya ugawaji wa Rasilimali za Maji kwa matumizi mbalimbali. Takwimu na taarifa hizo, pia hutumika wakati wa usanifu na ujenzi wa miundombinu ya skimu za maji, mabwawa na madaraja. Hadi kufikia Februari 2013, jumla ya vituo 120 vya kupima mtiririko wa maji mitoni (*hydrometric stations*) na vituo 45 vya hali ya hewa (*meteorological/weather stations*) vilijengwa, ikiwa ni pamoja na kufunga vifaa vya kupima mvua katika vituo 17 kote nchini. Ukarabati ulifanyika kwa vituo 43 vya kupima mtiririko wa maji mitoni. Katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu itaendelea na ujenzi na ukarabati wa vituo 338 pamoja na kukusanya takwimu kwenye mabonde yote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, uhifadhi wa mazingira na vyanzo vya maji. Wizara yangu imeendelea kutekeleza mikakati ya kuhifadhi vyanzo muhimu vya maji kwa kuvivekea mipaka na kuvitangaza kuwa maeneo tengefu. Katika mwaka wa fedha 2012/2013, jumla ya vyanzo 60

vilibainishwa kwa ajili ya kuanza utaratibu wa kuvitenga ili kuvikinga dhidi ya uchafuzi wa mazingira kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji ya mwaka 2009 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004. Aidha, chanzo cha maji cha Makutupora (*Well-field*) ambacho ni chanzo kikuu cha maji kwa mji wa Dodoma na bwawa la Kawa lilitoko Rukwa vilitangazwa kuwa maeneo tengefu. Katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Hifadhi ya Mazingira (*NEMC*) itaendelea kuhakikisha kwamba vyanzo vya maji vinatunzwa na kulindwa. Vilevile, Wizara itaendelea kubaini maeneo yanayofaa kutengwa ili kuyakinga dhidi ya uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ya athari za Mazingira ya Miradi saba ya Maji katika Miji ya Musoma, Mwanza, Bukoba, Morogoro, Iringa, Mbeya na Massasi (*Mchema Dam Water Supply*) imekamilika na kuwasilishwa *NEMC* ili ihakikiwe. Aidha, miradi mingine ya maji katika Miji ya Babati, Lindi, Mtwara, Sumbawanga, Kigoma na Tabora imefanyiwa tathmini ya awali (*Screening*) na mapungufu kadhaa yamegundulika. Mamlaka husika zimeagizwa kurekebisha kasoro zilizobainika kabla ya kupeleka *NEMC* kwa hatua zinazofuata. Mkataba kwa ajili ya kufanya Tathmini ya Athari za Mazingira ya mabwawa matano ya Itobo, Uchama, NkiniZiwa, Leken na Enguikument umesainiwa na tathmini zipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Miradi mingine mitano ya (Same -Mwanga -Korogwe; Nzega - Igunga -Tabora; Hai, Masasi – Nachingwea na Chalinze) ipo katika hatua mbalimbali za uandaaji wa hadidu za rejea ili iweze kufanyiwa Tathmini ya athari za Mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji. Katika kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji, Wizara yangu katika mwaka wa fedha 2012/2013 ilikagua viwanda, migodi, vituo vya mafuta na hoteli na kutoa maelekezo. Jumla ya viwanda 41 vilikaguliwa katika Mabonde ya Ziwa Victoria (18) Bonde la Pangani (19), Bonde la Rufiji (3) na Bonde la Ziwa Rukwa (1). Jumla ya vibali vinne vya kutiririsha majitaka yanayokidhi viwango kwenye vyanzo

vya maji vilitolewa na Bodi za Maji za Mabonde ya Ziwa Rukwa (1) na Rufiji (3) ambapo uongozi wa viwanda hivi uliagizwa kufuata maelekezo yaliyopo kwenye mipango yao ya usimamizi wa mazingira (*Environmental Management Plan*). Majitaka kutoka kwenye viwanda 37 vilivyopo kwenye Mabonde ya Ziwa Victoria (18) na Pangani (19) hayakuwa yanakidhi viwango vya ubora vinavyohitajika ili yaweze kutiririshwa kwenye mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, uongozi wa viwanda hivi uliagizwa kufanya Tathmini ya Athari ya Mazingira kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004, kuwa na mifumo madhubuti ya kusafisha majitaka, kufanya ufuutiliaji wa ndani wa ubora wa majitaka yanayotoka katika viwanda vyao na kuhakikisha kwamba majitaka yatokanayo na shughuli za viwanda yanakidhi viwango kabla ya kumwagwa kwenye mazingira. Jumla ya migodi 5 ilikaguliwa katika Mabonde ya Ziwa Victoria (4) na Ziwa Rukwa (1).

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya ukaguzi na ubora wa majitaka katika migodi ya Geita, Bulyanhulu na Buzwagi yalikidhi viwango ambapo uongozi wa migodi hii uliagizwa kufuata maelekezo yaliyopo kwenye mipango yao ya usimamizi wa mazingira (*Environmental Management Plan*). Matokeo ya ukaguzi na ubora wa majitaka katika migodi ya North Mara na Shanta Gold Mining Company hayakukidhi viwango. Wizara iliuagiza uongozi wa migodi hii kufanya ufuutiliaji wa ndani wa ubora wa majitaka na kuhakikisha kwamba majitaka yatokanayo na shughuli za migodi yanakidhi viwango kabla ya kumwagwa kwenye mazingira. Wizara pia iliuagiza uongozi wa mgodi wa North Mara kudhibiti uvujaji wa maji kutoka kwenye bwawa la kuhifadhia tope (*Tailings Storage Facility - TSF*). Wizara inaendelea kufuatilia ubora wa majitaka kutoka kwenye mgodi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, utafutaji wa vyanzo vipyta vya maji. Maji chini ya ardhi ni moja ya vyanzo vya maji vinavyotumika hapa nchini hasa katika maeneo kame. Katika mwaka 2012/2013, utafiti wa kubaini maeneo

yanayofaa kuchimba visima vya maji uliendelea katika maeneo 189 katika Mabonde ya Ziwa Tanganyika (15), Rufiji (4), Pangani (46), Ziwa Victoria (7), Ziwa Rukwa (10), Ruvuma (49), Ziwa Nyasa (3), Wami-Ruvu (17) na Bonde la Kati (38). Katika mwaka 2013/2014, Wizara itachunguza maeneo yanayofaa kuchimba visima virefu vya maji na kusimamia uchimbaji katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba yangu ya mwaka jana, nililiarifu Bunge lako Tukufu juu ya maandalizi ya mradi wa uchimbaji wa visima katika maeneo kame kwa kushirikiana na Serikali ya Misri. Mnamo tarehe 17 Januari 2013, Wizara yangu ilifanya uzinduzi wa visima 30 vilivyo chimbwa kwa ufadhili wa Serikali ya Misri katika Wilaya za Maswa, Same, Bunda, Magu, Tarime na Kiteto. Katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu itaendelea na uchimbaji wa visima vingine 70 vya awamu ya pili ya mradi huo ambavyo vitachimbwa katika maeneo kame ya Wilaya za Maswa, Bariadi, Magu, Tarime, Same, Rorya, Bunda na Kiteto. Utekelezaji wa mradi huo utaenda sambamba na utoaji wa mafunzo kwa wataalam wa Sekta ya Maji katika fani mbalimbali. Wizara yangu pia, itachimba visima 55 kwa kushirikiana na Serikali ya Watu wa China. Visima hivyo vitachimbwa katika Wilaya za Kilosa na Kisarawe katika bonde la Wami/Ruvu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu ina jukumu la kuratibu uchimbaji wa visima vya maji nchini. Uratibu huo unalenga kuhakikisha kwamba taratibu za kitaalam zinafuatwa ili kuhakikisha visima vina ubora kwa matumizi endelevu. Kwa mwaka 2012/2013, Wizara ilihakiki na kusajili kampuni tano za kuchimba visima na kuwa na idadi ya kampuni binafsi 131 hadi kufikia mwezi Machi 2013. Jumla ya visima 420 vilichimbwa na kat i ya hivyo, 162 vilichimbwa na Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa na 258 vilichimbwa na kampuni binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, taratibu za ujenzi wa Bwawa la Farkwa kwenye Mto Bubu, Wilaya ya Kondoa katika Bonde la Kati unaendelea. Bwawa hilo litakuwa ni

chanzo cha maji kwa Manispaa ya Dodoma na Miji ya Wilaya za Kondoa, Chamwino na Bahi. Katika mwaka 2012/2013, Mtaalam mshauri anayefanya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina, kuandaa vitabu vya zabuni ameajiriwa na ameanza kazi na taarifa ya awali imewasilishwa. Mkataba wa kutathmini athari za mazingira umesainiwa Septemba 2012 na taarifa ya awali imewasilishwa. Kazi hiyo inatarajiwa kukamilika katika mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea na maandalizi ya ujenzi wa Bwawa la Ndembera katika Bonde la Rufiji litakalotumika kudhibiti mwenendo na mtiririko wa maji katika kipindi cha mwaka mzima kwenye mto Ruaha Mkuu. Matumizi mengine ya bwawa hilo ni pamoja na kilimo cha umwagiliaji na kuzalisha umeme. Katika mwaka 2012/2013, Mtaalam mshauri kwa ajili ya upembuzi yakinifu, usanifu na kuandaa vitabu vya zabuni ameajiriwa na ameanza kazi. Katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu itakamilisha usanifu na maandalizi ya vitabu vya zabuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, matumizi bora ya rasilimali za maji. katika mwaka 2012/2013, Wizara yangu imeendelea kusimamia matumizi endelevu ya rasilimali za maji nchini; kwa kuhakikisha kuwa rasilimali hizo zinagawanywa kwa uwiano kulingana na mahitaji ya sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii na kufanya ukaguzi wa matumizi bora ya maji. Jumla ya vibali vya kutumia maji 196 katika mabonde ya Ziwa Victoria (15), Rufiji (87) na Ruvuma na Pwani ya Kusini (94) vilitolewa; na vibali sita vya kutupa majitaka vilitolewa katika bonde la Ziwa Victoria. Vilevile, matoleo 562 ya maji kwenye miradi ya umwagiliaji, yalikaguliwa na kusajiliwa katika mabonde ya Ziwa Victoria (5), Ziwa Rukwa (30) Rufiji (31), Ruvuma na Pwani ya Kusini (496).

Mheshimiwa Naibu Spika, ukaguzi huo ulibaini sababu za ubovu wa mabanio unaosababisha upotevu wa maji kutoka katika vyanzo, uchepushaji wa maji usiozingatia sheria na uchafu wa matoleo na mifereji ya maji. Wahusika walielekezwa kukarabati mabanio na kusafisha mifereji na

kuzingatia masharti ya vibali vyta kutumia maji. Katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu kuitia Bodi za Maji za Mabonde itaendelea kutoa elimu kwa wadau juu ya umuhimu wa kuwa na vibali vyta kutumia maji na kusimamia matumizi endelevu ya rasilimali za maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sita, mipango shirikishi ya usimamizi na uendelezaji wa Rasilimali za Maji. Katika mwaka 2012/2013, Wizara yangu iliendelea na utayarishaji wa Mipango Shirikishi ya Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji katika mabonde yote tisa. Kazi zilizofanyika ni pamoja na kutathmini wingi na ubora wa rasilimali za maji, kuainisha mahitaji ya maji ya sekta mbalimbali katika muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu. Wataalam washauri kwa Mabonde ya Rufiji, Wami/Ruvu na Bonde la Kati wamewasilisha taarifa za utayarishaji (*interim and draft final reports*) wa mipango hiyo na kwa mabonde ya Ruvuma na Pwani ya Kusini, Pangani, Ziwa Nyasa, Ziwa Rukwa, Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika, taarifa za awali (*Inception Reports*) zimewasilishwa. Katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu itakamilisha utayarishaji wa mipango hiyo katika Mabonde ya Rufiji, Ruvuma na Pwani ya Kusini, Pangani, Wami/Ruvu, Bonde la Kati, Ziwa Nyasa, Ziwa Rukwa na Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, saba, kuimarisha Bodi za Maji za Mabonde. Wizara yangu imeendelea kuzijengea uwezo Bodi za Maji za Mabonde kwa kutoa mafunzo kwa watumishi, ujenzi wa ofisi na ununuvi wa vitendea kazi. Katika mwaka 2012/2013, jumla ya wataalam 210 walipata mafunzo ya muda mfupi katika fani za usimamizi shirikishi wa rasilimali za maji, usimamizi wa takwimu, matumizi ya vifaa vyta utafiti wa maji chini ya ardhi, kujenga na kutumia vituo vyta hali ya hewa na vyta kupimia maji mitoni na kwenye Maziwa, pamoja na mafunzo ya namna ya kutatua migogoro itokanayo na matumizi ya rasilimali za maji. Vilevile, watumishi wapatao 22 wanaendelea na masomo ya fani mbalimbali katika ngazi ya Stashahada, Shahada na Shahada za Uzamili. Mafunzo hayo yatawezesha watumishi kuongeza ufanisi na tija katika usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafunzo kwa watumishi yaliyoainishwa hapo juu, Wizara imeendelea kuimarisha Bodi za Maji za Mabonde kwa kuzijengea majengo ya ofisi na maabara na kuzipatia vitendea kazi. Kwa mwaka 2012/2013 ujenzi wa jengo la ofisi ya Bonde la Ziwa Nyasa katika mji wa Tukuyu umeendelea, kwa sasa umefikia hatua za mwisho na jengo litakamilika mwaka huu wa fedha. Aidha, taratibu za kuwapata wakandarasi wa kukarabati na kujenga Ofisi za Bodi za Maji za mabonde ya Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Bonde la Kati zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nane, makusanyo ya maduhuli. Moja ya majukumu ya Bodi za Maji za Mabonde ni kuandaa na kutekeleza mikakati ya ukusanyaji wa maduhuli yatokanayo na ada za matumizi ya maji ili kufanikisha usimamizi, utunzaji na uendelezaji wa rasilimali za maji. Katika mwaka 2012/2013, jumla ya shilingi 658,692,000 zilizkusanya hadi kufikia mwezi Machi 2013. Makusanyo hayo ni sawa na asilimia 51 ya lengo la shilingi 1,300,000,000 zilizopangwa kukusanya ifikapo tarehe 30 Juni, 2013. Katika mwaka 2013/2014, Bodi za Maji za Mabonde zinakadiria kukusanya kiasi cha shilingi 1,768,887,000 kutokana na vyanzo mbalimbali vya mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, tisa, kudhibiti migogoro mionganoni mwa watumiaji wa maji. Bodi za Maji za Mabonde zimeendelea kusuluhisha migogoro katika matumizi ya maji kwa kushirikiana na Jumuia za Watumiaji Maji na pale inapobidi, vyombo vya kisheria vimekuwa vikitumika kutatua migogoro inayojitokeza. Katika mwaka 2012/2013, jumla ya migogoro 19 ya watumiaji maji ilijitokeza. Kati ya hiyo, migogoro saba ilipatiwa suluhisho katika Mabonde ya Maji ya Pangani (2), Wami/Ruvu (2), Ziwa Rukwa (1) na Rufiji (2). Katika mwaka 2013/2014, Serikali itaendelea kusuluhisha migogoro ya watumiaji maji iliyopo na kutoa elimu ya ugawanaji na utunzaji wa rasilimali za maji ili kudhibiti migogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, usimamizi wa rasilimali za majishiriki. Nchi yetu ina mabonde tisa ya maji. Kati ya hayo,

mabonde saba yanavuka mipaka ya nchi yetu ambapo tunalazimika kushirikiana na nchi nyingine 17 ambazo ni Angola, Botswana, Namibia, Zambia, Zimbabwe, Malawi, Msumbiji, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Misri, Ethiopia, Kenya, Rwanda, Sudan, Sudan Kusini, Uganda na Eritrea. Wizara yangu imeendelea kushirikiana na nchi hizo kwa kuunda vyombo vya pamoja na kuimarisha vilivyopo ili kusimamia matumizi endelevu ya rasilimali hizo. Ushirikiano katika mabonde hayo upo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Bonde la Mto Nile kwa sasa linajumuisha nchi 11 za Burundi, Eritrea, Ethiopia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Kenya, Misri, Rwanda, Sudan, Sudan Kusini, Tanzania na Uganda. Nchi ya Eritrea ni mtazamaji (*observer*) katika jumuiya hiyo. Nchi hizo zinashirikiana kupitia chombo cha mpito cha usimamizi wa rasilimali hiyo kinacho julikana kama Ushirikiano wa Nchi za Bonde la Mto Nile (*Nile Basin Initiative - NBI*). Madhumuni ya ushirikiano huo ni kuhifadhi, kuendeleza na kutumia kwa njia endelevu rasilimali za maji za Bonde hilo. Hadi sasa, nchi za Burundi, Ethiopia, Tanzania, Uganda, Rwanda na Kenya zimesaini Mkataba wa Kudumu wa Ushirikiano wa Nchi za Bonde hilo utakaoanzisha Kamisheni ya Bonde la Mto Nile. Nchi za Misri, Sudan na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo hazijasaini Mkataba huo. Kwa mujibu wa Mkataba, nchi wanachama zinatakiwa kuanza hatua za kuuridhia Mkataba baada ya nchi sita kusaini. Katika mwaka 2013/2014, Tanzania na nchi nyingine zilizosaini Mkataba huo zitaendelea na juhudzi za kuuridhia kwa kuzingatia sheria za nchi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa hifadhi ya mazingira ya Ziwa Victoria. Awamu ya pili ya Mradi wa Usimamizi na Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Victoria (*LVEMP II*) ilianza rasmi mwezi Agosti 2009. Nchi zinazotekeleza mradi huo ni pamoja na Kenya, Tanzania na Uganda. Madhumuni ya mradi ni kuimarisha usimamizi wa pamoja wa rasilimali za Bonde la Ziwa Victoria kwa kudhibiti uharibifu wa mazingira katika Ziwa hilo. Kwa upande wa Tanzania, mradi unalenga kuimarisha taasisi zinazohusika na hifadhi ya maji na samaki; ukarabati wa mifumo ya kusafisha majitaka

24 APRIL, 2013

katika Miji ya Mwanza, Musoma na Bukoba ambayo ipo kando kando ya Ziwa. Walengwa wengine ni Halmashauri za Wilaya ya Maswa, Bariadi, Magu, Meatu na Kwindu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya miradi midogo 126 ya kijamii yenye thamani ya Dola za Marekani 2,819,886 inatekelezwa. Vilevile, miradi tisa mikubwa ya kijamii (*Co – Management Interventions*) yenye thamani ya Dola za Kimarekani 2,067,563.44 imeanzishwa katika Wilaya za Musoma Mjini, Maswa, Bariadi, Kwindu, Magu, Meatu na Jiji la Mwanza. Katika mwaka 2013/2014, Wizara itasimamia utekelezaji wa miradi hiyo pamoja na kufuatilia ukamilishaji wa kazi zinazofanywa na wataalam washauri kuhusu uboreshaji wa Sera, Sheria, Kanuni na viwango vya utupaji majitaka katika Ziwa Victoria, mito na vyanzo vingine vya maji katika bonde la Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu ilishiriki kikamilifu katika kuhakikisha kwamba Sera mpya ya Matumizi ya Maji ya Ziwa Victoria imepitishwa na Mkutano wa 26 wa Baraza la Mawaziri la nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki uliofanyika mwezi Novemba, 2012. Kupitishwa kwa Sera hiyo kutasaidia kuunda chombo huru chenye wajumbe kutoka kila nchi husika ambacho kitafanya kazi ya ufuatilaji na uperembaji wa matumizi ya maji ya Ziwa Victoria. Katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu itaendelea kushirikiana na nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki kutekeleza sera hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, bonde la mto Zambezi. Tarehe 8 Februari 2010, Bunge lako Tukufu liliridhia Mkataba wa kuanzisha Kamisheni ya Bonde la Mto Zambezi (*Zambezi Watercourse Commission-ZAMCOM*). Mkataba huo umeanza kutumika rasmi kisheria tarehe 26 Juni, 2011 baada ya nchi sita, ambazo ni theluthi mbili kuridhia. Sekretarieti ya muda (*Interim ZAMCOM Secretariat*) inayoratibu shughuli za ZAMCOM, ilianza kazi rasmi tarehe 6 Mei, 2011. Sekretarieti hiyo imeongezewa muda wa mwaka mmoja kuanzia tarehe 1 Januari hadi 31 Desemba, 2013 ikiwa na jukumu la kushirikiana na nchi wanachama kukamilisha uundaji wa chombo cha kudumu. Jukumu jingine ni kuandaa mikakati

24 APRILI, 2013

na utekelezaji wa mipango mbalimbali ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji za Bonde la Mto Zambezi iliyokubaliwa katika vikao vya Baraza la Mawaziri wa Maji wa *SADC* vilivyopita. Katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu itaendelea kushirikiana na Sekretarieti ya *ZAMCOM* katika kuratibu kazi za Kamisheni hiyo hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bonde la Mto Ruvuma na Pwani ya Kusini kupitia Mradi wa Majishiriki unaoratibwa na *SADC*, lilitengewa jumla ya Dola za Kimarekani 800,000 mwaka 2012 kwa ajili ya kutekeleza miradi sita ya kijamii. Utekelezaji wa miradi hiyo ulianza mwezi Desemba, 2012 na utakamilika mwezi Juni 2013. Miradi hiyo inatekelezwa katika Wilaya tano za Mikoa ya Mtwara na Ruvuma ambazo ni Songea Vijiji, Tunduru, Tandahimba, Nanyumbu na Mbinga. Fedha za kutekeleza miradi hiyo ni msaada kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika kupitia Sekretarieti ya *SADC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, miradi miwili ya kijamii imeendelea kutekelezwa katika Wilaya ya Tunduru ambapo jumla ya miche ya miti 3,844 imepandwa katika Vijiji vya Daraja Mbili, Nandembo, Lelolelo na Majimaji kwa ajili ya kuzuia mmomonyoko wa ardhi na kutunza vyanzo vya maji. Vilevile, katika skimu ya umwagiliaji ya Namatuhi iliyoko Wilaya ya Songea Vijiji, ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji ikiwa ni pamoja na mfereji wenyewe urefu wa mita 2,000 imekamilika. Aidha, uchimbaji wa kisima kirefu cha mita 150 kwa ajili mradi wa usambazaji wa maji katika kijiji cha Mihamwe, Wilaya ya Tandahimba unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, kisima chenye urefu wa mita 60 kimechimbwa kwa ajili ya mradi wa kusambaza maji katika mji wa Mangaka ambaao ni makao makuu ya Wilaya ya Nanyumbu. Utekelezaji wa mradi wa kusambaza maji katika kijiji cha Mahande, Wilaya ya Mbinga umefikia asilimia 18. Kazi zilizofanyika ni ujenzi wa matanki mawili ya maji yenye lita 10,000 kila moja; matanki mengine mawili yenye lita 25,000 kila moja na vituo 18 vya kuchotea maji. Katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu itaendelea

24 APRIL, 2013

kushirikiana na SADC pamoja na Serikali ya Msumbiji kukamilisha miradi ya pamoja katika Bonde hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, bonde la Mto Songwe. Serikali za Tanzania na Malawi zinatekeleza kwa pamoja Programu ya Kuendeleza Rasilimali za Bonde la Mto Songwe. Utekelezaji wa Programu hiyo upo katika awamu tatu. Awamu ya kwanza ilihusu upembuzi yakinifu na ilikamilika mwaka 2003. Hivi sasa, utekelezaji wa awamu ya pili ya Programu hiyo unaendelea, ambayo ni usanifu wa kina wa miundombinu ya rasilimali za maji itakayojengwa kwa ajili ya kuzalisha umeme, kilimo cha umwagiliaji na kuzuia mafuriko.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara yangu imeendelea na shughuli za kuratibu utekelezaji wa awamu ya pili ya Mradi, pamoja na kutekeleza majukumu ya Tanzania kama yalivyo kwenye Hati za Makubaliano kati ya Tanzania na Malawi. Wizara yangu imemwajiri Mratibu wa Mradi (*National Project Coordinator*) kutoka Tanzania ambaye atasimamia maslahi ya Tanzania kwenye Mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, wataalam wengine wa kada tofauti wamepelekwa kwenye mradi. Mtaalam mshauri ameanza kazi mwezi Machi, 2013. Kazi zitakazofanyika ni pamoja na kuandaa dira ya maendeleo ya programu katika bonde kati ya sasa na mwaka 2050; usanifu wa kina wa miradi ya kipaumbele katika bonde; kufanya tathmini ya athari za mazingira na kijamii kuhusu miradi itakayosanifiwa; kuandaa mpango wa kuanzisha Kamisheni ya pamoja ya kusimamia programu na kujenga uwezo kwa watekelezaji wa programu katika ngazi ya halmashauri hadi Taifa. Katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu itaendelea kushirikiana na nchi ya Malawi kuratibu utekelezaji wa awamu ya pili ya mradi huo. Vilevile, Wizara itaongeza wataalam wengine kutoka Wizara zinazohusika na mradi ili kuweza kushiriki tangu hatua ya awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ziwa Tanganyika. Serikali ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, ilimwajiri mshauri

mwelekezi mwaka 2011 ili afanye tafiti ya athari za kijamii na mazingira (*Environmental and Social Impact Assessment*), tafiti ya kihaidrolojia (*Hydrology Study*) na usanifu wa michoro ya kihadisi (*Engineering Designs*) ili kujenga banio la Mto Lukuga ambalo lilikuwa limebomoka. Mshauri mwelekezi aliwasilisha taarifa za awali za utafiti huo katika kikao cha wataalam kutoka nchi zinazozunguka Ziwa Tanganyika mwezi Novemba 2011, na alitarajiwa kuikamilisha kazi hiyo mwezi Novemba, 2012. Wizara yangu inaendelea kuwasiliana na Serikali ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ili kupata rasimu ya mwisho ya taarifa ya Mshauri mwelekezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu itaendelea kushirikiana na Mamlaka ya Ziwa Tanganyika, nchi za Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Zambia pamoja na Washirika wa Maendeleo ili kuendeleza juhudhi za hifadhi ya Bonde la Maji la Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ziwa Chala, Ziwa Jipe na Mto Umba. Serikali za Tanzania na Kenya zimesaini Hati ya Makubaliano (*MoU*) tarehe 14 Februari, 2013 kuhusu utunzaji na uendelezaji wa ikolojia ya Maziwa ya Chala na Jipe; na Mto Umba. Hati hiyo imeweka misingi ya ushirikiano katika kusimamia na kuendeleza rasilimali zilizopo katika maeneo hayo ili matumizi yake yawe endelevu ikiwa ni pamoja na kulinda mifumo ya ikolojia. Chini ya makubaliano hayo, Bodi ya Maji ya Bonde la Pangani, Halmashauri husika, jumuiya za watumiaji maji, na taasisi zisizo za Kiserikali zilizopo katika bonde hilo zitaimarishwa na taasisi mpya zitaanzishwa kulingana na mahitaji. Nchi hizo kwa kushirikiana na Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria zimeandaa andiko la mradi kuhusu athari za uharibifu wa mazingira ya Bonde la Ziwa Chala na Jipe pamoja na Mto Umba na jinsi ya kuzitatua. Andiko hilo pia linaelezea mfumo wa uongozi wa pamoja wa kusimamia rasilimali hizo. Baadhi ya maeneo yaliyoainishwa katika andiko na ambayo yataanza kutekelezwa katika mwaka 2013/2014 ni pamoja na uondoaji wa magugu maji ambayo yamekithiri hasa katika Ziwa Jipe na ufuatiliaji wa wingi na ubora wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ubora na usafi wa maji. Mojawapo ya majukumu ya Wizara yangu ni kuhakiki ubora na usafi wa maji katika vyanzo vya maji kwa lengo la kulinda afya za wananchi. Katika kutekeleza jukumu hilo, maabara za maji zimeimarishwa kwa kupatiwa vifaa na madawa ya uchunguzi wa ubora wa maji. Vifaa na madawa hayo yameongeza tija ya upatikanaji wa takwimu za ubora wa maji kwa ajili ya kutoa maamuzi sahihi ya kujenga na kuendeleza miradi ya maji. Katika mwaka 2012/2013, Wizara ilipanga kukagua vyanzo vya maji kwa kuchunguza sampuli 8,000 za maji ili kuhakiki ubora wake na sampuli 1,000 za majitaka zilipangwa kuchunguzwa ubora wake ili kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji, kupunguza gharama za kusafisha na kutibu maji kwa matumizi mbalimbali pamoja na kuhifadhi mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwezi Machi, 2013, sampuli 3,957 kati ya sampuli 8,000 zilikusanywa kutoka katika visima, mitandao ya usambazaji maji na udhibiti wa vyanzo vya maji na kuhakikiwa ubora wake. Kati ya hizo, sampuli 1,861 sawa na asilimia 91.5 ya sampuli 2,034 kutoka kwenye visima, zilionesha kuwa maji yake yanakidhi viwango vinavyokubalika kitaifa. Sampuli 173 maji yake hayakukidhi viwango kwa sababu ya kuwa na chumvi, wingi wa madini ya *Nitrate* na *Fluoride*. Ushauri ulitolewa kutafuta vyanzo mbadala kukidhi mahitaji na kutumia teknolojia ya mifupa ya ngombe ili kuondoa madini ya *fluoride* kwenye maji ya kunywa na kupikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji yanayosambazwa Mijini yalihakikiwa ubora wake kwa kukusanya sampuli 1,666 kutoka kwenye mtandao wa kusambaza maji kwenye Miji ya Tanga, Mbeya, Mwanza, Babati, Mbinga, Iringa, Shinyanga, Singida, Musoma, Sumbawanga, Dodoma, Bukoba, Lindi, Mtwara, Nzega na Katesh na kufanyiwa uchunguzi wa kemikali na uwepo wa vimelea vya vijidudu. Kati ya hizo, sampuli 1,626, sawa na asilimia 97.6, maji yake yalikidhi viwango na sampuli 40 maji yake yalionesha uwepo wa vimelea vya vijidudu. Hivyo, Mamlaka za Maji Miji ni zilielekezwa kukagua mitambo ya kusafisha maji mara kwa

mara na kuweka kiwango sahihi cha dawa ya kutibu maji kabla ya kuyasambaza kwa watumiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sampuli 178 za maji yanayotumika kusindika minofu ya samaki viwandani katika Miji ya Mwanza, Bukoba, Dar es Salaam na Musoma zilifanyiwa uchunguzi wa uwepo wa vimelea vya vijidudu. Matokeo yalionesha maji hayo yanakidhi viwango vinavyokubalika kimataifa na samaki wanakuwa na ubora wa kusafirishwa nchiza nje. Aidha, sampuli 79, kutoka kwenye mito na Maziwa katika mabonde ya Ziwa Victoria, Tanganyika, Wami/Ruvu, Rufiji na Ruvuma zilikusanywa na kuchunguzwa ubora wake. Matokeo yalionesha maji hayo kuwa na ubora unaokubalika na takwimu hizo zinatumika wakati wa kutoa vibali vya kutumia maji na kusimamia utunzaji wa vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kudhibiti Uchafuzi wa Mazingira. Sampuli 410 za majitaka kutoka viwandani na mabwawa ya majitaka kwenye Miji ya Dodoma, Morogoro, Mwanza, Dar es Salaam, Tanga, Musoma, Bukoba na Iringa zilikusanywa na kuchunguzwa ubora wake. Kati ya hizo, sampuli 320, sawa na asilimia 81.7, zilikidhi viwango vya majitaka kumwagwa kwenye mazingira na sampuli 70 hazikukidhi viwango; hivyo ushauri ulitolewa kuboresha mabwawa au mitambo ya kusafisha majitaka ili yafikie viwango vinavyokubalika kabla ya kurudishwa kwenye mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu itaimarisha usimamizi wa utekelezaji wa shughuli za ubora wa maji kwa kuratibu ubora kwenye vyanzo vinavyotumika kwa matumizi ya nyumbani, viwanda, kilimo na mazingira; ambapo sampuli 8,000 za maji na sampuli 1,000 za majitaka zitakusanywa na kuchunguzwa. Usimamizi huo ni pamoja na kutekeleza Mkakati wa Kusimamia Ubora wa Maji na Kudhibiti Uchafuzi wa Maji (*Water Quality Management and Pollution Control Strategy*) unaoelekeza kuratibu madini tembo (*heavy metals*) aina ya Zebaki (*Mercury*), Arsenic, Urani (*Uranium*) na Cyanide katika vyanzo

24 APRIL, 2013

vya maji kwenye maeneo yenye shughuli za migodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ubora wa Madawa ya Kusafisha na Kutibu Maji. Maji yanayosambazwa kwa wananchi yanapaswa kusafishwa na kutibiwa ili yawe katika viwango vinavyokubalika, hivyo madawa yanayotumika yanatakiwa kuhakikiwa ubora wake. Katika mwaka 2012/2013, jumla ya sampuli 50 za madawa ya kusafisha na kutibu maji kutoka DAWASCO, Mamlaka za Maji za Iringa, Morogoro, Tanga na kampuni binafsi zilihakikiwa ubora wake. Kati ya sampuli hizo, 14 ni shabu (*Aluminium Sulphate*), 14 *Polyaluminium Chloride* ambazo hutumika kusafisha maji; na 22 *Calcium Hypochlorite* ambayo hutumika kuua vijidudu. Matokeo yalionesha kuwa madawa hayo yalikuwa na viwango vinavyokubalika na ushauri wa kitaalam ultolewa kuhusu matumizi yake sahihi. Katika mwaka 2013/2014, utaratibu wa kuhakiki madawa utaendelea ambapo sampuli 60 za madawa ya kusafisha na kutibu maji zitahakikiwa, ikiwa ni pamoja na kukagua mitambo ya kusafisha na kutibu maji katika Mamlaka za Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, uondoaji wa Madini ya *Fluoride* katika Maji. Serikali imeandaa mkakati wa kusambaza teknolojia ya kutumia mkaa wa mifupa ya ng'ombe (*bone chair*) kuondoa madini ya *fluoride* katika maji ya kunywa na kupikia. Mkakati huo utaanza kutekelezwa mwaka 2013/2014 na kazi zitakazofanyika ni pamoja na kuainisha mbinu za usambazaji wa teknolojia hiyo katika ukanda wa Bonde la Ufa na kutayarisha ramani (*fluoride mapping*) inayoonesha maeneo yenye kiwango kikubwa cha *fluoride* katika maji ambayo itasaidia kuyatambua maeneo hayo wakati wa kuainisha miradi ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maabara za Maji kupata Ithibati (*Accreditation*). Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, mnamo mwezi Julai 2012, Maabara za Iringa, Mwanza na Maabara Kuu zilishiriki katika zoezi la kujipima uwezo chini ya mpango wa *Southern Africa Development Community Measurement Traceability (SADCMET)* ambalo huratibiwa na Shirika la Maji la Namibia (*NAMWATER*).

Matokeo ya zoezi hilo, yalijotolewa mwezi Oktoba, 2012 yalionesha kuwa Maabara hizo zimeongeza uwezo wake kutoka asilimia 68 mwaka 2011/2012 hadi kufikia asilimia 70. Kwa hatua hiyo, maabara hizo zinaweza kujisajili kwa taasisi inayotoa ithibati (*SADCAS*) kwa ajili ya kukamilisha taratibu za kupata ithibati.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba wa kutoa ushauri wa kiufundi kuhusu namna ya kuboresha maabara za maji ili kupata ithibati, ambao utadumu kwa mwaka mmoja, ulisainiwa tarehe 19/09/2012. Hadi sasa, Mtaalam Mshauri amekagua maabara za Mwanza, Musoma, Bukoba, Shinyanga, Morogoro, Dodoma, Singida na Maabara Kuu iliyopo makao makuu ya Wizara kwa kuainisha mahitaji ya mpango mzima wa kupata ithibati. Mtaalam mshauri anaendelea kuandaa mwongozo wa ubora (*Quality Manual*) na makabrasha mengine kulingana na viwango vya kimataifa katika upimaji wa kimaabara. Katika mwaka 2013/2014, maabara ya Mwanza itapata ithibati; Maabara Kuu, Maabara za Iringa na Mbeya zitajisajili na kukaguliwa kwa ajili ya kukamilisha taratibu za kupata ithibati. Kupatikana kwa ithibati kwa Maabara hizo kutaziwezesha kutekeleza majukumu yake kwa kufuata kiwango cha utendaji cha kimataifa (*ISO 17025*), hivyo takwimu na taarifa za ubora wa maji zitakuwa za kuaminika na kukubalika, na endapo kuna mivutano ya kisheria zitatumika kutatta migogoro. Aidha, Maabara kupata ithibati ni matakwa ya Sheria ya Rasilimali za Maji ya mwaka 2009 na ya Mazingira ya mwaka 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu itakarabati Maabara Kuu na za Mikoa pamoja na kupanua ofisi ili kuweka mazingira mazuri ya kazi na kukidhi matakwa ya kupata ithibati ambapo tathmini huanzia kwenye majengo. Aidha, Maabara zitaimarishwa na kujengewa uwezo kwa kununua samani, vifaa vya maabara na madawa na watumishi kupatiwa mafunzo ili kuungeza ufanisi na tija katika usimamizi wa ubora wa maji. Vilevile ili kusogeza huduma za ubora wa maji karibu na jamii mahitaji ya ujenzi wa maabara kwenye Mikoa ambayo haina huduma hiyo yataainishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma ya maji na usafi wa mazingira Vijijini. Katika mwaka 2012/2013, Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI tunasimamia utekelezaji wa Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini kulingana na mipango na vipaumbele vyta kila Halmashauri. Programu inahusu kujenga miradi ya maji kwenye Vijiji 10 kwa kila Halmashauri, kukarabati na kupanua miradi ya maji, kujenga uwezo wa watekelezaji wa programu, kuhamasisha wananchi kuhusu usafi binafsi na usafi wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, uboreshaji wa Huduma za Maji Vijijini. Mradi wa maji kwenye Vijiji 10 kwa kila Halmashauri. Katika mwaka 2012/2013, Serikali imezipatia Halmashauri shilingi bilioni 98.4 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji kwenye Vijiji 10 kwa kila Halmashauri. Pia, shilingi milioni 279.6 zilitumwa kwenye Sekretarieti za Mikoa kwa ajili ya kufuatilia utekelezaji na kutoa ushauri wa kitaalam kwa Halmashauri. Aidha, shilingi bilioni 9.85 za Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji zimetumwa kwa Watekelezaji wa Kampeni ya Kitaifa ya Usafi wa Mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Utekelezaji wa Miradi ya Maji katika Vijiji 10 kwa kila Halmashauri. Katika mwaka 2012/2013 jumla ya Vijiji 682 vinajengewa miundombinu ya kusambaza maji, hii ikiwa ni wastani wa Vijiji vitano kati ya Vijiji kumi vilivyopangwa kujengewa miundombinu ya maji kwa kila Halmashauri. Ujenzi wa miradi ya maji katika Vijiji hivyo kwa kutumia fedha zilizotumwa na Serikali kwenye Halmashauri katika kipindi cha 2012/2013 unatarajiwu kukamilika mwezi Septemba 2013, ambapo jumla ya wananchi milioni 1.7 wanaoishi Vijijini watafaidika na huduma hiyo ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nililieleza Bunge lako Tukufu katika kuomba fedha za mwaka 2012/2013 kuwa, miradi hiyo ingekamilika ifikapo mwezi Juni 2013. Hata hivyo, kukamilika kwa miradi hiyo ya kwanza ya Vijiji vitano kumechelewa kutokana na kuchelewa kwa upatikanaji wa fedha. Hadi kufikia mwezi Machi 2013 fedha za ndani zilizokuwa

24 APRILI, 2013

zimetolewa ni shilingi bilioni 29 kati ya shilingi bilioni 140 zilizokasimiwa katika wizara katika mwaka 2012/2013 sawa na asilimia 20.7 tu. Kwa upande wa fedha za nje, shilingi bilioni 55.4 zilipatikana na kutumwa kwenye Halmashauri mwezi Desemba 2012 lakini zilipokelewa mwezi Machi 2013. Kutokana na kuchelewa kwa upatikanaji wa fedha hizo, Halmashauri nyingi zimechukwa muda kuwekeana saini na wakandarasi hata pale ambapo vibali vyote vimekwishatolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara itaendelea kutekeleza Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijiji ambapo jumla ya shilingi bilioni 184.05 zimetengwa. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 105.2 zitatumwa na Halmashauri kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya maji kwenye Vijiji 480 kwa lengo la kukamilisha wastani wa Vijiji vitatu kwa kila Halmashauri ambapo wananchi millioni 1.2 watapata huduma ya maji. Naomba kutumia nafasi hii kuzihimiza Halmashauri kusimamia kwa karibu Wakandarasi na Wataalam washauri wanaojenga na kusimamia ujenzi wa miradi hiyo ili kuhakikisha miradi ya maji inatekelezwa kwa wakati na kwa ubora unaotakiwa "*Value for money*". Aidha, shilingi bilioni 75.45 zimekasimiwa katika Fungu la Wizara ya Maji kwa ajili ya kugharamia miradi ya maji Vijiji, ujenzi wa mabwawa, uchimbaji wa visima na kujenga uwezo katika ngazi zote za utekelezaji. Shilingi billioni 108.6 zimekasimiwa kupitia mafungu ya Mikoa kwa ajili ya Halmashauri, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI na Wizara zinazoshiriki katika kutekeleza Kampeni ya Kitaifa ya Usafi wa Mazingira Vijiji. Kati ya hizo, kiasi cha shilingi milioni 300 zitatumwa na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI kwa ajili ya uratibu na ufuutiliaji, shilingi bilioni 1.2 zitatumwa na ofisi za Sekretarieti za Mkoa kwa ajili ya ufuutiliaji na tathmini, shilingi bilioni 12.208 zitatumika kwenye utekelezaji wa Kampeni ya Kitaifa ya Usafi wa Mazingira kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa lengo la kuepuka migogoro ya kimikataba na kuharakisha utekelezaji wa miradi ya maji katika Vijiji 5 kwa kila Halmashauri, Halmashauri

zote zimetengewa fedha za utekelezaji wa miradi ya maji kwenye Halmashauri zao ikiwa ni pamoja na miradi iliyopo kwenye Halmashauri zilizoanzishwa hivi karibuni. Hii ni kwa sababu Halmashauri hizo zina mikataba na Wataalam Washauri na Wakandarasi wanaojenga miradi hiyo. Hata hivyo, Halmashauri mpya zitawezeshwa katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi kwenye maeneo yao. Kwa miradi ya maji ambayo haijaanza kujengwa na ipo kwenye Halmashauri mpya zilizoanzishwa, fedha za utekelezaji wa miradi hiyo zitatumwa kwenye Halmashauri mpya. Halmashauri hizo zitaingia mikataba na wakandarasi watakaoeuliwa kutekeleza miradi hiyo. Halmashauri mpya zitapatiwa fedha za utekelezaji wa miradi ya maji kuanzia mwaka 2013/2014. Wizara itaendelea kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI katika kujenga uwezo wa Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa ili kuharakisha utekelezaji wa Programu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu iliendelea kushirikiana na Halmashauri kwa kuzipatia fedha na kutoa ushauri wa kiufundi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maji Vijiji. Katika mwaka wa 2013/2014, Wizara yangu itaendelea kushirikiana na Halmashauri husika kwa kuzipatia fedha na ushauri wa kiufundi katika kutekeleza miradi ya maji. Wananchi 563,679 watanufaika na huduma ya maji miradi hiyo itakapokamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji wa Wilaya za Moshi Vijiji na Hai. Mradi wa maji katika Wilaya ya Moshi Vijiji unahusisha miradi ya maji ya Kirua-Kahe na Mji Mdogo wa Himo. Mradi wa Kirua-Kahe ulianza kutekelezwa mwezi Aprili 2007 ukiwa na lengo la kuwahudumia wakazi 110,000 katika Vijiji 32. Mradi huu umekamilika mwezi Desemba, 2012. Katika Mji Mdogo wa Himo, ukarabati wa matanki mawili ya maji unaendelea na ufungaji wa mabomba yenye urefu wa mita 684 umefanyika. Mradi utakamilika mwaka 2013/2014 baada ya kukamilisha ujenzi wa mtandao wa kusambaza maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013,

24 APRILI, 2013

Wizara yangu kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (*KfW*) na Umoja wa Ulaya (*EU*) iliendelea na utekelezaji wa Mradi wa maji katika Wilaya za Hai na Siba. Ujenzi wa mradi huo umekamilika mwezi Desemba, 2012 baada ya kukamilisha skimu ya *North West Kilimanjaro*. Wananchi wapatao 5,000 wanapata huduma ya maji kutoka skimu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji Masoko. Mradi wa Maji Masoko katika Wilaya ya Rungwe ulianza kujengwa mwezi Septemba 2010. Lengo la mradi ilikuwa ni kujenga banio (*intake*) la maji la Mbaka na Kigange, kujenga chujio eneo la Kigange, kujenga matanki matatu ya kuhifadhi maji, kujenga beseni la kuchuja maji (*sedimentation tank*), kujenga chujio kubwa la maji (*treatment plant*), kujenga tanki la maji yanayorudi (*backwater tank*), ununuzi na ufungaji wa mabomba na ujenzi wa vituo 122 vya kuchotea maji. Mradi ukikamilika utanufaisha wakazi wa Vijiji 15.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Machi 2013, ujenzi wa mabanio (*intakes*) ya maji ya Mbaka na Kigange ulikuwa umekamilika, uchimbaji wa mtaro kutoka kwenye banio la Kigange kwenda kwenye tanki la kutuamisha tope kwenye maji (*sedimentation tank*) umekamilika na mabomba tayari yamelazwa na msingi wa chujio la maji (*treatment plant*) umechimbwa. Ujenzi wa matanki manne katika Vijiji vya Masoko, Lufumbi, Bulongwe na Kigange yako katika hatua mbalimbali ya utekelezaji. Hal mashauri imevunja mkataba na mkandarasi baada ya Mkandarasi kujenga baadhi ya miundombinu ya maji chini ya kiwango.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji katika Chuo cha Nelson Mandela. Mradi wa maji katika Chuo cha Nelson Mandela uliopo Wilaya ya Arumeru ulianza kutekelezwa mwaka 2009. Lengo la mradi ilikuwa ni kuchimba visima viwili, kujenga nyumba ya mitambo na kulaza mabomba katika maeneo ya chuo hicho. Hadi kufikia Machi 2013 visima viwili vimechimbwa na matanki mawili yamejengwa. Katika mwaka wa 2013/2014 nyumba ya mtambo wa kusukumia maji utajengwa, mabomba yatalazwa na mradi utakamilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji Kidete. Mradi wa maji Kidete uliopo katika Wilaya ya Kilosa ulianza kujengwa mwezi Septemba 2010. Kazi zilizopangwa kutekelezwa katika mradi huo unaohusu ujenzi wa bwawa ni uchimbaji wa utoro wa maji, uchimbaji wa msingi wa tuta, kulaza na kushindilia udongo kwenye msingi wa tuta, ujenzi wa miundombinu ya kutolea maji kwenye bwawa, ujenzi wa *crest weir* kwenye utoro wa maji na upangaji wa mawe kwenye upande wa ndani wa tuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Machi 2013, utekelezaji wa mradi ulikuwa umefikia asilimia 75, ambapo kazi ya kuhamasisha wananchi imefanyika, ujenzi wa tuta la bwawa umekamilika. Mradi unatarajia kuhudumia wananchi wapatao 15,000 katika Vijiji vitano. Katika kipindi cha mwaka 2013/2014, kazi zitakazofanyika ni kukamilisha ujenzi wa bwawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji wa Same – Mwanga – Korogwe. Mradi wa Same-Mwanga-Korogwe ulibuniwa mwaka 2006/2007 ukiwa na lengo la kupeleka maji katika Miji ya Same na Mwanga ambayo ina shida kubwa sana ya maji. Aidha, katika mwaka 2012/2013, Serikali kwa kushirikiana na *BADEA* na *OFID* naendelea na maandalizi ya mradi wa maji wa Same - Mwanga - Korogwe. Mtaalam Mshauri amekamilisha kupitia usanifu wa mradi kuanzia chanzo cha maji hadi katika tanki kuu la kuhifadhia maji. Hivi sasa anaendelea kusanifu mfumo wa kutoa maji kutoka tanki kuu hadi Miji ya Same na Mwanga. Mradi utakapokamilika utahudumia wananchi 122,000 kwenye Vijiji 38 vilivyo katika Wilaya za Same, Mwanga na Korogwe pamoja na Miji ya Same na Mwanga. Ujenzi wa mradi utaanza mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji Bungu. Mradi wa maji Bungu upo katika Wilaya ya Korogwe. Mradi huu unalenga kuhudumia Vijiji saba ambavyo ni Bungu, Bungu Msiga, Kwamshai, Ngulu, Mlunghi, Msasa na Manka. Kazi ambazo zimepangwa kufanyika ni ukarabati ambapo ulazaji wa bomba kilomita 1.5, ujenzi wa matanki mawili kila moja

lenye lita 90,000, ujenzi wa vituo vya kuchotea maji 54 na ulazaji wa bomba za usambaji urefu wa kilomita 26.8 utafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi Machi 2013, kazi zilizofanyika ni ujenzi wa mtandao wa maji wenye urefu wa mita 5,994, vituo vya kuchotea maji 15 umekamilika, tanki la kuhifadhi maji lenye lita 90,000 umekamilika katika kitongoji cha Gare. Mradi utakapokamilia wananchi 2,883 watapata huduma ya maji. Katika kipindi cha mwaka 2013/2014 kazi zilizobaki za ujenzi wa mradi zitakamilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji Vijiji katika Mkoa wa Tabora. Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Japan inatekeleza mradi wa maji Vijiji katika Mkoa wa Tabora. Mradi huo ulilenga kuwapatia huduma ya maji wananchi wapatao 41,744 katika Vijiji 20 vya Mkoa huo. Kutokana na maafa ya *Tsunami/yaliyoikumba* nchi ya Japan mwezi Machi, 2011, utekelezaji wa mradi ulisimama kwa muda. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa mwezi Februari, 2013, Serikali ya Japan iliridhia kuendelea na utekelezaji wa mradi huo. Katika mwaka 2013/2014, utafiti na usanifu wa kina katika maeneo yaliyoonesha kuwa na maji ya kutosha utafanyika na ujenzi utaanza. Utekelezaji unatarajiwu kuchukua miaka mitatu. Vijiji vilivyo lengwa kupata maji kuititia mradi huo ni Busomeke na Kalemela (Igunga); Isanga, Kitangili, Makomelo na Wela (Nzega); Kasandalala, Usunga na Mpombwe (Sikonge); Mabama, Ufuluma na Mpumbuli (Tabora/Uyui); Kakola, Misha na Uyui (Manispaa ya Tabora) na Imalamakoye, Kalembela, Kiloleli na Nsungwa (Urambo).

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji kwa Vijiji 100 kando ya Bomba Kuu la Ziwa Victoria. Katika mwaka 2013/2014, Wizara itaanza maandalizi na utekelezaji wa kuvipatia huduma ya maji Vijiji 100 vilivyo kandokando ya bomba kuu la mradi wa Kahama Shinyanga ndani ya kilomita 12 katika Wilaya za Mikoa ya Mwanza na Shinyanga. Lengo ni kuongeza idadi ya wananchi wa kunufaika na mradi huo. Mradi huo utatekelezwa kwa kutumia fedha za ndani. Ili kuharakisha

utekelezaji, kazi ya kusanifu miundombinu ya kusambaza maji katika Vijiji itatekelezwa na Wataalam wa Halmashauri za Wilaya husika na kuratibiwa na Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maji Kahama/Shinyanga (*Kahama Shinyanga Water Supply Authority*) KASHWASA. Ujenzi utatekelezwa na wakandarasi watakaoajiriwa na Mamlaka ya Maji ya Mradi wa Kahama na Shinyanga (KASHWASA). Katika kipindi cha mwaka 2013/2014, usanifu wa miradi utafanyika katika Halmashauri husika na ujenzi utaanza. Vijiji vitakavyohusika na mradi huo viko katika Jedwali Na. 15.1. Mradi huo utakapokamilika utawanufaisha wananchi zaidi ya 308,738.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Miradi Mingine ya Maji Vijijini. Katika mwaka 2012/2013, Serikali imeendelea kushirikiana na taasisi mbalimbali kujenga miradi ya maji Vijijini kupitia vyanzo mbalimbali vya fedha ambavyo havipo katika bajeti ya Wizara yangu. Juhudi hizo zinachangia kwa kiasi kikubwa katika kuinua kiwango cha upatikanaji wa huduma ya maji Vijijini. Katika mwaka 2013/2014, Serikali itaendelea kushirikiana na taasisi mbalimbali katika ujenzi wa miradi ya maji Vijijini ili kuongeza upatikanaji wa huduma hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uvunaji wa Maji ya Mvua. Serikali inaendelea kuhamasisha na kuhimiza jamii kuhusu uvunaji wa maji ya mvua kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoa na kila Halmashauri za Wilaya kuandaa mpango wa miaka mitano. Halmashauri zote zimeagizwa kutunga sheria ndogo zinazohakikisha kuwa michoro ya nyumba zote zinazojengwa zinajumuisha mifumo ya miundombinu ya kuvuna maji ya mvua kabla ya kuidhinishwa ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ambazo zimetekeleza agizo hilo ni Jiji la Tanga, Manispaa za Iringa, Arusha, Tabora, Halmashauri za Monduli, Meru, Moshi, Mtwara, Newala, Nanyumbu, Tandahimba, Rombo, Hai na Siha. Katika mwaka 2013/2014, kupitia mradi wa Vijiji 10 kwa kila Halmashauri, matanki na mifumo ya kuvuna maji ya mvua kupitia mapaa ya nyumba yataendelea kujengwa katika Vijiji viwili kwa kila Halmashauri husika ili wananchi waone na

kujifunza. Mafunzo pia yatatolewa kwa mafundi katika kila kijiji. Aidha, taasisi za umma na binafsi zimejenga matanki ya kuvuna maji ya mvua kwenye taasisi mbalimbali hapa nchini. Takwimu kuhusu idadi ya matanki ya kuvunia maji ya mvua yaliyojengwa kwa kila Mkoa na Halmashauri zinakusanywa ili kuwezesha kufuatilia utekelezaji wa sheria iliyowekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Kuainisha Vituo vya Kuchotea Maji. Wizara yangu imeendelea na mradi wa kuainisha vituo vya kuchotea maji Vijijiini kwa lengo la kupata takwimu sahihi zinazohusiana na huduma ya maji Vijijiini kwa kutumia mfumo wa kompyuta. Taarifa zitakazopatikana na ufahamu wa mtandao wa vituo vya kuchotea maji zitawezesha Halmashauri kufahamu upatikanaji wa maji katika Vijiji na kata, pia kuwezesha kupanga vipaumbele. Taarifa hizo pia zitasaidia katika ufuatiliaji wa uendelevu wa miradi ya maji nchini. Hadi kufikia mwezi Februari, 2013 takwimu za vituo 65,421 vya kuchotea maji katika Halmashauri 143 zimekusanywa. Kazi hiyo itakamilishwa katika mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uundaji na Usajili wa Vyombo vya Watumiaji Maji. Uundaji na usajili wa vyombo vya watumiaji maji ni mkakati wa kuisaidia miradi ya maji kuwa endelevu. Hadi kufikia mwezi Machi 2013, idadi ya vyombo vya watumiaji maji vilivyoundwa na kusajiliwa kwa Sheria ya Maji na Usafi wa Mazingira Namba 12 ya mwaka 2009 jumla yake ni 147 kwa mchanganuo ufuatao kiMkoa: Arusha (4), Iringa (3), Mbeya (4), Dodoma (2), Ruvuma (3), Kilimanjaro (28), Kagera (45), Lindi (10), Morogoro (7), Singida (11), Kigoma (10), Mwanza (15) na Rukwa (4). Aidha, Halmashauri zilizo nyingi ziko katika hatua mbalimbali za maandalizi ya usajiri wa vyombo vya watumiaji maji kwa kutumia Sheria ya Maji na Usafi wa Mazingira Namba 12 ya mwaka 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, Wizara yangu ilitoa mwongozo wa uundaji na usajili wa vyombo vya watumiaji maji, kwa mujibu wa kanuni inayohusu Usajili wa Vyombo vya Watumiaji Maji [*The Water Supply and Sanitation (Registration of Community Owned*

*Water Supply Organisations) Regulations, 2009, GN. No. 21 of 22/01/2010]. Hadi sasa Halmashauri zote zimeteua Wasajili wa vyombo nya watumiaji maji. Napenda kuchukua fursa hii kuwaomba Wasajili kuharakisha zoezi la uundaji na usajili wa vyombo huru nya kuendesha na kusimamia miradi ya maji. Hatua hii itasaidia kwa kiasi kikubwa kuifanya miradi ya maji kuwa endelevu kwa kuwa itasimamiwa na kuendeshwa na wananchi wenyewe.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ujenzi wa Mabwawa. Katika mwaka 2012/2013, Wizara yangu ilipanga kukamilisha ujenzi wa mabwawa matano ya Kawa (Nkasi), Sasajila (Chamwino), Mwanjoro (Meatu), Iguluba (Iringa Vijiji) na Ingondin (Longido). Ujenzi wa bwawa la Ingondin umekamilika kwa asilimia 100 baada ya kuimarisha utoro wa maji uliokuwa umeathiriwa na mvua. Ujenzi wa bwawa la Iguluba umekamilika kwa asilimia 75, mkandarasi anaendelea kukamilisha kazi zilizobaki kwenye utoro wa maji na makinga mchanga. Matarajio ya Wizara ni kuwa mabwawa hayo yatakamilika katika kipindi kilichobaki cha mwaka 2012/2013 isipokuwa kwa bwawa la Sasajila ambalo halina mkandarasi kwa sasa baada ya mkandarasi aliyejukwepo kushindwa kukamilisha kazi. Wizara inategemea kusaini mkataba na Mkandarasi mwingine baada ya kukamilisha taratibu za manunuzi ya mkandarasi huyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliendelea kuratibu upatikanaji wa fedha za ujenzi wa bwawa la Kidete linalosimamiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa ambalo ujenzi wake umefikia asilimia 75. Katika mwaka 2013/2014, ujenzi wa mabwawa ya Seke Ididi (Kishapu), Habiya (Bariadi) na Matwiga (Chunya) ambao ulisimama kutokana na wakandarasi wake kushindwa kazi na kuondoka maeneo ya kazi, utaendelea kwa kutumia wakandarasi wapya na kwa kadri fedha zitakavyopatikana. Kufuatia tathmini iliyofanywa na Wizara ya Maji, marekebisho yatafanywa kwenye Bwawa la Wegero ili kudhibiti utoro wa maji na kuongeza wingi wa maji. Ujenzi wa mabwawa madogo utatekelezwa na Halmashauri kulingana na vipaumbele vyake, ambapo Wizara yangu itatoa ushauri wa kiufundi utakaohitajika katika ujenzi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango Maalum wa Kuleta Matokeo ya Haraka. Serikali imechagua Sekta 6 za awali ambazo zitaanza utekelezaji wa mpango maalum ulioandaliwa wa "Tekeleza Sasa kwa Matokeo Makubwa" (*Big Results Now Program*). Mpango huo utatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia 2013/2014-2015/2016, Sekta ya Maji ni miongoni mwa sekta hizo zilizopewa kipaumbele ambapo mpango huo unalenga kuungeza upatikanaji wa huduma ya maji maeneo ya Vijiini. Hii ni kutokana na ukweli kwamba asilimia kubwa ya Watanzania wanaoishi Vijiini hawapati huduma ya maji ipasavyo kutokana na miradi mingi iliyopo kuchakaa, usimamizi duni, wananchi kutokuchangia gharama za uendeshaji ipasavyo, ukosefu wa vipuli na uwekezaji mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi zilizoainishwa ambazo zimepangwa kutekelezwa ni pamoja na:-

(a) Kuungeza idadi ya vituo vya kuchotea maji kwa kupanua miundombinu iliyopo, kukarabati na kujenga miradi mipya. Jumla ya Miradi 1,810 inatarajiwa kutekelezwa;

(b) Kuboresha usimamizi wa miradi ya maji ngazi ya jamii kwa kuunda na kuimarisha vyombo vya watumia maji na kuweka mazingira mazuri ya uwajibikaji na usimamizi; na

(c) Kuboresha mfumo wa upatikanaji wa vipuli na kuweka utaratibu wenye ufanisi wa matengenezo ya miradi ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango huu utahitaji kiasi cha shilingi Trillion 1.45 na utakapokamilika kutakua na ongezeko la wananchi milioni 15.4 waishio Vijiini watakaopata huduma ya maji na hivyo kuungeza idadi ya wananchi wanaopata huduma hiyo kutoka asilimia 57 za sasa hadi asilimia 75 ifikapo mwaka 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini. Katika mwaka 2012/2013, Wizara kuitia

Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini imeimarisha utoaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira. Kazi zilizofanyika ni kukarabati, kujenga na kupanua mifumo ya majisafi na majitaka pamoja na kuzijengea uwemo mamlaka za maji za Dar es Salaam, Miji Mikuu ya Mikoa, Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na miradi ya kitaifa ya maji ili kuwapatia wananchi wengi zaidi huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uboreshaji wa Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini. Miradi ya Maji Kukidhi Mahitaji ya Muda Mfupi. Katika mwaka 2012/2013, Serikali ilitekeleza mpango wa kukidhi mahitaji ya maji ya muda mfupi hadi 2015, kwa kujenga, kukarabati na kupanua vyanzo vya maji; kuchimba visima, kupanua mitandao ya usambazaji maji; na kujenga matanki ya maji katika Miji ya Babati, Lindi, Sumbawanga na Mtwara. Wizara yangu ilikamilisha ujenzi na kuzindua miradi ya maji katika Miji ya Babati mwezi Novemba 2012 na Lindi mwezi Machi 2013. Miradi hiyo ilizinduliwa na Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, hadi Machi 2013, ujenzi katika mji wa Mtwara umefikia asilimia 98 na Sumbawanga asilimia 80. Miradi hiyo itakapokamilika itakidhi mahitaji ya muda mfupi kwa asilimia; Babati (85%), Lindi (80%), Mtwara (100%) na Sumbawanga (80%).

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi ya Maji Kukidhi Mahitaji ya Muda wa Kati katika Miji Saba. Katika mwaka 2012/2013, Wizara yangu kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (*AFD*); imeanza ujenzi wa miradi ili kukidhi mahitaji ya maji ya muda wa kati katika Miji ya Bukoba na Musoma kwa gharama ya shilingi bilioni 68.2. Kazi zitakazofanyika ni kujenga mitambo ya kusafisha maji, mitambo ya kusukuma maji na kulaza mabomba ya maji katika Miji hiyo. Pia, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Ujeruman na Umoja wa Ulaya imeanza utekelezaji wa miradi katika Miji ya Lindi, Kigoma na Sumbawanga yenye gharama ya *Euro* milioni 62.59. Wakandarasi wameanza hatua za awali za ujenzi wa miradi hiyo na wanatazamiwa kukamilisha kazi mwezi Aprili 2015. Vilevile, Serikali ya Ujeruman kupitia *KfW* itatoa *Euro* milioni

24 APRILI, 2013

8.72 kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa majisafi na usafi wa mazingira Babati na Mtwara chini ya programu ya *Millenium Development Goal Initiative (MDGI-EU)*. Katika mwaka 2013/2014, utekelezaji wa miradi katika Miji hiyo utaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji Tabora. Katika mwaka 2012/2013, Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Uswisi kupitia Shirika lake la Maendeleo (*SECO*), iliendelea kutekeleza mradi wa kupanua na kukarabati mifumo ya majisafi katikati ya mji wa Tabora. Uboreshaji wa miundombinu ya uzalishaji katika bwawa la Igombe na upanuzi wa mfumo wa usambazaji majisafi umefikia asilimia 80 na unatazamiwa kukamilika mwezi Juni 2013. Aidha, upanuzi wa chujio la maji katika bwawa hilo umeanza mwezi Machi 2013 na utaendelea kutekelezwa katika mwaka 2013/2014, kwa kujenga mitambo ya kusafisha maji na kusukuma maji. Kukamilika kwa kazi hizo kutaongeza uzalishaji wa maji kutoka lita milioni 15 hadi kufikia lita milioni 30 kwa siku, wakati mahitaji kwa sasa ni lita milioni 24.97 kwa siku; na itagharimu shilingi bilioni 7.5. Hatua hiyo itakidhi mahitaji ya maji katika Mji wa Tabora kwa asilimia 100 mpaka mwaka 2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji Mjini Dodoma. Katika mwaka 2012/2013, Serikali ilianza kutekeleza mradi wa kuboresha huduma ya majisafi na majitaka ili kukidhi mahitaji katika Chuo Kikuu cha Dodoma; Mradi huo utajenga mfumo wa uondoaji majitaka unaojumuisha mtandao wa kukusanya majitaka wenye urefu wa kilomita 32 na mabwawa ya kutibia majitaka. Kwa upande wa majisafi mradi utajenga kituo cha kusukuma maji na matanki makubwa ya maji yenye ujazo wa lita milioni 12 katika Chuo Kikuu cha Dodoma. Kazi zinazotekeliza ni ulazaji wa bomba kuu la majisafi kilomita 15.5, ulazaji wa mabomba ya kusambaza majisafi kilomita 7.5. Gharama ya mradi huo ni shilingi bilioni 27.7. Katika mwaka 2013/2014, utekelezaji wa mradi huo utakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Korea Kusini inatekeleza mradi Sera ya wa maji katika mji wa Dodoma utakaogharimu shilingi

bilioni 49.62 ili kukidhi mahitaji ya muda wa kati. Mradi huo ulianza kujengwa tarehe 15 Januari 2013 kwa kukarabati visima 21 na kuchimba visima vipyta vitatu katika eneo la Mzakwe. Kazi zitakazotekelawa ni pamoja na ujenzi wa mtandao wa mabomba wenyewe urefu wa kilomita 6.5, ujenzi wa barabara za visimani zenye urefu wa kilomita 5, ulazaji wa bomba jipya lenye kipenyo cha milimita 600 kutoka Mzakwe hadi Mjini lenye urefu wa kilomita 31.2, ujenzi wa matanki mawili na ukarabati wa mitambo ya kusukuma maji. Vilevile, mradi huo utajenga *booster station* mpya eneo la Mailimbili na kununua mitambo ya kisasa ya kutibu maji pamoja na kujenga maabara ya kisasa ya kupima ubora wa majisafi na majitaka. Mradi huo utatekelezwaa katika kipindi cha miezi 24, hivyo unatazamiwa kukamilika mwezi Januari 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na ongezeko la kasi la watu katika mji wa Dodoma, Serikali imeanza usanifu wa Bwawa la Farkwa. Bwawa hilo litakuwa chanzo cha maji kwa Manispaa ya Dodoma na Miji ya Kondoa, Chamwino na Bahi ili kukidhi ongezeko la mahitaji ya maji katika Miji hiyo. Gharama za usanifu wa bwawa hilo ni Euro 627,930 na shilingi 219,385,000. Usanifu huo utakaokamilika Agosti 2013 utaonesha gharama halisi za ujenzi wa bwawa hilo pamoja na kiwango cha maji kitakachopatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji Mjini Singida. Katika mwaka 2012/2013, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Kiarabu (*BADEA*) pamoja na Mfuko wa Maendeleo wa Nchi Zinazozalisha Mafuta (*OPEC Fund for International Development-OFID*) iliendelea na ujenzi wa mradi wa uboreshaji wa miundombinu ya majisafi mjini Singida. Ujenzi huo unahusu uchimbaji wa visima virefu 10 vya kuzalisha maji katika eneo la Mwankoko na Irao na ujenzi wa miundombinu ya maji. Utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 98. Ujenzi wa matanki mawili katika maeneo ya *Airport* na kulaza bomba umekamilika na maji yamesukumwa hadi kwenye matanki na kwenye mtandao wa maji kwa eneo la Mandewa. Mradi huo uliogharimu shilingi bilioni 32.53, uliwekwa jiwe la msingi na Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho

24 APRILI, 2013

Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Novemba 2012. Kukamilika kwa mradi huo kutaongeza uzalishaji wa maji kufikia lita milioni 17.76 kwa siku na utakidhi mahitaji ya mji huo kwa zaidi asilimia 100 kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji Morogoro Mjini. Katika mwaka 2012/2013, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Changamoto za Milenia la Marekani (*MCC*), iliendelea na utekelezaji wa mradi wa kupanua na kuboresha upatikanaji wa maji safi katika Manispaa ya Morogoro kwa kukarabati matanki matatu na ulazaji wa bomba kuu la maji la urefu wa kilomita 1.8 pamoja na kupanua chujio la maji la Mafiga na kujenga mtambo wa kusafisha maji wa Mambogo. Gharama za utekelezaji wa mradi huo ni shilingi bilioni 10. Utekelezaji hadi Machi 2013 umefikia asilimia 60. Ujenzi ukikamilika uzalishaji wa maji utaongezeka kutoka lita millioni 23 kwa siku hadi lita millioni 33 kwa siku na kuboresha ubora wa maji hivyo kupunguza mlipuko ya magonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji katika Jiji la Mbeya. Katika mwaka 2012/2013, Wizara yangu kwa kushirikiana na *KfW* na *EU* ilikamilisha kutekeleza awamu ya pili ya Programu ya majisafi na majitaka katika Jiji la Mbeya kwa gharama ya *Euro* milioni 32.52. Mradi huo ulikamilika tarehe 21/12/2011 na kuzinduliwa na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Julai 2012. Kwa ujumla, mradi huo umeongeza hali ya upatikanaji wa majisafi katika Jiji la Mbeya kutoka asilimia 80 ya mwaka 2007 hadi asilimia 95.5 kwa sasa. Mradi huo una uwezo wa kutoa huduma ya majisafi kwa wakazi wapatao 490,000 na una uwezo wa kuzalisha maji kiasi cha lita milioni 49 kwa siku. Aidha, maboresho yaliyofanyika kwenye Mradi wa majitaka yatawezesha kutoa huduma kwa wakazi 57,000 kutoka wakazi 26,514 wa awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji katika Manispaa ya Iringa. Katika mwaka 2012/2013, Wizara yangu kwa kushirikiana na *KfW* na *EU* ilikamilisha kutekeleza awamu ya pili ya Programu ya majisafi na majitaka katika Manispaa ya Iringa kwa gharama ya *Euro* milioni 23.2. Mradi huo

unakidhi mahitaji ya maji kwa wakazi wapatao 300,000. Kiwango cha upatikanaji maji kimeongezeka kutoka asilimia 68 mwaka 2007 hadi asilimia 85 kwa sasa. Idadi ya wateja wapya 1,760 waliunganishwa katika mtandao wa majisafi na wateja 150 waliunganishwa katika mtandao wa majitaka. Changamoto iliyojitekeza baada ya kukamilika kwa mradi huo ni upotetu mkubwa wa maji kutokana na kuongezeka kwa wingi wa maji katika mfumo wa usambazaji maji wa zamani uliochakaa. Kazi za kukarabati mfumo wa usambazaji maji wa zamani imefanyika ili kupunguza upotetu wa maji kutoka asilimia 60 hadi kufikia asilimia 35 kwa sasa. Katika mwaka 2013/2014, Mamlaka itaendelea na jitihada za kupunguza upotetu wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji Songea Mjini. Katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu itakarabati chanzo cha mto Ruhira Mjini Songea kwa kujenga banio la maji (*weir*) ili kukabiliana na upungufu wa maji wakati wa kiangazi mjini Songea. Lengo ni kutega maji na hivyo kuboresha upatikanaji wa maji katika mto huo. Matokeo ya kazi hiyo yataongeza uhifadhi wa maji kutoka lita milioni 15 za sasa hadi kufikia lita bilioni moja. Kazi hiyo itagharimu shilingi bilioni 2.6, ambapo mwaka 2013/2014, Serikali imetenga shilingi milioni 400.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji katika Miji ya Geita, Sengerema na Nansio. Katika mwaka 2012/2013, Wizara iliendelea na awamu ya pili ya Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira wa Ziwa Victoria (*LWATSAN II*). Mradi huo unatekelezwa kwa pamoja na nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AFDB). Utekelezaji wa Programu hiyo kwa upande wa nchi yetu ni pamoja na kuboresha huduma ya maji na usafi wa mazingira katika Miji ya Geita, Sengerema na Nansio ambapo msimamizi wa Programu hiyo ni Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mhandisi Mshauri wa kusanifu na kusimamia kazi za ujenzi wa mradi huo alisaini mkataba mwezi Februari 2013. Usanifu utazingatia uwekezaji wa muda

mfupi na muda mrefu ili kukidhi mahitaji ya maji katika Miji hiyo. Mradi wa maji Geita ukikamilika utahudumia wakazi 68,500, sawa na asilimia 40. Kazi zitakazotekelawa ni kulaza mabomba ya usambazaji, kuunganisha umeme kwenye chanzo na kufunga dira za maji. Kazi hiyo itagharimu Dola za Marekani milioni 4.2. Aidha, katika mwaka 2012/2013, Halmashauri ya mji wa Geita kwa kushirikiana na mgodi wa madini wa Geita (*Geita Gold Mine – GGM*) imekamilisha kazi ya ujenzi wa chanzo, chujio la maji, bomba kuu na tanki moja. Mradi unatarajiwaa kuzalisha lita milioni 4.8 za maji kwa siku, hivyo kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji kutoka asilimia 3.5 hadi asilimia 40; ambapo mahitaji ni lita milioni 11.9 kwa siku. Katika mwaka 2013/2014, ujenzi wa miundombinu ya maji itakayoleta matokeo ya muda mfupi utaanza pamoja na usanifu wa uwekezaji wa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Sengerema, kazi zilizopangwa ni kujenga chanzo, mitambo ya kusafisha maji, mtandao wa kusambaza maji kilomita 25 na matanki ya maji. Gharama za mradi ni Dola za Marekani milioni 14. Katika mji wa Nansio, kazi zilizopangwa ni kujenga mitambo ya kusafisha maji, mtandao wa kusambaza maji kilomita 14 na matanki ya maji saba ya ujazo mbalimbali. Gharama za mradi ni dola za Marekani milioni 6.9.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na *UN-HABITAT* ilitekeleza programu ya *LWATSAN* iliyohusisha miradi ya kuboresha huduma za maji na usafi wa mazingira kwa Miji ya Muleba, Mutukula na Chato. Mradi huo ambaa umegharimu dola za Marekani milioni 5, upo katika hatua za mwisho za utekelezaji. Katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu itachangia shilingi milioni 700 ili kukamilisha mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi Mipyä katika eneo la Ziwa Victoria. Katika mwaka 2013/2014, Serikali kwa kushirikiana na *AFD*na *European Investment Bank (EIB)* itaanza utekelezaji wa miradi ya majisafi na usafi wa mazingira katika Jiji la Mwanza; vilevile, mradi huo utahusu uondoaji wa majitaka katika Manispaa za Bukoba na Musoma, pamoja na mradi wa majisafi na usafi wa mazingira katika Miji ya

Lamadi, Misungwi na Magu. Miradi hiyo itaongeza upatikanaji wa maji kutoka asilimia 35 hadi asilimia 90 kwa mji wa Magu; kutoka asilimia 5 hadi asilimia 90 kwa Mji wa Lamadi na kutoka asilimia 45 hadi asilimia 90 kwa Mji wa Misungwi. Mradi wa kuboresha usafi wa mazingira kwa Jiji la Mwanza utahusisha kupanua mtandao wa majitaka kutoka asilimia 13 hadi asilimia 30; kuwa na vyoo bora kwa shule zote za Jiji na masoko; kuwa na mfumo mzuri wa uondoshaji majitaka ya wakazi wa milimani. Mradi wa majitaka kwa mji wa Bukoba utahudumia asilimia 15; na mji wa Musoma ni asilimia 20 ya wakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi ya Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Miji inayozunguka Ziwa Tanganyika. Katika mwaka 2013/2014, Serikali kupitia Shirika la Umoja wa Mataifa la Makazi (*UN-HABITAT*) itaanza utekelezaji wa miradi ya pamoja ya kuboresha huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika Miji iliyopo kandokando ya Ziwa Tanganyika. Miji hiyo ni Kigoma, Kasulu, Mpanda na Namanyere. Fedha za kutekeleza mpango huo ambao utaanza utekelezaji wake katika mwaka 2013/2014 zinatoka COMESA na Jumuia ya Africa Mashariki (*EAC*). Mpango huo utatekelezwa katika nchi za Kongo (*DRC*), Burundi, Rwanda, Zambia na Tanzania. Kazi zitakazotekeliza ni pamoja na kuboresha huduma ya majisafi na usafi wa mazingira, taka ngumu, kujenga uwezo taasisi na walengwa wa mradi. Gharama ya utekelezaji wa mradi huo kwa mji wa Kigoma Dola za Marekani milioni 4.6; Kasulu Dola za Marekani milioni 2,3; Mpanda Dola za Marekani milioni 3.1 na Namanyere Dola za Marekani milioni 1.9. Aidha, katika kupunguza kero ya maji katika mji wa Namanyere, katika mwaka 2012/2013, Serikali imetuma shilingi milioni 100 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa dharura wa kuboresha huduma ya maji katika mji huo. Kazi zilizofanyika ni kulaza bomba la urefu wa mita 3,960 kununua pampu, jenereta na dira za maji 103.

Mheshimiwa Naibu Spika, uboreshaji wa Huduma ya Maji katika Miji Mikuu ya Mikoa Mipyä. Katika mwaka 2013/2014, Serikali itaboresha huduma ya majisafi katika Miji Mikuu ya Mikoa mipyä ya Mpanda, Njombe na Bariadi. Kazi zitakazofanyika katika Miji hiyo ni:-

(1) Mpanda, ni kujenga tanki la maji, mtambo wa kutibu maji, chanzo cha maji cha Manga na kupanua mtandao wa majisafi mjini Mpanda, Kununua pampu za kusukuma maji bwawa la Milala na dira za maji 1,500. Kazi hizo zikikamilika zitaongeza wingi wa maji kutoka lita milioni 2.8 za maji sasa hadi kufikia lita milioni 6.1 na upotevu wa maji utapungua kutoka asilimia 59 sasa hadi asilimia 35. Kazi hizo zitagharimu shilingi bilioni 1.5.

(2) Katika mji wa Njombe, kazi zitakazofanyika ni kujenga chanzo cha Wikichi, kulaza mabomba kutoka kwenye chanzo mpaka mjini, kukarabati mfumo wa maji mjini Njombe na kununua dira za maji 1,000. Matokeo ya kazi hii ni kuongezeka kwa wingi wa maji kiasi cha lita 604,000 kwa siku na ufungaji wa dira za maji utasaidia kupunguza kiasi cha maji yanayopotea kutoka asilimia 50 za sasa hadi asilimia 38. Wananchi zaldi 12,000 watapata huduma na kukidhi mahitaji ya maji kwa asilimia 62. Mradi huo utagharimu shilingi milioni 800.

(3) Katika mji wa Bariadi, kazi zilizopangwa ni kuchimba visima sita na kufunga pampu, kujenga tanki la maji, kupanua mtandao wa maji, kukarabati tanki la Somanda na kujenga ofisi ya Mamlaka ya maji. Mradi huo utagharimu shilingi bilioni 2. Aidha, katika mwaka 2012/2013, Serikali imetuma shilingi milioni 150 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa dharura majisafi mjini Bariadi. Kazi zilizofanyika ni ukarabati wa pampu na mota kwa ajili ya chujio la maji, tanki la maji Somanda, ujenzi wa nyumba ya mitambo na bomba kwa ajili ya visima vya Somanda, Sanungu na Isanzu. Kazi zinazoendelea ni pamoja na ujenzi wa mtandao wa kusambaza maji Kidinda pamoja na ujenzi wa vioski vinne na kuunganisha umeme kwa ajili ya visima vya Somanda, Sanungu, Isanzu na Kidinda. Mradi huu ukikamilika, kiasi cha maji kitaongezeka kutoka lita 861,000 hadi 1,560,000 kwa siku na huduma itaboreka kutoka asilimia 17 hadi 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, Usanifu wa Miradi ya Majisafi na Majitaka. Katika mwaka 2013/2014, Serikali itafanya usanifu wa kina na kuandaa vitabu vya zabuni kwa miradi

ya maji katika Miji Midogo na Miji Mikuu ya Wilaya ya Bihamarulo, Muleba, Ngara, Karagwe, Chato na Bunazi (Kagera); Kakonko (Kigoma); Namanyere, Chala na Laela (Rukwa); Manyoni na Kiomboi (Singida), na Mombo, Songe, Lushoto, Kasela, Korogwe na HTM(Tanga) pamoja na miradi ya majitaka mjini Bukoba na Singida ili kukidhi mahitaji ya muda wa kati. Vilevile, Serikali itafanya usanifu na kuandaa vitabu vyat zabuni kwa mradi wa kutoa maji Mto Ugala hadi Miji ya Urambo na Kaliua ili kuboresha huduma ya maji katika Miji hiyo. Taratibu za kuwapata wahandisi washauri wa kufanya usanifu huo zimeanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria hadi Tabora, Igunga, Nzega, Kagongwa, Isaka na Tinde. Taratibu za kuwapata Wahandisi Washauri wa kufanya usanifu na uandaaji wa makabrasha ya zabuni ya ujenzi wa mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria hadi Miji ya Nzega, Igunga na Tabora pamoja na mradi wa kupeleka maji katika Miji Midogo ya Kagongwa, Isaka hadi Tinde zinaendelea. Kazi zitakazotekelzwa 2013/2014, ni kufanya usanifu na kuandaa vitabu vyat zabuni na itaanza mwezi Julai, 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria hadi Bariadi, Mwanhuizi, Magu na Ngudu. Katika mwaka 2012/2013, taratibu za kumpata Mtaalam Mshauri atakayefanya upembuzi yakinifu, usanifu na uandaaji wa makabrasha ya zabuni kwa mradi wa kutoa maji kutoka Ziwa Victoria hadi Miji ya Bariadi, Mwanhuizi, Lagangabilili, Magu na Ngudu zinaendelea. Katika mwaka 2013/2014, upembuzi yakinifu, usanifu na uandaaji wa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya kutoa maji kutoka Ziwa Victoria na kuyafikisha katika Miji hiyo na Vijiji vilivyo jirani na bomba kuu utafanyika. Kazi hiyo itaanza mwezi Julai, 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji wa Chalinze. Katika mwaka 2012/2013, Serikali imeendelea na utekelezaji wa awamu ya pili ya mradi wa maji Chalinze, unaojumuisha usambazaji wa majisafi katika Vijiji 48 viliviyogawanywa katika makundi tisa ya utekelezaji. Mradi huo utakaonufaisha Wilaya tatu za Bagamoyo, Kibaha na Morogoro unatekelezwa na

24 APRILI, 2013

Serikali kwa kushirikiana na *BADEA*, Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China na Mfuko wa Pamoja wa Sekta ya Maji. Mradi huo utahudumia wakazi 109,648 katika Vijiji hivyo. Katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu itaendelea kutekeleza awamu hiyo ya mradi na utakamilika mwezi Agosti, 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2013/2014, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya India itaanza utekelezaji wa awamu ya tatu ya mradi Maji Chalinze. Kazi zitakazotekeliza ni pamoja na kupitia usanifu na kuanza ujenzi wa kuboresha chanzo cha maji kilichopo Mto Wami, upanuzi wa mtambo wa kusafisha maji, upanuzi wa mtandao wa majisafi na ujenzi wa matanki. Katika awamu ya pili, mradi utagharimu shilingi bilioni 51.3 na awamu ya tatu Dola za Marekani milioni 48.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Dharura kwa Jiji la Dar es Salaam. Katika mwaka 2012/2013, Serikali iliendelea kutekeleza Mpango wa Dharura wa Kuboresha Huduma ya maji katika Jiji la Dar es Salaam na Miji ya Kibaha na Bagamoyo. Madhumuni ya Mpango huo ni kuboresha huduma kwa kuongeza wingi wa maji kutoka lita milioni 300 za sasa hadi lita milioni 756 kwa siku, kuboresha usambazaji wa maji, kupunguza upotevu wa maji yasiyolipiwa, kuboresha utendaji wa *DAWASA* na *DAWASCO* kuongeza maduhuli; na kuongeza uwezo wa uondoshaji wa majitaka kutoka asilimia 10 za sasa hadi asilimia 30. Utekelezaji wa Mpango huo unalenga kukabiliana na changamoto zinazolikabili Jiji la Dar es Salaam zikiwa ni pamoja na uchakavu wa miundombinu ya majisafi na majitaka; kupungua kwa maji ya Mto Ruvu, hasa wakati wa kiangazi; ongezeko kubwa la idadi ya watu la asilimia 6 kwa mwaka ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 4.5 Miji ni kitaifa; ongezeko la makazi mapya katika maeneo yasiyopimwa; na ongezeko la shughuli za kiuchumi na kijamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2013/2014, Serikali itaendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali iliyopangwa katika mpango huo ulioanza rasmi mwezi Februari, 2011 na umepangwa kukamilika mwezi Desemba, 2014. Hadi sasa, miradi inayotekeliza ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Bwawa la Kidunda. Bwawa la Kidunda linatarajiwa kujengwa ili kuhakikisha kwamba maji katika mto Ruvu yanakuwepo kipindi chote cha mwaka na kuzalisha umeme wa megawati 20. Usanifu wa Bwawa umekamilika na vitabu nya zabuni viko tayari kwa ajili ya matangazo ya kumpata mkandarasi. Uendeshaji wa kituo cha umeme na usambazaji wake utatekelezwa na TANESCO chini ya makubaliano (*MoU*) yaliyosainiwa kati ya DAWASA na TANESCO tarehe 10/11/2012. Aidha, usanifu wa barabara ya kuingilia eneo la bwawa umekamilika kama ulivyopangwa na mtaalamu wa kufanya tathmini ya athari za kimazingira na kijamii (*ESIA*) amepatikana. Aidha, wananchi watakaoahamishwa kutoka maeneo yao ili kupisha ujenzi wa bwawa hilo watalipwa mwezi Mei 2013. Katika mwaka 2013/2014, ujenzi utaanza baada ya kulipa fidia pamoja na ujenzi wa barabara kwenda kwenye eneo la ujenzi wa bwawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, visima virefu nya Kimbiji na Mpera. Katika mwaka 2012/2013, mkandarasi wa kuchimba visima 20 katika maeneo ya Kimbiji na Mpera amepatikana na kazi ya uchimbaji itaanza mwezi Julai 2013 na itakamilika mwezi Julai 2014. Taarifa ya tathmini ya athari za kimazingira na kijamii (*ESIA*) iko katika hatua za mwisho. Uthamini wa maeneo yote ya mradi yenye ekari 7,300 umefikia shilingi bilioni 27. Aidha mkandarasi wa uchimbaji wa visima virefu vinane nya kukamilisha tathmini ya mwenendo wa maji ardhini alipatikana mwezi Septemba 2012. Uchimbaji umeanza mwezi huu wa Aprili 2013 na unatarajia kukamilika mwezi Desemba 2013. Makisio ya awali ni kupata maji lita milioni 260 kwa siku kutoka katika visima hivyo ifikapo mwaka 2014. Katika mwaka 2013/2014, Serikali itaendelea na uchimbaji wa visima 20, kazi ya kutathmini mwenendo wa maji ardhini na kulipa fidia kwa wananchi watakaoathirika na ujenzi wa mradi katika eneo la Kimbiji na Mpera.

Mheshimiwa Naibu Spika, upanuzi wa Mtambo wa Ruvu Juu. Usanifu wa mtambo wa Ruvu Juu na bomba kuu la kutoka mtamboni hadi Kibamba, pamoja na tenki jipyaa la Kibamba ulikamilika Novemba 2012. Taratibu za kumpata

msimamizi na mkandarasi wa ujenzi zitakamilika Juni 2013 na ujenzi utaanza Julai 2013. Upanuzi wa mtambo wa Ruvu Juu utaongeza uwezo wa mtambo kutoka lita milioni 82 kwa siku mpaka lita milioni 196 kwa siku ili kukabiliana na changamoto ya ukuaji wa kasi wa Miji ya Mlandizi, Kibaha na Jiji la Dar es Salaam. Katika mwaka 2013/2014, ujenzi wa mradi huo utaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, upanuzi wa Mradi wa Maji wa Ruvu Chini. Katika mwaka 2012/2013, Serikali kwa kushirikiana na *MCC*, iliendelea na upanuzi wa mradi wa maji wa Ruvu Chini. Hadi mwezi Machi 2013, utekelezaji umefikia asilimia 85 na utakamilika Julai 2013. Ujenzi wa bomba kuu la kusafirisha maji yatakayoongezeka kutokana na upanuzi wa mtambo Ruvu Chini hadi Jijini Dar es Salaam umeanza. Katika mwaka 2013/2014 ujenzi wa bomba kuu kutoka Ruvu chini utaendelea, lengo ni kukamilisha kazi hilo mwezi Februari 2014. Aidha, kazi ya ujenzi wa kingo za mto Ruvu katika eneo la Kidogozero unaendelea; hadi Machi 2013 kazi iliyokamilika ni asilimia 75, kazi hii itakamilika Agosti 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukarabati na upanuzi wa Mfumo wa Kusambaza Majisafi. Katika mwaka 2013/2014, Serikali itaanza kutekeleza mradi wa kujenga mfumo wa kusambaza maji katika maeneo ya Tegeta - Mpiji na Mpiji hadi Bagamoyo. Mradi huu ukikamilika jumla ya kilomita 732 za mabomba ya kusambaza maji yatalazwa, wateja 3,400 wataunganishwa na vioski 30 vitajengwa katika Bagamoyo na Tegeta. Vilevile, Serikali itaanza ujenzi wa mabomba na kuunganisha wateja maeneo ya Mbezi hadi Kiluvya. Mradi huo ukikamilika jumla ya kilomita 300 za mabomba ya kusambaza maji yatalazwa, wateja 10,000 wataunganishwa na vioski 30 vitajengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi mingine ya Kuboresha Huduma ya Maji Jijini Dar es Salaam. Katika mwaka 2012/2013, Wizara yangu kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Ubelgiji (*BTC*) na Umoja wa Nchi za Ulaya iliendelea na utekelezaji wa mradi wa kuboresha upatikanaji wa majisafi na usafi wa mazingira katika maeneo ya

Kibondemaji B, Mtoni Kijichi Misheni, Mbagala Kuu, Mgeninani, Mwanamtoti, Yombo-Dovya Msakala, Tandale, Kwembe, Tabata Darajani Kiswani, Kinyerezi, Minazi mirefu, Hondogo, Gongolamboto, Guluku Kwalala -Ulongoni, Kingugi, Mburahati- Barafu na Ugombolwa yaliyoko katika Manispaa za Temeke, Ilala na Kinondoni Jijini Dar es Salaam; kwa kujenga mifumo ya usambazaji maji kwenye maeneo yaliyochimbwa visima, vituo vya kuchotea maji na matanki ya kuhifadhi maji. Utekelezaji wa kazi ya kuboresha huduma ya maji umefikia asilimia 60 na ujenzi wa vyoo vya mfano katika maeneo ya shule, zahanati na masoko umefikia asilimia 85. Mradi huu umepangwa kukamilika ifikapo mwezi Juni 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia ziara ya Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Mei 2010 alipotembelea maeneo yenye kero ya huduma ya maji Jijini Dar es Salaam, aliagiza kuchimba visima virefu 27 ili kupunguza adha ya upatikanaji wa huduma ya maji kwenye maeneo hayo. Hadi kufikia mwezi Machi 2013, DAWASA imechimba visima virefu 33 (zaidi ya lengo la awali la visima 27) ambapo 15 vipo katika maeneo ya Mburahati National Housing, Shule ya Msingi Muungano, Kwa Shebe, Mavurunza, Malamba Mawili, Saranga, King'ongo na Kilungule katika Manispaa ya Kinondoni. Visima 14 vipo katika maeneo ya Keko Magurumbasi, Chang'ombe, Chang'ombe Toroli, Sandali, Sandali Mpogo, Sandali Mwembeladu, Mtoni, Mbagala, Kigamboni katika Manispaa ya Temeke. Visima vinne vipo katika maeneo ya Mongo la Ndege, Kipunguni, Mbondele na Mvuti katika Manispaa ya Ilala. Uchimbaji huo unaenda sambamba na utekelezaji wa Mpango wa dharura wa kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji katika Jiji la Dar es Salaam. Katika mwaka 2013/2014, Wizara itaendelea kutekeleza miradi ya namna hiyo ili kupunguza kero ya maji wakati wa kusubiri utekelezaji wa miradi mikubwa. Maeneo yatakayochimbwa visima hivyo ni Temeke, Kigamboni, Kiwalani, Vingunguti, Segerea, Kinyerezi, Goba, King'ongo, Msumi, Mbezi, Kerege, Kibaha na maeneo ya Kisarawe ya Kwala, Mtunani, Chole – Samvula na Yombo Lukinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Huduma ya Maji katika Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Kitaifa. Miradi ya Maji katika Miji ya Ikwiriri, Kibaigwa, Kilosa, Turiani, Mvomero, Kibiti, Gairo na Kisarawe. Katika mwaka 2012/2013, Wizara yangu imeendelea na ujenzi wa miradi ya maji katika Miji sita ya Ikwiriri, Kibaigwa, Kilosa, Turiani, Mvomero na Gairo ili kukidhi mahitaji ya wakazi wa Miji hiyo. Hadi kufikia mwezi Machi 2013, ujenzi wa miradi ya maji katika Miji hiyo upo katika hatua zifuatazo; Ikwiriri (95%), Kibiti (100%), Kibaigwa (85%), Gairo (86%), Turiani (77%), Kilosa (79%) na Mvomero (81%). Miradi hii inatarajiwa kukamilika katika kipindi cha 2013/2014. Katika Mji wa Kisarawe, mabomba ya kusambaza maji yamelazwa na uchimbaji wa visima virefu utaanza mwezi Mei 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi ya Maji Masasi/Nachingwea na Bunda. Katika mwaka 2012/2013, miradi ya kuboresha huduma za maji katika Miji ya Masasi, Nachingwea imetekelozwa. Utekelezaji huo umefikia asilimia 97. Katika mwaka 2013/2014, kazi ya kuunganisha Vijiji vinne vya Likwachu, Chinongwe, Litama na Chiumbati Shulen katika Wilaya ya Nachingwea itafanyika. Katika mji wa Bunda, kazi ya kulaza bomba lenye urefu wa kilomita 23.5 kutoka kwenye chanzo hadi kwenye matanki iliendelea katika mwaka 2012/2013. Katika mwaka 2013/2014, Serikali imetenga shilingi milioni 800 ili kukamilisha ujenzi wa mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji Orkesumet. Katika mwaka 2012/2013, utekelezaji wa mradi wa dharura mjini Orkesumet umekamilika, ambako kwa hivi sasa uzalishaji ni lita 144,000 kwa siku. Vilevile, vituo 13 vya kuchotea maji vilijengwa. Mahitaji kwa mji huo hivi sasa inakadiriwa kuwa lita 720,000 kwa siku. Ili kukabiliana na upungufu wa maji uliopo, Serikali imetafuta fedha kugharamia mradi katika mji huo. Mradi wa kukidhi mahitaji ya muda mrefu ya wakazi wa mji wa Orkesumet utatekelezwa kwa ushirikiano wa Serikali, *BADEA* na *OFID*. Mtaalam Mshauri atakayesanifu na kuandaa makabrasha ya zabuni ataanza kazi mwezi Mei 2013. Kazi ya kupitia usanifu wa mradi (*review*) itaanza baada ya *BADEA* kutoa kibali na itakamilika kwa kipindi cha miezi

mitatu. Wizara yangu itatangaza zabuni ya awali (*pre qualification notice*) ya kupata wazabuni wa ujenzi wenye uwezo pindi mkataba wa fedha utakaposainiwa kati ya Serikali na *BADEA/OFID*. Katika mwaka 2013/2014, ujenzi wa mradi huo utaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Uboreshaji wa Huduma ya Majisafi Muheza. Katika mwaka 2012/2013, Serikali imetuma shilingi milioni 100 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa dharura wa maji katika mji wa Muheza. Kazi zilizopangwa ni ununuzi wa pampu na matanki mawili ya lita 10,000 kila moja, ulazaji wa bomba la urefu mita 150, kujenga nyumba ya mtambo na kuunganisha umeme kwenye chanzo. Kazi zilizofanyika hadi Machi 2013 ni ujenzi wa nyumba ya mtambo, ununuzi wa pampu na kuifunga, ufungaji wa umeme jua, kulaza bomba kuu, kununua na kufunga matanki mawili kila moja lita 10,000 pamoja na kuchimba mtaro wa urefu wa mita 400. Kazi zitakazofanyika katika mwaka 2013/2014 ni kujenga mtandao wa kusambaza maji na vioski vya kuchotea maji. Kiasi cha shilingi milioni 300 zimetengwa kwa ajili ya mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Uboreshaji wa Huduma ya Majisafi Karatu. Katika mwaka 2012/2013, Serikali imetenga shilingi milioni 495 kwa ajili ya kuboresha huduma ya maji katika mji wa Karatu kama hatua za kutekeleza mradi wa dharura. Tayari kisima kirefu chenye kina cha mita 188 na uwezo wa kutoa maji lita 45,000 kwa saa kimechimbwa kwa gharama ya shilingi milioni 55. Serikali imejiandaa kuchimba visima vingine viwili, kujenga matanki ya kuhifadhi maji, kununua pampu na kujenga vioski kumi kwa ajili ya kupunguza kero ya maji katika mji huo. Kazi hiyo ikikamilika itaongeza upatikanaji wa maji kutoka lita 840,000 hadi lita 3,000,000 kwa siku, na kuboresha huduma ya maji kutoka asilimia 20 hadi asilimia 71.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuboresha huduma ya maji katika Miji Mikuu ya Wilaya na Miji Midogo kwa kukarabati na kupanua mifumo ya maji katika Miji hiyo. Katika mwaka 2013/2014, Serikali imetenga

24 APRILI, 2013

fedha kiasi cha shilingi bilioni 4.0 ili kuongeza upatikanaji wa maji kwa Miji ya Korogwe, Mafinga, Mwanga, Chunya, Karagwe, Makambako, Kibondo, Makete, Mahenge, Kilwa Masoko, Mvomero/Dakawa, Urambo, Nzega, Pangani, Sikonge, Kibaya, Ifakara, Ruangwa, Tunduma, Ilula, Katesh na Loliondo ikiwa ni hatua ya dharura ili kukamilisha miradi inayoendelea kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi ya Maji ya Kitaifa. Katika mwaka 2013/2014, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (*BADEA*) na Mfuko wa Maendeleo wa Saudia (*Saudi Fund for Development - SFD*) itaanza utekelezaji wa mradi wa majisafi wa Mugango/Kiabakari/Butiama. Mradi huo utagharimu Dola za Marekani milioni 30.69. Mradi huo utanufaisha wananchi 80,000 na kazi zitakazotekelawa zitahusu ujenzi wa chanzo, ujenzi wa mtambo wa kusafisha na kusukuma maji, kujenga matanki matatu, kulaza mabomba kutoka Mugango, Kiabakari, hadi Butiama urefu wa kilomita 32, kukarabati mitambo ya kusukuma maji ya Kiabakari na kulaza mabomba ya mtandao wa usambazaji maji Butiama hadi Bisalye. Usanifu utaanza Agosti, 2013 na ujenzi utaanza Machi, 2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na upungufu wa maji katika mradi wa kitaifa *HTM*; katika mwaka 2012/2013, Serikali imetuma shilingi milioni 73 kwa ajili ya ukarabati wa kituo cha kusukuma maji Segera; kununua na kufunga pampu katika kituo hicho. Ufungaji wa pampu hizo umeboresha upatikanaji wa maji kutoka saa sita mpaka saa nane kwa siku. Maeneo yatakayofaidika na uboreshaji huo ni Segera, Kabuku, Mgambo JKT, Mkata na Handeni mijini. Katika mwaka 2013/2014, Serikali itakarabati mifumo ya maji katika miradi ya kitaifa ya Wanging'ombe, Maswa, Handeni Trunk Main na Makonde. Kiasi cha shilingi milioni 400 kimetengwa kwa ajili ya kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuzijengeta uwezo Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini. Katika mwaka 2012/2013, Wizara yangu iliendelea kuzijengeta uwezo Mamlaka za maji za Miji Mikuu ya Mikoa, Miji Mikuu ya Wilaya, Miji

Midogo na miradi ya kitaifa ili ziongeze ufanisi katika utoaji wa huduma kwenye maeneo yao. Kazi zilizotekelawa ni pamoja na kuendelea na ujenzi wa ofisi ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira mjini Babati ambao umefikia asilimia 65 mwezi Machi 2013. Kuanza ujenzi wa ofisi katika Miji ya Wilaya ya Utete, Mpwapwa na mji mdogo wa Tunduma. Wizara yangu itaendelea kuziimarisha mamlaka za ngazi ya Mikoa, Wilaya, Miji Midogo na miradi ya kitaifa kwa kuzitengenezea mazingira mazuri ya kazi, katika kipindi cha mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwezi Februari 2013, Wizara yangu ilikuwa imechangia jumla ya shilingi milioni 500 katika gharama za uendeshaji wa miradi ya kitaifa kwa kulipia sehemu ya ankara za umeme wa mitambo ya kuzalisha maji. Katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu itaendelea kujengea uwezo miradi ya kitaifa na Mamlaka za daraja B na C ili hatimaye ziweze kujiendesha zenyewe na hivyo kuipunguzia Serikali mzigo wa kuchangia gharama za uendeshaji kwenye mamlaka zikiwemo gharama za umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara itaendelea kuwekeza katika miundombinu ya maji na kuzijengea uwezo Mamlaka za maji za ngazi ya Wilaya. Miji Midogo na miradi ya kitaifa ili kuongeza upatikanaji wa huduma ya majisafi katika maeneo ya Mamlaka hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi chini ya Wizara ya Maji. Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji. Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (*EWURA*) inatekeleza majukumu ya kudhibiti utoaji wa huduma kwenye sekta za umeme, mafuta ya petroli, gesi asilia, majisafi na majitaka nchini ikiwa chini ya Wizara yangu. Majukumu hayo ni pamoja na kutoa leseni, kusimamia utekelezaji wa masharti ya leseni, kudhibiti ubora na ufanisi wa utoaji huduma, kutathmini na kupitisha bei za huduma na kutatua migogoro. Kwa upande wa Sekta ya Maji, *EWURA* imeendelea na udhibiti wa huduma za maji zinazotolewa na Mamlaka za Maji 130 nchini. Kati ya Mamlaka hizo, 19 ni za Miji Mikuu ya Mikoa, 102 za Miji Mikuu ya Wilaya na Miji Midogo, *DAWASA*, *DAWASCO* na miradi saba ya kitaifa ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, *EWURA* ilichambua maombi ya leseni na kuzipatia leseni za kudumu Mamlaka za Maji 84 za Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na miradi ya kitaifa kwa ajili ya kutoa huduma ya majisafi na majitaka kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 17. Mamlaka hizo zilipatiwa leseni za daraja la C. Katika uchambuzi wa maombi ya leseni, imeonekana kuwa mamlaka nyingi za Miji ya Wilaya, Miji Midogo na miradi ya kitaifa zimeshindwa kupata leseni za daraja la B au A kutokana na kutokidhi vigezo vya kupanda daraja. Leseni zilizotolewa zitakuwa halali kwa kipindi cha miaka 10 na kwa mujibu wa leseni hizo, kila Mamlaka ya Maji inatakiwa iboreshe huduma zake ili ipande daraja ndani ya kipindi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, *EWURA* ilifanya mapitio ya mipango ya kibiashara (*Business Plans*) ya miaka mitatu iliyoadaliiwa na Mamlaka za Maji. Mipango ya kibiashara iliyopitiwa ni ya mamlaka za maji za Miji ya Mbeya, Arusha, Iringa, Singida, Tabora, Moshi, Tanga, Dodoma, Mwanza na Musoma. Mapitio ya mipango ya kibiashara ya Mamlaka hizo yamefanyika kwa kuzingatia mwongozo wa *EWURA* wa kutengeneza mipango ya kibiashara wa mwaka 2011. Mwongozo huo unalenga kuzifanya Mamlaka za maji ziwe endelevu kwa kutoa mwelekeo kwa kila Mamlaka ya Maji kuweza kukidhi gharama zote za uendeshaji na uwekezaji. Aidha, *EWURA* iliidhinisha bei mpya za maji kwa Mamlaka za Maji 8, ambazo ni Arusha, Tanga, Mbeya, Mtwara, Lindi, Mafinga, *Handeni Trunk Main (HTM)* na *DAWASA*. Bei zilizoidhinishwa zimelenga kuziwezesha Mamlaka hizo kutekeleza mipango yao ya kibiashara na kutoa huduma ilio bora zaidi na endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2012/2013, *EWURA* kwa ikishirikiana na Shirika la Maendeleo la Ujeruman (GIZ) iliboresha mfumo wa kompyuta wa taarifa za kila mwezi za utendaji wa mamlaka za maji nchini uitwao *Water Utilities Information System (Majls)*. Mfumo huo uliboreshwani ili ufanye kazi kwa kutumia teknolojia ya mtandao, yaani *Web Based*. Maboresho yaliyofanyika yameufanya mfumo huo kuwa salama zaidi kwa kupunguza

hatari ya kushambuliwa na virusi, kuwezesha kutumiwa na watumiaji wengi ndani ya Mamlaka moja na rahisi zaidi kutumia katika kuingiza takwimu na kuandaa taarifa. Mamlaka za maji za Miji ya Mikoa, DAWASA, DAWASCO na baadhi ya Mamlaka za Miji ya Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Kitaifa ya Mikumi, Kilosa, Gairo, HTM, Mugango-Kiabakari, Kibondo, Maswa, Ilula, Makambako, Mafinga, Kilolo, Tukuyu, Mbalizi, Chunya, Ilege, Namtumbo, Mbulu, Orkesumet, Magugu, Same, Dereda, Gapapo, Bashmet, Kibaya, Katesh, Loliondo na Usa River.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kusimamia utendaji wa Mamlaka za maji, EWURA ilikagua miundombinu na uendeshaji wa Mamlaka za maji 22 katika kipindi cha mwaka 2012/2013. Katika ukaguzi huo, EWURA ilifanya uhakiki wa taarifa na takwimu za utendaji zilizowasilishwa na Mamlaka hizo. Uhakiki huo ulihusu viwango vya uzalishaji maji kwa kukagua dira kubwa za maji, takwimu za ubora wa maji, taratibu za kushughulikia malalamiko ya wateja na utekelezaji wa maagizo ya EWURA. Mamlaka zilizokaguliwa ni Singida, Tabora, Shinyanga, Mwanza, Bukoba, Musoma, Kigoma, Tanga, Babati, Moshi, Mbulu, Same, DAWASA, Chalinze, Iringa, Mbeya, Sumbawanga, Morogoro, Dodoma, Lindi, Mtwara na Songea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, EWURA ilitathmini utendaji kazi wa Mamlaka za Maji zote nchini kwa kipindi cha mwaka 2011/2012. Tathmini hiyo ilibaini kuwa Mamlaka za Maji zimekuwa na mafanikio katika kuongeza kiwango cha uzalishaji maji, ufungaji wa dira za maji, idadi ya wateja wa majisafi na majitaka, ukusanyaji wa mapato na kuongeza ufanisi katika matumizi ya rasilimali watu. Pamoja na mafanikio hayo, imebainika kuwa ongezeko la kiasi cha maji yanayozalishwa ni kidogo ukilinganisha na ongezeko la mahitaji ya maji yaliyosababishwa na ongezeko la idadi ya watu na shughuli nyine za kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini hiyo pia ilibaini kuendelea kuwepo kwa upotevu wa maji unaozidi kiwango

24 APRILI, 2013

kinachokubalika kitaifa cha kutozidi asilimia 20, kupungua kwa saa za upatikanaji wa maji, uchakavu wa miundombinu na upungufu wa watumishi wenyewe sifa hasa kwa mamlaka za maji zinazotoa huduma katika Miji ya Wilaya, Miji Midogo na miradi ya kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, *EWURA* iliandaa Mwongozo wa Udhibiti wa Uendeshaji wa Visima Binafsi vya Maji na Mwongozo wa Udhibiti wa Biashara ya Maji kwa kutumia Magari Binafsi (*Water Tankers*) katika eneo linalosimamiwa na *DAWASA* kwa lengo la kudhibiti ubora na bei ya huduma ya maji inayotolewa na sekta binafsi. Miongozo hii imetayarishwa ili kuelekeza, kusimamia na kudhibiti shughuli za uendeshaji wa visima binafsi na magari binafsi katika eneo hilo ambapo huduma ya maji itolewayo na *DAWASCO* haikidhi mahitaji au haijafika. Aidha, rasimu ya kanuni zitakazotumika kudhibiti huduma hizo zitolewazo na sekta binafsi kwa ajili ya Dar es Salaam na kwa ajili ya mamlaka zote za maji zimeandaliwa. Aidha, matayarisho kwa ajili ya kudhibiti sekta binafsi ya maji kwa Jiji la Dar es Salaam yameshaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, *EWURA* iliendelea kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko ya wateja wa mamlaka za maji walioyawasilisha *EWURA*. Malalamiko yaliyowasilishwa yanahusu ankara za majisafi na majitaka zisizo sahihi, ukosefu wa maji, kukatiwa huduma ya maji kimakosa na udhaifu wa huduma kwa wateja. Katika kipindi hicho jumla ya malalamiko 19 yaliwasilishwa *EWURA* ambapo kati ya hayo malalamiko manne yamepatiwa ufumbuzi wakati malalamiko 15 yaliyobaki yako katika hatua tofauti za utatuza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2013/2014, *EWURA* itaendelea kuimarisha udhibiti wa huduma ya maji itolewayo na mamlaka za maji hapa nchini kwa kuzingatia vipaumbele muhimu kama ifuatavyo:-

(i) Kufuatilia utendaji wa mamlaka za maji nchini kwa kuchambua na kuhakiki taarifa za utendaji na kufanya ukaguzi wa miundombinu na utendaji wa mamlaka za maji;

(ii) Kuhakikisha kuwa mamlaka za maji zinaandaa na kutekeleza mipango yao ya kibashara (*Business Plans*) kwa kuzingatia mwongozo uliotolewa na *EWURA*;

(iii) Kuendeleza uwekezaji katika sekta ya maji kwa kuziwezesha mamlaka za maji kupata fedha kwa ajili ya kujenga miradi mipya, kuibua vyanzo vipyta vya maji na kukarabati miundombinu iliyopo;

(iv) Kufuatilia udhibiti wa huduma za maji zinazotolewa na sekta binafsi kuititia visima na magari binafsi kwa Jiji la Dar es Salaam na Mikoa mingine;

(v) Kutoa elimu kwa umma kuhusu haki na wajibu wao katika kufanikisha utoaji bora wa huduma ya maji; na

(vi) Kuhimiza mamlaka za maji kuboresha ukusanyaji wa mapato yatokanayo na ankara za maji; kubainisha na kutatua sababu za upotevu wa maji, kuanzisha na kupanua mifumo ya majitaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Maendeleo na Usimamizi wa Maji. Chuo cha Maendeleo na Usimamizi wa Maji, kiliendelea na jukumu lake la kujenga uwezo wa kitaalam wa fani za ufundi zinazohitajika katika utoaji wa huduma za maji na usimamizi wa rasilimali za maji. Katika mwaka 2012/2013 chuo kilidahili wanafunzi 358 na kukifanya kuwa na jumla ya wanafunzi 757 wa stashahada (*water technicians*). Jumla ya wanafunzi 91 walihitimu mafunzo yao katika fani mbalimbali kama ifuatavyo: katika fani ya uhandisi wa mifumo ya ugavi wa maji safi na usafi wa mazingira (*water supply and sanitation*) (47), utafutaji wa maji ardhini na uchimbaji wa visima vya maji (*hydrogeology and water well drilling*) (13), Haidrolojia (2), na Teknolojia ya maabara za uchunguzi wa ubora wa maji (*water quality laboratory technology*) (29). Aidha, Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) ilifadhili wanafunzi wa kike (34) katika kozi ya kuwawezesha kujunga na masomo ya stashahada (*Access Course*). Hii imewezesha kuongeza udahili wa wanafunzi wa kike kutoka

29 mwaka 2011/2012 hadi 67 katika mwaka 2012/2013. Vilevile washiriki 136 walipewa mafunzo ya muda mfupi katika fani mbalimbali zinazohusu sekta ya maji. Ushauri juu ya ubora wa maji kwa wateja 54 waliowasilisha sampuli zao ultolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha utoaji wa elimu chuoni, Wizara yangu ilikamilisha mchakato wa upatikanaji wa ithibati (*accreditation*) na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundı (*NACTE*) lilitoa ithibati hiyo tarehe 01 Oktoba, 2012. Ithibati hiyo inakiwezesha chuo kuanza kutoa mafunzo ya shahada ya kwanza ya Uhandisi wa Rasilimali za Maji na Umwagiliaji (*Bachelor of Engineering in Water Resources and Irrigation*). Pamoja na uboreshaji huo, Serikali kwa kushirikiana na GIZ imeandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi kwa ajili ya upanuzi wa Chuo (*Land Use Master Plan*). Katika kukabiliana na upungufu wa watumishi, Chuo kiliajiri watumishi 17.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha utoaji wa huduma, Chuo kilifanya ukarabati wa darasa la kompyuta na ofisi (5). Pia, ununuzi wa samani mbalimbali za ofisi, maabara, zahanati, na madarasa ulifanyika. Vilevile, ununuzi wa *fax machine* (1), kompyuta (100), *Photocopier* (2), *printer* (2), *projector* (3), vitanda (122), magodoro (60), madawati (191) na jenereta moja ya *KVA* 250 ulifanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2013/2014, Chuo kitatoa mafunzo katika ngazi ya stashahada (*Water Technician*) kwa wanafunzi 1,056, sambamba na kuanzisha mafunzo ngazi ya shahada kwa wanafunzi 40. Mafunzo ya muda mfupi kwa washiriki 500 yatasolewa. Pia ujenzi wa jengo la ghorofa sita lenye madarasa, maabara, kumbi za mikutano na maktaba, pamoja na ukarabati wa majengo ya chuo utafanyika. Chuo kitanunua vifaa vya Haidrolojia, Upimaji wa maji ardhini na uchimbaji visima, upimaji wa udongo, uchunguzi wa ubora wa maji, na hali ya hewa. Katika kuboresha utoaji wa elimu, Chuo kitaajiri watumishi 26 wa kada mbalimbali na kuwaendeleza watumishi waliopo kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Uchimbaji wa Visima na Ujenzi wa Mabwawa. Katika mwaka 2012/2013, Wakala wa Uchimbaji wa Visima na Ujenzi wa Mabwawa (*DDCA*) ulichimba visima virefu 162 hadi Machi 2013 na visima 300 vinatarajiwa kuchimbwa nchini kote ifikapo Juni 2013. Wakala umekamilisha ujenzi wa Bwawa la Misozwe liliopo katika Wilaya ya Muheza. Aidha, uchunguzi wa maji chini ya ardhi kwa ajili ya uchimbaji visima virefu umefanyika katika maeneo 185 na ifikapo Juni 2013 maeneo 265 yatakuwa yamechunguzwa. Vilevile, ujenzi wa mabwawa matatu ya Mwavi (Bagamoyo), Norband na Maole (Mkomazi- Same) umekamilika. Katika kuendelea kuujengea uwezo Wakala, Serikali imeupatia mitambo minane kwa ajili ya shughuli za uchimbaji visima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala ulifanya uchunguzi wa udongo katika mradi wa ujenzi wa kiwanda cha sementi Lindi. Aidha, Wakala umejenga matanki ya kuhifadhi maji na kuweka pampu za kusukuma maji katika Hospitali ya *St. Francis* iliyopo Ifakara, Morogoro. Ifikapo Juni 2013, Wakala utakamilisha ujenzi wa tanki la kuhifadhi maji *NHC - Kibada Kigamboni* na kukarabati mabwawa matatu katika Wilaya ya Monduli.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana wakati nawasilisha makadirio ya Wizara yangu nililiarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wakala ingenunua mitambo minne na vifaa vyake (*Drilling rigs and accessories*) kwa ajili ya uchimbaji wa visima na uchunguzi wa maji chini ya ardhi. Vifaa hivyo havikununuliwa kutokana na kuchelewa kusainiwa kwa mkataba wa fedha kati ya Serikali ya Tanzania na *NORAD*. Katika mwaka 2013/2014 Wakala utanunua vifaa hivyo baada ya taratibu hizo kukamilika. Vifaa hivyo vikipatikana Wakala utakuwa na uwezo wa kuchimba visima virefu 450 kwa mwaka. Vilevile, Wakala itakuwa na uwezo wa kufanya utafiti wa maji katika maeneo 300, kujenga bwawa moja, usanifu wa maeneo manne kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa na uchunguzi wa udongo kwa shughuli mbalimbali. Serikali kwa kushirikiana na *JICA* itaujengea uwezo Wakala ili uweze kuboresha utoaji wa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bohari Kuu ya Maji. Katika mwaka 2012/2013, Bohari Kuu ya Maji iliendelea kutekeleza majukumu yake ya kununua, kuhifadhi na kusambaza vifaa na dawa za kusafisha na kutibu maji pamoja na kuendelea na taratibu za kuibadili Bohari hiyo kuwa Wakala wa Serikali. Bohari Kuu ya Maji imeweza kusambaza vifaa mbalimbali vya maji ikiwa ni pamoja na pampu za maji na viungio vya mabomba katika Halmashauri na Mamlaka za maji mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu itaendelea na taratibu za kuibadili Bohari hiyo kuwa Wakala wa Serikali. Lengo ni kuiboresha ili iweze kutoa mchango mkubwa zaidi katika upatikanaji na usambazaji wa vifaa vya miradi ya maji. Aidha, Bohari itakamilisha ujenzi wa uzio na itaanza ukarabati wa baadhi ya maghala (*godowns*).

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala mtambuka. Sheria. Katika mwaka 2012/2013, Wizara iliendelea kutoa elimu na ushauri wa kisheria kuhusu utekelezaji wa sheria na hatua za kuchukua dhidi ya ukiukwaji wa Sheria za Maji. Elimu na ushauri umetolewa kwenye Halmashauri, Ofisi za Maji za Mabonde, Mamlaka za maji na wadau wengine wa sekta ya maji pamoja na jamii kwa ujumla kupitia warsha, mikutano, makongamano na mafunzo maalum. Aidha, nakala 840 za Sheria za Maji na Kanuni zake zimesambazwa kwa wadau. Vilevile kazi ya kutafsiri Sheria za Maji kwa lugha ya Kiswahili inaendelea ambapo maoni ya wadau yamekusanywa na maboresho yanaendelea kufanyika kabla ya kuwasilishwa kwenye Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi nyingine zilizofanyika katika mwaka 2012/2013 ni pamoja na kukamilisha kanuni saba, oda na notisi nne za kisheria ambazo kwa sasa zipo katika hatua ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. Kanuni hizo ni:-

- (i) Oda ya kutangaza Bonde la Makutupora

(Dodoma) kuwa eneo tengefu la hifadhi ya maji (*Declaration of Makutupora groundwater controlled area*) Order, 2012;

(ii) Oda ya kutangaza Bwawa la Kawa (Nkasi) kuwa eneo la hifadhi ya vyanzo vya maji (*Prohibition of Human activities beyond sixty metres at Kawa Dam*) Order, 2012;

(iii) Notisi ya kutangaza wajumbe watatu wa Bodii ya Maji ya Taifa (*Appointment the National Water Board Members*) Notice, 2012;

(iv) Kanuni za Usimamizi wa Maji chini ya Ardhi (*Ground Water (Exploration and Drilling) Licensing Regulations* 2013);

(v) Kanuni za Mfuko wa Uwekezaji wa Maji wa Taifa (*The National Water Investment Fund*) Regulations 2013;

(vi) Kanuni za Usalama wa Mabwawa (*Dam Safety*) Regulation, 2013;

(vii) Kanuni ya Usambazaji wa Maji (*The Water Supply*) Regulations, 2013;

(viii) Kanuni za Uteuzi na Ukomo wa Wajumbe wa Baraza la Ushauri la Watumiaji. *Ewura* (*Appointment and Tenure of EWURA CCC Members*) Regulations 2013;

(ix) Kanuni za Uteuzi na Sifa za Wajumbe wa Bodii ya Ewura. *Ewura* (*Appointment and Qualifications of Board Members*) Regulations, 2013;

(x) Kanuni za Uteuzi na Ukomo wa Wajumbe wa Baraza la Ushauri wa Serikali. *Ewura* (*Appointment and Tenure of GCC Members*) Regulations 2013; na

(xi) Notisi ya kutangaza Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira ya Masasi-Nachingwea (*Masasi-Nachingwea Water Supply and Sanitation Authority*) Notice, 2013.

24 APRILI, 2013

Mheshimiwa Naibu Spika, rasimu ya marekebisho (*amendment*) ya Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (*DAWASA*) Na. 20 ya mwaka 2001 ilitayarishwa na maoni ya wadau yalikusanywa na kufanyiwa kazi na sasa iko kwenye hatua ya kuwasilishwa kwenye Baraza la Mawaziri kabla ya kuwasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara itaendelea kutoa ushauri wa kisheria kuhusu utekelezaji wa sheria za maji na kuendelea kutayarisha kanuni nne za sheria za maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Maji. Wakati nikihitimisha Hotuba ya Bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2012/2013, nilieleza mpango wa Serikali wa kuanzisha Mfuko wa Maji ili kuongeza fedha za uwekezaji katika Sekta ya Maji. Sheria Namba 12 ya mwaka 2009 ya Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira, imetamka uanzishaji wa Mfuko wa Taifa wa Uwekezaji wa Maji (*National Water Investment Fund*) na kubaini vyanzo vya mapato ikiwa ni mchango wa Serikali Kuu na Washirika wa Maendeleo. Aidha, Serikali itaendelea kuutunisha Mfuko huo kwa kubaini vyanzo vingine vya mapato ikiwa ni pamoja na ada na tozo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kufikia azma hiyo, Wizara yangu imeandaa Kanuni za uendeshaji wa Mfuko wa Maji (*National Water Investment Fund Regulations, 2013*) ambazo ziko mbioni kuchapishwa kwenye Gazeti la Serikali na kuanza kutumika. Katika bajeti ya mwaka 2013/2014 shilingi 100,000,000 zimetengwa kama kianzio (*seed money*) cha Mfuko huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Habari, Elimu na Mawasiliano. Katika mwaka 2012/2013, Wizara iliendelea kutoa elimu na taarifa mbalimbali kwa wananchi kuititia tovuti na vyombo mbalimbali vya habari. Wizara yangu ilishiriki kikamilifu katika maonesho ya Kilimo ya Nanenane mwaka 2012 yaliyofanyika Nzuguni Mjini Dodoma ambapo jumla ya vipeperushi 4,000 vilivyo husu hatua mbalimbali na mafanikio yaliyopatikana katika kuwapatia wananchi huduma ya maji vilitolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, machapisho 3,000 na vipindi sita vya redio na televisheni vilitolewa katika maadhimisho ya Wiki ya Maji ambayo kwa mwaka huu yalifanyika kitaifa Mkoani Lindi, vipindi hivyo vililenga katika kufafanua na kuelimisha masuala mbalimbali ya Sekta ya Maji. Makala ya filamu (*documentary film*) ya mafanikio ya Sekta ya Maji katika kipindi cha miaka mitano ya awamu ya nne ililandaliwa na kurushwa. Kwa ujumla, makala 15 ziliandikwa na kutolewa magazetini na kwenye mitandao ya kijamii ya mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu itaendelea kuelimisha wananchi na kutoa taarifa mbalimbali zinazohusu Sekta ya Maji kwa kufufua Jarida la Maji Yetu; kuandaa na kutangaza vipindi katika luninga na redio na kuboresha tovuti ya Wizara ili wananchi wengi zaidi waitumie.

Mheshimiwa Naibu Spika, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano. Wizara yangu imeendelea kuboresha mfumo wake wa utendaji na utoaji wa huduma kwa kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA). Katika mwaka 2012/2013, upatikanaji wa taarifa na takwimu za utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji kwa njia ya mfumo wa kielektroniki (*Water Sector Management Information System*) umeboreshwa. Vilevile, Wizara imejenga uwezo wa matumizi ya mfumo huo ambapo hivi sasa taarifa za utekelezaji wa mikataba na matumizi ya fedha za Programu zinatumwa Wizarani kutoka kwa watekelezaji kupitia mfumo wa kieletroniki. Jumla ya watumishi 525 walipata mafunzo kuhusu mfumo huo katika ngazi zote. Aidha, watumishi watano wa Wizara walipata mafunzo ya kitaalam kuhusu TEHAMA.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inaboresha mtandao wa mawasiliano katika Ofisi zake za Makao Makuu Ubungo kwa kuunganishwa na Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano (*National Fibre Optic Cable*). Aidha, kazi nyiningine inayofanyika katika kipindi hiki ni uchambuzi wa kina, kutathmini hali halisi ya upatikanaji wa maji Vijijini baada ya kazi ya ukusanyaji wa takwimu na utayarishaji wa ramani za

vituo vya kuchotea maji (*Water Point Mapping*) kwa kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano inayojulikana kama "*Geography Information System – GIS*" kukamilika katika Halmashauri zote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2013/2014, kazi zifuatazo zitatekelezwa:-

- (i) Kupanua mfumo wa kielektroniki wa takwimu na taarifa ili kusaidia masuala ya ufuatilaji na tathmini ya utekelezaji wa mipango na miradi kwenye sekta ya maji (*scaling up/out MIS to cover other M&E functions – physical aspects*). Mafunzo yatatolewa kwa watumiaji;
- (ii) Utekelezaji wa Mfumo wa kielektroniki wa utunzaji na menejimenti ya nyaraka na kumbukumbu (*electronic documents & records management system*);
- (iii) Utekelezaji wa matumizi ya mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji wa takwimu na utayarishaji wa ramani za vituo vya kuchotea maji Vijijini. Vifaa vya kisasa vitanunuliwa na mafunzo yatatolewa; na
- (iv) Kuendeleza juhudzi za Serikali za utekelezaji wa Serikali Mtandao (*e-Government*) kwa kushirikiana na Wakala ya Serikali Mtandao (*e-Government Agency*). Hii itahusisha kujenga uwezo wa Wizara na Taasisi katika matumizi ya Serikali Mtandao ili kuboresha huduma ndani ya Sekta ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jinsia. Wizara yangu imeendelea kutekeleza Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002 na Sheria za Maji za mwaka 2009 kwa kuhamasisha uwepo wa uwiano wa kijinsia baina ya wanawake na wanaume kwenye vyombo vya kusimamia Sekta ya Maji. Vyombo hivyo vina maamuzi makubwa katika usimamizi na matumizi ya maji katika maeneo yao. Asilimia ya wanawake katika vyombo hivyo ni kama ifuatavyo: Wizara (asilimia 33), Bodi ya Taifa ya Maji (asilimia 33), Bodi za Mabonde ya Maji (asilimia 35), Bodi za Mamlaka za Maji (asilimia 33) na Bodi za Wakala (asilimia 50). Katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu

itaendelea kutoa fursa za uwiano kwa jinsia zote katika ngazi za maamuzi na uongozi. Aidha, jamii itaendelea kuhamasishwa kusajili jumuiya za watumiaji maji na kupewa mafunzo ya usimamizi wa utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, ambayo yatawashirikisha wanaume na wanawake katika jumuiya zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vita Dhidi ya Rushwa. Katika mwaka 2012/2013, Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ilitoa mafunzo ya maadili kwa maafisa wakuu wa Wizara yaliyolenga kusisitiza umuhimu wa watumishi kuzingatia maadili. Katika mwaka 2013/2014, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma itatoa mafunzo ya maadili kwa watumishi wengine wa Wizara yatakayolenga kusisitiza umuhimu wa watumishi kuzingatia maadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara yangu imeendelea na Mpango wa kutekeleza shughuli zake kwa uwazi (*Open Government Partnership – OGP*) kwa kuweka taarifa ya mpango wa kati wa mapato na matumizi (*MTEF*) na taarifa ya fedha ya mwaka 2012/2013 kwenye tovuti ya wizara, kuboresha mfumo wa upokeaji malalamiko kutoka kwa wadau wa sekta ya maji kwenye tovuti ya Wizara. Watumishi wa Ofisi ya Bonde la Wami – Ruvu na Maafisa Mahusiano wa Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira Miji ni wamepatiwa mafunzo juu ya utendaji na utekelezaji wa *OGP*. Katika mwaka 2013/2014, Wizara itaendelea na utoaji wa elimu juu ya *OGP* katika Ofisi za Mabonde.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imefungua Dawati la Malalamiko linaloshughulikia malalamiko ya wadau mbalimbali wa Sekta ya Maji na ya watumishi. Kwa mwaka 2012/2013, Dawati hili limeshughulikia malalamiko yapatayo 59 na kuyapatia ufumbuzi. Malalamiko hayo yalihusu utoaji wa huduma za maji kwa wananchi. Dawati litaendelea kupokea na kujibu hoja na malalamiko ya wadau kadri yatakavyojitekeza.

24 APRILI, 2013

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma itaendelea kutoa mafunzo kwa watumishi wa ngazi zote wa Wizara kuhusu namna ya kuwasilisha malalamiko yao kwenye ofisi ya malalamiko iliyoanzishwa na Wizara. Wizara itaendelea kuwakumbusha watendaji na watumishi wote kwa ujumla kufanya kazi kwa bidii kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, UKIMWI. Katika mwaka 2012/2013, Wizara imeendelea kuwapa elimu ya kujikinga dhidi ya Virusi Vya Ukimwi kwa watumishi wa Sekta ya Maji kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na vipeperushi na machapisho. Aidha, Wizara yangu imeendelea kugharamia lishe kwa watumishi tisa walijiweka wazi kwa mwajiri kuwa wanaishi na VVU. Kwa sasa Wizara ipo kwenye maandalizi ya kufanya tathmini ya masuala ya Ukimwi kwa Watumishi wote katika Sekta ya Maji (*Situation Analysis*). Tathmini hiyo, itatumika kuandaa mpango mkakati (*Strategic Action Plan*) ambao utatokana na mapendekezo yaliyojitekeza na hali halisi kama ambavyo tathimini itabainisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maendeleo ya Watumishi. Wizara yangu imeendelea na jitihada za kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi kwa lengo la kuongeza ufanisi na usimamizi wa mipango ya kisekta. Watumishi 100 wa kada mbalimbali wanatarajija kupandishwa vyeo katika nafasi mbalimbali. Katika mwaka 2012/2013, Wizara imepewa kibali cha kuajiri watumishi 63 na ajira mbadala 33 za wataalam wa kada mbalimbali. Hadi kufikia mwezi Machi 2013, Wizara imepokea watumishi 12 kutoka Sekretarieti ya Ajira. Kati ya hao, wahaidrojiolojia wawili, wahandisi wawili, mchumi mmoja, afisa maendeleo ya jamii mmoja, maafisa habari watatu, mhasibu mmoja, opareta wa kompyuta mmoja na mkaguzi wa ndani mmoja. Wizara bado inaendelea kufuatilia upatikanaji wa wataalam 63 wa ajira mpya watakaojaza nafasi za Kada mbalimbali na nafasi 21 za ajira mbadala kwa ajili ya kujaza nafasi wazi za kada mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013,

Wizara kwa kushirikiana na taasisi zinazotekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, inaendelea kutekeleza mpango wa kuwajengea uwezo watumishi (*capacity development plan*). Hadi sasa, watumishi 47 wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu na 389 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi. Katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu itaendelea kutekeleza mpango wa kuwapatia watumishi mafunzo ambapo watumishi 20 watapatiwa mafunzo ya shahada/stashahada ya uzamili yatakayowawezesha kukidhi sifa za miundo ya kada mbalimbali za utumishi. Aidha watumishi 150 watapatiwa mafunzo ya muda mfupi yatakayohusu, huduma bora kwa mteja, stadi za mawasiliano, matumizi sahihi ya teknolojia ya habari na mawasiliano pamoja na mfumo wa kupima utendaji kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuititia mradi wa kujenga uwezo wa sekta unaotekeliza na Serikali kwa kushirikiana na JICA; Jumla ya watumishi 26 walipatiwa mafunzo ya aina mbalimbali. Watumishi 19 kutoka Bodi za Maji za Mabonde ya Ziwa Tanganyika, Ziwa Victoria, Rukwa na Bonde la Kati; pamoja na watumishi saba kutoka katika Timu za Maji na Usafi wa Mazingira katika Halmashauri za Singida, Mwanza na Tabora. Kwa mwaka 2013/2014, Wizara itaendelea kuwapatia mafunzo watumishi na wadau wengi zaidi katika kutekeleza mpango wa kuwajengea uwezo watumishi (*Capacity Development Plans*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Uratibu wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji. Katika kutekeleza Sera ya Maji ya mwaka 2002, Serikali inatekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (*Water Sector Development Programme 2006 - 2025*). Programu hiyo ina programu ndogo nne ambazo ni: Programu ya kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji inayotekeliza katika mabonde tisa ya maji nchini; Programu ya maji na usafi wa mazingira Vijiji inayotekeliza katika halmashauri zote nchini; Programu ya majisafi na uondoshaji wa majitaka Miji ni inayotekeliza katika Mamlaka za Maji za Miji Mikuu ya Mikoa 19, DAWASA, Mamlaka 109 za Miji Mikuu ya Wilaya na Miji Midogo na miradi ya maji ya kitaifa; na Programu ya kujenga uwezo

kiutendaji na kuimarisha taasisi za sekta ya maji. Programu hiyo inatekelezwa kwa awamu za miaka mitano mitano kuanzia mwaka 2007/2008. Awamu ya kwanza ya miaka mitano ya utekelezaji ilianza mwezi Julai, 2007 na ilipangwa kukamilika mwezi Juni 2012. Ili kukamilisha miradi mingi, Serikali kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo iliamua kuongeza muda wa utekelezaji wa awamu ya kwanza kutoka Juni, 2012 hadi Juni, 2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwa na utekelezaji wenye ufanisi wa Programu, Wizara yangu imekuwa inaratibu mikutano ya majadiliano kati ya Serikali, Washirika wa Maendeleo na Mashirika yasiyo ya Kiserikali yanayohusiana na Sekta ya Maji. Lengo la mikutano hiyo ni kupitia, kukubaliana na kutolea maamuzi masuala mbalimbali yanayohusu utekelezaji wa Programu kama vile, mipango ya upatikanaji wa fedha na bajeti za miradi ya maji na usafi wa mazingira; na kuzijadili changamoto mbalimbali zinazoikabili Programu na kuzitafutia suluhisho. Katika mwaka 2013/2014, Wizara itaweka juhudu katika majadiliano hayo ili yawe na matokeo chanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maandalizi ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji Awamu ya Pili. Mtaalam Mshauri anayetathmini utekelezaji wa awamu ya kwanza, anaendelea na kazi ambapo tathmini hiyo itahusisha wadau wote wa sekta ya maji ambao watatoa maoni na ushauri wao utakaotumika kuboresha utekelezaji wa awamu ya pili ya Programu. Matayarisho ya awamu ya pili yanaendelea ambapo mapendekezo ya muundo wa awamu hiyo yatakamilika mwezi Juni, 2013. Katika awamu hiyo, Serikali itaweka kipaumbele katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoa na:-

(i) Kukamilisha miradi iliyoanza kutekelezwa katika awamu ya kwanza ikiwemo, miradi ya majisafi na usafi wa mazingira unao tekelezwa na kila Halmashauri na kubaini Vijiji vyia ziada ili vipatiwe maji;

(ii) Kukamilisha Mpango wa dharura wa maji

katika Jiji la Dar es Salaam, kuendelea kutafuta vyanzo vipyta  
vya maji kukidhi mahitaji makubwa ya maji na kuboresha  
huduma za majitaka Jijini;

(iii) Ujenzi wa miradi ya maji Miji Mikuu ya Wilaya  
na Miji Midogo na kuendelea kuboresha huduma za maji  
katika Miji Mikuu ya Mikoa kukidhi mahitaji yanayoongezeka  
kwa haraka; na

(iv) Kuanza utekelezaji wa mipango shirkishi ya  
usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji na ujenzi wa  
mabwawa makubwa na uchimbaji wa visima katika kukidhi  
mahitaji ya maji kwa sekta mbalimbali ya kijamii na kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza bajeti ya  
2012/2013, Wizara ilikabiliana na changamoto mbalimbali  
wakati wa utekelezaji. Changamoto zillizojitekeza na hatua  
zinazochukuliwa kuzikabili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuongezeka kwa idadi ya  
watu na shughuli za kiuchumi na kijamii. Utoaji wa huduma  
ya maji unakabiliwa na changamoto ya kuongezeka kwa  
idadi ya watu kusikoendana na uwekezaji. Hali hiyo ni dhahiri  
katika maeneo ya Miji ni ambapo kiwango cha ongezeko  
watu kwa mwaka ni asilimia 4.5 tofauti na maeneo ya Vijijini  
ambapo wastani wa ongezeko la watu kwa mwaka kitaifa  
ni asilimia 2.3. Mathalan, Jiji la Dar es Salaam linakabiliwa na  
uhaba mkubwa wa maji kutokana na ongezeko kubwa la  
watu la asilimia 5.5 kwa mwaka tofauti na wastani kitaifa  
wa asilimia 4.5. Ongezeko jingine ni kukua kwa shughuli za  
kiuchumi ikiwa ni pamoja na ongezeko kubwa la viwanda  
na kupanuka kwa ujenzi wa makazi. Kutokana na ukuaji huo  
wa kasi, Serikali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali  
ikiwa ni pamoja na:-

(i) Kushirikisha wananchi hususan katika maeneo  
ya Vijijini katika hatua zote za miradi ikiwa ni pamoja na  
kubuni, kujenga, kusimamia, kuendesha na kuchangia  
gharama za uendeshaji; na

(ii) Kukarabati na kujenga miradi ya kipaumbele ambayo inatoa huduma kwa wananchi wengi zaidi ikiwa ni pamoja na ujenzi wa mradi wa maji wa Vijiji 10 kwa kila Halmashauri; Mradi wa dharura wa kuboresha huduma za maji Jijini Dar es Salaam ikiwa ni pamoja na kujenga bwawa la Kidunda na kuchimba visima vya maji vya Mpera na Kimbiji, kujenga Mradi wa Maji wa Mwanga-Same-Korogwe, kujenga Bwawa la Farkwa kwa ajili ya mji wa Dodoma na kutekeleza mradi wa maji wa Masasi-Nachingwea.

Mheshimiwa Naibu Spika, hujuma kwenye miundombinu ya maji. Biashara ya vyuma chakavu imechangia kwa kiasi kikubwa uharibufu kwenye miundombinu ya maji hali inayoathiri upatikanaji wa huduma ya majisafi na uondoaji wa majitaka kwa jamii. Serikali imekuwa ikitoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa ulinzi shirikishi katika kulinda miundombinu ya maji kupitia maonesho na shehere mbalimbali za kitaifa kupitia Wiki ya Maji na maigizo kwenye luninga na redio pamoja na usambazaji wa vipeperushi. Aidha, Mamlaka za Majisafi Miji ni zimeendelea kushirikiana na Uongozi wa Mikoa, Jeshi la Polisi na Wananchi ili kubaini wanaojihusisha na hujuma hizo ikiwa ni pamoja na kutoa Zawadi ya fedha kwa watoa taarifa. Vilevile, Wizara imetua Waraka kwa Mamlaka zote nchini kutokununa vifaa vya maji viliviyotumika kama vile mita za maji, mabomba na vipuli vya mitambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko ya tabianchi. Mabadiliko ya tabianchi yanasaababisha kutokutabirika kwa msimu na mtawanyiko wa mvua, ukame wa muda mrefu, mafuriko ya mara kwa mara hali inayoathiri ujenzi wa miundombinu ya maji na upatikanaji wa rasilimali za maji. Hatua zinazochukuliwa kukabiliana na changamoto hiyo ni pamoja na:-

(i) Kujenga mabwawa madogo na makubwa kwa ajili ya hifadhi ya maji kwa ajili ya matumizi mbalimbali;

(ii) Kuimarisha ukusanyaji wa takwimu zinazohusu rasilimali za maji na mabadiliko ya tabianchi;

(iii) Kutoa mafunzo kwa wataalam na kuelimisha umma ili kuongeza weledi kuhusu mabadiliko ya tabianchi;

(iv) Kutumia utaalam asilia (*Indigenous knowledge*) katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi;

(v) Kushirikisha wadau mbalimbali katika kutunza vyanzo nya maji kwa kuvitambua na kuviwekea mipaka, kupanda miti, kuzuia shughuli za kiuchumi na kijamii katika maeneo oevu, maeneo ya milimani na katika chemchem, kudhibiti matumizi holela ya maji kwa kutoa kibali cha kutumia maji na kudhibiti uchafuzi wa vyanzo nya maji na uharibifu wa mazingira kwa kutumia Sheria za Maji, Mazingira na Sheria ya Misitu pia kwa kutumia sheria ndogo ngazi za halmashauri;

(vi) Kuendeleza matumizi ya teknolojia sahihi za umwagiliaji zinazotumia maji kwa ufanisi; na

(vii) Kushirikiana na taasisi za kiserikali na zisizo za kiserikali zinazofanya utafiti kuhusu mabadiliko ya tabianchi kwa lengo la kufanya utafiti wa pamoja na kutathmini matokeo ya tafiti mbalimbali ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupungua kwa rasilimali za maji. Pamoja na nchi yetu kuwa na maji mengi yanayopatikana kwenye mito, Maziwa, chini ya ardhi na maeneo oevu, baadhi ya maeneo hukumbwa na uhaba wa maji kutohana na mabadiliko ya tabianchi. Vilevile, maji yanayofaa kwa matumizi mbalimbali yanaendelea kupungua mwaka hadi mwaka kutohana na ongezeko la watu, ongezeko la uzalishaji mali katika sekta mbalimbali ikiwa ni pamoja na uzalishaji wa umeme, kilimo cha umwagiliaji, na matumizi ya viwandani na majumbani. Aidha, uharibifu wa mazingira na ukataji ovyo wa misitu na uharibifu wa maeneo oevu hupunguza sana rasilimali za maji. Katika kukabiliana na changamoto hiyo Serikali inaendelea kusimamia na kuhakikisha vyanzo nya maji vinatunzwa dhidi ya uharibifu na uchafuzi na kuhakikisha maji yanatumika kwa njia

24 APRILI, 2013

endelevu kwa kutumia sheria za maji na kanuni zake na kuzihimiza Halmashauri kutunga sheria ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati mwingine wa kukabiliana na uhaba wa maji ni kuweka muundo bora wa kitaasisi kwa ajili ya usimamizi endelevu wa raslimali za maji katika mabonde ya maji kwa kuhakikisha uwepo wa mgawanyo yakinifu na matumizi bora ya maji kwa ajili ya mahitaji ya kijamii na kiuchumi. Vilevile, Serikali itaendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria Na. 11 ya mwaka 2009 ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji Kidogo wa Fedha kwa Sekta ya Maji. Changamoto nyininge inayoikabili Wizara yangu kwa kipindi kirefu sasa ni kuendelea kupata bajeti kidogo ya fedha za matumizi mengineyo (*OC*) na fedha za ndani za kutekeleza miradi ya maendeleo. Viwango vinavyokasimiwa na kutolewa kwa Sekta ya Maji, huwa pungufu ya kiwango kinachoidhinishwa na kutolewa kwa kila mwaka. Mathalani, Fedha za ndani zilizoidhinishwa kwa mwaka 2012/2013 ni shilingi bilioni 140.016 hadi kufikia mwezi Machi, 2013 jumla ya shilingi bilioni 29.000 zilizotolewa sawa na asilimia 20.7 ya fedha zilizokasimiwa. Fedha za matumizi mengine (*OC*) zilizoidhinishwa katika mwaka mwaka 2012/2013 ni Shilingi bilioni 3.8 hii ikiwa ni asilimia 23 ya Shilingi bilioni 16.5 zilizoombwa kukidhi mahitaji ya msingi ya kuiwezesha Wizara ya Maji kujindesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali hiyo, Wizara imekuwa na malimbikizo makubwa ya madeni yanayofikia Shilingi bilioni 10.2. Mchanganuo wa madeni hayo ni pamoja na malimbikizo ya madeni ya watumishi ilkiwa ni stahili zao za ajira, Shiling bilioni 2.8, malimbikizo ya madeni ya wazabuni watoa huduma Wizarani Shilingi bilioni 2.2 na malimbikizo ya ankara za umeme za mamlaka daraja B na C na miradi ya kitaifa Shilingi bilioni 5.2. Malimbikizo ya madeni ya wakandarasi wanaotekeleza miradi ya maendeleo yaliyofikia Shilingi bilioni 19. Kiwango cha fedha za maendeleo kilichokasimiwa na kutolewa kuanzia mwaka 2006/2007 hadi mwezi Machi, 2013 ni kama ifuatavyo:

24 APRIL, 2013

**Kiwango cha fedha za ndani za maendeleo  
kilichokasimiwa na kutolewa kwa Wizara ya Maji  
kuanzia 2006/2007 hadi 2011/2012**

Na.	Mwaka	Kiasi kili-chokasimiwa	Kiasi kilicho-tolewa
1	2006/2007	77,864,997,000	53,570,000,000
2	2007/2008	70,754,004,000	55,193,116,236
3	2008/2009	46,463,379,000	36,463,379,000
4	2009/2010	50,463,379,000	15,847,952,375
5	2010/2011	30,721,712,000	25,004,329,071
6	2011/2012	41,565,045,000	24,746,549,522
7	2012/2013	140,015,967,000	29,000,000,000*

*\*Kiwango cha fedha kilichotolewa Robo ya kwanza na ya pili 2012/2013*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Maendeleo zinatolewa kwa wakati na kwa kiwango cha kuridhisha, Wizara imeimarisha mawasiliano na wadau hususan Wizara ya Fedha na Washirika wa Maendeleo kwa kuchukua hatua zafuatazo:-

(i) Kushirikiana kwa karibu na Wizara ya Fedha (HAZINA) na Washirika wa Maendeleo katika hatua zote za kuandaa bajeti ya mwaka ya Wizara ili kupanga vipaumbele vya kutekeleza kulingana na fedha za ndani ambazo tuna uhakika wa kuzipata;

(ii) Kuandaa na kuwasilisha kwa wakati Mpango Kazi (*Action Plan*) wa kutekeleza bajeti ya mwaka pamoja na mahitaji ya fedha kwa kila kipindi cha Robo mwaka Wizara ya Fedha na Tume ya Mipango. Mpango kazi huo ndiyo unaotumika katika utoaji wa fedha kwa upande wa Serikali na Washirika wa Maendeleo;

(iii) Kuandaa na kuwasilisha kwa wakati taarifa za utekelezaji wa miradi Wizara ya Fedha, Tume ya Mipango

na kwa Washirika wa Maendeleo kwa lengo la kupatiwa fedha kwa wakati na kwa kiwango kinachotakiwa kwa ajili ya utekelezaji katika kipindi cha Robo mwaka inayofuatia; na

(iv) Kufanya majadiliano na Washirika wa Maendeleo (Wahisani) juu ya utoaji na matumizi ya fedha za *WSDP*. Majadiliano hayo yamewezesha kukubaliana kuanza utoaji wa fedha kwa kipindi cha miezi sita sita badala ya utaratibu wa kutoa fedha kidogo kidogo kulipa madeni ya wakandarasi. Hatua ya kuanza kutoa fedha za miezi sita kuanzia robo ya pili ya 2012/2013 ni baada ya Wizara kuboresha mfumo wake wa utunzaji wa taarifa za fedha na kuimarisha mfumo wa usimamizi kutekeleza miradi ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu wa Wataalam wa Maji. Sekta ya Maji nchini inakabiliwa na upungufu mkubwa wa wataalam kutoekana na serikali kutoajiri kwa muda mrefu, kustaa fu kwa wataalam wa maji, watumishi wapya kuacha kazi na ikama mpya ya Muundo wa Sektretariati za Mikoa ambayo imeifanya Sekta ya Maji kuwa idara kamili. Mahitaji ya wataalam ni kama ifuatavyo:-

(i) Watumishi wa wizara wanaotakiwa ni 1,801 waliopo ni 1,558;

(ii) Wahandisi wanaotakiwa kwenye Sekretariati za Mikoa yote 25 ya Tanzania Bara ni 100 lakini waliopo ni 24 tu, Wahaidrojolojia wanapaswa kuwa 25 waliopo ni 3, wataalam hawa watasaidia kufanya utafiti wa maeneo yanayofaa kuchimbwa visima;

(iii) Wahandisi wa Maji wanaotakiwa kwenye Halmashauri zote ni 760 waliopo ni 147 Mafundi Sanifu wanaotakiwa kwenye Halmashauri ni 1,672 waliopo ni 182, wanahitajika kwenye ujenzi, uendeshaji na kufanya matengenezo ya miradi ya maji;

(iv) Mafundi Sanifu Wasaidizi wanaotakiwa ni 2,880 lakini waliopo ni 329, wanahitajika kuwasaidia mafundi

24 APRIL, 2013

Sanifu kufanya kazi za mikono na kiufundi kwenye Miradi ya Maji inayotekelizwa nchini na kufanya matengenezo ya miradi ya maji Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na upungufu wa watumishi, Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma imewahamishia kwenye halmashauri mafundi sanifu 39 waliokuwa kwenye ofisi zilizokuwa za Wahandisi wa Maji wa Mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sasa kutumia fursa hii kuwashukuru wale wote waliochangia kuiwezesha Wizara yangu kufanikisha majukumu yake. Nakiri kwamba mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2012/2013 ni kutokana na jitihada za pamoja, ushirikiano na misaada ya kifedha na kitaalam kutoka kwa washirika wa maendeleo, ikiwa ni pamoja na nchi wahisani, mashirika ya misaada ya kimataifa, taasisi zisizo za kiserikali, mashirika ya kidini na taasisi za kifedha. Napenda kuzishukuru Serikali za Ujeruman, Uholanzi, Uingereza, Marekani, Japan, Ufaransa, China, Uswisi, Ubeligiji, Ireland, Korea ya Kusini, Sweden, Denmark, Norway, India na Misri.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, napenda kutoa shukrani kwa taasisi za fedha za kimataifa ikiwa ni pamoja na Benki ya Dunia (*WB*), Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*), Benki ya Maendeleo ya Ujeruman (*KfW*), Benki ya Maendeleo ya Ufaransa (*AFD*), Benki ya Uwekezaji ya Umoja wa Ulaya (*EIB*), Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika (*BADEA*), Mfuko wa Maendeleo wa Nchi Zinazozalisha Mafuta (*OPEC Fund for International Development-OFID*), Mfuko wa Maendeleo wa Saudi (*SFD*) Umoja wa Ulaya (*EU*), Shirika la Marekani la Changamoto za Milenia (*MCC*), Shirika la Misaada ya Maendeleo la Norway (*NORAD*), Taasisi ya Maendeleo ya Uingereza (*DFID*), Shirika la Kiufundi la Ujeruman (*GIZ*), Mpango wa Umoja wa Mataifa wa Maendeleo (*UNDP*), Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan (*JICA*), Mpango wa Umoja wa Mataifa wa Makazi Duniani (*UN Habitat*), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (*UNICEF*), Shirika la Misaada ya Maendeleo la Sweden (*SIDA*), Shirika la Misaada ya

24 APRILI, 2013

Maendeleo la Canada (*CIDA*), Shirika la Misaada ya Maendeleo la Denmark (*DANIDA*), na Shirika la Misaada la Marekani (*USAID*) kwa misaada ya fedha na michango yao ya kitaalam katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu na malengo ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nayashukuru pia, mashirika ya kidini ya *World Islamic League*, Shirika la *Ahmadiya Muslim Jamaat Tanzania*, *Islamic Foundation*, Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania, Kanisa la Kilutheri la Ujerumani, Baraza Kuu la Waislam Tanzania, Kanisa Katoliki Tanzania, Kanisa la Kianglikana Tanzania, *Catholic Agency for Overseas Aid and Development (CARITAS)*, *Adventist Development Relief Agency (ADRA)*, *Norwegian Church Aid* na *Livingwater International*. Nashukuru pia, taasisi zisizo za kiserikali za *Tanzania Water and Sanitation Network (TAWASANET)*, Wahamasishaji wa Maji, Maendeleo na Afya (*WAMMA*), *Southern Highlands Participatory Organizaition (SHIPO)*, *WaterAid*, *World Vision*, *Plan International*, *Concern Worldwide*, *Netherlands Volunteers Services (SNV)*, Shirika la Kimataifa la Kuhifadhi Uasili na Mali Asili (*IUCM*), *World Wide Fund for Nature (WWF)*, *African Medical Research Foundation (AMREF)*, *Clinton HIV Aids Initiative (CHAI)* na *Bill and Melinda Gates Foundation*, na wale wote ambao kwa njia moja au nytingine wameendelea kuisaidia Sekta ya Maji kufanikisha malengo yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Mhandisi Dr. Binilith Satano Mahenge (Mb), Naibu Waziri wa Maji, kwa msaada na ushirikiano anaonipatia katika kuiongoza Wizara ya Maji. Naomba pia, nitoe shukurani zangu kwa Mhandisi Christopher Nestory Sayi, Katibu Mkuu, Mhandisi Bashir Juma Mrindoko, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote na Wakuu wa Vitengo, Maafisa na Watendaji Wakuu wa Mashirika, Wakala na Taasisi zilizo chini ya Wizara yangu, wataalam na watumishi wote kwa kujituma katika kusimamia utekelezaji wa majukumu tuliyopewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishukuru familia yangu kwa upendo na kunipa kila msaada ili niweze kumudu

24 APRIL, 2013

majukumu yangu. Mke wangu Kudula Maghembe yuko hapa, kwenye *gallery*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 398,395,874,000 kwa ajili ya matumizi ya Wizara yangu kwa mwaka 2013/2014, ili Wizara iweze kutekeleza majukumu na malengo yaliyoelezwa katika hotuba hii. Kati ya fedha hizo, Matumizi ya Kawaida ni shilingi 18,952,654,000 ambapo shilingi 13,319,877,000 ni Mishahara ya Watumishi (*PE*), na shilingi 5,632,777,000 ni fedha za Matumizi Mengine (*OC*). Jumla ya Bajeti ya Maendeleo ni shilingi 379,443,220,000 ambapo kati ya fedha hizo shilingi 138,266,164,000 ni fedha za ndani na shilingi 241,177,056,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tena nitoe shukurani zangu za dhati kwako wewe mwenyewe na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kuniskiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika Tovuti ya Wizara ya Maji kwa anwani: [www.maji.go.tz](http://www.maji.go.tz).

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa Hoja. (*Makofî*)

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Maghembe kwa hotuba yako na hoja imetolewa na imeungwa mkono. Tunakushukuru sana kwa kutusomea hotuba nzuri sana. Kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge nimshukuru Mama Kudula Maghembe kuwepo maana mambo haya *pressure* inaweza ikapanda, ikashuka, sasa angalau mama anakuwa karibu kidogo. (*Makofî/Kicheko*)

Mwenyekiti wa Kamati!

24 APRILI, 2013

**MHE. SAIDI J. NKUMBA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (7) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, kwa niaba ya Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2012/2013 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji ni hitaji la msingi la maisha na uhai wa viumbe vyote. Aidha, shuguli mbalimbali za maendeleo ikiwa ni pamoja na uzalishaji wa umeme na bidhaa za viwandani, matumizi ya majumbani na usafi wa mazingira zinategemea uwepo wa maji ya kutosha. Katika Nchi yetu huduma ya maji bado haijatosheleza mahitaji hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati ya kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji ilikutana na Wizara ya Maji tarehe 26-27 Machi, 2013 katika Ofisi ndogo ya Bunge ya Dar es Salaam na tarehe 17 April, Bungeni Dodoma, ili kuchambua taarifa ya utekelezaji wa Bajeti, utekelezaji wa maoni ya Kamati, changamoto zilizojitokeza kwa mwaka 2012/2013 na kuchambua makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kupitia na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2012/2013, Kamati ilitoa maoni na ushauri kwa Serikali. Napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kwa kiasi kikubwa Serikali imeyafanya kazi maoni na ushauri wa Kamati. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla Kamati imeridhika na utendaji wa Wizara isipokuwa kwa maeneo ambayo utekelezaji wake ulikwamishwa na upungufu na ucheleweshwaji wa fedha pamoja na sababu mbalimbali za kiutendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada kubwa

zinazofanywa na Wizara katika kutekeleza majukumu yake, Wizara inakumbana na changamoto mbalimbali ambazo zimekuwa ni kikwazo katika kufikia malengo iliyojivekeea. Baadhi ya changamoto hizo ni:-

(a) Kiasi kidogo cha fedha zinazotengwa na ucheleweshwaji wa utoaji wa fedha za maendeleo na hivyo kuathiri kasi ya utekelezaji wa baadhi ya miradi ya Wizara;

(b) Hujuma kwenye miundombinu ya maji, ambapo biashara ya chuma chakavu imechangia kwa kiasi kikubwa uharibifu wa miundombinu ya maji. Hali hii inaathiri upatikanaji wa huduma ya maji safi na uondoaji wa maji taka kwa jamii;

(c) Kuongezeka kwa idadi ya watu na shughuli za kiuchumi na kijamii nchini. Kwa mfano katika maeneo ya Miji ni miundombinu ya maji ni ya zamani na chakavu hivyo kusababisha wananchi wengi kutofikiwa na huduma ya maji;

(d) Mabadiliko ya tabianchi yamesababisha kutotabirika kwa msimu na mtawanyiko wa mvua. Hii imesababisha ukame wa muda mrefu na kukauka kwa vyanzo vya maji kwa baadhi ya maeneo. Maeneo mengine yamekumbwa na mafuriko;

(e) Uchafuzi wa vyanzo vya maji kutokana na matumizi ya kemikali katika maeneo ya uchimbaji wa madini; na

(f) Kutopatikana kwa wakati takwimu sahihi na taarifa za utekelezaji wa programu kushirikisha taasisi mbalimbali ambazo Wizara ya Maji haina mamlaka nazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi ya fedha na malengo ya bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Ili kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara ya Maji chini ya Fungu 49 inaomba jumla ya shilingi 398,333,474,000/=. Kati ya fedha hizo, shilingi 18,890,254,000/= ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi

24 APRILI, 2013

379,443,220,000/= ni kwa ajili ya Miradi ya maendeleo. Kati ya fedha za maendeleo, shilingi 138,266,164,000/= ni fedha za ndani na shilingi 241,177,056,000/= ni fedha kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hizi zinazoombwu hazikidhi kabisa mahitaji ya msingi ya Wizara ambayo ni kutoa huduma ya maji kwa makundi mbalimbali ya jamii. Kamati imepitia kwa undani taarifa ya bajeti na kugundua kuwa Wizara ya Maji kwa kipindi kirefu imekuwa ikipata bajeti ndogo kutoka fedha za ndani kutekeleza miradi ya maendeleo na fedha za matumizi mengine. Aidha, fedha zinazoidhinishwa na Bunge hazitolewi zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Kamati ilibaini kuwa makubaliano kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo wanaogharamia kutekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (*WSDP*) ni kuwa Serikali itachangia Shilingi bilioni 75 kila mwaka katika awamu ya Kwanza (2007/2008 – 2013/2014). Hata hivyo, kiwango hicho hakijawahi kufikiwa kama inavyoonyeshwa katika jedwali Na. 1

#### **Jedwali Na.1 Mtiririko wa fedha za maendeleo unaotolewa na Serikali**

Na.	Mwaka	Kiasi kilicho-kasimiwa	Kiasi kilicho-tolewa	Kiwango kilichotolewa dhidi ya Ahadi ya Serikali ya Shs. Bilioni 75	
1	2006/2007	77,864,997,000	53,570,000,000	71%	
2	2007/2008	70,754,004,000	55,193,116,236	74%	
3	2008/2009	46,463,379,000	36,463,379,000	49%	
4	2009/2010	50,463,379,000	15,847,952,375	21%	
5	2010/2011	30,721,712,000	25,004,329,071	33%	
6	2011/2012	41,565,045,000	24,746,549,522	33%	
7	2012/2013	140,015,967,000	29,000,000,000*	39%	

*\*Kiwango cha fedha kilichotolewa hadi mwezi Machi, 2013*

24 APRILI, 2013

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuongezeka kwa mahitaji ya usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya maji inayotekelawa nchi nzima, kiasi cha fedha zinazotengwa kwa matumizi ya kawaida (*OC*) zimekuwa zikipungua mwaka hadi mwaka kama ilivyoonyeshwa katika jedwali Na.2

**Jedwali Na.2 Mtiririko wa fedha za matumizi mengine zinazotolewa na Serikali:**

Mwaka	Kiasi (Tsh).
2006/2007	Bilioni 16.8
2007/2008	Bilioni 8.7
2008/2009	Bilioni 9.5
2009/2010	Bilioni 9.5
2010/2011	Bilioni 6.6
2011/2012	Bilioni 4.3
2012/2013	Bilioni 3.8

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za ndani za miradi ya maendeleo ziliendelea kushuka wakati mahitaji ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, hususan ngazi za Halmashauri, Miji ya Wilaya na Miji Midogo. Hali hii inasababisha miradi ya maji katika ngazi hizo kutekelezwa kwa kasi ndogo na kusababisha miradi kutokukamilika kwa wakati au kutotekelezwa kabisa kutokana na ukosefu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenendo huu wa uchangiaji mdogo wa Serikali katika ujenzi wa miradi unawakatisha tamaa Washirika wa Maendeleo wanaochangia katika Programu ya Maji. Hali hii inaweza kuwa tatizo katika uchangiaji wa Washirika hao wa Maendeleo katika Awamu ya Pili ya miaka mitano ya Programu itakayoanza kutekelezwa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati kwa Wizara kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Nyongeza ya fedha. Kamati hairidhishwi na kitendo cha

24 APRILI, 2013

Serikali kupunguza bajeti ya maji ambayo mahitaji yake yanaongezeka kwa kasi mwaka hadi mwaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mtiririko ulivyoonyeshwa katika Jedwali na 1 & 2, Kamati inaishauri Serikali ione umuhimu wa kutoa fedha zote na kwa wakati zinazoidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huu, Kamati inaiomba Serikali kuiongezea fedha Wizara hii ili iweze kutekeleza majukumu yake ya msingi na kupunguza tatizo la maji hasa maeneo ya Vijiji ambako tatizo ni kubwa zaidi. (*Makofii*)

Kamati inaishauri Serikali kuiongezea Wizara kiasi cha shillingi billioni 184.5 za ziada kwa matumizi yafuatayo:-

(a) Kuendeleza utekelezaji wa Programu ya upelekaji maji Vijiji katika kumi, kwa kuongeza Vijiji viwili au vitatu katika kila Halmashauri kwa gharama ya shillingi bilioni 65. Hatua hii itaongeza huduma ya maji kwa wananchi wapatao 980,000 hadi Juni, 2014. (*Makofii*)

(b) Kujenga miundombinu ya kuwasambazia maji wananchi kutoka katika mabwawa kumi yaliyojengwa katika Wilaya kame kwa gharama ya shillingi billioni 13. Hatua hii itawapatia huduma ya maji safi na salama wananchi wapatao 480,000 pamoja na mifugo yao ifikapo Juni, 2014.

(c) Kujenga miundombinu ya pampu na mabomba ya kuwasambazia maji wananchi kutoka katika visima virefu vya maji vilivyochimbwa katika maeneo mbalimbali nchini. Gharama za kutekeleza kazi hiyo ni shillingi bilioni 11.2 na utawapatia huduma ya maji safi na salama wananchi wapatao 640,000 pamoja na mifugo yao ifikapo Juni, 2014.

(d) Kupanua, kukarabati na kujenga miundombinu kwenye miradi katika Wilaya mbalimbali

ambayo kwa sasa haitoi huduma ipasavyo kutokana na uchakavu kwa gherama ya shilingi bilioni 10.8. Wananchi wapatao 440,000 watanufaika ifikapo Juni, 2014.

(e) Kujenga miundombinu ya kusambaza maji kwa wananchi kutoka katika miradi mikubwa ambayo usanifu umekamilika na miradi mikubwa inayohitaji ukarabati. Miradi hii itahitaji jumla ya shilingi bilioni 8.

(f) Kufanya usanifu na ujenzi wa mradi wa Ugala, Urambo na Kaliua – Mkoa wa Tabora. Mradi huu utagharimu shilingi bilioni 12.1.

(g) Miradi mingine iliyoainishwa kwenye taarifa ya Waziri itakayoleta matokeo ya haraka itagharimu shilingi bilioni 53.568. Miradi hiyo itahudumia watu 614,780.

Mheshimiwa Naibu Spika, kodi za madawa ya maji. Kamati inaipongeza Serikali kwa kupunguza Kodi za Ongezeko la Thamani (VAT) kwenye madawa ya kutibia maji kutoka 18% hadi 9.9%. Hata hivyo, Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kuiondoa kabisa kodi hii na kuwa 0% (*zero rated*) ili gherama za maji zipungue. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mgawanyo wa bajeti. Kamati imebaini kuwa kuna tofauti kubwa sana kati ya bajeti inayotengwa kwa ajili ya maji Mijini na Vijiini. Matokeo yake ni kwamba, watu wanaopata maji safi na salama Mijini ni asilimia 86 na Vijiini ni asilimia 58.6 tu ikizingatiwa kwamba asilimia 80 ya Watanzania wanaishi Vijiini. Kamati inaishauri Serikali kuongeza bajeti ya maji Vijiini ili kupunguza tatizo kubwa la maji linalokabili maeneo mengi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vyanzo vya maji. Kwa kuwa mahitaji ya maji yanaongezeka siku hadi siku kutokana na ongezeko la watu, mifugo pamoja na shughuli za kiuchumi na kijamii, vyanzo vingi vya maji nchini vimeanza kukauka. Kamati inaishauri Serikali pamoja na wananchi kutunza vyanzo vyake vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, uvunaji wa maji. Kwa kuwa uhaba wa maji ni tatizo kubwa kwa nchi yetu, Kamati inaishauri Serikali iendelee kuhimiza na kuhamasisha jamii kwa kutoa elimu ya utaratibu wa uvunaji wa maji ya mvua kwa kutumia njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na ujenzi wa mabwawa, malambo na uvunaji wa maji ya paa. Aidha, Serikali ihmize Halmashauri kutunga sheria ndogo ili kuwepo na utaratibu wa uvunaji wa maji ya mvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa Mradi wa Maji katika Vijiji Kumi. Mradi huu ulipoanzishwa ulionekana wenye tija na kwamba ungepunguza tatizo la maji Vijijini kwa kiwango kikubwa. Aidha, visima vinavyochimbwa ni vichache na baadhi havitoi maji na vingine hutoa maji kwa muda mfupi. Kamati inasisitiza Serikali kufanya yafuatayo:-

- (a) Serikali ione umuhimu wa kuongeza fedha za ndani ili kuharakisha utekelezaji wa mradi huu.
- (b) Serikali iangalie namna ya kupunguza gharama kwa kuipa kampuni moja kufanya kazi ya upimaji na uchimbaji. Utaratibu huu utarahisisha uwajibikaji iwapo maji hayatapatikana na hata gharama zitapungua. (*Makof*)
- (c) Serikali ipitie upya Sheria ya Manunuzi (*PPRA,2004*) ili kupunguza gharama za miradi na urasimu.
- (d) Kwa kadri inavyowezekana, Serikali inashauriwa kutumia Wataalam Waelekezi wetu badala ya kutumia wataalam toka nje kwa nia ya kupunguza gharama. (*Makof*)
- (e) Maeneo yenyeye madini kama chumvi na *fluoride* yaangaliwe namna ya kupata maji kwa njia nyingine kama mabwawa ili kupunguza athari zinazoweza kutohana na matumizi ya maji hayo.
- (f) Serikali iendelee kutoa elimu kwa wananchi kuhusu ubora na utunzaji wa pampu za maji ili kuepuka uharibifu unaotokana na matumizi yasiyo sahihi.

24 APRIL, 2013

Mheshimiwa Naibu Spika, uharibifu wa Miundombinu ya Maji. Kamati imebaini kuwa maeneo mengi ambayo miundombinu yake imeharibiwa ni kwa sababu pamoja na mambo mengine ya biashara ya chuma chakavu ambapo wananchi wahalifu wanabomoa miundombinu ya maji. Kamati inashauri Serikali kuangalia uwezekano wa kujenga miundombinu isiyotumia chuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, miundombinu chakavu. Kamati imebaini kuwa maji mengi hypotelea njiani kabla ya kumfikia mtumiaji kwa sababu ya miundombinu chakavu. Kamati inaishauri Serikali kufanya ukarabati wa miundombinu hiyo na kudhibiti wizi wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho. Napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa hii. Aidha, natoa shukrani zangu za dhati kwa wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na kazi nzuri wanayofanya. Wajumbe wa Kamati ni hawa wafuatao:-

Mheshimiwa Prof. Peter Mahamudu Msolla-Mwenyekiti, Mheshimiwa Said J. Nkumba-Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Prof. David Homeli Mwakyusa, Mheshimiwa Subira Mgusu, Mheshimiwa Asaa Othman Hamad, Mheshimiwa Abdusalaam S. Ameir, Mheshimiwa Abdalla Haji Ali, Mheshimiwa Namelok E. M. Sokoine, Mheshimiwa Dkt. Christine G. Ishengoma, Mheshimiwa Sylvestry Francis Koka, Mheshimiwa Moshi S. Kakoso, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Meshack Jeremia Opulukwa, Mheshimiwa Philemon Kiwelu Ndesamburo, Mheshimiwa Sadifa Juma Khamis, Mheshimiwa Mch. Peter Simon Msigwa, Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi, Mheshimiwa Donald Kelvin Max, Mheshimiwa Magdalena Hamisi Sakaya, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Jitu Vrajlal Soni, Mheshimiwa Dkt. Lucy Sawere Nkya na Mheshimiwa Lolesia Masele Bukwimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Maji Fungu 49 kwa mwaka wa fedha 2013/2014 jumla ya shilingi

24 APRILI, 2013

398,333,474,000/= na nyongeza inayooombwa ya shilingi bilioni 184.5. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Said Nkumba kwa maoni hayo ya Kamati ambayo ni mazuri sana. Sasa naomba kumwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara hii ya Maji, naye ni Mheshimiwa Cecilia Pareso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO (K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha hotuba kuhusu makadirlo ya matumizi na mapato ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la upatikanaji wa maji safi na kuweza kushughulikia majitaka ni sehemu ya makubaliano ya kimataifa ambayo nchi yetu imeridhia kuingia mathalani Malengo ya Milenia (*MDGs*); lengo namba saba (7) shabaha 10; la kupunguza nusu ya watu waoishi bila maji safi na salama ya kunywa na usafi wa msingi katika mazingira wanayoishi. Hatua za haraka za kuboresha upatikanaji wa maji safi na ushughulikiaji wa maji taka ni muhimu kama sehemu ya haki za binadamu. Jambo hili lina tija pia katika uzalishaji mali na uchumi wa nchi kwa kuwa tafiti zinaonyesha kwamba kudumu kwa matatizo hayo kunazigharimu nchi za Afrika, Tanzania ikiwemo wastani wa asilimia sita (6) ya pato la taifa (*Gross Domestic Product*).

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti uliofanywa na Stockholm *Environment Institute* kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo Afrika mwaka 2006 kuhusu uhusiano kati ya maji na umaskini Afrika kwa kutumia mfano wa nchi yetu (*Water and Poverty Linkages in Africa: Tanzania Case Study*) umebainisha wazi kwa vielelezo namna ilivyo vigumu kupima

24 APRIL, 2013

Tanzania inavyosonga mbele katika utekelezaji wa malengo ya maendeleo ya milenia yanayohusu maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, utafiti huo umeeleza namna ambavyo bila kushughulikia kwa haraka matatizo ya maji jitihada za kupambana na kupunguza na kutokomeza umaskini zitakuwa ni ndoto kwani hatutaweza kupiga hatua ya maana katika mapambano hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa kadiri ya Tathmini ya Hali ya Watu na Afya ya mwaka 2010 (*Demographic and Health Survey, 2010*); ni asilimia 4.8 tu ya kaya zilizopo Vijiji ndiyo zinazopata maji katika eneo lao la kaya (*water on premises*) wakati ni asilimia 19.4 tu ya kaya kwa Mijini ndizo zenye maji katika kaya zao. Hivyo kaya nyngi za Tanzania zinawekwa katika mazingira hatarishi kwa magonjwa ya mlipuko na mengine ambayo si ya mlipuko kutokana na uhaba wa maji, ambapo inaelezwa kuwa hali ni tete zaidi katika maeneo yasiyopimwa yenye msongamano mkubwa wa watu katika maeneo ya Majiji na Miji mbalimbali (*slums*) hapa nchini mwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la maji ni kubwa kuliko tunavyofikiria na hasa Vijiji. Vijiji vingi havina huduma ya maji ya uhakika na hii inatokana na sababu nyngi. Vipo Vijiji ambayo miundombinu ya maji ilijengwa zaidi ya miaka 30 iliopita na kwa kuwa haukuwepo mfumo endelevu wa kuikarabati, sehemu kubwa imekuwa ni chakavu na maji mengi kupotea, vyanzo vya maji vingi kupungua maji na vingine kukauka kabisa kutokana na madhara ya mabadiliko ya tabia nchi na kuongezeka kwa idadi ya watu kulinganisha na wakati vyanzo na miundombinu hiyo ilipokuwa inawekwa. Hivyo basi, ni bora ufanyike ukaguzi hakiki (*inventory*) upya wa miundombinu na vyanzo vya maji kwa kila kijiji ili kujua ni Vijiji vingapi na watu wangapi wanapata huduma ya maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii ya ukosefu wa maji

safi na salama kwenye maeneo mbalimbali ya nchi yetu imeathiri sana uzalishaji mali kwani imesababisha nguvu kazi kubwa kupotea kutokana na muda mwangi kutumika katika kufuatilia maji muda wa uzalishaji na hata kinamama wengi ambaao ndio nguzo muhimu ya uzalishaji, wamejikuta hawana muda wa kutosha kwenye shughuli za uzalishaji kutokana na kutumia muda mwangi kufuatilia maji maeneo ya mbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inashangazwa na Serikali hii ya CCM pamoja na tatizo kubwa la maji nchini bado leo Serikali inaleta bajeti ya maji ya shilingi bilioni 397.4 ambayo ni 2% tu ya bajeti nzima ya nchi kwa mwaka huu wa fedha wa 2013/2014. Wakati Mpango wa Mendeleo wa miaka mitano kwa mwaka huu unaonyesha kuwa Serikali ilitakiwa kutenga shilingi bilioni 529.032 kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwenye sekta ya maji. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa ufanuzi, je Mpango wa Maendeleo wa Miaka mitano unazingatiwa kwa kiasi gani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya Taifa katika upatikanaji wa maji. Majwedwali yafuatayo hapo chini yanaonyesha mwenendo wa hali yetu kama taifa na upatikanaji wa maji Vijijini na Miji ni kwa vipindi tofauti kuanzia mwaka 1995 hadi 2010 na jinsi hali inavyozidi kuwa mbaya kadiri muda unavyokwenda mbele

### **Maji Mijini-Makadirio kwa Matumizi kwa Mwaka 2012**

Mwaka	%Jumla -maji safi	%Maji ya Bomba	%Vyanzo vingine salama	%Vyanzo vingine visivyo	%Maji ya juu salama
1990	94	35	59	3	3
1995	90	31	59	7	3
2000	86	28	58	11	3
2005	83	25	58	14	3
2010	79	22	57	18	3

24 APRIL, 2013

### Maji Vijijini Makadirio kwa Mwaka 2012

Mwaka	%Jumla -maji safi	%Maji ya Bomba	%Vyanzo vingine salama	%Vyanzo vingine visivyo salama	%Maji ya juu
1990	46	1	45	29	25
1995	46	1	45	30	24
2000	45	2	43	32	23
2005	45	3	42	34	21
2010	44	3	41	36	20

### Jumla ya Makadirio ya Upatikanaji wa Maji Safi na Salama

Mwaka	%Jumla -maji safi	%Maji ya Bomba	%Vyanzo vingine salama	%Vyanzo vingine visivyo salama	%Maji ya juu
1990	55	7	48	24	21
1995	55	7	48	25	20
2000	54	8	46	27	19
2005	54	8	46	29	17
2010	53	8	45	31	16

Chanzo cha takwimu: *WHO / UNICEF, Joint Monitoring Programme for Water Supply and Sanitation. Estimates for the use of Improved Drinking-Water Sources, Updated March 2012, United Republic of Tanzania.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa takwimu hizo zinaonyesha kuwa matatizo ya maji nchi hii yamezidi kuwa makubwa kila baada ya kipindi cha utawala mmoja kwenda mwingine. Kama ilivyojitokeza kwenye sekta ya elimu, vivyo hivyo utawala wa Serikali ya Awamu ya Nne chini ya CCM, umesababisha huduma ya maji kuendelea kuwa mbaya nchini kwetu kwa kushindwa kusimamia utekelezaji wa Sera ya Maji ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgawanyo wa fedha za maendeleo katika miradi ya maji kwa mwaka 2013/2014. Katika hali ya kushangaza na kusikitisha ni kuwa Wizara haionyeshi italishughulikaje tatizo la maji katika nchi yetu kwani kwa mujibu wa randama ya Wizara hii, nitaelezea mgawanyo wa fedha hizi katika maeneo mbalimbali nchini na udhaifu wa mgawanyo huo kimradi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Programu ya maji na usafi wa mazingira Vijiji. Mradi Na.3216, kupanua na kukarabati miradi ya maji Vijiji ambayo inaendelea, zimetengwa shilingi 15,014,211,000, fedha hizi ni kwa ajili ya miradi ya Vijiji vyote ambavyo vina miradi ya maji kwa nchi nzima. Kambi ya Upinzani inahoji, hivi kwa nchi yenye Vijiji vyote hivi vyenye matatizo ya maji kwa mgawanyo huu, lini tutaweza kuwapatia maji wananchi wote wa Vijiji?

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi Na.3223, uchimbaji wa visima na ujenzi wa mabwawa Vijiji zimetengwa shilingi bilioni 6.0. Kambi ya Upinzani inahoji fedha hizi ni kwa ajili ya Vijiji vingapi vyta nchi hii? Au tunawahadaa Watanzania waishio Vijiji kuhusiana na suala la kuweza kupata maji kwenye Vijiji vyao? Kwa mujibu wa taarifa ya Tume ya Mipango iliyowasilishwa na Mheshimiwa Wassira ilionyesha kuwa tangu Disemba 2005 hadi Disemba 2012, ni ongezeko la asilimia la aslimia 2.83 tu ya wananchi wapya wa Vijiji walioweza kupata maji kwa kipindi chote cha miaka nane. Kwa mwendo huu wa kinyonga, ni lini tutawafikia wananchi wetu wanaohangaika kupata maji kwa ajili ya uhai na afya bora?

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi Na.3341 kuboresha huduma ya maji katika Miji ya Same -Mwanga. Mradi huu umetengewa kiasi cha shilingi bilioni 32.0 na kati ya fedha hizo, kiasi cha shilingi bilioni 20.6 ni fedha za ndani na katika miradi yote ya maendeleo ya mwaka huu katika miradi ya maji, hakuna mradi mwingine wowote ambaa umetengewa kiasi kikubwa hivyo cha fedha za ndani, isipokuwa mradi wa kuboresha huduma za maji katika Jiji la Dar Es Salaam uliotengewa bilioni 43 za ndani. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa mujibu wa maelezo ya Serikali yaliyowasilishwa mbele ya Kamati ya Bunge na Waziri wa Maji (Taarifa ya Wizara kwa Kamati kuhusu utekelezaji wa mpango na bajeti 201/2013 uk.81), alisema kuwa mradi huu unalenga kuhudumia Vijiji 38 na unategemea kugharimu shilingi bilioni 147, na kuwa Wizara ilisaini mkataba na Mtaalamu Mshauri wa kufanya usanifu, kuandaa makabrasha ya zabuni na makadirio ya ujenzi kwa awamu ya kwanza na ya pili na kazi ilitegemewa kukamilika mwezi Machi 2013 na awamu ya kwanza ya ujenzi ilitegemewa kuanza mwezi Mei 2013 na kukamilika mwezi Disemba 2014 na makisio ya gharama yake ni shilingi bilioni 56.1 na kuwa tayari *OPEC* watachangia dola milioni 12 na *BADEA* dola milioni 10 na kilichobaki kitatolewa na Serikali kwa awamu hii ya kwanza ya ujenzi wa mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mradi huu ujenzi wake wa awamu ya kwanza ni shilingi bilioni 56.1 na tayari kuna wafadhili ambao wameshakubali kutoa zaidi ya shilingi bilioni 35 (*OPEC & BADEA*) na kwa mwaka huu wa fedha zimetengwa shilingi bilioni 20.6 za ndani, maana yake ni kuwa mradi huu umetengewa fedha zote asilimia 100 kwa mwaka wa kwanza wa fedha kabla hata tathimini ya gharama za ujenzi kwa awamu ya kwanza hazijajulikana kwani ripoti ya Mshauri anayefanya tathimini ya upembuzi yakinifu ilikuwa hajatolewa bado.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inataka kupata maelezo ya kina kama fedha zinaweza kutolewa wakati upembuzi yakinifu hajatolewa kwa mradi husika. Je, ni kwanini maeneno mengine yanashindwa kupatiwa fedha kwa kigezo kuwa upembuzi yakinifu bado? Tathmini ya upembuzi yakinifu imekwamisha miradi mingi ya maji hapa nchini. Hali hii inapaswa kutolewa maelezo ya kina ili kuondoa manung'uniko ya dhana ya upendeleo katika miradi ya maji na hasa huu ambao upo kwenye Wilaya anayotoka Waziri wa Maji wa sasa ya fedha kutolewa kabla ya tathmini ya upembuzi yakinifu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili ni la hatari sana na hasa ikizingatiwa kuwa mradi huu haukuwa kwenye mpango

wa bajeti wa mwaka 2012/2013, sasa leo fedha zinaondolewa kwenye miradi mingine na kurundikwa kwenye Wilaya anayotoka Waziri wa Maji au ni nini kilipelekea mgawanyo huo wa fedha? Hasa ikizingatiwa kuwa fedha zilizotengwa kwa ajili ya uchangiaji wa miradi ya maji ya Vijiiji 10 kwa Halmashauri zote nchini mwaka huu wa fedha 2013/2014 zimetengwa shilingi bilioni 12.3 tu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya maji kwa ajili ya Mikoa yote mipyä imetengewa shilingi bilioni 4.3, miradi ya maji kwa ajili ya Miji ya Masasi na Nachingwea imetengewa shilingi milioni 750, mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria hadi Miji ya Nzega, Igunga na Tabora ikiwa imetengewa shilingi milioni 450, pamoja na miradi mingine mingi imetengewa kiasi kidogo sana cha fedha za ndani. Kambi ya Upinzani, haikubaliani na mgawanyo huu wa rasilimali za Taifa na hasa kwenye sekta ya maji na ndio maana moja ya mapendekezo yetu kwenye Katiba Mpya ni kuachana kabisa mfumo huu wa Mawaziri kutokana na Wabunge, huu ni mfano mmojawapo wa madhara yatokanayo na mfumo huu mbovu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Programu ya Majisafi na Majitaka Mijini. Katika eneo hili jumla ya fedha za ndani zilizotegwa kwa ajili ya kutatua matatizo ya maji kwenye Miji na Majiji yetu mwaka huu wa fedha ni shilingi bilioni 74.712 na hizi ni kwa ajili ya miradi mikubwa kama ya kuboresha huduma za maji Masasi na Nachingwea, miradi ya kutoa maji toka Ziwa Victoria hadi Miji ya Kahama/Shinyanga, kuboresha huduma za maji Jiji la Dar Es Salaam, ujenzi wa Bwawa la Kidunda, mradi wa maji wa Kimbiji na Mpera na kujengea uwezo Wizara pamoja na mamlaka za maji Mijini ili kutekeleza *WSDP*. Kambi ya upinzani, inataka kujua Serikali ina mpango gani madhubuti na wa kujitegemea katika kuwapatia wananchi wake maji safi na salama na jinsi inavyoshughulikia tatizo la maji takatika Miji yetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ndogo ya sekta ya maji na utegemezi wa fedha kutoka nje. Tunategemea wafadhili na misaada kutoka nje kwa ajili ya kugharamia miradi hii kiasi cha shilingi bilioni 179.383 kwa mwaka huu wa 2013/

2014, utegemezi wa wahisani kutoka nje ni mkubwa kwa kiwango cha kuathiri miradi mbalimbali ya maji pamoja na upatikanaji wa maji katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Hii ni kinyume na makubaliano yetu hapa Bungeni pamoja na agizo la Kamati ya Bunge mwaka jana kuwa tupunguze utegemezi wa fedha za maji kutoka kwa wafadhilli na wahisani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa taarifa ya Hali ya Umaskini na Maendeleo ya Watu mwaka 20112 (*PHDR*), fedha za ndani za kutekeleza bajeti ya Sekta ya Maji imekuwa ikishuka mwaka hadi mwaka toka 57% katika mwaka wa fedha 2005/2006 hadi 10% kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Hali hii imesabababisha kukithiri kwa utegemezi katika vyanzo vya mapato toka nje na kwa wabia wa maendeleo kuwezesha miradi ya maji; fedha ambazo hazipatikani kwa wakati na kwa kiwango kinachokidhi mahitaji.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2011/2012 tumeshuhudia kutokutimizwa kwa azimio la Serikali la kutenga kiasi cha Dola za Kimarekani 128 milioni kutekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Maji (*WSDP*) huku bajeti pangwa ikiwa ni dola za kimarekani 28 milioni tu kwa mwaka huo 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2012/2013 umeendelea kuonesha upungufu katika utoaji wa fedha za miradi ya maendeleo katika sekta ya maji, taarifa zinaonyesha kwamba katika kipindi cha miezi sita ya kwanza Jumla ya shilingi bilioni 29 tu ndizo zilitolewa ikiwa ni sawa na asilimia 36 katika fedha za ndani. Kiwango hiki ni kidogo ikizingatiwa kuwa kiwango kilichoidhinishwa na tume ya mipango kilikuwa ni shilingi 48,326,792,184 kwa kipindi cha robo ya kwanza pekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa taarifa ya matumizi ya Serikali kwa sekta ya maji (*Public Expenditure Review of water sector Report*) ya mwaka 2009 inaonyesha kuwa sehemu kubwa ya fedha za bajeti za maendeleo kwenye sekta ya maji zinapelekewa kwenye Mamlaka za maji

Miji ni na Mamlaka za Mabonde badala ya kuzipeleka kwenye utekelezaji wa miradi inayosimamiwa na Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko ya mfumo wa kuifanya Wizara kuwa mwezeshaji badala ya kuwa mtekelezaji, hadi mabadiliko ya mfumo huu mpya yaeleweke na kukubalika na watendaji inaweza chukua muda kidogo kwani ni ukweli uliowazi kuwa uwezo wa watendaji kuweza kuhimili utawala wa fedha bado ni mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa (*Public Expenditure Review of water sector Report*) ya mapitio ya matumizi ya Serikali kwenye sekta ya maji ya mwaka 2009 inasema kwamba ili kutoa huduma kwa kiwango cha kukidhi malengo ya Millenia inatubidi kila mwaka sekta ya maji itumie dola za Marekani milioni 567.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ili kukidhi kwa kiwango cha juu cha malengo ya milenia katika utoaji wa huduma inatakiwa Serikali itumie jumla ya dola za Marekani bilioni 1.1 kila mwaka. Hivyo basi, kutohama na gharama za utoaji huduma hiyo kati ya Mijini na Vijijini kuwa tofauti, ile jamii inayotumia huduma bora zaidi za maji katika maeneo hayo inatakiwa kuchangia zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kigezo hiki hapa kwetu ni kinyume kabisa kwani wale wanaopata huduma bora za maji ndiyo wanaolipa fedha kidogo za matumizi na wale wanaopatiwa huduma ya chini ndio wanaolipa fedha nyingi sana. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuliangalia suala hili kwa makini kwani linazidi kuwa kubwa sana na hivyo kusababisha kutokea kwa matabaka katika nchi yetu, hasa katika huduma muhimu kama hii kwa ajili ya uhai wa binadamu ye yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu unaojitezea katika utekelezaji wa mipango ya Serikali hususan katika ugawaji wa rasilimali fedha ambazo zimeidhinishwa na Bunge katika huduma muhimu za jamii kama maji, matokeo yake ni kuwa na huduma mbovu, ni dhahiri kwamba kupungua huku kwa kiwango cha bajeti katika sekta ya maji kunapingana hata

na Azimio la Sharm el Sheikh la nchi za Umoja wa Afrika la mwaka 2008 la kutaka dhamira na azma ya kuongeza kipaumbele cha kisiasa katika utengwaji na kuwekwa wazi kwa bajeti kwa ajili ya sekta ya maji safi na maji taka. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuchukulia sekta ya maji kama sekta kichocheo cha maendeleo ya uchumi na hivyo bajeti yake inatakiwa kuongezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa programu ya maji na usafi wa mazingira vijijiini. Tangu mwaka 2000 Bunge hili limekuwa likipewa ahadi za utekelezaji wa Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijiini (RWSSP). Wakati maeleo ya kuanza kwa mpango huo yalipoletwa Bungeni mwaka 2003, wakati huo ukiitwa mpango wa Vijiji kumi (*quick wins*), yapo maeneo katika Jiji la Dar es salaam ambayo yalikuwa na Vijiji na yallingizwa katika mpango huo. Hata hivyo, mpaka leo miaka takribani kumi baadaye mwaka 2013 maeneo hayo yakiwa yameshapanda hadhi na kuwa mitaa miradi hiyo haijatekelezwa kwa ukamilifu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Programu hii ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijiini ilipaswa kutekelezwa kwa awamu nne, ambapo utekelezaji wa awamu ya kwanza baada ya kucheleweshwa toka mwaka 2003 ulipaswa kuanza mwaka 2005/2006 na kukamilika mwaka 2010/2011. Kwa maneno rahisi ni kwamba hadi kufikia hivi sasa ilipaswa tayari maji yawe yameshapatikana katika Vijiji kumi vya kila Halmashauri nchini, hata hivyo ukomo wa muda wa awali ukiwa umeshapita kwa zaidi ya mwaka mmoja; utekelezaji katika maeneo mbalimbali nchini haukufanyika hata robo. Mfano ni katika Wilaya ya Karatu ambapo kati ya Vijiji kumi vilivyoahidiwa, ni kijiji kimoja tu mradi umeanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali iko hivyo, wakati ambapo fedha zimetumika bila maji kupatikana; katika hatua hiyo ya kwanza jumla ya shilingi bilioni 96.4 zimetumika kwenye "quick wins" hadi kufikia mwanzoni mwa mwaka 2012 ilhali maji katika maeneo mengi hakuna hadi sasa; hali ambayo ni matumizi mabaya ya rasilimali za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ripoti ya Tathmini (*Appraisal Report*) ya Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (*Rural Water Supply and Sanitation Program*) ya mwaka 2010 inaonyesha namna ambavyo awamu ya kwanza kati ya mwaka 2007 mpaka 2010 ilivyoshindwa kutekelezwa kwa ufanisi. Kambi ya Upinzani Bungeni inataka uwepo usimamizi wa kutosha wa Kibunge kuhakikisha awamu ya pili (*RSSWP Phase II*), ambayo awali ilipangwa ifanyike kuanzia mwaka 2011 mpaka 2014, inafanyika kwa kuanza na ukaguzi wa awamu iliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba iliyotolewa Bungeni na Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji mwezi wa Februari, 2011, ikiwa ni Kauli ya Serikali Kuhusu Utekelezaji wa Programmu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini; ukiangalia taarifa hiyo jedwali la 4 linalosema "Visima vilivyochimbwa katika Halmashauri ya Hanang' ni 25". Taarifa inaonyesha Hanang vilichimbwa Visima 15 na visima vyenye maji ni 8. Katika wilaya ya Karatu mradi huo wa vijiji kumi ni kijiji kimoja tu ndipo mradi umeanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa iliyotolewa na Halmashauri ya Wilaya ya Hanang tarehe 25.02.2011 ikiwa ni baada ya Mheshimiwa Waziri wa Maji kutoa kauli ya Serikali kuhusu utekelezaji wa Programu ya Maji inaonyesha kuwa mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (*RWSSP*) katika vijiji 10 (Hirbadaw, Wandela, Gawawja, Galangal, Darajamede, Ishponga, Simbay, Gidagarbu, Getasam na Ng'aida) hakuna kazi yoyote iliyofanyika, bali hadi kipindi hicho usanifu mitandao na uandaaji wa nyaraka za zabuni ndio uliofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa maelezo ya usahihi wa takwimu zake kuhusiana na miradi hiyo ya maji kwenye Wilaya ya Hanang' na kwингineko nchini. Vilevile, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa maelezo ya kina yenye usahihi wa takwimu zake kuhusiana na program ya maji na usafi wa mazingira Vijijini katika Wilaya mbalimbali hapa nchini.

Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Serikali kutoa taarifa juu ya matumizi ya shilingi billioni 96.4 za mradi wa maji safi na mazingira Vijiji katika Jiji la Dar es Salaam na Halmashauri zote nchini ili kasoro hizo zisijirudie katika awamu ya pili ya programu hiyo inayotarajiwa kuanza mwezi Juni mwaka 2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, mabonde ya usimamizi wa rasilimali za maji. Nchi ya Tanzania imejaliwa kuwa na vyanzo vya aina mbalimbali vya maji. Vyanzo hivyo ni mito, maziwa, ardhi oevu na maji chini ya ardhi. Wizara ya Maji na Umwagiliaji imeweka utaratibu wa usimamizi wa rasilimali za maji katika ngazi za mabonde ili kuweza kuleta usimamizi endelevu wa rasilimali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na vyanzo vingi vya maji, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Serikali kutoa maelezo ya kina, je, Mamlaka ya Usimamizi ya Mabonde ya Maji inavitumiaje vyanzo hivyo kwa uzalishaji endelevu na hivyo kuondokana na tatizo la upungufu wa chakula unaolikabili taifa letu mara kwa mara? Aidha, tunaitaka Serikali itoe takwimu ni jinsi gani mabonde hayo yanavyoweza kujientesha bila kutegemea ruzuku kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwekezaji katika miradi ya maji. Ripoti ya karibuni kabisa mwaka 2012 ya Shirika la Kimataifa la *Water Aid* juu ya utafiti uliofanywa ukihusisha wataalamu kutoka *Overseas Development Institute* na Chuo Kimoja cha nchini Uingereza (*SOAS*) iliyofuatilia uwekezaji wa miradi ya maji Miji ni katika nchi za Ghana, Burkina fasso na Tanzania (*Strengthening pro poor targeting of investments by African utilities in urban water and Sanitation*) ikiwemo namna miradi mbalimbali ya maji, ilivyoshindwa kuwajali maskini na maeneo mengine kiwango cha hali ya maji safi na salama kutokupatikana kwa urahisi kinyume na malengo yaliyowekwa wakati wa kuanza kwa mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge ni mkakati gani wa makusudi

24 APRILI, 2013

wa kuhakikisha wananchi wanaoishi maeneo ya pembezoni au wenyе kipato cha chini wanapata huduma ya maji kwa gharama/bei nafuu kulinganisha na wanavyolipa sasa. Mfano gari la lita elfu kumi, maji ya yanauzwa kuanzia takribani shilingi 100,000/- hadi 170,000/- kulingana na umbali kutoka kwenye vioski. Lakini watu wenyе vipato vikubwa wanapata maji kwa gharama za chini sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo ya kuwa na mabomba yasiyotoa maji hayapo tu katika mabomba waliyofungiwa wananchi majumbani bali pia kwenye visima na 'vioski'/maghati ya jumuiya. Kuna udhaifu wa kuanzisha miradi ya jamii na kuacha kusimamia uendelevu (*sustainability*) wake na hatimaye baada ya muda mfupi miradi hiyo iliyotumia fedha za umma inabaki kuwa 'miradi hewa'.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti wa vituo vya maji uliofanywa June 2009 na *Overseas Development Institute (ODI)* chini ya udhamini wa Shirika la Water Aid hapa nchini ulibainisha ni asilimia 54 tu ya vituo vya maji vilivypo ndivyo vinatumika kwa kutoa huduma ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo kwa wastani baada ya miaka miwili tu ya kujengwa karibu nusu ya visima na vioski huwa haviendelei tena kufanya kazi. Utaratibu wa kukimbilia kutumia fedha za miradi ya maji kwa mwaka wa kibajeti mpya bila kuzingatia taarifa za utekelezaji na ufuatiliaji wa miradi ya nyuma ni hatari kwa uendelevu wa kuwepo kwa huduma ya maji kwa siku zijazo kama hatua za haraka hazitachukuliwa kuzingatia matatizo yaliyojitokeza katika miradi iliyopita na kuzingatia ubora na ufanisi katika miradi ya maji nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, kweli kwa mtindo huu, Tanzania tunaweza kufikia malengo ya Milenia ambayo yanataka ifikapo mwaka 2015 nusu ya watanzania iliyokuwa haipati maji iwe inapata maji safi na salama?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini utafiti uliotolewa

24 APRIL, 2013

mwaka 2011 wa *Water and Sanitation Programme (WSP)*, unaonyesha kuwa kwa sasa uwekezaji katika sekta hii ni chini ya asilimia 0.1 ya pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji kuwa ikiwa asilimia hiyo ya chini ya 0.1 nayo inategemea kutoka kwa wafadhili, je ni kweli hapa kuna nia na umakini wa dhati wa serikali kujali (uhai) wananchi wake?

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti uliofanywa na *Economic and Social Research Foundation*, umebaini utofauti wa utekelezaji wa miradi ya Serikali na mashirika binafsi katika kuhakiki ubora wa matumizi ya fedha na huduma kwa jamii. Utafiti ulibaini kuwa katika miradi iliyofadhiliwa na mashirika ya maendeleo, wastani wa asilimia 67 ya vioski vilivionekana kufanya kazi; wakati miradi ambayo imefadhiliwa na Serikali ni wastani wa asilimia 45 ya vioski vya maji vilikuwa vikifanya kazi katika maeneo hayo hayo. Utafiti huo ulihusu Mikoa ya Singida na Dodoma. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ni mbaya zaidi kwa upande wa Dar es Salaam ambapo kwa mujibu wa utafiti mwininge wa Shirika la *Water Aid* uliobainisha kuwa asilimia 85 ya vioski vilivyounganishwa Jijini Dar es Salaam havitoi maji, asilimia 10 vinatoa maji kwa kususua na asilimia tano tu ndivyo ambavyo vinatoa maji kwa uhakika. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tafiti hiyo ya miradi inayofadhiliwa na fedha za walipa kodi inaonyesha wizi na ubadhirifu mkubwa na ndio sababu Waziri Kivuli, Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI aliitaka Serikali kuingia ubia na Asasi za Kiraia kufuatilia utendaji wa miradi inayotumia fedha za walipakodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kasoro katika utendaji na uwajibikaji wa mamlaka na vyombo vinavyohusika na utoaji na udhibiti wa huduma ya maji. Majukumu ya utoaji wa huduma ya maji Jijini Dar es Salaam na baadhi ya maeneo ya Kibaha na Bagamoyo yanafanywa na Mamlaka ya Majisafi na Majitaka (*DAWASA*) ambayo ni mmiliki, mkodishaji na

msimamizi wa utoaji wa huduma ya majisafi na maji taka na ina wajibu wa kupanga na kugharamia utekelezaji wa miradi ya miundombinu, kuiendeleza na kugharamia matengenezo ya dharura na makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, muundo wa kimajukumu wa DAWASA hauna tofauti na miundo na majukumu ya mashirika ya maji ya DUWASA-DODOMA, BUWASA-BUKOBA, MOROWASA-MOROGORO, MUWASA-MWANZA, AUWASA-ARUSHA, na kadhalika hivyo basi matatizo ya kiuendeshaji na ubadhirifu yanayoikabili DAWASA yanarandana kabisa na mashirika mengine ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2005, DAWASA illingia mkataba wa miaka kumi (10) wa uendeshaji na Shirika la Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam (*DAWASCO*). Chini ya mkataba huo majumu ya DAWASCO ni kuendesha mitambo, kusimamia usambazaji wa maji na uondoshaji wa maji taka, kuuza maji kwa wateja, kutoa ankara kwa wateja, kukusanya maduhuli, kulipia gharama za uendeshaji, kutekeleza matengenezo makubwa yanayoghamariwa na DAWASA na kutekeleza uunganishaji wa maji kwa wateja wapya kwa kutumia mfuko wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kisheria na kimkataba DAWASA ina wajibu wa kuisimamia DAWASCO iliyoingia nayo mkataba; hata hivyo kwa kuwa yote ni taasisi na mashirika ya umma ambayo bodi zake na watendaji wake wakuu huteuliwa na mamlaka zile zile na kuripoti kwa watu wale wale, hali hii imekuwa na athari kubwa kwenye utendaji na uwajibikaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hauwezi ukazungumzia upatikanaji wa maji safi na na utoaji/udhibiti wa maji taka katika Jiji la Dar es Salaam bila kutaja DAWASCO (*Dar es salaam Water Supply and Sewerage Company*) ambayo imepewa mkataba na Mamlaka ya Maji Safi na Maji taka Dar es Salaam na DAWASA (*Dar es Salaam Water Supply and Sewerage Authority*). Mkataba huu wa miaka kumi ambao DAWASA imeingia na DAWASCO unazidi kutia shaka

wananchi wa Dar es Salaam hasa ukiangalia hali halisi ya upatikanaji wa maji safi na udhibiti wa maji taka katika Jiji la Dar es Salaam ambao hauridhishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhara yaliyotokana na utendaji usioridhishwa wa *DAWASCO* umeelezwa vizuri sana kwenye Hoja Binafsi aliyawasilisha Mbunge wa Jimbo la Uchaguzi Ubungo Mheshimiwa John J. Mnyika katika kikao cha Bunge liliopita. Hoja hiyo ilipendekeza mkataba huo ambao *DAWASA* iliingia kufanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokamilika kwa miradi mingi ya maji ambayo tayari ilishatengewa fedha, kutokutoa maji kwa miradi mingi iliyokamilika mfano mradi wa kusambaza mabomba maarufu kama 'mabomba ya mchina' na baadhi ya visima viliyvo chimbwa na kuzagaa kwa maji taka katika sehemu mbalimbali ya jiji la Dar es Salaam hasa kipindi cha mvua ni ushaidi tosha *DAWASCO* kama kampuni liliopewa kazi ya kushughulikia tatizo ili imeshindwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati umefika sasa wa mkataba huo kati ya *DAWASA* na *DAWASCO* kuwekwa wazi kwa umma; kufanyiwa tathmini ya miaka zaidi ya mitano iliyopita ya utekelezaji; kufanyiwa marekebisho kwa ajili ya kipindi kilichobaki na kuanza maandalizi ya mfumo bora unaopaswa kuandaliwa baada ya kuisha kwa mkataba huo mwaka 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, *EWURA* na majukumu ya kuthibiti bei ya maji. Utoaji wa huduma ya maji unamhusu pia mdhibiti ambaye ni Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma ya Nishati na Maji (*EWURA*) yenye mamlaka ya kudhibiti utoaji wa huduma, kuidhinisha bei ya huduma ya maji safi na uondoaji wa maji taka pamoja na kutoa leseni za uendeshaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, *EWURA* imekuwa ikitoa kipaumbele zaidi kwenye kutumia mamlaka yake kudhibiti kwa karibu sekta ya nishati, huku udhibiti kwenye sekta muhimu ya maji hususan kwa upande wa watoa huduma binafsi ukiachwa uwe katika mfumo wa soko holela

na kuchangia katika ongezeko la bei ya maji pamoja na ubovu wa huduma. Huu ni udhaifu mkubwa kwa upande wa *EWURA* ambayo kimsingi iko chini ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji lakini utaona kazi zao (za udhibiti) kubwa zinafanyika kwenye Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya *The Energy and Water Utilities Regulatory Authority Act* (Sura ya 414), kifungu cha 6 ambacho kinaelekeza bayana kwamba wajibu wa *EWURA* ni pamoja na kulinda maslahi ya walaji na kuhamasisha upatikanaji wa huduma inazozidhibiti ikiwemo maji wa watumiaji wakiwemo wa kipato cha chini na walio pembezoni au katika mazingira magumu (*low income and disadvantaged consumers*). Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 7 cha sheria hiyo majukumu ya *EWURA* ni pamoja na kupanga viwango cha ubora, viwango vya ugavi, kufuatilia utendaji ikiwemo uwekezaji na upatikanaji, kudhibiti bei na tozo na kushughulikia malalamiko na migogoro. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwaeleza Watanzania ambaao kwa kiasi kikubwa wanatumia huduma ya maji inayotolewa na mamlaka za maji nchi nzima kuwa, chombo cha kuangalia na kudhibiti ubora na viwango vya maji kimeshindwa ila kimejikita kwenye udhibiti wa mafuta ya petrol na dizeli, hivyo wao watafute njia mbadala ya kuwajibisha watoa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango maaalum wa kutatua tatizo la maji katika Jiji la Dar es Salaam. Mradi wa visima virefu Kimbiji na Mpera. Moja ya mikakati ambayo Waziri alilieleza Bunge wakati wa kutoa Kauli ya Serikali kuhusu mpango wa kutatua tatizo la maji katika Jiji la Dar es Salaam mnamo 7 Novemba, 2012 ni uchimbaji wa visima ishirini (20) katika maeneo ya Kimbiji na Mpera na kujenga bomba la kusafirishia maji kutoka maeneo hayo mpaka Jijini Dar es Salaam ambapo pia matanki ya kuhifadhi maji yanategemewa kujengwa. Mradi huu unategemewa kuongeza kiwango cha maji yanayo ingia Dar es Salaam kwa lita milioni 260 kwa siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa ahadi ya Waziri wa Maji ni kuwa Visima vya Kimbiji na Mpera

vilitigemewa kuanza kuchimbwa mwezi Januari, 2013 na kukamilika mwezi Juni, 2015. Hadi sasa uchimbaji wa visima hivi haujaanza na adha ya upatikanaji wa majisafi katika Jiji la Dar es Salaam imezidi kuongezeka badala ya kupungua kama serikali ilivyo ahidi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kueleza kwa nini mradi huu umechelewa kuanza tofauti na ahadi iliyolewa na Serikali kuhusu kuanza kwa mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Bwawa la Kidunda. Mpango wa kujenga bwawa la Kidunda ambalo pia ni sehemu ya kuokoa Jiji la Dar es Salaam katika uhaba wa maji uliokithiri bado unasuasua. Serikali iliahidi kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi huo katika mwaka wa fedha 2012/2013 ili kuwezesha mradi huo kuanza katika mwaka wa fedha 2013/2014. Hata hivyo, mradi huu ambaao ullikadiriwa kugharimu billioni 175 hadi sasa hata fidia kwa wananchi watakaopisha mradi hazijalipwa na kwa mwaka wa fedha 2013/2014 ambapo mradi huu ulitegemewa kuanza umetengewa shilingi bilioni tatu (3) tu nazo ni kwa ajili ya kulipa fidia na si kwa ajili ya kuanza kazi ya ujenzi wa bwawa hili lililoelezwa kuanza kujengwa katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kasi ya utekelezaji wa miradi ya Ruvu juu na Ruvu chini ambayo ndio kitovu cha upatikanaji wa maji katika Jiji la Dar es Salaam na mpango wa kukarabati miundombinu ya maji katika Jiji la Dar es Salaam hauridhishi. Ikumbukwe kuwa ahadi ya Serikali ya kumaliza tatizo la majisafi katika Jiji la Dar es Salaam kufikia 2013 lilikwama kutokana na Serikali kuwa na mipango mingi kwenye karatasi na isiyotekelizuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuchukua hatua za haraka zaidi kuhakikisha miradi hii inakamilika kwa wakati uliopangwa. Pia miradi hii lazima iendane na kasi ya usambazaji wa mabomba ya maji katika kaya za wananchi ambazo hazijafikiwa na mabomba ya maji katika maeneo mbalimbali ya Jiji.

24 APRILI, 2013

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama za maisha ya wakazi wa Dar es Salaam zimepanda mno, huku tatizo la upatikanaji wa maji liliwa moja ya chanzo cha kupanda kwa maisha. Kwa sasa maji lita 20 yanauzwa kuanzia shilingi 300 na 700 katika maeneo mbalimbali katika Jiji hilo. Hii inasababisha maisha ya watu wa kipato cha chini kuwa magumu na kupelekea hatari ya kukumbwa na magonjwa ya mlipuko kutokana na mazingira wanayoishi kutokuwa safi kwa sababu ya kukosa maji safi na salama kwa ajili ya matumizi mbalimbali. Serikali hii, sikivu, kama inavyopenda tuamini inabidi iangalie suala hili la upatikanaji wa maji katika Miji mbalimbali nchini na Jiji la Dar Es Salaam ikiwa sehemu mojawapo ili kuokoa muda ambao wananchi wana utumia kutafuta maji na kuboresha maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujisadi katika miradi ya maji nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kumbukumbu Rasmi za Bunge, alipokuwa anachangia Mbunge wa Bukombe, Mheshimiwa Prof.Kahigi alisema nanukuu:-

*"Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya bajeti, Bukombe imetajwa kuhusiana na miradi ya Maji ya Benki ya Dunia. Bukombe imetajwa katika jedwali Na.12 ukurasa 98. Wilaya ilipokea Sh. 2,902,990,461 kati ya mwaka 2007 - 2012 kwa ajili ya miundombinu na Sh.144,266,260 kwa ajili ya kujenga uwezo. Swali ninalotaka nijibiwe ni je, fedha hizi zote zilitumika katika miradi ipi?"*

*Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya bajeti, Bukombe pia imetajwa kwamba ilichimba visima 16 na vyenye maji ni 15. Je, Waziri anaweza kuniambia visima hivyo 16 au 15 viko wapi ?" Mwisho wa kunukuu.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa ufanuzi wa kina kuhusiana na matumizi ya fedha hizo alizohojii mwakilishi wa wananchi katika Jimbo hilo kwani hayajawahi kutolewa majibu kuhusiana na fedha hizo na miradi ambayo ilitajwa katika

24 APRIL, 2013

maelezo hayo ya Mbunge, kama ambavyo awali ilikuwa imesomwa kwenye Kauli ya Serikali Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mfululizo huo huo, Mbunge wa Jimbo la Urambo Magharibi Mheshimiwa Prof.Kapuya naye alihoji kama ifuatavyo, nanukuu:-

*"Kuhusu vijiji vya Kaliua Mashariki, Kaliua Magharibi na Ushokola ambavyo kwa ujumla wao ndiyo vinaunda Makao Makuu ya Wilaya, vilikuwa miongoni mwa vijiji hivyo. Wananchi tulichangisha na tukatimiza hizo millioni tano kwa kila kijiji jumla shilingi milioni 15 ili tupate shilingi milioni 600 toka Benki ya Dunia. Tulipata surveyor wa maji toka Mkoani Tabora akaja kupima na kuelekeza mahali ambapo maji yatapatikana. Kampuni ya kuchimba visima ikaja kuchimba, kwa bahati mbaya visima tisa kati ya 12 vilivyochimbwa vilikuwa havina maji katika vijiji hivi. Kwa Viji vya Kaliua Mashariki, Kaliua Magharibi na Ushokola ni kisima kimoja tu ndiyo kilipatikana na maji. Kwa hiyo, vijiji hivi havina maji mpaka leo.*

*Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanauliza maswali yafuatayo:-*

- (a) *Katika hali kama hii mwenye kosa ni nani? Wao si Wataalam wa Maji, wameambiwa wachange wamechanga tena kwa shida sana. Leo wanaambulia mashimo tu.*
- (b) *Hasara hii aibebe nani?*
- (c) *Lini watapata maji?*
- (d) *Je, fedha yao watarudishiwa?" Mwisho wa kunukuu*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri alijibu:-

*"Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini imetokea matatizo; watu wamelipwa fedha, wamechimba visima vile vya uchunguzi havina maji, wakaenda hatua mpaka ya kujenga miundombinu wakati wanajua maji hayapo! Niseme kwamba, hili ni tatizo la utekelezaji, ambalo sisi kama Wizara tumelichukua na tunaendelea kulifuatilia"*

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni utapeli uliofanywa na makampuni hayo, tunataka Serikali itoe taarifa ni kesi ngapi za makampuni mangapi ya kitapeli kama haya, ziko Mahakamani hadi sasa? Utapeli wa namna hii unaofanywa na wakandarasi kwa kushirikiana na watendaji wa Serikali umeenea sana maeneo mengi ya nchi hii. Jambo hili kwa kiasi kikubwa limepelekeea wananchi waendelee kupata taabu ya maji. Tunataka kujua hatua gani za kisheria zimechuliwa kwa wakandarasi hao waliohusika pamoja na wengine wengi ambao wamefanya hivyo kwenye maeneo mengi katika nchi yetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la ujisadi mkubwa na wa kutisha katika miradi mbalimbali ya maji hapa nchini ndio jambo ambalo limepelekeea wananchi wengi kuteseka kutokana na kukosa maji safi na salama na hivyo kujikuta wakikumbwa na magonjwa mbalimbali ya milipuko katika maeneo mengi nchini. Hapa Kambi Rasmi ya Upinzani itataja baadhi ya miradi ambayo kutokana na ujisadi wananchi wamekoseshwa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mabomba ya ‘Mchina’ yamekuwa bila maji na miradi hewa katika maeneo ya wananchi wa kipato cha chini Jijini Dar es Salaam. Kati ya mwaka 2003 mpaka 2010, Serikali ilitekeleza Mradi wa Ukarabati na Upanuzi wa Miundombinu ya Majisafi na Majitaka Jijini Dar es Salaam na maeneo ya Bagamoyo na Kibaha (*Dar es Salaam Water Supply and Sanitation Project-DWSSP*). Mradi huo uliotumia dola milioni 164.6. Hata hivyo, hadi sasa katika maeneo mengi, mtandao wake maarufu kama mabomba ya ‘Wachina’ hautoi maji huku kukiwa na upungufu katika uzalishaji, upotevu wakati wa usafirishaji, udhaifu katika usambazaji na tuhuma za ujisadi katika matumizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba kuwasilisha. (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Cecilia Paresso, kwa usomaji wako kwa niaba ya Kambi ya Upinzani. Nakushukuru pia kwa sababu ya kutumia muda vizuri; ahsante sana.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**NAIBU SPIKA:** Sasa namwita Mheshimiwa Kangi Lugola.

**MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako, ukurasa wa 61 kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Naomba kwa ruhusa yako nisome maneno haya anasema: "Katika Mji wa Bunda kazi ya kulaza bomba lenye urefu wa kilomita 23.5 kutoka kwenye chanzo hadi kwenye matanki illiendelea katika mwaka 2012/2013."

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona niombe mwongozo wako, Wananchi wa Bunda wanaomsikiliza Mheshimiwa Waziri wameshangazwa sana na kauli hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa ninavyozungumza, hakuna bomba hata moja ambalo limelazwa kwenye Mradi huo wa Maji wa Bunda na Bunda wana tatizo la maji la muda mrefu. Kitendo cha kuwapaka asali kwenye mdomo Wananchi wa Bunda kwa kauli hii, nimesikitika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba Mheshimiwa Waziri na nipo tayari kuweka rehani Ubunge wangu, mimi ni mdau mkubwa wa maji haya, atuthibitishie hii kauli kaitoa wapi na hata mitalo yenyewe kuchimbwa haijakamilika. Wizara haitaki kupeleka pesa watalaza mabomba gani watalaza miti.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Mheshimiwa Waziri ama afute kauli yake hii, kwa sababu siyo ya kweli na kwenye suala la maji Wananchi wa Bunda hatutache ka na

mtu, hatutamwangalia Waziri usoni. Leo tunataka kuja ukweli juu ya kauli hii ameitoa wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako tutachukua hatua gani kwa kauli kama hii kwa Waziri kwa kuwamaanisha Wananchi wa Bunda kwamba mabomba yanalazwa ilhali hakuna cha mabomba; tutachukua hatua gani kwa Mheshimiwa Waziri huyu? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kangi Lugola, nakushukuru kwa ushauri ulioutoa kwa Kiti na Serikali. Ujumbe wako umefika. Ushauri wangu ni kwamba, kwa sababu tunaanza mjadala wa mambo haya, Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha hoja yake ni moja ya mambo ambayo atayafafanua vizuri tu.

Sasa wachangiaji wangu ni wengi, naomba tuokoe muda twende moja kwa moja. Wachangiaji wangu wa kwanza watatu watakuwa Mheshimiwa Esther Lukago Midimu, Mheshimiwa Amina Amour ajiandae na Mheshimiwa Susan Lyimo atafuatia. Mheshimiwa Esther Lukago.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia. Maji ni uhai, maji ni afya. Mwaka 2011 nilisimama hapa nikaomba maji na leo nimesimama tena naomba maji Mkoa wa Simiyu. Mwaka 2011 nilliomba Wizara ipeleke maji Simiyu, lakini mpaka sasa hatuoni kitu chochote kinachoendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Simiyu tumejaliwa kuwa na vyanzo vya maji, tuna Mto Simiyu, tuna Mto Duma na tuna Mto Manonga na pia tupo jirani na Ziwa Victoria. Tunaiomba Serikali ifikirie sasa kuvuta maji kutoka Ziwa Victoria kuleta kwenye Wilaya zetu; Wilaya ya Bariadi na Wilaya ya Maswa, Wilaya ya Meatu na Wilaya ya Busega. Huo ndiyo utakuwa Mradi pekee wa kuweza kusuluuhisha tatizo la maji Mkoa wa Simiyu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ipeleke maji Wilaya ya Busega katika Kijiji cha Chingara, Mwasamba

na Sanga. Wanawake wa Wilaya ya Busega wanahangaika sana na maji, kiasi kwamba wameshindwa kufanya shughuli zingine za maendeleo kutwa nzima wanatafuta maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wanatembea zaidi ya kilomita 16 kutafuta maji, hata wanafunzi wa shule ya msingi wanaotoka katika vijiji hivyo, naomba uamini wanaenda shuleni bila kuoga, kwa sababu ya uhaba wa maji. Naiomba Serikali bwawa liliopo Mwanjoro, Wilaya ya Meatu, limalizike ili liweze kusaidia Wananchi wa Wilaya ya Meatu. Wananchi wa Wilaya ya Meatu wanateseka na maji, wanachimba maji chini lakini pia wanavuna maji ya mvua kwenye mapipa; inasikitisha sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ilifufue Bawawa la Bariadi ili Wananchi wa Bariadi tuweze kupata maji mapema iwezekanavyo. Wananchi wa Mkoa wa Simiyu siyo wavivu, tunaweza kufanya kazi, tuleteeni maji tulime kilimo cha umwagiliaji ili tuweze kujikomboa na umaskini. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, Bwawa la Kijiji cha Habia limeanza kuchimbwa mwaka 2009 mpaka leo halijakamilika. Wananchi walinyang'anywa mashamba wakitegemea kwamba watapata maji, mpaka leo hakuna maji wala hakuna mashamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ichimbe visima kwenye shule za sekondari, wanafunzi wanahangaika kuchota maji wakitoka shuleni jioni, matokeo yake asubuhi wanashindwa kusoma na hata kumsikiliza mwalimu hawawezi kwa sababu ya kusinzia. Naomba Serikali ifanye hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Esther Midimu, kwa uchangiaji wako mzuri sana na kwa kweli umeutumia muda vizuri sana; nakupongeza.

Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Amina Amour, atafuatiwa na Mheshimiwa Susan Lyimo. Mheshimiwa Amina Amour.

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nitajikita kuchangia mambo mawili tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza na suala la uchimbaji wa visima. Pamoja na Serikali kujikita kuchimba visima vingi, lakini utafiti haufanyiki ipasavyo na hii inadhihirisha pale ambapo kisima kimeshachimbwa mpaka mwishoni maji hayatoki na kwa nini hiki kisima kiwe kimeshafanyiwa utafiti halafu maji yasitoke. Hilo ni suala kubwa na mimi sijawahi kuliona. Kule kwetu Zanzibar nilivyozaea na ninavyoona ni kwamba, mahali pakishafanyiwa utafiti lazima maji yatoke.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naishauri Serikali iende kule Zanzibar ikajifunze na ikatafute wataalam wanaochimba visima. Fedha nyangi za Serikali zinapotea kwa sababu ya utafiti na matokeo yake kwa kila visima kumi, vitatu havitoi maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nami siungi mkono hoja hii mpaka Mheshimiwa Waziri aniambie kuwa atakwenda Zanzibar kufanya utafiti. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, hii bajeti ni ndogo sana. Kwa kweli Serikali haiko *serious* kutatua tatizo la maji, hii ni bajeti ndogo mno. Naiomba Serikali vyovyote iwavyo, waende wakakope, bila ya kukopa tukapata fedha za kutosha, itakuwa kila siku tunaendelea kupeleka Sekta ya Maji lakini tatizo lipo hapo hapo. Sasa naiuliza Serikali kwa nini inafanya kigugumizi kwenye kukopa? Tatizo wanasema deni kubwa! Deni kubwa lisiwashughulisheni, ninyi mnajiamini, lazima mfanye maamuzi magumu.

Kwa nini msiamue tukaenda kukopa fedha hizi tukapeleka kwenye maendeleo? Ingekuwa fedha zile zinapelekwa kwa mambo mengine lakini maendeleo

yatapatikana; kwa nini hamji na maamuzi magumu mkaenda mkakopa mkamaliza tatizo la maji lote kwa mwaka huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiendelea tena kuhusu wizi wa maji Dar es Salaam ni mkubwa mno. Tunasoma kwenye magazeti wanakamatwa hawa, naomba *DAWASCO* wafuatilie kila nyumba wapatikane watu wanaoiba haya maji kwa wingi halafu wanakaa wanayauzu kwa fedha nyangi na Serikali inapata hasara. Pia kuna wengi wanakosa maji kutokana na watu wengine wanachukua maji kwa wingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la nne, nitazungumzia kidogo kuhusu hawa wenyewe makampuni makubwa. Kuna makampuni makubwa yanatumia maji kama Azam, kuna *Tanzania Breweries* na makampuni mengine. Pamoja na kwamba, yanalipa lakini ipo haja ya Serikali kuyafuata makampuni haya ikayaambia yachangie maji. Wajikite wote wachangie Sekta ya Maji na hizo fedha zikipatikana zitaweza kuisaidia Sekta ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu bajeti kuwa ndogo, nimeombia Serikali iende ikakope, isiwe na kigugumizi, bila kukopa tatizo la maji litaendelea na ufumbuzi hautopatikana. Tayari tunaweka vipaumbele vingi, kwa nini tuweke vipaumbele vingi tusiweke viwili tu tukimaliza mwaka mwingine tufanye vingine viwili? Safari hii tujikite kwenye maji na elimu na tukishamaliza tatizo la maji na elimu, bajeti inayokuja tutakuja na mambo mengine, japokuwa tuna mpango wa mwaka huu lakini tufumbe macho kwa yale mengine tumalize tatizo la maji na tatizo la elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amina Amour, nakushukuru sana. Mheshimiwa Suzana Lyimo, atafuatiwa na Mheshimiwa Saleh Pamba.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze

kuchangia katika Sekta hii muhimu ya Maji, kama ambavyo wenzangu wamesema na inajulikana kwamba maji ni uhai na maji ni kila kitu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na bajeti. Kama kweli maji ni uhai, lakini tumeshuhudia ni jinsi gani bajeti ya maji inaendelea kuwa finyu mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia bajeti ya mwaka jana ya maendeleo, illikuwa shilingi 465,756,000,000, wakati bajeti ya mwaka huu ya maendeleo ni shilingi 379,000,000,000; hii ikiwa na maana kwamba, tuna upungufu wa shilingi zaidi bilioni 86 huku tukitaka kusema kwamba, tunataka kuhakikisha Wananchi wanapata maji safi na salama. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wote tunatambua kwamba, Tanzania zaidi ya nusu ya wagonjwa, watoto wa chini ya miaka tano, kila zaidi ya watoto 20,000 wanafariki kwa sababu ya magonjwa yanayotokana na maji machafu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa takwimu hizi ni wazi kwamba, tunapoteza nguvu kazi na vilevile ni wazi kwamba, bado Serikali haijalipatia ufumbuzi wa kina tatizo la maji hapa nchini. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia takwimu zinaonesha wazi kwamba, huduma za maji vijiji na mijini fedha zake zimekuwa zikipungua. Jambo la kushangaza na hapa nikubaliane na Mheshimiwa aliyesoma Hotuba ya Kambi ya Upinzani na Kamati inayoshughulikia Wizara hii. Pamoja na kwamba, Wananchi zaidi ya asilimia 75 wanaishi vijiji lakini fedha iliyotengwa kwa ajili ya vijiji mwaka hadi mwaka, kwa mwaka huu ni shilingi bilioni 75 wakati ile ya mijini ni shilingi bilioni 254 na wakati huohuo mijini tuna watu asilimia 25 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazi kwamba, Wananchi wa Vijiji ndiyo wazalishaji wakubwa, lakini athari zake ni nini?

Takwimu zinaonesha na ni wazi kwamba, akina mama na watoto wanatembea zaidi ya kilomita kumi, wanatumia zaidi ya saa mbili mpaka saba kila siku kwa ajili ya kwenda kuteka maji na maji hayo ni ndoo moja tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inaonesha ni jinsi gani sasa akina mama hawa na watoto hawa wanashindwa kuzalisha au kufanya kazi nyingine za maendeleo katika Taifa hili huku wakitafuta maji tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala la elimu, tumeona ni jinsi gani baadhi ya shule zimefungwa kwa sababu ya ukosefu wa vyoo. Vilevile hawana umeme kwa sababu ya maji. Haya ni matatizo makubwa na kama kweli Serikali haitalipa kipaumbele suala la maji, tunaenda kupoteza nguvu kazi ya Taifa hili na tunapoteza vijana. Tumeona jinsi gani wanafunzi wanatumia kigezo cha kutokuwa na maji katika utoro. Tumeona jinsi gani watoto wanatoroka mashulen i kwa sababu wanakwenda kutafuta maji na watoto wa kike wakipata mimba kutokana na haya haya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ihakikishe tatizo la maji linapatiwa ufumbuzi wa kina.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwa kweli nchi yetu imejaliwa vyanzo vingi sana vya maji, maji yaliyopo kwenye *surface* lakini vilevile maji ya *underground*.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba, sisi tunawazidi Wakenya kwa maji mara tatu na Waganda kwa asilimia 37, lakini bado takriban nusu ya Watanzania hawapati maji safi na salama; hii ni aibu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwenyezi Mungu ametujalia vyanzo vya maji; kwa mfano, tuna mito mikubwa, achilia hii midogo midogo, mito mikubwa 11 hapa nchini na labda niitaje; kuna Ruaha, Kagera, Kalambo, Malangarasi, Mara, Rufiji, Ruvuma, Rufirozo, Thibitihuba na Wami, lakini bado vyanzo hivi havitumiki vizuri. Vilevile tuna Maziwa Makuu

ambayo sitaki kuyataja, bado Serikali haijafanya kazi yake ya kuhakikisha Wananchi wanapata maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani mtu anazunguka Ziwa Victoria halafu hapati maji. Haiwezekani mtu yupo karibu na mto hapati maji. Kwa nini hatupati maji, maji yetu yote yanaenda mpaka Misri lakini wale waliopo pale wanakosa maji! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ihakikishe inalipatia ufumbuzi wa kina.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije katika maeneo yangu na niseme tu, nimefurahishwa sana na naomba Wananchi wa kule Moshi Vijiji wafurahie; nimesoma ukurasa wa 145 na ninamshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri wakati ule Mheshimiwa Christopher Chiza, tulienda naye Moshi akaona matatizo na leo hii naomba niseme kwamba, Wananchi wangu wa kule Kolini Kusini na Kolini Kaskazini wafurahie kwamba Mradi wa Maji utakuwa tayari mwaka huu na niwapongeze sana Wananchi hao kwa juhudhi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na chanzo hicho cha maji, Wananchi wa Kijiji cha Kolini Kusini waliamua kuchanga fedha kwa ajili ya kuweza kupata maji katika chanzo kingine cha Chemchemi ya Mangi pale Rahu. Wamejitahidi sana kwa nguvu zao, lakini bado wanahitaji Serikali iweze kuwasaidia na ninaamini kabisa Serikali itawasaidia ili Wananchi hawa wasitegemee chanzo kimoja tu, kwa sababu watu wa Kilimanjaro pamoja na kwamba kuna ukame, lakini pale ambapo kuna maeneo yenye vyanzo vya maji, Wananchi wanaomba juhudhi ya kuchangishana, basi Serikali iweze kuwasaidia na waweze kupata maji safi na salama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi kama mwanamke, naomba niseme tu kwamba ni wazi pamoja na kwamba wanawake wanafanya kazi kubwa sana, lakini wote tunajua kwamba tuna tatizo kubwa la UKIMWI nchini na wale wagonjwa wa UKIMWI mara zote akina mama ndiyo

wanakuwa wanawasaidia. Tunatambua kwamba, wagonjwa wanapofikia zile *stages* za mwisho wanahitaji maji mengi sana na hawa akina mama wanachukua muda mrefu sana kwenda kuchota ndoo moja. Kwa hiyo, ninaomba sana Serikali ihakikishe inawekeza vijijini kwa sababu kule vijijini kuna matatizo makubwa sana ya maji kuliko hata mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, niseme kwa Dar es Salaam nimepata taarifa, ni wazi kwamba, tumelizungumza suala la wizi wa maji, lakini naambiwa kwamba sasa hivi kumekuwa na operesheni kubwa sana ya kukamata watu hawa. Mimi nakubaliana na Serikali, lakini naambiwa zoezi lile limechukua sura mpya kwamba, sasa wanakamata watu ambao hata hawahuksiki na vilevile wamekuwa wakichukua rushwa kwa Wananchi hao. Kwa hiyo, ninaomba Serikali ihakikishe zoezi hili linaleta manufaa na kuhakikisha hawawatendei vibaya Wananchi ambao hawana hatia. Wale wenye hatia wakamatwe lakini wasio na hatia, ninaiomba sana Serikali iliangalie jambo hili kwa kina.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie vilevile kwa kusema, suala la Bwawa la Kidunda Dar es Salaam ni wazi katika hotuba ya mwaka jana, Mheshimiwa Waziri alisema kwamba, fedha zimeshatengwa kwa ajili ya fidia, lakini mpaka leo hawajapata.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa  
muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Saleh Pamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Mchungaji Getrude Rwakatare.

**MHE. SALEHE A. PAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niungane na wenzangu katika kuchangia Hotuba ya Wizara ya Maji. Kwanza, napenda niseme kwamba, naunga mkono Hotuba hii asilimia mia kwa mia. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Chama cha Mapinduzi kilipoenda kutafuta kura kwa Wananchi tuliahidi katika llani yetu ya Uchaguzi kwamba, tutaondoa tatizo la maji vijijini kwa asilimia 65 na tutaondoa tatizo la maji mijini kwa asilimia 90. Hadi sasa kufuatana na Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, tumefikia asilimia 57 vijijini na tumefikia asilimia 75 mijini. Hiyo ni hatua kubwa sana na lazima tuipongeze Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Kwa sababu katika miaka miwili iliyobaki kwa upande wa vijijini nina hakika kabisa kwa Miradi ambayo imetajwa na Mheshimiwa Waziri katika Hotuba hii, ina-cover nchi nzima pamoja na Mji wa Karatu kwamba tutafikia asilimia 90 na asilimia 65 kwa wananchi wetu walio vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumzie masuala matatu makubwa ambayo yametajwa kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Suala la kwanza linahusu umuhimu wa kutunza vyanzo vya maji. Nimepitia katika taarifa mbalimbali hasa Taarifa ya *Water Aid* na Taarifa ya Benki ya Dunia ya mwaka jana. Katika Taarifa hizo mbili wanasema nini kuhusu Tanzania kuhusu hali ya maji. Wanasema kwamba, kutokana na tatizo kubwa la ongezeko la watu (*population growth*), pamoja na masuala mengine ya kuharibu vyanzo vya maji katika miaka mitano ijayo, itakapofika mwaka 2020, Tanzania tutakuwa na kitu ambacho kinaitwa *water stress*, tutakuwa na tatizo kubwa sana la maji. Kwa hiyo, ninachoiomba Serikali ni kwamba, iendelee kutenga fedha za kutosha hasa katika kuhifadhi vyanzo vya maji.

Hivi sasa tumetenga asilimia 8.5, ambalo ni jambo zuri sana, lakini Kimataifa wanasema kwamba, lazima tutenge angalau asilimia kumi ya bajeti ya maji kwa ajili ya kuhifadhi *water resources*. Naiomba Serikali yangu kwamba, tumetenga fedha safari hii shilingi bilioni 19.7, natumaini katika bajeti ijayo na hasa kutokana na matatizo haya yanayotokana na uharibifu wa vyanzo vya maji, basi tutatenga bajeti ya kutosha ili tusipate tatizo hili ambalo Benki ya Dunia inazungumzia juu ya suala la *water stress*.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ambalo nataka kulizungumzia ni la jumla na limezungumzwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Mifugo na limezungumzwa na Wabunge waliotangulia, nalo ni suala la bajeti ndogo ya maji. Bajeti hii kwa sasa hivi tunaiona ndogo, lakini kihistoria bajeti hii imeendelea kukua mpaka kufikia shilingi bilioni 380. Tatizo kubwa tunalolipata katika bajeti hii ni uwiano mdogo uliopo kati ya bajeti hii hasa kwa maji mijini na maji vijijini. Lazima tufike mahali ambapo tunabadilisha mwelekeo huu tupeleke nguvu zetu za maji hasa kule vijijini ambapo Watanzania asilimia 80 wanaishi. Kwa mfano, katika bajeti ya shilingi bilioni 380 ambayo tutaitisha baadaye, ni asilimia 30 tu ya bajeti hiyo tunapeleka vijijini. Lazima *trend* hii tubadilishe ili tuweze kuhakikisha kwamba, vijijini nako wanapata maji na tukipata maji vijijini, yatatusaidia katika maeneo mawili makubwa sana kwa upande wa Serikali na kwa upande wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, tukipeleka maji safi na salama vijijini tunapunguza magonjwa, tunapunguza maradhi yanayotokana na maji au wanaita *waterborne diseases* na tunapunguza gharama zetu za kununua madawa katika zahanati. Fedha ambazo tutazi-save tutazitumia katika maendeleo mengine katika nchi yetu kama kilimo, elimu na kadhalika. Kwa hiyo, naomba Serikali ihakikisha tunabadilisha mfumo huu wa bajeti. La pili ni kwamba, ukiangalia katika bajeti hii ya maji, sehemu kubwa sana ya fedha ambazo tumezitenga ni za wafadhili. Kwa hiyo, tunatakiwa tubadilishe hiyo *trend* ili tuingize fedha zetu wenyewe kama tulivyofanya katika barabara, kama tulivyojenga barabara kwa fedha zetu wenyewe tuendelee hivyo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kutoa shukrani zangu kwa Wizara ya Maji hasa kwa Jimbo langu la Pangani. Mheshimiwa Waziri na Wizara yake, imenipatia shilingi 260,000,000 kwa ajili ya kukarabati maji kwa Mji wa Pangani; nasema ahsanteni sana. Kwa sababu kwa vyovyote vile Halmashauri ambayo inapata shilingi 10,000,000 kwa mwezi haiwezi ikatengeneza Mradi kama huu, hii ni hatua kubwa sana. Tunayo mipango ya maji vijijini, tayari

tumekwishawaleta *proposal* zetu, tumeshachagua mkandarasi kwa vijiji vitatu ili tuweze kukamilisha Mradi huo. Kwa hiyo, ninaomba Wizara iharakishe tupate *no objection* kusudi tuendelee, tuhakikishe kwamba katika vijiji vile, katika zile kata tatu ambazo tumeziombea maji, Kata ya Bweni na Kikumbwi zipate *no objection* na Miradi iweze kuendelea kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, napenda nirudie tena kusema kwamba, hatua hii ni nzuri na nina imani tutakopofika mwaka 2015 tutakaporudi kwa Wananchi tena, tutakuwa tumeifikia zile asilimia ambazo tumezisema katika llani yetu ya Uchaguzi. Tumeahidi na nina uhakika kwamba, tutakuwa tumetekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Saleh Pamba, kwa uchangiaji wako. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Kamishna.

Mheshimiwa Dkt. Getrude Rwakatare, atafuatiwa na Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya.

**MHE. MICH. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Awali ya yote, naomba nichukue nafasi hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kwenda Bukoba katika Kijiji cha Igwilibi, kumzika mume wangu Kenneth Rwakatare, ambaye ametangulia mbele za haki tarehe 9 Aprili, 2013. Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi. Mungu alitupa na Bwana ametwaa jina la Bwana libarikiwe; *Amin.*

Pili, napenda kulishukuru Kanisa langu la *Mlimwamoto Assemblies of God Mikocheni*, Viongozi, Wazee wa Kanisa na Waumini wote. Vilevile nawashukuru Wabunge wenzangu waliosikia jambo hili wakanitumia pole hata kwa simu, wengine walinipigia, walinitumia *message* na wengine walikuja nyumbani. Ningependa kusema ahsante kwa mchango wenu wa kunifariji kwa hali na mali. Mungu

awabariki na ninyi mpate kuvuna, leo mimi kesho wewe, sisi ni ndugu. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nijikite katika kuchangia Hotuba hii ya Wizara ya Maji. Kwa masikitiko makubwa, mwanzo kabisa naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Wanasema "Mvumilivu hula mbivu", lakini mimi naona uvumilivu wangu umezidi na sasa utanishinda. Kwa sababu huu ni muhula wangu wa pili Bungeni na ni mara yangu ya nne kusimama kuchangia bajeti ya Wizara ya Maji nikisema habari ya Wilaya ya Kilombero na hasa Miji ya Ifakara na Mji wa Mlimba.

Wakazi wa Kilombero hasa Wanawake na Watoto, wamenituma nimwulize Mheshimiwa Waziri; je, lini Kilombero au Miji ile mikubwa ya Ifakara na Mlimba tutapata maji safi na salama? Maana mara nne kusimama na kuongea jambo moja watu wanasema utu uzima dawa, pamoja na utu uzima wangu lakini ninaona jibu hili halipatikani; inasikitisha. Ninaomba jamani mlifanyie kazi ili watu hawa waweze kupata maji. Jambo la kusikitisha lingine ni kwamba, Wilaya ya Kilombero ina mito 38; mito 38 ni vyanzo vizuri kabisa vyaa maji, lakini hatupati maji ya kudumu, maji safi na maji salama na tukipata tunapata kwa msimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilikuwa naomba mwangalie kama kuna vyanzo vyaa maji mito 38 bado sehemu hiyo inakuwa na uhaba wa maji, inakuwa maji ndiyo tatizo sugu na kubwa kweli tunamaanisha kuwasaidia watu hawa. Kila aliyekuwa Waziri wa Maji, nilimwendea na Mradi wetu tukapeleka lakini sioni majibu. Naomba safari hii hatutavumilia, kama sioni mabadiliko nakwenda kumchukua Waziri na Naibu wake, twende Ifakara na Kilombero mkaone tabu wanayoipata ya wanawake na wakazi wa kule japo tuna vyanzo vyaa maji.

Watu wanaweza kupata maji kutoka Ziwa Victoria yakaenda mbali lakini sisi maji yako palepale kuyapata ni mbinde, tunaishi kwa maji ya visima vyaa mdundiko ambavyo vyenyewe pia ni vyaa muda; inasikitisha sana. Naomba

tushughulike, kwa sababu kitu tunachoambulia Kilombero unakuta ni mafuriko au kitoweo cha samaki, lakini maji kwenye majumba yetu hamna. Hili ni jambo la kusitikisha sana, mpaka twende tukachote na ndoo na vilevile wakati wa kiangazi maji hamna watu wanahangaika, haya mahangaiko yataisha lini? Namwuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji. Kwa mfano, Mji wa Ifakara ni Mji amba miundombinu yake ya maji ni ile ya miaka 1970 au 1980, michakavu, mizee, ya siku nydingi wakati huo wakazi walikuwa 7,000 tu.

Sasa hivi tuna wakazi karibu laki moja, sasa kweli hii miundombinu ya miaka 1980 itatosha; ndiyo maana unaona kuna mahangaiko mengi na masikitiko mengi. Tunaomba mlifanyie kazi sasa hivi Ifakara umekuwa mji mkubwa, umekua, umepanuka; una wakazi wengi na vilevile kuna taasisi nydingi, kuna Chuo Kikuu cha Madaktari, kuna vyuo karibu 18, kuna mashule mengi, kuna shule za *international*, shule za kawaida, kuna hospitali, kuna vituo vya afya, kuna kaya nydingi lakini zote hizi maji ni matatizo. Sasa mnaposema maji ni uhai, maji ni afya; je, sisi watu wa Kilombero hamtutakii kuwa na afya njema tuugue? Hiyo inasikitisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ifakara mjini kwenyewe, mji ule mdogo umezungukwa na mito miwili mikubwa; Mto wa Kilombero na Mto Lumemo, lakini pamoja na kwamba kuna mito hii mikubwa bado maji ni matatizo kuyapata. Jamani naomba tatizo hili sugu la muda mrefu liondoke tusikae tena kuchangia tukiomba maji kwa ajili ya wakazi wa Kilombero, kwa sababu hakuna sababu ya kutokuwapa maji safi wakati vyanzo vyote vya maji viro. Jamani, sitaki nionekane kama vile ni mtu mbishi, lakini ninaomba tusaidiane hili ili tatizo liweze kuondoka.

Ahadi ya Rais, katika mwaka 2005, 2010 alituambia ahadi yenu nawaahidi daraja, maji tunashukuru Mungu daraja limeanza, matayarisho yake ya ujenzi, pia tunashukuru lakini Wizara hii ya Maji bado hajatimiza ahadi hiyo. Sasa hili jambo sielewi tatizo ni nini; ni pesa au nini? Shilingi bilioni 395, mnashindwa kutoa hela kidogo tu kwa ajili ya Wilaya moja jamani au sisi siyo watu wa thamani, kama ni watu wa

thamani, naomba safari hii ombi hili ambalo kwa sasa ni mara ya nne nasimama mbele ya Bunge hili kuliomba na vilevile kulitafakari na kuwaambia vyanzo vyote nya maji, ninaomba sasa lipate majibu ya kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Mradi wa Maji ya kutega, huu Mradi wa Kiburugtu. Mradi huu nimewapelekea Mawaziri waliokuwepo, ambao thamani yake ni shilingi bilioni mbili. Huu Mradi ni wa kudumu siyo wa kurudiarudia, lakini wanasema Mradi wa shilingi bilioni mbili ni mkubwa mno, ni nydingi mno. Shilingi bilioni mbili jamani miaka yote kumi ya Rais Kikwete ni nydingi kwa ajili ya Kilombero badala yake wanawapa visima, wanachimba visima nya mdunduko, visima vitatu au visima vitano kila mwaka. Sasa hapo kweli unaondoa tatizo si bado unaendeleza hili tatizo liendelee wakati ungetoa hela mara moja. Fumba macho toa hela mara moja shilingi billioni mbili puu, tengeneza miundombinu ya maji pale Ifakara ili vyuo viweze kufanya vizuri, vyuo vikuu vifanye vizuri na wakazi wa pale waweze kufaidika na maji hayo.

Ninaamini ya kwamba, safari hii Mheshimiwa Maghembe, Waziri wa Maji, hili jambo litatimia na tutafurahi na wakati wa kufungua hakika itakuwa ni sherehe na shangwe.

Tatizo la maji katika Mji Mdogo ule wa Mlimba. Mlimba nao ni mji, ipo Stesheni ya Tazara kubwa na vilevile kimji kikubwa kilichochangamka lakini tatizo kubwa ni maji. *World Bank* walichimba pale, kuna Mradi pale wa visima unatumia umeme na umeme ni wa msimu. Leo kuna umeme kesho hamna, kwa hiyo, wakati mwingine inabidi watu kwenda kutafuta maji na ndoo kwenda mbali.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mchungaji Rwakatare, kwa kuwasemea Wananchi wa Kilombero hasa Mji wa Ifakara. Kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge, ambao hawakuwa wamefahamu kuhusu msiba mkubwa uliokupata wa kuondokewa na mzazi mwenzako, naomba

tukupe faraja kwa kusema pole sana; "Bwana alitoa, Bwana ametwaa, jina la Bwana Lihimidiwe."

Baada ya Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, atakayefuata ni Mheshimiwa Dkt. Cyril Chami.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nitoe mchango wangu kidogo katika Sekta hii muhimu ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kusema kwamba, kwanza, maji ni muhimu na maji ni uhai. Maji yanahitajika majumbani, mahali pa kazi, mashulenzi, viwandani, maeneo ya sokoni na sehemu mbalimbali katika kilimo na mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna vyanzo vingi sana nya maji, lakini nasikitika kusema kwamba, Serikali imeshindwa kutupatia maji safi na salama na kila anayesimama hapa nafikiri wewe mwenyewe unasikia jinsi wanavyotoa kilio cha maji na kweli maji ni shida Tanzania. Mfano, tukiangalia *trend* ya bajeti inavyokwenda; mimi sitaki kwenda kwenye Bajeti Kuu, nataka tuangalie *subvote 3001* kwenye Kitabu cha Maendeleo, ukurasa wa 81, utaona kabisa jinsi tunavyotegemea wafadhili katika Miradi yetu mbalimbali ya Maji. Hii inasikitisha. Ukiangalia katika *rehabilitation and expansion of urban water supply* katika miaka ya 2012/2013 na 2013/2014 jinsi *trend* inavyokwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa bajeti uliopita tuliona kwamba, tunategemea wafadhili kwa shilingi bilioni 135.8 wakati fedha za ndani tulikuwa tumetenga shilingi bilioni mbili. Mwaka huu wa 2013/2014 pia tunaona tumetenga pesa za ndani shilingi bilioni 4.8 wakati tunategemea wafadhili kwa shilingi bilioni 49.2; kwa kweli sidhani kama tunawenza tukatatua matatizo yetu kwa kutegemea wafadhili kwa kiasi hiki. Naomba kuuliza kwa nini Serikali isiamue suala la kushughulikia maji liwe la kwake; kwa sababu tatizo la maji ni kubwa mno na ione kwamba ni muhimu na ni wajibu wake kwa Wananchi wake kuhakikisha kwamba maji yanapatikana bila kutegemea wafadhili?

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakubaliana na wale wote waliosema kwamba, kuna haja Serikali ione umuhimu wa kuanzisha Mfuko wa Maji kama tulivyo na Mfuko wa Barabara. Hii itasaidia kupunguza utegemezi kibajeti. Tarehe 17 Aprili nilikuwa najibiwa hapa swalii kuhusu matatizo ya maji. Nakumbuka Waziri wa Mazingira akasimama akasema kuwa, tatizo la maji ni la kidunia na ni kutokana na mabadiliko ya tabia nchi. Nakubaliana naye lakini pia nitakataa; tuna matatizo ya maji kwa kipindi kirefu lakini vilevile tuna vyanzo vingi vya maji. Hayo matatizo ya mabadiliko ya tabia nchi hayakuanza miaka mingisana, yameanza hapa nyuma. Cha msingi ni kuhakikisha tunalinda vyanzo vyote vya maji ili tuweze kuvitumia vizuri. Kwa hiyo, Serikali iache visingizio itekeleze wajibu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, Kigoma tuna shida sana ya maji; ukienda Kibondo, Kankoko, Muhambarwe, Kasulu, kila sehemu tuna shida sana ya maji lakini tuna Ziwa Tanganyika. Nikianza na Kigoma Manispaa, baadhi ya maeneo tunapata maji mara moja kwa wiki, eneo la Mwanga, Katubuka, Majengo, Ujiji, Mlole, Vamia kote ni vilio vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, toka Bunge la Tisa mimi nakumbuka tuliuliza maswali mengi ya maji. Nakumbuka vilevile katika michango mbalimbali niliyokuwa nikitoa, majibu ambayo Serikali ilikuwa ikijibu ni kwamba, hakuna umeme kwa hiyo pampu inashindwa kusambaza maji. Sasa hivi umeme tunao, lakini kwa nini hatuna maji?

Vilevile walikuwa wanasema kwamba, mabomba ni chakavu, yaliwekwa muda mrefu, miundombini inafanyiwa marekebisho. Mpaka sasa kimya maji bado ni tatizo. Hebu tunaomba Serikali itupe majibu fasaha ni nini tatizo. Vilevile tunaongeza umaskini kwa Watanzania kwa sababu sasa hivi tunategemea maji yanachotwa wapi; wanawenua galoni la maji kwa shilingi 500 mpaka 1000, maisha ni magumu sana tunaongeza umaskini kwa Watanzania. (*Maskini*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia Kigoma Vijijini,

tatizo ndiyo kubwa zaidi, kuna Mji Mdogo unaitwa Mwandiga ni kijiji ambacho kinakua haraka, kipo karibu kabisa na mjini, pale maji ni shida mno. Mimi nashauri mtandao wa *KUWASA* ungeibeba na hii Mwandiga kwa sababu siyo mbali sana na eneo la Mjini. Vilevile Mji wa Kuzulamimba unakua mno, kwa hiyo, maji yaliyopo hayatoshi. Ninaomba Serikali iangalie uwezekano wa kuwapatia maji lakini vijiji kumi vyta mradi pia navyo vinasuasua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na muda nitaongea kidogo kuhusu suala la Kasulu. Kuna Mradi wa Ruhita wa 2011/2012, ambapo mzabuni alipewa kazi lakini inaonekana *engineer* wa eneo lile hafanyi kazi yake vizuri. Wananchi walichangia shilingi milioni 30, mabomba yaliyonunuliwa kwa kweli yalikuwa *substandard*, yalikuwa yakivunjika wakati wanatandaza mabomba chini. Mtandao wa maji Heru Juu na maeneo ya Kahunga na Muhunga, kuna utaratibu wa kubadilisha mabomba yaliyopo ambayo yalifungwa tangu miaka ya 1970. Sasa pesa zilizotolewa ni kidogo sana, inahitajika kama shilingi milioni 300, lakini wametengewa shilingi milioni 80 na ni Mradi ambao ultakiwa utekelezwe ndani ya miezi sita ila mpaka sasa bado unasuasua na vijiji vingine vyta Nyoshe, Mruti, Kidya, Kigondo, Msambala kote maji ni shida wanahitaji maji. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesekia kuna *slogan* inayosema "*Big Result Now*" siamini kama itafikiwa na hiyo *result* tutaipata haraka kulingana na trend ya Bajeti jinsi ilivyo.

Nikiangalia ukurasa wa 119, kifungu kidogo cha 87(a) cha Ilani ya CCM ya mwaka 2010, kinasema kwamba, kutakuwa na kuongezeka kwa upatikanaji wa maji safi na salama kufikia mwaka 2015, vijijini asilimia 75, mijini asilimia 95. Nasema kwamba, sidhani kama tutafikia kulingana na hali halisi kwamba sasa hivi tuko asilimia 57 vijijini na 75 mijini na hali yenye ya kibajeti jinsi ilivyo. Vilevile sera ya maji inasema, maji yapatikane umbali wa mita 400. Sasa hivi watu wanatembea muda mrefu sana; ni lini Mwananchi atatafuta maji umbali wa mita 400 tu?

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshasema mengi sana, tunaomba Serikali ituambie ina mikakati gani inayohakikisha kwamba Mtanzania anapata maji na malalamiko ya Wabunge yanakwisha? Nashukuru kwa kunipa nafasi. Ahsante. (*Makofii*)

**MHE. DKT. CYRIL A. CHAMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia Bajeti hii ya Wizara ya Maji. Naanza kwa kusema kwamba, naunga mkono bajeti hii, lakin nachukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maji na Naibu Waziri wake na Katibu Mkuu - Engineer Sai, kwa kazi kubwa wanayoifanya katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, natumia fursa hii kuwapa pole, nawapa pole kwa sababu mzigo tulio wapa ni mkubwa, lakin rasilmali za kufanya kazini ndogo na killo cha Wabunge wote walioko hapa, hakuna Mbunge mwenye Jimbo anayeweza kusimama hapa akasema Jimboni kwake ni salama, kwa maana ya maji, salama kwa watu wote; ama atasema kwamba Jimbo lake lote lina shida ya maji au atasema kwamba sehemu fulani ya Jimbo lina tatizo. Kwa maana hiyo, nataka niwasihii Wabunge wenzangu, badala ya kuelekeza shutuma kwa Waziri na Watendaji, tukae kama Bunge tuishauri Serikali namna gani ya kupata vyanzo vya fedha vya kuondokana na tatizo la maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Maji na Wasaidizi wake wanahitaji kusaidiwa na Bunge hili na siyo kutuhumiwa wala kulaumiwa. Hakuna Waziri hata mmoja ambaye angekaa kwenye nafasi ya Mheshimiwa Profesa Maghembe pale, ambaye leo Waheshimiwa Wabunge wasingemlalamikia. Waheshimiwa Wabunge tunapolalamika tuna haki kwa sababu na sisi tunalalamikiwa katika Majimbo yetu. Kwa hiyo, tuache kulalamika, tukae chini tutafakari na mimi nachukua fursa hii kumnu kiongozi mmoja wa nchi yetu, huwa anasema tufanye maamuzi magumu. Tufanye maamuzi magumu tuseme kwamba suala la maji tulitafutie ufumbuzi. Kama alivyosema mse maji aliye pita, kwa hakika miundombinu mingi, iwe ya kiuchumi, iwe ya afya, haiwezi

kufanikiwa kama hakuna maji, maji ndiyo muundombinu ambao kila mahali unahitajika. (*Makoff*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, jambo litakalotutoa 2015 ni kuhakikisha kwamba nchi hii inapata maji kila Wilaya, kila Kata na kila Kijiji. Tukifanya maamuzi magumu, Chama changu cha Mapinduzi kitashinda kwa kishindo 2015. Nataka niombe kabisa Wabunge ambao wengi ni wa CCM tuliomo humu na Serikali yenyewe ambayo ni ya CCM, tufanye maamuzi haya magumu kwa sababu utatuzi wa shida hii ya maji ndiyo ambao utawafanya Watanzania wote waone kwamba, maisha bora yaliyoahidiwa kweli wameyapata.

Zipo tuhuma zimetolewa hapa kuhusu Waziri wa Maji kwamba, amechukua fedha nyingi akapeleka Jimboni kwake. Naomba nisimame hapa nitoe ushuhuda kwamba, mwaka 2005 wakati Mgombea wa Urais kwa tiketi ya CCM ambaye sasa hivi ni Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, alipotembelea Kilimanjaro, Wananchi wa Mwanga, Same, walimlilia sana kuhusu suala la maji. Sisi kule Hai na Moshi Vijiji na Vunjo na Rombo, tukamlilia kuhusu barabara za lami. Leo hii fedha zimekwenda Hai kujenga barabara za lami hakuna mtu analalamika. Fedha zimekuja Moshi Vijiji barabara za lami zinajengwa, mimi siye Waziri wa Miundombinu, hakuna anayesema nimetembelewa. Fedha zimekwenda Rombo Jimbo la Upinzani, barabara ya lami imejengwa pale, fedha ambazo Serikali ya CCM imetoa, hakuna mtu analalamika. Kwa nini fedha zikienda Mwanga na Same kujenga Mradi wa Maji ambao Mheshimiwa Rais aliahidi tunakuwa na malalamiko? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimwombe Mheshimiwa Waziri akaze buti, asikatishwe tamaa, hii siyo ahadi ya Mheshimiwa Maghembe ni ahadi ambayo Mheshimiwa Rais aliitoa mwaka 2005, 2010 ameirudia tena na kila mara anapokuja Kilimanjaro huwa anakumbusha ahadi hii. Haiwezekani; Mheshimiwa Maghembe, kama Mradi huu hautakamilika mwaka 2015, CCM haitavuna kitu pale Mwanga na kule Same, Lushoto na Korogwe. Kwa maana

hiyo, wale wote wanaosema Mradi huu usipewe fedha ni njama ya kufanya CCM ishindwe katika maeneo hayo na mimi nataka niiombe Serikali kwa ujumla kwa kweli iangalie. Mimi sina wasiwasi kwamba kuna maeneo mengine ambayo kilio cha maji kipo kama ambavyo wamesema.

Inategemea maji yameahidiwa lini. Kama mtu ameahidiwa miaka miwili iliyopita na haya ya miaka minane, lazima yapate kipaumbele. Sasa Waziri huyu ambaye amechukua Wizara ambayo imeshaongozwa na Mawaziri wengine, anapokuja kuitisha fedha ambayo imeshapitishwa huko nyuma, mimi naomba kabisa jamani tusimlaumu, tumtie moyo. Mheshimiwa Maghembe, unapohangaika na Mradi wa Masasi, Nachingwea, Mradi wa Handeni, Lake Victoria, Shinyanga, Tabora, Lamadi, Meatu, Farqwa Kondoa, kuja hapa Dodoma na Miradi mingine ile ambayo umeitaja ukurasa wa 31 mpaka ukurasa wa 40, nakusih sana usisau Mradi huu wa Mwanga, Same na Korogwe, kwa sababu tu ya kelele za watu ambao wanapenda kutafuta jambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nje kwenye Jimbo langu la Moshi Vijijiini. Namshukuru sana Mheshimiwa Susan Lyimo, amesema vizuri kuhusu Kolini Kusini na akasema ni watu wake kwa sababu amezaliwa Kolini Kusini, lakini mimi ndiyo Mbunge wao. Pale kuna Mradi ambao unashughulikia vijiji viwili; Kolini Juu ambayo hakuitaja na Kolini Kusini. Naishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi pale tumepokea shilingi bilioni 1.027 na hivi sasa mkandarasi yuko kwenye site, Mradi umekamilika kwa asilimia 20. Wananchi wa Kolini Juu na Kolini Kusini wanashukuru sana na mara ya mwisho kutembelea pale wanategemea uenze kama alivyosema Mheshimiwa Lyimo mwaka huu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Chemchemi ya Mangi ambao amesema unaongozwa na Prof. Elisante wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ni kweli wananchi wamechangia lakini Mheshimiwa Lyimo akasahau kusema kwamba na Mbunge naye aliquwepo naye akachangia shilingi milioni tano. Unajua mambo haya ya siasa, lakini namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwa sababu Mradi wa

Kilema Juu, Kilema Kati na Kilema Boro, ambao ni wa takriban shilingi bilioni mbili, nafurashi kusema fedha zimekwenda na Mkataba umeshaandaliiwa. Jana nimeongea na Mkurugenzi kwa maelekezo kutoka Wizarani, nimewaruhusu wasaini ule mkataba, fedha ifike kazi ianze kwa vijiji hivyo. Vilevile kwa mwaka unaokuja Wananchi wa Mande Tela watapata fedha pale shilingi milioni 824 kwa ajili ya kijiji chao.

Mheshimiwa Naibu Spika, shida ya maji iko kila mahali Tanzania. Kwa upande wa Moshi Vijiji kuna Kijiji cha Mwasi Kaskazini na Mwasi Kusini, hivi viko Uru Mashariki, bado kabisa pale suala la maji ni tatizo. Kuna kijiji cha Ungoma na Njari, Kata ya Uru Kaskazini, bado tatizo la maji liko palepale. Halafu kuna vijiji ambavyo havijatajwa mahali popote, maana hivi nilivyovitaja angalau vimetajwatajwa katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Kwa mfano, eneo la Mabogini, eneo la TTC, eneo la Kindi na vilevile maeneo mengine ya Uru Mashariki na Uru Kusini, maeneo ya Kitandu, Longuo na Kariwa, hakuna maji. Sasa mimi siko hapa kulalamika, kwa sababu tukilalamika kwa nini hakuna maji, tutakuwa kama hatuelewi hali halisi. Mimi nataka nishauri mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza, ambalo Mheshimiwa Waziri amelisemea vizuri, nataka niwashauri Watanzania wote, bila kujali itikadi zao, bila kujali kwamba wako Serikalini au wako nje ya Serikali, kwa kweli tuikumbatie teknolojia ya kuvuna maji ya mvua. Tuanze kuvuna maji ya mvua kwa namna yoyote ile, katika ngazi ya kaya, katika ngazi ya kijiji na ikiwezekana katika ngazi ya Kata. Nataka niziombe kabisa Taasisi za Dini, kwenye misikiti na makanisa, waanze kuonesha mifano na taasisi za elimu katika mashule yetu yote ya *Primary* na *Secondary*, tuanze kuhakikisha kwamba, tunavuna maji ya mvua ambayo yanapotea bure. Tukisubiri Serikali imalize tatizo hili itachukua muda mrefu sana. Tutamtesa Waziri na Naibu wake pale, ambaye anahangaika sana, hatutafanikiwa. (*Makof*)

Tufanye kama tunavyochangia fedha za harusi na *send off* na zinafanikiwa. Nataka niwaombe Watanzania wote tuamue kila mahala tulipo tujichangishe kwa ajili ya

kuvuna maji ya mvua. Nataka nimshauri Mheshimiwa Waziri wa Maji, ashirikiane na Waziri wa Viwanda na Biashara, kuna Kituo cha CAMARTEC, kina utaalam wa jinsi ya kuvuna maji katika ngazi ya kaya na katika ngazi za juu zaidi kwa maana ya maji ya vijijini, kata na kadhalika. Hilo ni moja ambalo nataka niwaombe Watanzania wote, tuweke itikadi kando, tuweke siasa kando, kila mtu hata ikiwezekana katika kaya, ajitahidi kufanya jambo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo nataka nilishauri Bunge lako Tukufu na niishauri Serikali, narudia; tufanye maamuzi magumu kama ambavyo tumeweke kipaumbele kwenye miundombinu ya barabara na tumeona matunda yake na kama ambavyo tunapigania miundombinu ya reli, tuweze kuwa na reli na bandari; nataka nipayendekeze Serikali na Wabunge tuamue tutenge hiyo shilingi trillioni 1.8, ambayo inatakiwa kwa miaka mitatu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Cyril Chami kwa mchango wako, ndiyo utakuwa mchangiaji wetu wa mwisho kwa asubuhi ya leo na kwa kweli nikushukuru sana. Kwa sababu kama Wabunge hilo ndilo jukumu letu kufikiri kwa pamoja katika matatizo mazito yanayowagusa wananchi wetu namna gani tunavyoweza kuja na majibu ya kuweza kutatua matatizo badala ya kufikiri kwamba akiwa fulani pale basi ni kurusha mawe tu, haisaidii sana. Nakushukuru mno kwa kutusaidia kutuwekea mwelekeo huo. Jioni tutaendelea na uchangiaji orodha imejaa kabisa naomba mtu asiniletee karatasi yoyote ataanza Mheshimiwa Dunstan Kitandula, Mheshimiwa Innocent Kalogeris na Mheshimiwa Zabein Muhita.

Waheshimiwa Wabunge, naomba kusitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja jioni.

(*Saa 7.00 mchana Bunge lilitfungwa mpaka saa 11.00 jioni*)

(Saa 11.00 jioni Bunge ilirudia)

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea kuhusiana na hoja ya Serikali ambayo imewasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Maji asubuhi ya leo kwamba, Bunge sasa likubali kujadili na kuitisha Matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Tuko katika hatua ya uchangiaji, na kama nilivyosema kipindi cha asubuhi mchangiaji wetu wa kwanza ni Mheshimiwa ni Mheshimiwa Dunstan Kitandula na Mheshimiwa Innocent Kalogeris ajiandae na Mheshimiwa Zabein Mhita aendelee kujandaa. Mheshimiwa Dunstan!

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi nichangie kwenye hotuba ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye kila uchao anazidi kutupa baraka zake. Nitumie fursa hii kuipongeza na kuishukuru Serikali, tarehe 13 mwezi huu wa Aprili, Mheshimiwa Rais alifanya ziara katika Mkoa wa Tanga, alifika Mkinga kufungua barabara ya Tanga-Horohoro. Tunapongeza na kuishukuru sana Serikali kwa kukamilisha barabara hiyo. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mheshimiwa Rais akiwa pale alisikia kilio cha watu wa Mkinga kwamba Makao yetu Makuu hayana maji na alituahidi Shilingi milioni 200 kwa ajili ya ufumbuzi wa haraka wa tatizo lile. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais na Serikali. (Makof)

Vile vile naishukuru Serikali kwa ajili ya kukamilika kwa Mradi wa maji wa Daluni wananchi wa Daluni Kibaoni, Bombo Mtoni na Ng'ombeni wanapata huduma ya maji kwa uhakika ninawashukuru sana. Tunatarajia sasa mradi mradi ule mwingine wa mapatano uanze. Mradi ule sisi wa Wilaya ya Mkinga tumekamilisha kila kinachohitajika, tunachosubiri ni

wenzetu wa Wizarani m-pushili tuweze kupata ile *no objection* tuweze kuanza mradi ule. (*Makofii*)

Ikumbukwe kwamba hiki kitakuwa ni kijiji cha pili katika vile vijiji 10 vya utekelezaji wa vijiji 10 vya Mradi wa Benki ya Dunia. Kwa hiyo, tunaomba Wizara ifanye jitihada mradi huu uanze kwa haraka kwa maana mradi huu unatakiwa kuanza kwenye *financial year* hii. Mradi ule ukianza, tunaamini kuwa watu wa Machimboni, Kongena, Bantu na hata watu wa Mienzani wataweza kufaidika kwa kupata huduma ya maji safi na salama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefurahi kuona kwamba baada ya kupiga kelele kwa muda mrefu, sasa mradi wa Kasera umeingizwa kwenye bajeti hii. Naishukuru sana Serikali. Kuweka mradi ule kwenye mpango wa mwaka huu ni jambo moja, lakini utekelezaji ni jambo muhimu zaidi. Tunalomba Serikali fedha za mradi ule zije kwa haraka, upembuzi ufanyike ili watu wa Mkinga waondokane na adha ya maji. Mradi ule tunategemea ukiweza kufanikiwa basi maeneo ya Bamba Mavengero, Bamba Mwarongo, Doda, Barungu Kasera na Makao Makuu yetu ya Wilaya ya Kasera watapata maji kwa uhakika. (*Makofii*)

Jambo hili ni muhimu sana kwa sababu maendeleo ya Mkinga yanategemea sana Makao Makuu ya Wilaya yaye yametulia. Tunaomba mtusaidie tuweze kujenga Mji ule ili maendeleo yaweze kupatikana katika Wilaya yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa nizungumze kwa ujumla kuhusu sekta ya maji. Waliotangulia kusema wamesema hapa kwamba maji ni uhai, nami niongeze kwamba maji ni ustaarabu, maji ni ishara ya binadamu kustaarabika. Bila maji, hakuna ustaarabu. Sasa katika nchi yetu tuna tatizo kubwa la maji na tatizo hili linatuondolea utu wetu. Heshima ya utu wetu inaondoka. Haingii akilini mpaka leo Watanzania tunagombea maji ya kunywa, maji ya matumizi na mifugo. Hili siyo jambo zuri, linatuondolea utu wetu na hadhi yetu ya ubinadamu.

Hatujafanya vizuri katika sekta hii. Naiomba Serikali iongeze jitihada ili tuondoe kero hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefurahi kuona kwamba sasa tunaanzisha Mfuko wa Maji, lakini fedha zilizoko pale ni kidogo. Lazima kama Taifa tupanue uwigo wa mfuko ule. Ni lazima tubuni vyanzo vipyta vya kukuza mfuko ule. Ukiangalia katika taarifa mbalimbali za kibenki, wanasema mabenki yetu sasa hivi yanapata faida kubwa. Tuna uwezo wa kukaa na mabenki tukazungumza nao wachangie angalau asilimia moja ya *pre tax profit* ya mfuko huu. Kama Benki inapata faida ya Shilingi bilioni 80 *CRDB, NMB* Shilingi bilioni 103 na Mabenki mengine hivyo hivyo haituzui kukaa nao meza moja, wao kama watu wanaofaidika na huduma za kijamii katika nchi yetu wakachangia kwenye mfuko huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile wakati Watanzania wanaendelea kufa kwa madhila ya matatizo ya maji, siyo vibaya kama viongozi tukaonyesha njia, tukafunga mkanda. Kuna jambo limekuwa likipigiwa kelele muda mrefu ya *OC*. Naamini *OC* inafanya mambo mengi lakini kuna kile kipengele cha chai kinapigiwa kelele. Hebu tuamue na kusema kuwa tunaacha mwaka huu kunywa chai na fedha yote ile au hata 5% ya kifungu hicho ielekezwe kwenye mfuko huo ili tuwaokoe watu wetu na tatizo hili la maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri vilevile tuangalie kuwa na *tax exempt bond* ambayo tukizi-float hizi tunaweza kupata *source* nytingine. Watanzania wanaathirika na tatizo la maji. Nilisema kipindi kilichopita kwamba hii itakuwa ni hoja ya uchaguzi mwaka 2015. Ushahidi umejionyesha dhahiri kuwa kila Mbunge aliyesimama alipiga kelele kuhusu tatizo la maji. Ifike mahali sasa tuone uwezekano wa kuhakikisha kwamba bajeti ya maji inaongezeka. Haiingii akilini hata kidogo kwamba 75% ya Watanzania wako vijijini, lakini fedha tunazoelekeza kwenye Sekta ya Maji Vijijini ni 30%. Haiwezekani, haikubaliki! Hata hiyo 30% tunayoisema mimi nimepitia haya ma-book kuitafuta hiyo 30% sioni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naisihi sana Serikali yangu ifanye kila linalowezekana tuifungue bajeti hii tuuiongezee fedha za kutosha ili tuondokane na tatiozo hili la maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, nakushukuru sana Mheshimiwa Dunstan Kitandula. Sasa kama nilivyosema, ni zamu ya Mheshimiwa Innocent Kalogeris, atafuatiwa na Mheshimiwa Zabein Mhita.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia bajeti ya Wizara ya Maji ambayo iko mbele yetu. Maji ni Uhai lakini pia ni hitaji la msingi la maisha kwa viumbe vyote duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hotuba nzuri na yenye matumaini ambayo imetolewa na Mheshimiwa Waziri, lakini bado mpangilio wa bajeti haukidhi mahitaji halisi ya watu, hasa Vijijini kama mchangiaji aliyepita Mheshimiwa Kitandula alivyosema kwamba upendeleo mkubwa unaonekana uko katika maeneo ya Mjini na Vijijini bado ni matatizo. Mfano halisi tu, Halmashauri yangu ya Wilaya ya Morogoro Vijijini mwaka 2012 tulipata Shilingi milioni 11 tu kutoka Wizarani, mwaka huu tumeomba Shilingi milioni 484 lakini tumepata Shilingi milioni 267, angalau tunashukuru, lakini nadhani bado hazitoshi kukidhi mahitaji ya maji Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile mfumo wa uendashaji wa Wizara yenye, kusimamia miradi lakini vilevile Wizara kupeleka miradi katika Mamlaka za Maji za Miji, Majiji na baadhi ya Halmashauri, ni dhahiri kwamba dhamira ya Serikali katika kutekeleza llani ya Uchaguzi ya Chama chetu cha Mapinduzi haitawenza kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia 80 ya Watanzania wanaishi vijijini na wanahitaji huduma hii ya maji. Nadhani Wizara inahitaji kuwa na kiungo kati ya Wizara, Mkao na Halmashauri katika kutekeleza majukumu yake. Hili

nililizungumza katika Bunge la Bajeti liliopita, niliombwa Wizara ianzishe utaratibu kama wa Wizara ya Ujenzi kuanzisha Wakala wa Maji nchini na ninakumbuka Mheshimiwa Waziri wakati anafanya majumuisho, alisema hili ni jambo jema na aliahidi kuleta Muswada wa kuanzisha Wakala wa Maji nchini.

Nashukuru katika bajeti ya mwaka huu tunaonyesha kuna Mfuko, lakini nadhani lile ombi langu lilikuwa bora Wizara ikalifanya. Kwasababu kuwa na Mfuko wa Maji bila kuwa na Wakala wa Maji na kuwa na Bodi ya Maji itakuwa ni hadithi tu. Kwa maana huu Mfuko wa Maji utakuwa unatoa fedha na kupeleka kwenye Mamlaka za Maji za Mjini na watu wa Vijijini wataendelea kutopata huduma za maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wazo la kuwa na Wakala wa Maji wa Taifa na Bodi ya Maji ya Taifa ninadhani ndiyo suluhisho la kudumu. Tunasema kuwa Mfuko wa Maji utachangiwa, namshukuru ndugu yangu Mheshimiwa Kitandula ambaye amemaliza kuongea sasa hivi ametoa hata maelekezo. Mimi nadhani Bodi ya Maji ya Taifa tukiwanayo kama Bodi ya Barabara, inaweza kukopa fedha Benki kwasababu biashara ya maji ni biashara. Maji siyo huduma ambayo inakwenda kavukavu, maji ni biashara ya huduma ambayo inakwenda kibashara, inaweza kukopa Benki na inaweza kutusaidia kuendesha miradi yote ambayo tunayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu bado kwa Wizara ya Maji, wakati Mheshimiwa Waziri anatoa majumuisho angetuambia ni sababu zipi za msingi siku ile alikubali, lakini amekuja na wazo lingine, hatuoni hili wazo la kuanzisha Mamlaka za Maji, lakini pia hatukuona ile Sheria ambayo pengine ingefanya sasa tukawa na Mamlaka za Maji. Tukiendelea katika *style* hii mimi naomba niseme tu kwamba llani yetu ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi mwaka 2015 tutakapokwenda kwa wananchi, tutakwama.

Mimi ninajua llani yetu ilikuwa inalenga siyo kwa ajili ya kushinda uchaguzi, ila kuwatumikia wananchi. Ombi langu kwa Wizara, tafadhalini, tusaidieni katika hilo. Njooni katika

style ambayo itatufanya wote kwa pamoja Watanzania tunapata huduma za maji. Mimi katika Halmashauri yangu sina la kusema lolote. Hakuna visima, mradi wa vijiji 10 haujatekelezeka kwasababu hakuna mawasiliano kati ya Halmashauri na Wizara, sasa naweza kusema kwamba tumeshindwa katika miradi hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini ninachotaka kuzungumzia ni suala la kuwa Bodi ya Maji, suala la kuwa na Wakala wa Maji Kitaifa litataufanya Wabunge katika Mikoa yetu kuweza kufanya mapambano au kuweza kuchanganya au kujadiliana kwa kina kwasababua pale kutakuwa na *Regional Manager* wa Maji na katika Bodi ya Maji Mkuu wa Mkoa ndio anakuwa Mwenyekiti wa Bodi kama vile kwenye barabara. Lakini Wabunge tutakuwa ni Wawakilishi wa wananchi, kutakuwepo na Wenyeviti wa Halmashauri, Watakuwepo ma-Meya wa Miji, na katika kikao kile yatakayofanyika yatasaidia badala ya kusubiri Waheshimiwa Wabunge hapa kupambana na Wizara katika Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana kaka yangu Profesa Maghembe na ndugu yangu Bwana Mahenge, Naibu wake, kuna mmoja alisema mchana katika uchangiaji wake, nadhani wakati wa kufanya maamuzi magumu, nami naomba, huu ni wakati wa kufanya maamuzi magumu wa kuwa na Wakala wa Maji Tanzania na kuwa na Bodi ya Maji Tanzania kwa ajili ya kupata huduma kwa wananchi. Naamini ukifanya hivyo, kaka yangu Professor utaondoka kwenye Wizara hiyo, Watanzania watakukumbuka na ninaamini kuwa suluhisho la kero ya maji kwa Vijijini na hata Mijini litakuwa limekwisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nitumie nafasi hii kupongeza Wizara, nimeona mwaka huu kwenye Bwawa la Kidunda mmetenga fedha kwa ajili ya kuliendeleza Iakini vilevile umetueleza katika kitabu chako cha hotuba ya bajeti kwamba mmetenga fedha kwa ajili ya kulipa wananchi fidia mwezi wa Tano. Huu ni mwezi wa Nne ninataka kukwambia kuwa ahadi ni deni, na kwa mwanadamu ukiahidi ni lazima utekeleze. Tuliwaahidi wananchi wa Kata ya Serimbala,

wananchi wa Kata ya Mkulazi mwaka 2012 kwamba tutawapatia fidia yao lakini vilevile tutawapatia viwanja, tutawaijengea miundombinu na wahame wapishe ujenzi wa Bwawa la Kidunda.

Kwa ahadi yako hii, nakuomba malipo hayo mwezi wa Tano yaende sambamba na kulipa Halmashauri ya Morogoro Vijiji kiasi cha karibu Shilingi bilioni 1.2 ambapo Shilingi milioni 970 kwa ajili ya kujenga miundombinu, lakini vilevile Shilingi milioni 185 kwa ajili ya kupima viwanja ili wananchi hawa wakipata fedha hizi za fidia waende kwenye makazi ambayo tayari yameshaandaliwa, waende wakatumie pesa zao kwa shughuli ya kujenga. Kwa maana kama utampa mtu pesa kabla hujampa kiwanja, kama makubaliano yetu tulivyokubaliana, kabla hujatujengea huduma zetu za Msingi, Shule, Zahanati na nyumba za ibada, ni kielelezo tosha kwamba watachukua fedha hizi na baada ya muda pesa zile zitakwisha na hawataweza kujenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile namwomba Mheshimiwa Waziri wakati anafanya majumuisho ikiwezekana mradi huu, juzi kulikuwa na mafuriko katika Kata ile, Kata nzima ilizama, nikielelezo tosha kwamba tukijenga bwawa tukawalipa wengine wakaondoka na wengine wakabaki, mafuriko mengine yakitokea yanaweza kuleta athari kubwa kwa wananchi na huko tunaweza kusababisha maafa makubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nadhani kuna kila sababu ya kuangalia upya mradi huu kwa wale ambao hawapo kwenye Kata ile wakaingizwa ili tukiondoa tuweze kuwasalimisha wananchi wote wa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia, nimwombe tu Mheshimiwa Waziri kuwa mwaka huu mmetupa Shilingi milioni 267, basi pamoja na mahitaji yetu yalikuwa karibu Shilingi milioni 500 tupate pesa hizo zote kwa pamoja au tuzipate zote bajeti katika 100% ili kusudi tuweze kukamilisha huduma za msingi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba vilevile katika mradi wa vijiji 10, mtie msukumo ili uanze katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja nikiamini kwamba fedha ikipatikana, haya yote niliyoyaomba yatakekelezeka.

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Innocent Kalogeresi. Mheshimiwa Zabein Mhita, Mbunge wa Kondoa atafuatiwa na Mheshimiwa Agness Hokororo.

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kondoa Kaskazini nami niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Aidha, namshukuru Allah Sub-hanah-Wataallah kwa kunipa uwezo na afya kuweza kusimama mbele yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba nichukue nafasi hii kushukuru Serikali yetu kwa ajili ya fedha ya Mfuko wa Maji zilizotengwa katika Halmashauri ya Kondoa kiasi cha Shilingi bilioni 1.7. Naiomba Serikali itoe hizo fedha mapema ili ziweze kufanya kazi ambayo imekusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wastani wa upatikanaji maji Vijiini katika nchi yetu ni asilimia 58 lakini katika Jimbo la Kondoa Kaskazini upatikanaji wa maji hayo ni asilimia 30 tu. Asilimia hiyo 30 maji hayo yote siyo safi wala siyo salama. Kwa hiyo, inaonesha jinsi ambavyo tatizo hili liliyvo kubwa na liliyvo sugu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji vingi havina maji kabisa katika Wilaya ya Kondoa. Naomba nitaje vichache tu kwa leo kutohana na muda. Vijiini vya Chubi, Hachwi, Salanka, Isongolo, Ikengwa, Humai, Chandimo, Kilele cha Ng'ombe, Makirinya, Mwembeni, Majengo, Matangalimo, Gaara, Thawi, na Mauno. (*Makofî/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata katika Mji wa Kondoa ambaao ni Mji Mkuu wa Wilaya bado kuna maeneo ambayo

hayana maji. Mfano Tura, Bicha, Kwapakacha, Bamai na Wisi Kwantisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa kutoa uwiano sawa wa miradi ya maji kwa Wilaya zote uangaliwe upya kwani kuna Wilaya ambazo zinapata asilimia mpaka sabini mpaka themanini wakati Wilaya nyingine mfano Kondo ni asilimia 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, nioneshe masikitiko yangu makubwa. Wanawake na wasichana ndio wana jukumu la kutafuta maji, na kwa kusema kweli wanakwenda masafa marefu wanatumia masaa mengi, na kwa kweli wanaathirika sana kwa sababu huko wanapokwenda kuchota maji kwenye makorongo, kwenye mito, ndiko ambako vile vile wanyama wakali wanakwenda kunywa maji.

Wapo wanawake wengi wamekwishapoteza baadhi ya viungo vya miili yao na kuna wengine ambao wamepoteza maisha yao kabisa kwa ajili ya kushambuliwa na hawa wanyama wakali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunalo bwawa la Itaswi, bwawa hili lilijengwa mwaka 1958. Wiki mbili zilizopita kumekuwa na mafuriko makubwa sana kwenye bwawa hili na lipo katika hatari ya kutoweka kabisa. Bwawa hili linahudumia vijiji na vitongoji saba. Hata hivyo, naomba niwashukuru watalaam kutoka Wizara ya Maji na kutoka Bonde la Maji la Kati ambao wamefika kwa wakati na wanafanya tathmini na watatoa taarifa na nitaomba taarifa hiyo tuipeleke Wizarani ili hatua za haraka na za makusudi kabisa ziweze kuchukuliwa ili kunusuru bwawa hili, vinginevyo wananchi wa hivi vijiji saba wataathirika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Wizara kwa kuweka vijiji vilivyoko katika mtaro wa Ntomoko katika mpango wa kukarabatiwa katika mwaka 2013/2014, kwa sababu mtaro huu wa Ntomoko ni mkombozi mkubwa lakini hata hivyo, ninaomba Kijiji cha Ntomoko ambacho ni chanzo cha mtaro huo nacho kipatiwe maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu haiingii akilini na haieleweki wakati wananchi ambao wanatunza na kuhifadhi chanzo hiki cha maji wao hawana maji kabisa. Wananchi hawa wamekuwa wavumilivu kwa miaka mingi. Waswahili wanasema, mvumilivu hula mbivu, lakini muda ukiwa mrefu, mvumilivu hula mbovu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri Mkuu alipofika Ntomoko kukagua mradi huo aliahidi kuwa kijiji hicho cha Ntomoko kitapatiwa maji. Hivyo naomba ahadi ya Waziri Mkuu iweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umuhimu wa maji na kama tunavyoolewa kwamba maji ni uhai, naiomba Serikali basi iongeze fedha kwa ajili ya miradi ya maji ili Wilaya ambazo zina matatizo makubwa mfano wa Kondoa nazo ziweze kuhudumiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya miradi ya maji ni ndogo sana, kwa maana kwamba hata Mheshimiwa Waziri angekuwa na utalaam gani, hawezি kufanya chochote! Atashindwa! Kwa hiyo, naomba hiyo bajeti iweze kuongezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri, kaka yangu, *Rumburya*, utakapokuwa unahitimisha hotuba yako uwaeleze basi wananchi wa Jimbo la Kondoa Kaskazini ni hatua gani na za haraka zitakazochukuliwa na Wizara yako ili kuweza kuwanusuru. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi pamoja na wananchi wa Jimbo la Kondoa Kaskazini tunayo matumaini makubwa sana na Waziri wa Maji pamoja na Naibu wake. Hivyo basi, nikiwa na matumaini makubwa pamoja na wananchi, tunaamini kwamba Jimbo letu la Kondoa Kaskazini litapewa kipaumbele katika upatikanaji huu wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina sababu yoyote ya kutounga mkono bajeti hii. Naiunga mkono kwa asilimia mia moja. Ahsanteni sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Zabein Mhita kwa matumizi mazuri ya muda. Sasa namwita Mheshimiwa Agness Elias Hokororo atafuatiwa na Mheshimiwa Freeman Mbewe na Mheshimiwa Stella Manyanya ajiandaye.

**MHE. AGNESS E. HOKORORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia hoja iliypopo Mezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikijitahidi kutafuta ufumbuzi wa upungufu wa huduma ya maji kwa wananchi wake katika kipindi hiki hasa katika Serikali hii ya Awamu ya Nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili linadhihirika wazi, tukiangalia hata katika vitabu ambavyo tumepata katika mwaka 2006 watu milioni 16.3 ndiyo walikuwa wanapata huduma ya maji, na ilipofika mwaka 2012 ni takribani watu milioni 20.6. Kwa hiyo kuna ongezeko.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ongezeko hilo kubwa, lakini bado pia Serikali yangu imeendelea kutambua kuwa upatikanaji wa maji Mijini na Vijijini bado ina changamoto kubwa ambayo inahitaji kufanyiwa kazi kwa umakini na kwa mapana zaidi. Ndiyo maana pia kupitia ilani yake ya CCM Serikali imejipangia kuwa ifikapo mwaka 2015 tunatakiwa tufikie kwa maji Mijini upatikanji wake ufikie asilimia 95 na kwa Vijijini asilimia 65. Hiyo ni nia nzuri na njema kwa Serikali. Naipongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kwa kuwa Sekta hii ya Maji ni muhimu na kila Mbunge hapa amekuwa akisema maji ni uhai, nami natambua kuwa maji ni uhai, bado naishauri Serikali na Wizara kuongeza kasi na kutafuta mbinu mpya zaidi katika kuhakikisha upungufu huu ambao Waheshimiwa Wabunge hapa tumekuwa tukiulalamikia unaondoka kwa kasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, athari za upungufu wa maji zinakwenda moja kwa moja kwa akina mama, ninamaanisha

wanawake. Katika maeneo mengi ya Tanzania wanawake ndio wasaka maji na wamekuwa wakitembea umbali mrefu, wamekuwa wakitumia muda mwingu na kwa masikitiko katika maeneo mengine kama kule Kilwa, hata vitendo vya udhalilishaji vinafanyika, wanawake wakiwa katika harakati za kusaka maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali yangu pia kuendelea kuongeza kasi ya kupunguza vikwazo vinavyokwamisha wanawake katika shughuli zao za kimaendeleo. Ni dhahiri pia kwamba wakati wanawake hawa wanaendelea kutafuta maji kwa masaa mengi, wanakuwa pia hawawezi kushughulika katika shughuli za kimaendeleo. Hizo athari zote nilizozitoa hapo zinawaumiza akina mama kijamii kwa maana ya kisaikolojia, kiafya na kimaendeleo pia kwa sababu ule muda ambaao walipaswa kwenda shambani kwenye Sekta ya Kilimo, wao wamekuwa wanatumia muda mwingu kutafuta maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu SPika, kwenye maeneo ya kwetu Mkoa wa Mtwara pia tatizo hizo bado lipo. Kwa mfano, Kijiji cha Nanjota wanawake wanatumia karibu masaa 24. Ina maana mchana mmoja na usiku mmoja, kwa hiyo, utaona dhahiri ni kwa namna gani wanawake tunashindwa kushiriki moja kwa moja kwenye shughuli za uzalishaji na hivyo tunaendelea kudorora. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wastani katika Mikoa ya Kusini pia kwa upande huu wa Sekta ya Maji bado tupo nyuma. Kwa mfano, katika Mkoa wa Mtwara, wastani wa maji Mijini na hapa ninamaanisha Makao Makuu ya Wilaya, tunapata kwa asilimia 58 na Vijijini tunapata kwa asilimia 42.5. Hivyo hivyo kwa Mkoa wa Lindi Makao Makuu ya Wilaya tunapata kwa asilimia 57.2 na Vijijini kwa asilimia 39. Ukiangalia, bado huduma hii kwa Mikoa hiyo iko nyuma. Pamoja na kazi nzuri na jitihada kubwa iliyo fanywa na Serikali yangu kwa mradi wa Mbwinji ambaao utatoa huduma ya maji katika Miji ya Masasi na Nachingwea na Mradi wa Makonde ambaao unatoa maji kwa Wilaya za Newala, Tandahimba, na Mtwara Vijijini, lakini naiomba Serikali kuhakikisha kwamba

ile mipango mizuri iliyoweka kwa mfano kwenye Mradi wa Makonde, ule mradi wa kuongeza watumiaji wa maji kwenye vijiji ambavyo mradi huo unapita, ni vyema ikaongeza kasi na kwa sababu upembuzi yakinifu ulishakamilika, basi Wizara ihakikishe zile fedha zilizotengwa kwa ajili ya mradi huo zinakwenda ili wananchi katika Wilaya za Tandahimba, Newala na Mtwara Vijiji waweze kufikiwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo litawezesha pia kupunguza gharama za utengenezaji wa miundombinu kwa sababu kwenye maeneo mengine ambapo maji yamekuwa yakipita tu wananchi wakati mwagine wanakuwa wakiiharibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya za Masasi na Nanyumbu bado pia tuna upungufu mkubwa. Pamoja na huo mradi mkubwa wa Mbwinji, lakini kwenye Wilaya hizi maji yake hata kwenye visima ambavyo vimechimbwa, bado yanakuwa hayapatikani. Kwa mfano, katika mradi wa ujirani mwema kisima cha Mangaka kilichochimbwa kati ya Msumbiji na Tanzania, kisima cha kwanza kilipatikana lita 400 tu kwa saa na kisima cha pili lita 1,500 na lengo ni kupata lita 15,000 kwa saa. Kwa hiyo, utaona kabisa bado hatuna vyanzo vya uhakika vya maji. (*Makof*)

Ninaishauri Wizara kama ambavyo kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu amesisitiza kwamba ipo haja sasa ya kutumia mbinu mpya. Naiomba sana Wizara kuangalia sasa mbinu mpya. Hapa ninashauri, kwenye maeneo haya Wilaya hizi za Masasi na Nanyumbu ni vyema sasa tukatumia maji ya mto Ruvuma ili kuweza kuondoa tatizo hili na iwe ni historia kwa upande wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suluhisho lingine ni lile la kuchimba mabwawa. Katika maeneo ya vijiji Wilaya ya Masasi kama vile Nambawala, Mpanyani, Mraushi na Nanjota huko kuna kiu, yaani tatizo la maji kwa kiasi kikubwa. Ndilo maana hata hili jina la Nanjota yaani kumekuwa hakuna maji kabisa. Kwa hiyo, huko kunahitajika pia ufumbuzi wa haraka haraka wananchi wapatiwe mabwawa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Wizara kuona namna ya kuondoa wananchi katika maneo haya hasa wanawake ili wasiwe wanalala huko visimani usiku na mchana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya Benki ya Dunia ipo, lakini miradi hii inakwenda taratibu sana, haiendi kwa kasi. Hii nikiangalia inatokana pia na zile hatua zake za utekelezaji kwa mfano, ukimaliza hatua moja unatakiwa kupeleka taarifa hiyo Wizarani. Kwa mfano, katika Wilaya za Masasi na Ruangwa tangu mwezi wa Desemba kazi imetangazwa, mzabuni amepatikana, lakini mpaka sasa tunasubiri kibali kutoka Wizarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiwa tunatumia miezi mitano au miezi mine, ni dhahiri kwamba utekelezaji wa miradi hii haitakamiliika kwa wakati. Hii inatoa malalamiko mengi sana kwa wananchi lakini na Watendaji pia wamekuwa wakilalamikiwa kwamba hawatimizi wajibu wao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Wizara ya Maji iangalie namna bora zaidi ya kuona ufuatiliaji na utekelezaji wa miradi ya Benki ya Dunia unafanyika kwa wepesi kuliko ilivyo sasa, kila hatua Watendaji wanatoka kwenye maeneo wanakwenda Makao Makuu na hivyo kuwasababishia sasa kutokufanya kazi nyingine na kuchelewesha hatua za utekelezaji hata ya miradi hiyo ambayo wamekuwa wakiifuatilia Wizarani. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwenye kitabu hiki pia, pamoja na hizo jithada nzuri za Serikali, kwenye Mradi wa Vijiji 10, kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, ni vijiji vinane tu ndiyo vilivyoorodheshwa.

*(Hapa kengele illia kuashiria muda wa  
mzungumzaji kwisha)*

**MHE. AGNESS E. HOKORORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Agness Hokororo. Namwita Mheshimwia Freeman Mbewe, atafuatiwa na Mheshimiwa Amina Makilagi.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji katika Wizara hii muhimu sana ya maji.

Kwanza nachukua nafasi hii kumpa Waziri na Naibu wake pole sana kwa sababu kwa umuhimu wa Wizara hii na kwa idadi ya fedha ambayo Wizara hii imepangiwa katika bajeti ya mwaka huu, ni dhahiri kwamba Watanzania wataendelea kulia kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nakubaliana na Mheshimiwa Waziri kwamba alivyozungumza katika hotuba yake mwenyewe na kukiri kwamba kuna changamoto kubwa ya upatikanaji wa fedha au upatikanaji wa fedha pungufu ya zile zinazopangwa katika Wizara hii. Ni changamoto kubwa ambayo kwa kweli kama Taifa, kama hatutatambua umuhimu wa maji na ulazima wa kugawa fungu la kutosha kwenye Idara ya Maji ama kwenye Wizara ya Maji, bado tutakuwa hatujaweza kuthamini kwamba maji siyo tu kwamba ni uhai, lakini vile vile maji ni utajiri mkubwa kwa Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea mbele zaidi, nishukuru vile vile kwamba katika hotuba ya Waziri ametambua tatizo kubwa sana la maji ambalo lipo katika Wilaya ya Hai hasa katika upande wa tambarare wa Wilaya ya Hai.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la tambarare la Wilaya ya Hai kuna vijiji ambavyo vina tatizo kubwa sana la maji. Inaweza ikawa siyo rahisi kwa watu wengi kuamini kwamba katika Mlima Kilimanjaro kuna vijiji vina tatizo kubwa sana la maji, lakini ni ukweli kwamba katika eneo la tambarare ambapo kina Kata za KIA, Kata ya Masama Rundugai na Kata za Machame Weruweru katika Vijiji vya Sanya Station, maeneo ya Matakuja, maeneo ya Vijiji vya

Tindigani kuna tatizo kubwa sana la maji. Tatizo kubwa zaidi la maji katika vijiji hivi ni kwamba maji ya *gravity* yanayotoka katika Mlima Kilimanjaro hayajafika kwenye vijiji hivi, lakini vile vile uchimbaji wa maji katika maeneo haya umeshindikana kwa sababu maji yaliyoko katika eneo lote hilo yana *level* kubwa sana ya *floride*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri amekiri katika ukurasa wa 116 wa hotuba yake ametambua kwamba, utafiti uliofanywa katika maeneo ya Zarau, *Sanya Station*, Mtakuja, *KIA Village*, Mkoraya, Bomang'ombe na Majengo Kat, kuna tatizo kubwa la *floride* ambapo kiwango cha kawaida kinachokubalika cha *floride* ni 4.0, lakini katika maneo hayo kuna from 9.2 mpaka 39 ya *level* ya *floride* ambayo ni kubwa sana, haifai kwa matumizi ya binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri katika majumuisho yake, aniambie kwamba, pamoja na kwamba, vijiji hivi vimetajwa katika mpango wetu wa Serikali wa mwaka huu wa fedha na mwaka ujao wa fedha kwamba, mwaka huu wa fedha Kijiji cha Mbatakerero, Ngosero, *Sanya Station* na Mtakuja pamoja na Chenka, vitapatiwa maji, lakini ukweli ni kwamba, mpaka dakika hii ni Kijiji kimoja tu cha Mbatakerero na Ngosero, ambao angalao mradhi wa maji umeanza kwa mbali. Lakini vilevile bado havijapata maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile katika mwaka ujao wa fedha kimewekwa kijiji cha Tindigani, Kwa-Sadala, Kimashuku na Bomang'ombe. Ni kweli Bomang'ombe kuna maji, lakini maji yamepungua sana kutokana na kukua kwa Mji wa Bomang'ombe. Kwa bahati mbaya sana katika maeneo haya haitawezekana kuchimba maji ya ardhini kwa sababu ya *floride level* iko juu sana. Kwa hiyo, wananchi hawa wanateseka sana na nitashukuru sana katika majumuisho kama Mheshimiwa Waziri atawea kusema chochote kuhusu uwezekano wa kuhakikisha kwamba maji katika vijiji yanapatikana na yanakuwa ni maji ya *gravity* ambayo yanatoka katika *scheme* za maji katika Mlima wa Kilimanjaro. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo ni la kwanza la msingi ambalo ningependa nilizungumze kwa niaba ya wananchi wangu wa Hali. Sasa niingie katika suala la *water as a natural resource* na *water management*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii ina *policy* ya maji. Nimeisoma sana *policy* ya maji ya mwaka 2012. Pamoja na kwamba ina miaka 10, lakini bado ina mambo ya msingi sana ambayo kama yan gezingatiwa na yakafanyiwa kazi na yakepewa *resources*, tuna Sera ya Maji ambayo ni Sera nzuri ambayo inahitaji tu kuipatia fedha. Ikitekelezeka hakika maji yatakuwa ni utajiri mkubwa kwa Taifa hili. Lakini kwa bahati mbaya sana ukiangalia maji yetu katika Taifa hili yanasimamiwa na mabonde tisa ya maji, kwa maana ya Bonde la Pangani, kuna Bonde la Ruvu pamoja na Wami, kuna Bonde la *Lake Victoria*, kuna *Lake Tanganyika*, kuna *Lake Rukwa*, kuna Ruvuma pamoja na *Southern Coast*, kuna *Eyasi Basin*. Ziko *basin* kama tisa. Lakini ukiangalia idadi ya fedha ambazo *Basins* hizi zimepewa ili ziweze kusimamia maji au *resource* ya maji kwa nchi nzima ni fedha kidogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka huu wa fedha, bajeti ya mwaka huu, pesa pekee ambayo imetolewa kwa ajili ya *reserve* zote hizi ni Shilingi bilioni 1.8 ambayo ndiyo fedha za ndani. Hizi fedha ni kwa ajili ya kulipa mishahara tu. Kwa hiyo, *programme* nydingi za kuendeleza mabonde haya hazina fedha za ndani. Hizi ni fedha za kulipa mishahara na *capacity building* kwa ajili ya watumishi wachache. Lakini fedha nydingine zote ambazo zinategemewa ambazo ni Sh. 17,487,000,000/= ni fedha kutoka kwa wafadhili. Ina maana wasipotoa wale wafadhili, hatuna mkakati wowote wa ndani wa kuweza kusimamia rasilimali maji, ambayo ni muhimu sana kwa Taifa hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tusiyaangalie tu maji kama kitu cha kunywa ama kutumia kwa matumizi ya kibinadamu ya kawaida. Ni kweli hiyo ndio *priority namba one*. Lakini maji vilevile yanaweza yakawa ni *source* kubwa sana ya kuondoa umasikini katika maeneo yetu ya vijiji. Kwanza maji katika hatua yua kwanza ni lazima yatumike kama maji ya kutumiwa

na binadamu, lakini katika hatua ya pili maji yaonekane kama rasilimali muhimu mno, kwamba, huwezi kuzungumza kuondoa umasikini kwa wananchi 80% wanaoishi vijijini kama huna mkakati na programu ya kusimamia na ku-manageyale maji yako yaweze kutumika kwa ajili ya shughuli za maendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa haya mabonde yetu sita ambayo ndiyo yanasmamia rasilimali maji katika Taifa, ukiangalia idadi ya fedha ambazo tumegawia hizi Mamlaka ni fedha kidogo sana. Nichukue kwa mfano Bonde la Pangani, ambalo linasimamia karibu wakazi milioni nne. Bonde la Pangani imeandikwa ripoti moja nzuri sana, wamefanya *situational analysis* ya Bonde la Pangani, wameeleza *crisis* ambayo ni *imminent*, ambayo ni lazima itajitokeza katika Bonde la Pangani kama hatua za makusudi hazikuchukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wanapigania maji kati ya Wakulima na Wafugaji. Kuna kupigania maji kati ya *Wildlife* pamoja na matumizi mengine ya *Hydro-Power*. Kama hakuna *management* ya mambo yote haya, ni lazima patatokea *crisis* kama ambayo tunaona katika maeneo mengi wafugaji na wakulima wanapigana kwa sababu ya maeneo ya kulisha, sasa itakuwa ni kwa sababu ya maeneo ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile niseme tu jambo moja kwa niaba ya Mkoa wa Kilimanjaro, maji mengi yanatoka katika Mlima Kilimanjaro yanakwenda katika *lower basin*, ambako yanatumika kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kimaendeleo na za kijamii. Lakini vilevile tumekuwa hatuna sera maalum ya uvunaji wa maji ya mvua. Nimesikia baadhi ya Wabunge wengi hapa wamechangia, hatuna mkakati wa makusudi wa kuvuna maji ya mvua. Kuvuna maji ya mvua siyo tu kwa sababu ya matumizi ya nyumbani, ni hata kwa matumizi mengine ya kiuchumi katika matumizi mengine ya umwagiliaji maji. Hatuwezi kuzungumzia suala la *food security* kama hatuna mpango wa kuvuna maji. Yale machache yanayochuruzika kutoka mlimani, tukisema tuyatumie kwa ajili ya *irrigation*, watu katika ukanda wa tambarare watakosa

maji. Lakini maji ni mengi. Mvua zinanyesha, wakati wa kunyesthesia mvua zinanyesha mvua kubwa, kuna mabonde makubwa ambayo yangekuwa ni rahisi sana kujenga *dikes*. Tunajenga *dikes* tunatengeneza *dam*, tuna-reserve maji kwa ajili ya matumizi ya mwaka mzima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, idadi ya *rainfall* inayonyesha Tanzania ukilinganisha na *rainfall* inayoanguka Botswana, tusingestahili kulalamika tatizo la chakula. Sisi Kilimanjaro tumechoka kuomba chakula kwa Mheshimiwa Lukuvi, tunaomba tafadhalii sana Serikali iweke mpango makini kupitia *Pangani Water Basin* wa kujenga *reserve* ya maji katika mabonde ya Mlima Kilimanjaro. Kwanza ni gharama nyepesi mno, kwa sababu kuna mabonde makubwa ambayo ni *natural*, unajenga tu *dikes* kidogo unazuia maji. Unaweza ukazuia maji mengi sana na yakatumika *throughout the year* bila kutegemea kupewa chakula cha msaada na Mheshimiwa Lukuvi, ambayo ni fedheha sana kuomba chakula cha misaada. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niseme katika mabonde haya, Bonde la Mto Kikavu, Bonde la Mto Weruweru, kuna Bonde la Mto Makoa, kuna Bonde la Mto Semira, yako mabonde mengi ambayo yanaweza yakahifadhi maji mengi mno ambayo yanaweza yakatumika mwaka mzima. Maji hayo yanaweza yakapatikana wakati wa mvua kwa sababu wakati huo kuna mvua nyingi sana. Hatuwezi kutegemea yale maji yanayochuruzika kutoka vyanzo vingine vya maji, tutumie haya maji ya mvua, tuyareserve haya maji. Haya maji yatatumika kwa ajili ya *gravity irrigation* katika maeneo ya chini na nina uhakika kwa utaratibu huo tutakuwa tuna *food security* ambayo ni ya uhakika kuliko hali ilivyo sasa hivi. (*Makoffi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hiyo vilevile inakwenda katika Majimbo ya Moshi Vijijiini, Jimbo la Siha, Jimbo la Vunjo na hata Jimbo la Rombo. Yako mabonde mengi makubwa ambayo yangejengewa *dikes* ndogo tu, wala siyo miradi mikubwa ya kutisha, ila ni miradi ile ambayo inahitaji uthubutu ku-preserve yale maji, yangeweza kutumika katika ukanda

mzima wa tambarare wa Mlima wa Kilimanjaro na watu wakapata chakula bila kuwa na tatizo lolote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima sasa Serikali yetu ione maji kama inavyoyaona madini. Tusiyaone maji kama jambo la kunywa tu, tuone maji kama fedha. Tunaporuhusu mvua zinyeshe halafu maji yote yanakimbilia baharini, halafu wiki ijayo tunalalamika mvua, tukikosa maji kwa msimu mmoja tu tunalalamika chakula. Hatuwezi kuendelea kama Taifa kama tunashindwa *ku-contro/* maji ambayo tunapewa na Mungu halafu tunalalamika. Tunalalamika nini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli, ni lazima uwepo mpango wa makusudi tena mpango wa ndani wa kuhifadhi maji yetu ya mvua. Mikoa yote inanyesha mvua, kila maeneo nchi hii inanyesha mvua. Zinanyesha mvua nyingi tu, mvua zinanyesha nyingi, maji yanakwenda baharini, yanapotea, halafu tunalalamika tena hatuna chakula. Umekuwa ni utaratibu wa kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Sera yetu ya Maji ya Mwaka 2002, katika ukurasa wa 17 wa Sera ile Mheshimiwa Waziri angalia; hatujatoa *priority* katika uvunaji wa maji ya mvua. *Priority* yetu katika Sera yetu ya Maji inazungumzia yale maji ambayo ni *naturaly available*. *Lakini harvesting* ya maji ya mvua hatujaiona ni *priority*, hatujaitambua katika Sera yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nakushukuru Mheshimiwa Freeman Mboge. Sasa namwita Mheshimiwa Makilagi atafuatiwa na Mheshimia Dkt. Pudenciana Kikwembe.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kutoa mchango wangu mdogo katika sekta hii muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kusema kwamba, maji ni uhai na kwa kweli, maji ndiyo kila kitu. Bila maji hakuna kilimo, bila maji hakuna afya, bila maji hakuna uchumi wa Taifa letu la Tanzania. Lakini unapozungumzia maji, unamzungumzia huyu mwanamke ambaye kwa kweli ndiye tunamtegemea katika uzalishaji wa uchumi wa Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze moja kwa moja kuunga mkono bajeti hii kwa sababu, kwanza mimi mwenyewe ni mdau wa maji, lakini vilevile niko katika Kamati ya Maji, lakini vilevile naunga bajeti hii mkono kwa sababu, kwanza, Wizara imejiaandaa vizuri sana safari hii. Hata ukisoma kitabu chenyewe kimesheheni, bango kitita hili linatupa sisi Wabunge fursa ya kujua kila kitu kilichopangwa kufanywa na Serikali na hata kilichofanyika. Kwa kweli, naomba nimpongeze sana Waziri na timu yake yote kwa kazi nzuri sana waliyoifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono bajeti hii kwa sababu, Chama cha Mapinduzi, kama tulivyoahidi kwenye llani kwamba, tutajitahidi kufikisha maji katika Miji na Vijijini kwa kweli, ukipitia kitabu hiki kazi imefanyika sana. Nilikuwa nasoma, naona sasa suala la upatikanaji wa maji Mijini tumeshafikia 86%, ni ukombozi kusema ukweli. Lakini siyo kuishia 86% peke yake, ukisoma kitabu hiki utaona hata mipango sasa ya kufanya Miji yetu ya Tanzania yote sasa inapata maji kwa kiwango cha asilimia cha ya juu zaidi. Naomba nipongeze sana mpango huu na ninaiomba Serikali, iendelee, ikaze buti ili Miji yetu yote ipate maji. Nimefurahishwa sana kusikia sasa hata Jiji la Dar es Salaam ambalo mwaka 2012 nilisimama hapa nikasema kama hamtatenga fedha za kutosha mwaka huu sitaunga mkono, nimefurahi sasa fedha za ndani zimetengwa karibu zaidi ya Shilingi bilioni 40. Naomba niipongeze sana Serikali yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimefurahishwa na mpango sasa, Serikali yetu sasa imewasiliza wananchi wa Same kilio chao, kule Mwanga na maeneo mengine, Serikali

inakuja na mpango makakati wa kuhakikisha wananchi wale waliopiga kelele kwa muda mrefu sasa wanapata maji safi na salama. Siyo pale tu, maeneo mbalimbali ya nchi yetu, kwa kweli, kitabu hiki kimenifurahisha na ndiyo maana naunga mkono asilimia mia kwa mia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuunga mkono, sasa naomba nilete kilio cha wanawake wa Tanzania na kwa kweli, natoa pia kilio cha wananchi wa Tanzania. Mimi Ubunge wangu ni wa Tanzania nzima kwa mujibu wa Sheria. Kwa bahati njema kabla sijaja hapa Bungeni, huwa nafanya ziara nakutana na wananchi na huwa sifanyi maandamano. Huwa nafanya Mikutano ya Hadhara, naongea na wanawake, naongea na wananchi wote. Katika Mikutano yangu, huwa nawapa nafasi wananchi waulize maswali baada ya mimi kuongea na wao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Mikutano ile nimeshakwenda Mikoa mbalimbali kule Lindi, Morogoro, Pwani, Mtwara, kila mahali nimefika. Nimeshatembelea Mikoa 10 kabla sijaja hapa. Katika ile Mikutano nimejaribu kuuliza maswali, katika wananchi 10 waliopata fursa ya kuongea na katika maswali waliyoniuiliza na katika mambo waliyonituma niyalete hapa Bungeni, wale wote nilioongea nao, katika watu 10 walioniuliza maswali, watu nane walilia kilio cha maji; na watu wawili waliobaki ndio waliozungumzia mahitaji mengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata Wabunge humu ndani, nilipotoka huko ziara nimejaribu kuongea na Wabunge, nimeshaongea na Wabunge zaidi ya 200 na hata wa Upinzani wakiwemo, asilimia ya Wabunge wote wanasema kilio cha maji ndiyo kipaumbele namba moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba niwasilishe kilio hicho kabisa kwa heshima kubwa na unyenyekevu, tuiombe Serikali yetu ambayo ni sikivu, safari hii ifanye maajabu. Kama walivyosema Wabunge wenzangu, bajeti imekuja, naomba kabisa tuungane na maoni ya Kamati. Kama yalivyoelezwa vizuri kuanzia ukurasa wa tano

mpaka ukurasa wa saba, Serikali itafute fedha za ziada Shilingi bilioni zaidi ya 100 tuweze kutekeleza miradi kama ilivyooneshwa kwenye kitabu hiki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu kusema ukweli, watu wanahangaika sana. Ninapozungumza hivi akina baba walio wengi wanajua; kazi yao huwa ni kusema nataka maji ya kuoga, nataka maji ya kunywa, nataka maji ya kufua, nataka niwe msafi. Wanaohangaika na kutembea tangu asubuhi mpaka saa 12 wanahangaika ni wanawake ambao kusema ukweli ndiyo nguvu kazi ya Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, najua chini ya Kamati ya Mzee Chenge, kwa sababu pia ni Kamati makini sana, chini ya Serikali yetu madhubuti, nina imani Kamati ya Bajeti, itasikia kilio cha Kamati ya Fedha, chini ya Uongozi wa Mwenyekiti wetu Mzee Msolwa na watathubutu na watafanya uamuzi wa busara kutenga fedha kabisa za kutosha kupeleka katika Sekta ya Maji kwa manufaa ya Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo nina imani mmenisikia, na kusema ukweli mimi ninasema ninaunga mkono. Nami ninavyoona, Waswahili wanasesma dalili njema huanza asubuhi. Nimeona Kamati ya Bajeti kila wakati inakutana, na Serikali wakati wote inaangalia, nina imani jambo hili kabla ya kuhitimisha bajeti hii na pengine mara baada ya kukamilisha mjadala huu na hata baada ya kumaliza Bunge, tutapata majibu namna ya kuongezewa fedha ili kazi ziende zikafanyike. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hilo, naomba sasa niende moja kwa moja kuzungumzia matatizo ya dawa ya maji. Kwa mujibu wa taarifa tuliyopokea hapa na Kamati imeunga mkono, kwamba kodi ya dawa ya maji imepunguzwa. Naomba niungane na maoni ya Kamati kwamba, badala ya kupunguzwa, tunaomba iondolewe kabisa. Kwa sababu Mamlaka za Maji hapa nchini zinaendesha maji kama huduma. Kusema ukweli gharama za maji huko Vijijini ndoo inauzwa Sh. 20,000/=, Sh. 10,000/=

kwa ndoo. Suala la maji ni huduma, sio biashara. Ninaomba hii kodi ya madawa ya maji iondolewe kabisa, sio kupunguzwa ili wananchi waweze kupata maji safi na salama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nilete kilio sasa cha wale wananchi wanaoishi katika mazingira makame na wananchi wanaoishi katika mazingira ambayo wakichimba maji hawayapati. Hata wakiyapata, wakati mwingine yanahamahama, mfano Mkoa wa Mtwara, Wilaya ya Nanyumbu. Nanyumbu wakichimba maji wanayakuta, lakini yana chumvi, lakini baada ya muda mfupi yanahama. Kuna Miji kama ya Kisarawe kule Vikumburu, kuna Miji kama ya Longido kule Ngorongoro, kuna kule Nzega, kuna kule Igunga na maeneo mengine. Wana hali ngumu sana, hakuna mito, hakuna nini, tulikuwa tunaomba sana maeneo haya yapewe kipaumbele katika mpango huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefurahishwa sana kuitia kitabu hiki kimetuonesha kabisa, jinsi ambavyo Serikali imejipanga kupeleka maji katika kila Halmashauri. Tumeona mpaka fedha zilizopelekwa kwa kila Halmashauri, zinajieleza kabisa na kwa kweli tumefurahi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi naomba niseme kwamba pamoja na mipango hii bado hivi vijiji vilivyoainishwa hapa havitoshi. Kilio cha maji ni kikubwa sana, tunaomba kabisa fedha zitakapopatikana tuongeze miradi zaidi kwa ajili ya kuimarisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nizungumzie upotevu wa maji. Serikali inafanya kazi nzuri, tunajenga miundombini, lakini baadhi ya maji yanapotelea barabarani. Naomba sasa Serikali, kuitia Taasisi zetu za Mamlaka za Maji Nchini na kuitia Bodi zote za Mamlaka za Maji zidhibiti na ziweke mkakati maalum kama walivyofanya Bodi ya Maji DAWASA. Tujitahidi kuwabaini wale wote wanaofanya hujuma katika miradi hii. Tujitahidi kabisa kwa sababu wapo watu wanafanya hujuma humu barabarani, wanapita wanachukua vyuma vichakavu, wanapita wengine

wanajiunganishia mabomba, wanapita wengine wanafunga mita zisizofaa, wale wote tuwadhibiti na hata Watendaji wetu pia wasiokuwa waaminifu. Anapewa kazi ya kwenda kununua mita ya Sh. 10,000/= ye ye anachukua fedha nyingine anaweka mfukoni, anakwenda kununua mita ambayo ni ya chini ya kiwango. Anapewa fedha akanunue bomba la maji, anakwenda kununua bomba chini ya kiwango na fedha nyingine anaweka mfukoni. Wote hao tuwabaini na Serikali ichukue hatua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata Serikali ingefanya namna gani, lazima tushirikiane na wananchi kuhakikisha suala la maji linatataluka. Naiomba niimbe Serikali na kwa sababu Sera ya Maji imetamka kabisa na kwa sababu Miongozo ilishatoka na hata katika Bunge liliopita Kamati ya Maji tulisema kwamba hebu tusaidie kuhamasisha wananchi waanzishe utaratibu wa kuvuna maji kwa kutumia nyumba tunazozijenga. Serikali hapa ilituahidi kwamba sasa inakwenda kuelekeza Halmashauri zote nchini kutunga Sheria itakayofanya sasa kila nyumba inayojengwa hapa Tanzania, angalau inakuwa na michoro ya kuvunia maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipokuwa kwenye Kamati na taarifa hapa inaonyesha kwamba tangu agizo lile limetoka mpaka leo tunavyozungumza ni Halmashauri mbili tu ndiyo zimetekeleza agizo hili. Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa ana-*wind up* atuambie sasa Serikali inasema nini na inawaagiza nini Halmashauri katika suala zima la kuhakikisha inatunga Sheria kwa ajili ya uvunaji wa maji kwa ukombozi wa Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitazungumzia Mkoa wa Mara ambao ndio ninatoka. Pamoja na kwamba Ubunge wangu ni Tanzania nzima, lakini na mimi nina nyumbani na nyumbani ni Mkoa wa Mara. Nimefurahishwa sana kuona mipango iliyowekwa hapa ya kuimarisha Mkoa wa Mara na wenyewe sasa unapata maji safi na salama kama Mikoa mingine. Nimefurahishwa sana na Mpango wa Serikali wa kutupelekea maji Musoma Mjini kutoka 86% mpaka karibu 95%. Naomba

niupongeze sana mpango huo. Naomba mpango huu sasa uende mpaka Wilaya nyingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Amina Makilagi. Sasa namwita Mheshimiwa Pudenciana Kikwembe atafuatiwa na Mheshimiwa Moses Machali.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia katika hoja hii iliyoko mbele yetu. Mimi naomba niende moja kwa moja kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri katika ukurasa wa 52, sehemu ya uboreshaji wa huduma ya maji katika Miji Mikuu ya Mikoa Mipyä. Lakini nitajikita moja kwa moja katika Mkao wangu mpya wa Katavi, Wilaya ya Mpanda Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maelezo ya Mheshimiwa Waziri, inaonesha kwamba, huu mpango wa kujenga tanki la maji Mjini Mpanda, mtambo wa kutibu maji kutoka katika chanzo cha Mto Manga; hii imeelezwa tu kwamba ni mpango ambao unaonekana kama vile ni mpango wa baadaye. Kwa nini nasema hivyo? Kwa sababu hakuna mahali panapoonesha huu mpango unaanza lini? Utakamilika lini? Upembuzi yakinifu umefanyika ama haujafanyika? Tofauti na miradi mingine ambayo imeorodheshwa humu ndani, kwa mfano miradi ya Ruvu, Kimbiji, imeoneshwa inaanza lini mpaka lini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Waziri atakapokuwa anafanya majumuisho awaambie Wananchi wa Mpanda kwa sababu mpaka sasa hivi ninavyoongea pamoja na kwamba mvua zinanyesha, wanatumia maji ya mvua, hawana maji kwenye mabomba. Huu mradi ndiyo mradi ambao ni tegemezi kwa Mkao wa Katavi Wilaya ya Mpanda. Kwa hiyo, tunaomba tupatiwe majibu mradi huu utaanza lini? Utakamilika lini? Mchakato wake ukoje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na hayo nakwenda pia moja kwa moja kwenye mgawanyo wa bajeti. Katika mgawanyo huu wa bajeti, bajeti hii uklisoma vizuri na ukichanganua pesa za maendeleo, nyingi zinakwenda Mijini. Je, wananchi wa Vijijini hawana haki ya kupata huduma hii ya maji? Nami pia natoka Kijijini, najua taabu ya maji wananchi wanayopata Vijijini. Pamoja na mradi wa hivi visima kumi kwa kila Halmashauri mnavyosema lakini bado havijaweza kutatua tatizo la maji Vijijini. (*Makofii*)

Mhehimiwa Naibu Spika, Vijijini ndiko kwenye watu wengi, ndiko kwenye wakulima, ndiko kwenye wakulima wa mboga na matunda, ndiko kwenye umwagiliaji, sasa tusipopeleka pesa za kutosha kwenye hii miradi ya vijijini: Je, tunategemea kweli tutaondokana na umaskini? Kilimo Kwanza tutakifanyaje bila kuwepo na upatikanaji wa maji? Maana yake tunatoka sasa kwenye awamu ya mvua sasa hivi tunaingia kwenye kiangazi. Kwenye kiangazi ndipo tutakapoweza kuanza kulima bustani za mboga mboga na matunda na vitu vinginevyo ambavyo vinahitaji umwagiliaji. Vinginevyo, mtu akishavuna, akiuza mazao yake atakaa anasubiri tena msimu ujao *which means* kuanzia mwezi wa Sita mpaka mwezi wa Kumi na Moja mwananchi wa Kijijini atakuwa amekaa bure kusubiri msimu wa mvua unaokuja kwa sababu hiki kipindi hana uwezo wa kuweza kulima bustani za mboga ama za matunda kwa sababu hana miundombinu ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anafanya haya majumuisho, azingatie sana maoni ya Kamati iliyowaomba Serikali kuongeza karibu Shilingi bilioni 185 katika bajeti hii na wala siyo ijayo, ili wananchi wa Vijijini hasa akina mama wapate maji. Haya mambo ya kusema hela hii tunapeleka sasa Ruvu chini tunasahau Katavi, tunasahau Rukwa, tunasahau Songea Vijijini, tunasahau Kyerwa huko, kwa nini? Wananchi wa Vijijini tumekosa nini? Maendeleo yote yanaelekezwa Mjini: Je, tutapunguza hili wimbi la kusema kwamba wananchi wanahama kutoka Vijijini kwenda Mijini? Hatuwezi kuipunguza *rural urban migration* kama hatutawenza

kuangalia *disparity* iliyopo kati ya *rural and urban development.* (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naipongeza Serikali kwa juhudzi zake zote zinazofanya lakini naomba sana tena sana kwa niaba ya Wana-Katavi na Wana-Rukwa wenzangu na Watanzania wote hasa tunaoishi Vijijini, hii pesa Serikali ifikirie katika bajeti hii kuitoa ili iweze kuongezeka katika hii bajeti iliyopo hapa, wananchi tuweze kupata maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengi wamekwishasema hapa kwamba maji ni uhai, maji ni usafi, maji ni afya, ni ukweli usiopingika, bila maji hatutapunguza maradhi, bila maji hatutapunguza umaskini. Kwa hiyo, mimi naomba mipango ni mizuri sana iliyowekwa humu uwagiliaji maji, sijui vitu gani, lelele, vipo vingi sana! Ni vizuri, lakini vitafanyika vipi? Kama hii bajeti imejjelekeza zaidi Mjini kuliko Vijijini, hawa wananchi wa Vijijini wana makosa gani? Kosa ni kukaa Vijijini? Siyo kosa na wakulima wengi tunajua wako Vijijini. Asilimia 85 ni wakulima na ndiyo wananchi wanaokaa Vijijini. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana Serikali isikilize na kwa kweli nawaomba Wabunge wenzangu hakuna ambaye amesimama hapa hajasema suala la maji. Naomba kabisa tukubaliane na tuishinikize Serikali iongeze hiyo hela katika bajeti hii na wala siyo ya mwaka kesho, kwa maana ya kwamba hata kwa mwaka kesho napo longezeke, bajeti iwe inaongezeka kwa kuangalia vyanzo vyta mapato vyta ndani na siyo tu kutegemea pesa za kutoka nje. Hizi pesa za kutoka nje zinakuja kujazia tu. Wakizitoa hata ukiangalia kwenye haya *ma-book*, utasoma kwenye hii *vote*, hela nydingi iko Mjini. Iko Ruvu, Dar es Salaam, Kimbiji sijui wapi, hakuna Vijijini humu hela. Sasa tunafanya je kazi? Wananchi tunawaambiaje kule Vijijini? Tunawaambia nini? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii katika kata ya Mamba maji ndoo moja ni Sh. 1,000/=. Nimeambiwa na Peramiho, ndoo moja Sh. 1,000/=. Mwananchi kule hana uwezo. Sasa hivi ndiyo anaanza kuvuna mazao. Muhula wa shule ujao unakuja, anatakiwa kutoa ada, ana familia

nyumbani ya watu siyo chini ya 12. Atatumia ndoo ngapi kwa siku? Shilingi ngapi kwa siku ata-*spend* kwenye maji? (*Makofi*)

Nimeongelea mwaka jana kwenye bajeti, vyanzo nya maji Mkoa wa Katavi na Rukwa tunavyo vingi. Wizara ya Maji na Katibu wake niliongea naye mwaka 2012 akaniahidi ataleta timu ya wataalam kuja kuchambua na kuchukua *sample* ya maji yanayotoka kule, yanatiririka kati ya Kata ya Muze pamoja na Kasanza na Mamba. Tuna vyanzo vizuri sana na picha nilimbletea yule Katibu. Hakuna kilichofanyika hata kimoja! Tukisema, mnasema wanasiasa wanapiga kelele. Hizi siyo kelele, haya ni matatizo ya wananchi, ni matatizo ya kina mama, ni matatizo ya wananchi Watanzania hasa wanaoishi Vijiji. Wataalam wamekuwa na tabia kwamba mkiongea wanakwambia kelele za wanasiasa hizo. Achaneni nao! Hatuwezi kufanya kazi kwa mtindo huu! Hatuwezi kufika, katika malengo tuliojilweke ya maendeleo. Lazima tuwe na *commitment*, tufanye kazi wananchi wanataka maendeleo, wananchi hawataki porojo, wananchi hawataki maneno, wananchi wanataka vitendo ambavyo vitawalet ea maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana, mimi nakaa Kijiji kama nilivyokueleza kuwa hiyo adha za Vijiji, nazijua tofauti na wengine wanaotoka Mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa maji katika kila Vijiji kumi, kwa namna ambavyo kama tutaufanya tathmini inaonekana kama tumeshindwa. Sasa tunafanyaje? Naomba Wizara iangalie tunafanyaje ili kuhakikisha mradi huo tunauendeleza na tunaumaliza na tunaendelea na mambo mengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, napenda kuongelea uhifadhi wa vyanzo nya maji hasa mabonde ya maji, kwa mfano, Ziwa Rukwa. Mwaka 2012 nimeongelea sana kuhusu Ziwa Rukwa, nimewaambia Wizara ya Maji kwa kushirikiana na Wizara ya Mazingira wakae waangalie, lile Ziwa lipo hatarini kupotea. Kwa nini lipo hatarini kupotea? Sasa hivi mvua zikinyesha, maporomoko yale ya

udongo yanakuja kufukia Ziwa. Ziwa limehama na nilimwomba Mheshimiwa Waziri wa Maji pamoja na Waziri wa Mazingira na wataaalam wake waende kwenye lile Ziwa Rukwa wakaliangalie, lakini hakuna mpaka leo. Mheshimiwa Malocha Mbunge wa kule ni shahidi yangu, kama walikwenda, aseme hapa. Naamini hakwenda mtu yejote kwa mwaka 2012 wote mpaka leo hii. Kisa, tupo Vijiji. Sasa wote tutahamia Mijini, hii Miji itatosha kweli? Maana yake ndiyo tutahama sasa tufuate maendeleo Mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana, wananchi wa Vijiji wana mchango mkubwa sana katika maendeleo ya Taifa hili. Naomba katika bajeti hii, Kamati imetoe mapendekozo ya kuongezewa angalau Shilingi bilioni 185, zitafutwe na ninajua Serikali ina uwezo wa kufanya hivyo. Kwa hiyo, itafute hizo pesa iongeze kwenye hii bajeti, wananchi wa Vijiji nao wanufalke na mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja lakini kwa msisitizo hizo hela zitafutwe. Ahsante. (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kimwembe. Sasa namwita Mheshimiwa Machali, atafuatiwa na Mheshimiwa Salome Mwambu.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru nami kwa kunipa fursa nichangie hoja ya maji. Naomba nianze kwa kujielekeza ukurasa wa 184 na ukurasa wa 192.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ridhaa yako naomba ninukuu Mheshimiwa Waziri hapa amejibu hapa katika ukurasa wa 184 mgawanyo wa fedha za Mfuko wa Maji kwa kila Halmashauri kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014.

Naomba ni-*appreciate* mmtenga pesa japo pesa ni kidogo, lakini masikitiko yangu yanajielekeza kwenye ukurasa wa 192, kuna sehemu moja linatolewa angalizo, naomba ninukuu: "Halmashauri mpya za Mijini hazikupata fedha kwa sababu hazina miradi ya maji ya Vijiji." Halmashauri hizo

zimetajwa ikiwemo Halmashauri ya Mji wa Kasulu. Naambiya kwamba na Tarime Mbunge wa Tarime anaeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo cha kuonekana kwamba baadhi ya Halmashauri za Miji ikiwemo Halmashauri ya Mji wa Kasulu ambayo ina Vijiji vingi ambavyo vina tatizo la maji, jambo hili ni kutokuwatendea haki wananchi wa Halmashauri ya Mji wa Kasulu ambayo ni Halmashauri mpya hasa wananchi wa Vijiji kama vya Erujuu, kule Mhunga, Kalunga, Kidiamma, Kigondo na maeneo mengine. Sasa ningeomba Serikali mkae mliangalie hili kwamba huu ni uzembe wa Mhandisi wa Maji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu kwa kutokuona umuhimu wa kuomba fedha kwa ajili ya miradi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa kweli Waziri aangalie na bahati nzuri tumekuwa tunawasilliana. Nimepata kumweleza kwa mfano Mradi wa Maji wa Erujuu kwamba ni muhimu sana tangu mwaka 2012 na *this time* hakuna fedha na hivi ndivyo Vijiji miongoni mwa Vijiji ambavyo vina tatizo sugu la maji kwa Halmashauri ya Mji wa Kasulu. Nitaomba wakati Mheshimiwa Waziri anafanya majumuisho angalau atafute fedha kidogo. Kwa mfano, hii Kata moja ya Muhunga ambayo ina Vijiji vya Erujuu, Kalunga pamoja na Muhunga wanahitaji takribani Shilingi milioni kama 300, maji yakipatikana, na pale kuna miundombinu ya maji ni mradi ulijengwa toka miaka ya 1970 kwa kuwa haukuwa unafanyiwa *rehabilitation*, matokeo yake mradi ulikuwa. Wanachi wanataabika, wanakosa maji. Miundombinu baadhi kama matenki, kuna tenki kubwa sana limekaa pale limechakaa, fedha hazikutengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa kweli katika suala hili Mheshimiwa Waziri ili kusudi niweze kuunga hoja, wakati anapo-*wind up* angalau aseme chochote juu ya mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ukiangalia katika kitabu chetu hapa juu ya miradi ambayo inatekelezwa mwaka huu, upo mradi mmoja wa maji ambaa unafadiliwa kwa hii miradi

ya *World Bank*, unatekelezwa katika Kijiji cha Nyumbigwa katika Halmashauri ya Mji wa Kasulu hali kadhalika. Mradi huu umegubikwa na utata, ulipaswa ukamilike ndani ya miezi sita. Mradi umeanza kujengwa tangu mwaka 2012 mwezi wa Novemba, Desemba lakini maajabu Mkandarasi aliyepewaa kazi hakuweza kujenga, mradi ule alianza kwa kujenga tenki limeishia kwenye *foundation stage*. Tuhesabu miezi kuanzia Novemba hadi leo hii mwezi huu unakwenda kwisha, miezi sita imekwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni wazi kabisa kwamba Serikali imeweza kumpatia Mkandarasi zabuni ya kuweza kutekeleza mradi huu, mtu asiyekuwa na uwezo wa kufanya kazi. Naomba yule mtu afukuzwe mara moja kwa sababu anachokifanya pale ni danganya toto.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu pia jambo lingine wakati ndiyo wameanza kujenga, nilikwenda pale nikakuta kuna mchanga wa ovyo, nikasema mkijenga mtabomoa. Hii ni kutokana na ushauri wa Mhandisi wa Ujenzi ambaye ameshatoa ushauri kwamba mchanga fulani usitumike, ni kama vile ni udongo.

Sasa ningeomba kwa kweli wakati Mheshimiwa Waziri ana-*wind up*, huyu Mkandarasi ambaye anatokea Mbeya, jina la Kampuni yake hapa linatajwa kuwa ni *Consultant Engineers Research Associates Limited* ya Dar es Salaam nao wanaonekana tu wako pale hawawezi kuishauri Serikali vizuri na ndiyo maana unaweza kuona kwa kipindi cha miezi sita wamejenga tenki limeishia kwenye *foundation stage*. Hii haikubaliki! *Contractor ni M/S Earth Plan Contractors Limited* ya kutoka Mbeya. Mambo gani haya wanakuja kutuchazea akili? Mheshimiwa Waziri naomba kwa kweli katika hili uweze kuangalia kwamba watu hawa wanafanya nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tunaona kwamba vimetajwa baadhi ya Vijiji ambavyo pia vitawezza kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Nilikuwa nawasiliana hapa na Mheshimiwa Mbunge wa Arumeru Mashariki, kuna baadhi ya Vijiji mmeandika kwamba mradi

unatekelezwa, havipo katika maeneo haya. Kwa hiyo, takwimu ambazo mnapewa Waheshimiwa Mawaziri, mmpewa takwimu ambazo ni feki kwa mujibu wa Mheshimiwa Mbunge. Kwa mfano, Kijiji cha Kasanumba kule Meru Mheshimiwa Mbunge anasema hakuna Kijiji hicho ambacho miradi ya *World Bank* inatekelezwa.

Sasa nafikiri hebu mjaribu kwenda ku-deal na watu wenu ambao wako kule kwenye Halmashauri, kwa nini wanawapa taarifa za uongo ambazo mnazileta hapa Bungeni? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Nkasi ukurasa wa 52 mmeonyesha kwamba Serikali kuna miradi ambayo mnatekeleza katika Halmashauri za Wilaya ya Kasulu, kule Nkasi hali kadhalika kwa Mheshimiwa Ally Kessy ambaye anasema mara nyingi huwa anaoga akiwa hapa Bungeni kwamba akiwa huko huwa haogi kwa sababu ya shida ya maji.

Hebu tuombe basi haya maeneo kama katika Halmashauri za Wilaya ya Kasulu, huko Nkasi, Namanyere, hizi fedha ambazo tumesema ni kwa ajili ya maji safi pamoja na usafi wa mazingira, zipelekwe na miradi tuone ikitekelezwa isije tu kuwa kwamba ni suala la kuandika kwamba mna mipango mizuri lakini utekelezaji wake ni kidogo, itakuwa haitusaidii.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, hebu niombi mtufafanulie vizuri, maana yake kwa mfano nimeona katika Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu mmesema kwamba kiasi cha takribani dola 2,300,000 zitatumika kwa ajili ya *program* ya usafi pamoja na maji safi, mnakwenda kutekeleza kwa maana ya kujenga miradi? Maana yake hii bado ni kauli ambayo ni tata.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupata ufanuzi katika hili. Mnapozungumzia *program* ya maji safi pamoja na usafi wa mazingira, mnamaanisha nini? Mtaweza kuchimba mitaro na tuone sasa kwamba mabomba

yanaunganishwa kwenda kwenye Vijiji mbalimbali au inakuwaje? Hili jambo bado halijakaa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningependa Wizara kwa kweli hizi fedha japokuwa bado ni kidogo lakini tuone zikitumika vizuri.

Tatizo kubwa ambalo linajitokeza ni usimamizi mbovu huko katika Halmashauri zetu, ndio maana unakuta, mfano mradi huu nimewaambia, miezi sita inakwisha tenki bado liko kwenye *foundation stage*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni tatizo. Ni wazi kwamba Mhandisi wa Maji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu ameshindwa kusimamia mradi huu. Nitawashangaa sana kama miezi sita, huyu anapaswa kuwa *sample* tu pamoja na huyo Mkandarasi ambaye mmempatia kazi. Miezi sita wamejenga tenki ambalo tukiangalia kipenyo chake ambacho ni kidogo sana, miezi sita wameishia kwenye *foundation stage* halafu tunamwacha kwamba huyu Mkandarasi anaendelea kufanya kazi na Mhandisi yuko pale!

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa na mashaka, nitaanza kuhoji wakati mwingine sasa pengine uwajibikaji wenu nyinyi kama Mawaziri angalieni isije kuwa miongoni mwa Waheshimiwa Wabunge ambao huwa wanasesma Mawaziri mwajibike kwa sababu mmeshindwa kufanya kazi yenu vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sisemi sasa hivi, lakini kama mtamwacha Mhandisi huyu ambaye anashindwa kusimamia kazi yake vizuri na mtamwacha huyu Mkandarasi ambaye kwa kipindi cha miezi sita mradi ambao ni mkubwa unaogharimu zaidi ya Shilingi milioni 850 amefanya kazi kwa kuweza kujenga *foundation* halafu ameacha leo

anakwenda kudai malipo alipe, nimemwambia Mkurugenzi ukimlipa fedha, huyu Mkandarasi hizo pesa zitawagharimu nyinyi pamoja na Mkurugenzi wenu. Tutaanza hapa hapa!

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishie hapa, nitahitaji ufanuzi katika maeneo hayo ambayo nimeya-*address* Bungeni. Ahsante. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Moses Machali. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Salome Mwambu, atafuatiwa na Mheshimiwa Blandes na Mheshimiwa Ole-Sendeka ajiandae.

**MHE. SALOME D. MWAMBU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa kipekee naomba nitoe shukurani zangu. Najua shukurani zimesitishwa, lakini kwa unyeti wa jambo lillilonipata naomba niwashukuru wananchi.

Kwanza kabisa, nawashukuru Madaktari na Manesi walionihudumia wakiniombea mpaka sasa hivi nipo hapa na Mwenyezi Mungu akasikia sala zao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kweli nilipatwa na hali ambayo kila mtu hakutegemea kuwa mimi ningeweza kusimama tena hapa, lakini kwa ajili ya uwezo wa Mwenyezi Mungu akanisaidia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliokuwa wananiombea, wengine walikuwa wanatumwa *message* kwenye simu, wengine Makansani na Misikitini, dua hizo Mwenyezi Mungu akazisikia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sina budi kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Iramba Mashariki, Wilaya mpya ya Mkalama, kwa utulivu na kunivumilia ule muda wote niliokuwa naumwa, lakini hawakusita kuendelea kujishughulisha na shughuli zao za maendeleo. Wakati huo huo wakiniombea.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijikite katika mambo mawili au matatu tu. Kwanza kabisa, kuhusu maji; maji limekuwa tatizo la Kitaifa. Kila mahali kama Waheshimiwa waliotangulia walivyoongea, tatizo kubwa ni maji. Hili tatizo linaathiri watu wachache. Sana sana ni wanawake na watoto na wanafunzi wanachelewa kwenda mashulenii kwa ajili ya kutafuta maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Serikali iongeze bajeti angalau hili tatizo la maji tulimalize. Ni tatizo ambalo kwa kweli sasa hivi, mpaka imekuwa aibu kuliongelea kila wakati. Tunaongea kila wakati tunashida ya maji, tuna hiki, tuna hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maeneo ambayo maji hayapatikani. Mfano, katika Wilaya yangu ya Iramba Mashariki, Kijiji cha Matongo, mwamba ni mgumu ambao hauwezi ukapasuliwa wala kutobolewa. Kwa hiyo, wananchi hao tangu uhuru wana shida, hawajaona maji safi na salama. Naomba Mheshimiwa Waziri atamke kitu atakapokuwa anafanya majumuisho, kuhusu hawa wananchi wa Kata ya Matongo, wana shida sana na maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nashauri Serikali iangalie huo msimamo ilioweka wa wananchi wote kuchangia miundombinu ya maji hasa kwenye ukarabati. Kuna mahali pengine wanashindwa, kwa hiyo, linakuwa ni tatizo. Tukiangalia wananchi wana mambo mengi ya kuchangia. Wachangie mashule, wachangie vituo vya Afya, Zahanati na kadhalika. Hili suala la maji bajeti ya Serikali ingeongezwa ili wananchi wachangie mambo mengine, lakini siyo miundombinu ya maji inapokuwa imeharibika. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhili nisipoipongeza Serikali ya CCM kwa jitihada zake inazojitahidi kuhakikisha maji yanafika vijijiini. Katika *phase* ya kwanza kwenye Wilaya yangu ya Mkalama, kuna visima 10 nilivyopatiwa. Nimepatiwa visima vya Uguguno, Isene, Nyahaa, Bumanga, Kikonda, Mitala, Ndikutu, Kidarasa na kadhalika, hivi visima kweli vimetobolewa maji yapo, lakini vimekuwa kama pambo, kwa sababu viko ndani ya mradi wa Benki ya Dunia. Imekuwa muda tangu maji yatobolewe, lakini miundombinu ya kusambaza inasuasua kuwafikia walaji au watumiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vile vile Serikali na Wizara ihakikishe basi na yenyewe inaweka mkono wake mahali ambapo tunajua fedha za wafadhili zinachelewa kuja au wanatoa wenyewe wanapoamua, kwa Serikali kuweka fedha zake illi longezee hapo kwenye hizo fedha, tusitegemee wafadhili tu. Ninachokiomba ni hicho, Serikali isikie kwa sababu ni kilio kikubwa cha wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hii awamu ya pili, tumeomba visima 30 katika Wilaya ya Mkalama, hivyo visima vitekelezwe kwa sababu sisi ni wamojawapo ambaao tupo kwenye maeneo ambayo hayana vyanzo vya kudumu vya maji. Illi kulipunguza tatizo hili, basi Serikali na Wizara iangalie namna gani iongeze matenki ya kuvuna maji ya mvua. Pamoja na maeneo ambayo yanafaa kujengwa mabwawa angalau kwa matumizi ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iliangularie hilo, bajeti iongezwe kwa kweli. mifugo inakuwa haina maji kiangazi kinapoanza. Waziri anayehusika na hii Wizara, natumaini atakuwa amesikia hili, basi atusaidie kwani sisi ni Wilaya mpya. Sasa hata ule ujenzi wa Wilaya mpya tutaufanyaje kama hakuna maji?

Mheshimiwa Naibu Spika, maji ni muhimu, tunaomba Serikali itupe kipaumbele, maji yapatikane katika Wilaya ya Mkalama, illi na sisi tuweze kuishi maisha kama wanavyoishi katika Wilaya nyingine, siyo kila siku usiku watu wanapishana

na ndoo wanaondoka kwenda kutafuta maji. Kwa hiyo, naomba sana tuchimbiwe visima vingi ili tuweze kujenga hiyo Wilaya mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mengi sana tunayakosa kwa ajili ya kukosa maji. Kwa hiyo, ninachoomba Wizara na Serikali isikie na hizi Wilaya zijitegemee kama zilivyotangazwa. Sasa hivi tumeshakuwa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, Halmashauri haina maji, makao makuu yake hayana hata visima vya kuweza kusambaza maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hao watumishi wataishije kwenye Halmashauri ya Mkalama. Watumishi wa Serikali wanaoletwa, watafikia shida ya maji, basi haitachukua muda wataanza kuomba uhamisho na kuondoka. Naomba Serikali iliangalie hilo na ilitupie macho mawili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, nazidi kuwatangazia wananchi wangu wa Iramba Mashariki kuwa Mungu anazidi kuniimarisha kiafya kwani afya yangu imekuwa nzuri, kwa hiyo tupo pamoja. Mbunge nipo, waliokuwa wanasema Mbunge hayupo, Mbunge nipo, naendelea kuijenga Wilaya yangu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mwalimu Salome Mwambu, kwa kweli na mimi nashuhudia kwa wana Iramba Mashariki kwamba, Mbunge yupo! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Gosbert B. Blandes atafuatiwa na Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Mheshimiwa Lugola na Mheshimiwa Clara Mwatuka wajiandae.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii. Nimejaribu kusoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwa umakini sana kuanzia ukurasa wa kwanza mpaka wa mwisho. Kwenye ukurasa mmojawapo, Mheshimiwa Waziri ametukumbusha kwamba mwaka 2009

tulitunga Sheria hapa Bungeni ya kuanzisha Mfuko wa Maji. Ni miaka mitano iliyopita kwa sababu ni Sheria ya mwaka 2009 nami pia nilishiriki kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa, hadi leo hii miaka mitano imepita, Mheshimiwa Waziri anakuja Bungeni kutwambia kwamba sheria hii haijaanza kufanya kazi. Hili ndio chimbuko la mgogoro wa maji katika nchi yetu kwa sababu Mfuko huu ungekuwepo tusingekuwa leo tunalumbana. Nimitake Mheshimiwa Waziri na timu yake, wafanye haraka Mfuko huu uanze kazi, ili wananchi wa Tanzania wapate maji ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kupata mradi wa maji katika eneo lake la Same na Mwanga. Wengi wamezungumzia suala hili, lakini nakujia katika mtazamo tofauti. Hapa Mheshimiwa Waziri ametuambia kwamba, ahadi hii ni ya Mheshimiwa Rais ya mwaka 2005, ni sawa na nakubali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Mheshimiwa Rais alitoa ahadi sehemu mbalimbali ikiwa pamoja na Jimbo la Karagwe mwaka 2005. Nimengalia kwa makini, kwenye eneo la Mheshimiwa Waziri la Same na Mwanga kuna bilioni 30 zimetengwa, ahadi ya Karagwe ya mwaka 2005 haihitaji hata bilioni moja, yenyewe inahitaji angalau shilingi milioni 400 au 500, lakini sijaona ahadi hii ya Rais ikikumbukwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Wanasheria tuna usemi mmoja, tunasema kwamba, haki siyo kwamba itendeke tu, lakini haki lazima ioneckane inatendeka. Pengine na mimi ningekuwa Waziri wa Maji, ahadi yangu ya Mheshimiwa Rais ingeonekana hapa na ningesema Mheshimiwa Rais aliahidi ndio maana iko hapa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefuatilia sana ahadi ya Mheshimiwa Rais kwenye ofisi ya Waziri wa Maji, nimekwenda, nimeandika barua mbalimbali kwa Waziri, kwa Naibu Waziri, kwa Katibu Mkuu, mpaka leo sijajibowi. Sasa sijui ahadi ya Mheshimiwa Rais ya Karagwe aliyoifanya, aliyoitoa

kuwapatia maji wananchi wa Karagwe sijui imesahaulika au imetupwa kapuni. Nataka Mheshimiwa Waziri wakati anajumuisha anifahamishe ni kwa nini Mji wa Omurushaka, Mji wa Kayanga, Vijiji vya Kishao, Lukole, Bugene, Nyakahanga na sehemu nyingine hazina maji. wakati Mheshimiwa Rais aliahidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo Karagwe tu peke yake, zipo ahadi mbalimbali, Tarime kwa mfano, kwa mtani wangu Mheshimiwa Nyangwine. Kuna ahadi ananikumbusha kuanzia enzi za Mzee Mwinyi, enzi za Mzee Mkapa, enzi za Mzee Kikwete, anakumbusha ahadi hizo na wananchi wa Tarime wanamshangaa anakaa hapa anaunga mkono hotuba hii, wakati hizo ahadi hazijatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Ngara kwa Mzee Ntukamazina na Kyerwa kwa Mzee Katagira, ahadi zetu sisi Mkoa wa Kagera, leo nilikuwa nasoma hapa, tumeambiwa kwenye ukurasa wa 54, kwenye bajeti hii utafanyika usanifu wa miradi ya maji safi na maji taka tu. Huu ni usanifu, hakuna hela ambazo zimetegwa kwa ajili ya kutapatia maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri awe muungwana katika bajeti hii, nchi hii ni ya kwetu wote, naomba sana, maji ya Karagwe pale ninapozungumza Karagwe Mjini na Omurushaka ni kilometra nne kutoka ambako chanzo cha maji kipo, hela inayotakiwa siyo zaidi ya shilingi milioni 500. Katika bilioni 30 ambazo zimetengwa kwenda Same na Mwanga, naomba amege shilingi milioni 500 tu ili wananchi wangu wa Karagwe wajue kwamba nchi yao inawajali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani wengi mnafahamu jiografia ya Mkoa wa Kagera. Mkoa wa Kagera Mwenyezi Mungu ametujalia tumekuwa na vyanzo vingi vya maji. Tuna Ziwa Victoria, tuna Mto Kagera, Tuna Mto Ngono, tuna Mto Lubuvu .

**MBUNGE FULANI:** Mto Ngono!

24 APRIL, 2013

**MHE. GOSBERT B. BLANDES** Eeh, ndio kuna Mto Ngono na kuna maziwa mbalimbali. Hata hivyo, kwa masikitiko makubwa Mkoa wa Kagera pamoja na Mara na Mwanza ndio Mikoa inayoongoza kwa ukame wa maji. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Blandes, tunatoa wito jina hilo libadilishwe, litafutwe jina mbadala. (*Kicheko*)

**MBUNGE FULANI:** Haiwezekani!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Blandes endelea kuchangia!

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, aweke mpango mkakati, badala ya kutoa maji Ziwa Victoria kupeleka Mikoa mingine, sisi ambao tumezungukwa na hilo Ziwa na tunalitunza, lakini tunabaki kuwa waangaliaji ni kwa nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye mgawanyo wa fedha za maji katika Halmashauri zetu za Wilaya. Nimeona Kondoa wamepata bilioni 1.7, Geita bilioni 1.8, Kigoma bilioni 1.3, Rombo 1.1, Karagwe ambayo ina Wilaya mbili Karagwe na Kyerwa imetengewa shilingi milioni 912. Kwa maana hiyo itapata shilingi milioni 456 tu. Mheshimiwa Waziri naomba uiangalie Karagwe kwa jicho la huruma tafadhali sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri na Kamati imeshauri hapa, bajeti ya maji iongezewe shilingi bilioni 181, nadhani hilo halina mjadala, Serikali ijipange vizuri ili tupate maji. Pia, napendekeza kama tulivoanzisha *TANROAD*, ambayo iko kila Mkoa, kwa nini tusianzishe kitu kinachoitwa *TANWATER*, tukawa nacho, tukajipanga vizuri kwa ajili ya kupeleka maji kwa watu wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, namwomba sana Mheshimiwa Waziri yeye na timu yake, waangalie kwa makini Wilaya ya Karagwe. Sisi tuko mjini lakini Mji wangu wa Karagwe unapata maji asilimia sifuri (0%), sasa sijui

wanatutenga kwa sababu sisi tuko pembezoni huko, hata Ngara sijaona kwa Mzee Ntukamazina na kwa Mzee Katagira kule Kyerwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tafadhali Serikali ijitahidi katika bajeti hii, sisi hatutaki kusubiri, wakati mnajumuisha mtuambie Mkoa wetu wa Kagera katika Jimbo langu la Karagwe kwa Blandes mmenitengea shilingi ngapi, ambazo na mimi nikiondoka hapa niende kifua mbele kama ambavyo Mheshimiwa Waziri atafanya atakapokwenda Jimboni kwani na yeye ni Mbunge kama mimi. Naomba hili kwa sababu nitakosa mambo ya kusema pale Jimboni kwangu, wataniuliza umetuwalkilisha nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani Mheshimiwa Waziri amenisikia na Naibu wake na timu yake. Naomba maji katika Wilaya yangu na Jimbo langu la Karagwe. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ole-Sendeka atafuatiwa na Mheshimiwa Lugola na Mheshimiwa Clara Mwatuka ajiandae.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii muhimu kwa mustakabali wa maisha ya Watanzania. Nianze kwanza kabisa kuwakumbusha kwamba, sisi wa Chama kinachotawala, katika llani yetu ya uchaguzi, tulieleza nia yetu ya kuwatoa Watanzania kutoka uchumi ulio nyuma na tegemezi na kuwaelekeza katika uchumi wa kisasa wa Taifa linalojitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, huwezi kufikia malengo hayo kama huna miundombinu ya kisasa ya umwagiliaji, miundombinu ambayo unakinga maji na kuyavuna, ili wakulima waweze kuwa na uhakika wa kilimo waondokane na kilimo cha kutegemea mvua ili waweze kuongeza tija katika kilimo chao. Pia, huwezi kuleta mapinduzi hayo ya

kuwatoa wafugaji kutoka uchumi ulio nyuma na tegemezi na kuwapeleka katika uchumi wa kisasa, wenyewe tija na ufugaji wa kisasa, kama mifugo yenyewe haina uhakika wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni rai yangu basi niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuomba Serikali yetu sikivu iongeze fedha katika miradi ya maji, ili wengine kama rafiki yangu Blandes waweze kurudi Majimboni wakifurahi badala ya kuondoka wamenuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema nianze hivyo, lakini pia naomba tukumbushane sisi sote ni Wabunge, hata Mawaziri ni Wabunge, kwa hiyo, tunapojenga hoja zinazoelekea kuwalamu hata pale ambapo hawana makosa, tunakuwa hatuwatendei haki wao na wapiga kura waliowaleta katika Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu, Mradi wa Mwanga, Same, Korogwe ulibuniwa na kutengewa fedha za usanifu pamoja na Mradi wangu wa Maji wa Orkesmet kutoka Mto Ruvu, na ilitengewa jumla ya shilingi bilioni moja ambayo tuligawana milioni 500 kila upande na baadaye Serikali ilitafuta fedha kutoka *BADEA* na *OPEC Fund*.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tumesikia kwamba, kuna fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi hiyo miwili. Nataka niwambie wakati haya yakifanyika kama alivyosema Profesa Mwandosya wala Profesa Jumanne Maghembe wakati huo hakuwa Waziri katika Wizara hiyo, alikuwa kwenye Wizara nyingine. Kwa hiyo, nataka niseme wazi kabisa kwamba, katika hili wala Mheshimiwa Maghembe hakujipendelea kama ambavyo baadhi ya watu walitaka tuamini hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, nataka niwaambie Mradi wa Maji wa Olokesmeti ambao leo umetamka kutengewa shilingi bilioni 15.5 siyo mradi wa leo. Mwaka 1974 wakati hayati Mzee Rashidi Mfaume Kawawa akizindua Wilaya ya Kiteto wakati tunatengana na Wilaya ya Monduli, aliyekuwa Mbunge wetu wa pamoja

Mheshimiwa hayati Edward Moringe Sokoine, alieleza nia ya Serikali ya kuvuta maji kutoka Mto Ruvu kuja Makao Makuu ya Wilaya iliyokuwa imeamuliwa kwamba ni Orkesmet.

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo ni wazo la mwaka 74 na leo baada ya miaka, kwa wanaojua mahesabu wanajua kabisa huu siyo mradi uliobuniwa juzi, ni mradi uliobuniwa tangu mwaka 74. Kwa hiyo, kutengewa bilioni 15.5 nataka nimwambie Waziri wa Maji, Waziri Mkuu na Rais Jakaya Mrisho Kikwete mmeandika historia na wananchi wa Simanjiro kamwe hawatawasahau, kwamba jambo hili sasa mkilitekeza litakuwa ni jambo jema.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nasema hilo siyo upendeleo kwetu, ukienda kwenye Randama ya Waziri, ukurasa wa 78 wa Randama hiyo, Wilaya ya Hai iliwhahi kutengewa *euro* milioni 55 ambayo ni sawasawa na zaidi ya shilingi bilioni 100 kwa sasa kwa *exchange* ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mradi huo pia, miaka hiyo hiyo, Wilaya ya Moshi Vijijini ilitengewa *euro* milioni 9.6. Hii yote ni katika kuhakikisha kwamba tunawasaidia Watanzania ili waondokane na tatizo la maji na wakati huo wala Majimbo haya hayakuwa yanawakilishwa na Mawaziri wa Maji. Kwa hiyo, nataka niwaambie kwamba hii ni nia njema tu ya Serikali ya CCM ya kuendelea kuwashudumia Watanzania bila upendeleo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Simanjiro iko miongoni mwa Wilaya zilizoko kwenye ukame, mwaka huu peke yake, Wilaya ya Simanjiro Mabwawa karibu manne yamebomolewa na maji ya mvua iliyonyesha miezi miwili iliyopita. Bwawa la Nalakawe limebomoka, la Lengai, la Lengumumwe, na Mabwawa mengine ya Leberela katika Kata ya Ruvu Remiti. Naiomba Serikali litupie macho jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtakumbuka kwamba, Bunge hili lilipitisha shilingi bilioni 1.8 kufuatia ahadi ya Rais ya

kupunguza makali ya maji katika Wilaya ya Simanjiro, katika Bajeti ya 2010/2011, lakini hadi sasa hatujapata hata shilingi moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana Mheshimiwa Profesa Maghembe atakapokuwa anafanya majumuisho yake, awaeleze wananchi wa Simanjiro hiyo bilioni 1.8 ya Mradi wa dharura ambaو utawazuia wananchi wa Simanjiro kuhamia Kilindi wakati wa kiangazi itapatikana lini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niwakumbushe pia kama alivyosema rafiki yangu Mheshimiwa Freeman Mbwe ambaye tumepakana, maeneo ya Mtakuja na maeneo ya Mererani, ni ukanda mmoja, pamoja na Kata ya Naisinyai, ya Indiamtu na ya Shambalai. Maeneo yote hayo maji yake yana *fluoride* kwa kiasi kikubwa, kwa hiyo, wananchi na watoto wanapata matatizo ya *fluoride* na watoto wanapinda miguu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwaambieni, ukanda wote huu unaopakana na *Kilimanjaro International Airport*, unafanana. Kwa hiyo, rai yangu bado ni kwamba, Serikali ione uwezekano wa kuvuta maji kutoka Mlima Meru au Mlima Kilimanjaro na kuweza kuupatia maji Mji wa Mererani na Kata yote ya Indiamtu, ya Shambalai na ya Naisinyei.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, bado ni rai yangu kwamba, Wizara ione uwezekano wa kuwasaidia watoto wa Mererani, watoto wa Kata ya Naisinyei, ya Shambalai ambaو wanapinda miguu. Nilitaka niwaleti picha ya watoto waliopinda miguu, lakini nilishawaleteeni, lakini nikasema madhali Serikali hii nilishaionesha, naamini itakuwa sikivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tuna maji ambayo yanamwagika kutoka Mlima Meru ambayo yanapitia kwenye Jimbo la rafiki yangu, mdogo wangu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo, Mheshimiwa Nasari, ambayo leo

yameleta maafa makubwa katika Kata ya Shambalai, kwenye Vijiji vya Oldiri, Kilombero na Shambalai yenyewe na kuathiri baadhi ya maeneo ya Mererani na Naisinyai.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji yale yangetunwa, wananchi wa ukanda huo wa Tarafa ya Mbuguni kwa upande wa Arumeru na Tarafa ya Shambalai, Tarafa ya Mwaipo, wote tungeondokana na kupiga simu kila siku, kwa Mheshimiwa Lukuvi kuomba chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni rai yangu pia kwa Serikali kwamba, sasa hivi tunatambua Serikali yetu imeweka kodi kwenye mabomba ya maji. Nashauri kodi hiyo ifutwe ili miradi yote ya maji iweze kuwa ya bei ndogo au ya gharama ndogo na wananchi waweze kupata huduma hiyo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaja mabwawa ambayo yalivunjika, lakini nilitaja maeneo ambayo vijiji vyake kufikia mwezi wa saba wananchi wanahama na Walimu wanakwenda zaidi ya kilometra 30 kufuata maji na wakati mwingine wanasubiri maji ya punda kama matrekti hayajapatikana. Maeneo hayo ni Lerumo, Lendanai, Okutu, Rorbene, Orjohonyori, Lengumumwa, Namarulu, Lengai, Rekuid, Elinorili pamoja na maeneo mengine ya Kata ya Losnyei. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niambie Serikali, hii ni aibu sana, ninyi mnazungumza habari ya kufuata maji ya kunywa umbali wa mita 400, kutoka Lerumo kwenda Ruvulemiti ni kilometra 32, kutoka Langai kwenda maeneo ambayo kuna maji ni kilometra 25 kwenda na kurudi ni kilometra 50. Hiyo ndiyo hali ya Simanjiro tunayowaambieni, hatuzungumzi habari ya maji ya kufuata kilometra 10, acheni mita 400 ambayo ni hadithi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu Serikali hii iamue, kwa wananchi wa Simanjiro na Watanzania, itenye fedha kwa ajili ya kusaidia miradi ya maji. Maana mkizungumza hata mradi kabambe wa maji Orkesmet, unazungumza Simanjiro

ambayo ina kilometa za mraba elfu 20, sawasawa na Mkoa mzima wa Kilimanjaro, karibu sawasawa na Mkoa wa Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, unaposema kwamba, unasaidia Wilaya ya Rombo, eti utegemee na wananchi wa Same wakanywe maji Rombo, hiyo haiwezekani! Nataka niwaambieni tu kwamba, umbali ndio kama huo niwaowaelezeni, ni sawasawa na kuwa na maji Kilindi, utegemee na wananchi wa Muheza wakanywe maji ya Kilindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nitaiunga mkono Bajeti hii bila kigugumizi, nikiamini kwamba, ahadi ya Rais Kikwete ya bilioni 1.8 itafika Simanjiro, nikiamini kwamba mradi kabambe hautakuwa wa maneno utatekelezwa, lakini nikiamini pia kwamba Wizara itaongeza fedha katika Bajeti hii ili Wilaya zingine katika nchi yetu iweze kupunguza matatizo ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na Waheshimiwa Wabunge waliopendekeza kama ikibidi kufunga mikanda, tufunge mikanda na ikibidi hata kuanzia kwenye Bunge hili, tutoe baadhi ya fedha ambazo zinatumika hata katika vinywaji vyetu, soda au kitu chochote, tuelekeze huko na baadhi ya posho zielekee kwenye miradi ya maji. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukianza kuonesha mfano sisi Wabunge, Watanzania watatuelewa. Naiomba Serikali itusaidie katika mradi huo wa Mererani, kulikuwa na fedha za *Société Générale* ambapo Benki ya Ufaransa walionesha nia ya kusaidia Mradi wa Maji wa Orkesmet, tusaidieni. Fedha hizo za *Société Générale* zinaweza zikatatua tatizo la maji la Wilaya ya Hai kwa upande wa Bomang'ombe, Mtakuja. Pia itasaidia Arumeru kwa Tarafa ya Mbuguni, itasaidia Simanjiro kwa Kata za Naisinyai, Mererani na Shambalai.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ikiamua kuchukua fedha hizo zichukueni, riba yake ni ndogo, inaweza kumaliza tatizo hilo. Dola milioni 40 inaweza kutatua tatizo hilo kwa

kiasi kikubwa na wananchi wa ukanda huo, na ukanda wa tambarare wa Meru na ukanda wa tambarare wa Hai na ukanda huo wa Mererani na Naisinyei na Lengai *City*, watakuwa wametatuliwa tatizo lao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Ole-Sendeka kwa mchango wako.

Sasa namwita Mheshimiwa Lugola, atafuatiwa na Mheshimiwa Clara Mwatuka.

**MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba, ewe Mwenyezi Mungu, epusha Bunge hili na ushabiki wa Vyama katika suala la maji. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kweli kila mmoja anasema maji ni uhai, hainilingii akilini kuunga mkono hoja hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, Bajeti hii imesheheni miradi mingi, lakini imesheheni miradi ya upendeleo katika nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, imesheheni miradi isiyotekelzeza katika nchi yetu. Kwa nini nasema hivyo, Bajeti hii ni mchezo wa karata tatu, hapA Waheshimiwa Wabunge tunaliwa kekundu.

**WABUNGE FULANI:** Ni kweli. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu mwaka 2007, tulipata mradi wa Vijiji 10; Kijiji cha Karukekere, hadi ninavyozungumza, mradi huu hausongi mbele, wananchi hawapati maji. Mwaka 2007 tuliunga mkono, mpaka 2012 tuliendelea kuunga mkono, nina sababu gani ya kuunga mkono kwenye mwaka wa nane juu ya miradi isiyotekelzeza? (*Makof*)

24 APRIL, 2013

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Buramba, mpaka leo hakuna mradi unaotekelezeka. Tuliendelea kuunga mkono miaka sita yote Bajeti hii ipite, hainishawishi leo mwaka wa nane, kuendelea kuunga mkono bajeti hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2007 tulikuwa na mradi wa maji Kibara, hadi leo, hakuna fedha inayopelekwa. Tumeunga mkono miaka sita, leo mwaka wa saba, itakuwaje niunge mkono bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa Bunda, Mheshimiwa Waziri amelidanganya Taifa, amewadanganya wana Bunda na wana Mwibara ambako maji yanaanza. Hadi ninavyozungumza, hakuna cha mabomba yanayolazwa, kinachoendelea pale, ni kuchimba mitaro, mitaro ambayo haijafika hata kilomita 10 ndani ya kilomita 23.5. Nina sababu gani ya kuunga mkono bajeti hii, nitawaambia nini wana Mwibara, nitaingia nyumba ya nani katika Jimbo la Mwibara!

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mtu mmoja anaitwa Musa, kwenye Biblia, aliwaongoza wana wa Israel kutoka nchi ya Misiri kule utumwani, kwenda nchi ya ahadi ya Kanani. Walisafiri muda mrefu sana, walipata matatizo mengi na jangwani walianza kuumwa na nyoka, wakawa wanakufa, lakini Mungu akasema na Musa, akamwambia, tengeneza nyoka wa shaba, halafu umtundike hapo. Kila atakayekuwa anang'atwa na nyoka, amtazame nyoka wa shaba atakuwa mzima, na yule ambaye hatatazama pale, hakika atakuwa. Sasa leo nimekuja na nyoka wa shaba na nitaomba upokee picha hizi za akinamama, ambazo zinaonesha kero ya maji katika nchi yetu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kisima cha maji mama ana pampu hakitoi maji, kuna akinamama wawili wana ndoo wanagombea maji, kuna akinamama wengine wameshika mashavu, wanaskitika, lini watapata maji katika nchi yao! (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, naomba niwape ushauri wa

bure na Mheshimiwa Naibu Spika naomba uniruhusu nitundike picha hii ya akinamama ili kila Mbunge atakayekuwa anachangia hapa, awe anatazama picha hii, kama nyoka wa shaba. Vinginevyo nawaambieni, msipotazama picha hii kama nyoka wa shamba, hakika Majimboni mwenu akinamama hawatawarudisha ndani ya jengo hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, najua utasema Kanuni haziruhusu, naomba utumie Kanuni ya 5, pale ambapo hakuna Mwongozo unaosema kwenye Kanuni, uniruhusu *Seargent at Arms* na wahudumu, watundike picha hii ya kero ya maji katika nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaiwasilisha kwako, ole wenu Waheshimiwa Wabunge msitazame nyoka wa shaba, akinamama, hawatawarudisha. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, akinamama wanatembea umbali mrefu, kuanzia saa kumi wanarudi saa tano. Rafiki yangu Hokororo amesema akinamama wanadhalilishwa. Katika mazingira ambayo akinamama wanadhalilishwa, kwa nini Kange Lugola nипитиshe bajeti hii kwa mama aliyenizaa kutoka tumboni mwake akiwa anadhalilishwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kule kwetu, kutokana na akinamama kutumia muda mrefu kutafuta maji, wako akinababa ambao wana upendo uliopindukia, nadhani ninyi mnaita vivu, wanakwenda kuthibitisha huko kwenye maji kama kweli wake zao wako kule.

Wengine wakifika kule wanapanda juu ya miti mirefu ili waweze kuona kama wake zao wako kwenye visima vya maji. Hakika nawaambieni, yamewatokea wale ambao macho yao hayakuona vizuri, wakadhani wake zao hawapo, walidondoka chini ya miti na wengine ni vilema. (*Kicheko*)

Hakika nawaambieni na natoa ushauri wa bure...

**NAIBU SPIKA:** Hawa watu wa Mwibara wana vivu kweli hawa. (*Vicheko*)

**MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, maneno ya suala la maji katika nchi yetu yamekuwa ni ya muda mrefu, ya miaka mingi, tumeunga mikono, tumeunga, tumeunga, Waheshimiwa Wabunge, tutaunga unga mikono mpaka lini? Wakati maji hayapatikani!

Leo ni muda mzuri Waheshimiwa Wabunge, nawaona mna nyuso za kuwahurumia akinamama na kila mmoja anayetazama kulia, kushoto, nyuma na huku mbele, naona wote mnaamini mmezaliwa na mwanamke, tuwahurumie akinamama, leo tutumie Bunge hili kutatua kero ya maji katika nchi hii. Hakika nawaambieni, tukiwaunga mkono, wataendelea kuja na Bajeti ambazo hazitekelezeki. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ole-Sendeka ni rafiki yangu wa siku nyingi, kuniambia kwamba, Mheshimiwa Maghembe ni mgeni kwenye Wizara hili, hivyo hakujipangia fedha kwa sababu hakuwepo, nakubaliana na wewe, lakini kuna upendeleo mionganoni mwa Mawaziri, wanapendelea Mawaziri wenzao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapa wosia na ushauri wa bure kwa Waheshimiwa Mawaziri kwamba, wapendeleeni na Wabunge, na wao wanahitaji maji kwenye Majimbo yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Ziwa Victoria, Kijiji cha Mwibara ni cha mwisho, kiko kilomita nane kutoka upande wowote wa Ziwa. Hivyo, hainiingii akilini, kila siku mnatafuta visima vya kudanganya watu na hakuna maji, mnakula fedha wakati maji yako kilomita sita. Kuna Mlima Nyamitweibiri pale, mkiweka matenki na kuna miundombinu tayari ya pampu ya maji, vijiji vyote vya Mwibara, hakika nawaambieni, vitapata maji kutoka ndani ya Ziwa Victoria. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mambo ya kutuletea visima, sijui Wakandarasi, Watafiti, visiwa havitoi maji, hii ni miradi ya ulaji. Mwibara hatutaki miradi ya ulaji, maji tunayaona, weka pampu kule, sisi tupate maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, wakati naelekea kukabidhi nyoka wa shaba, ambao ni akinamama wanaopata adha ya maji, naomba niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge, mwaka jana, bajeti hii ilikuwa na matatizo mengi, tulitoa ushauri mwingi. Nashangaa leo Kamati ya Maji, inakuja hapa inashawishi Bunge hili kwamba, Wizara ya Maji imefanya mambo vyta kutosha, wakati mambo tulioelekeza hayakufanyika na bado kuna tatizo la maji na hasa ukifika kwenye Miji mikubwa kama Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda pale nina chumba kimoja cha kupanga pale, niliwahi kusema, hata nilipokwenda Ludewa kwa rafiki yangu Deo Filikunjombe, nilipotaka kuoga asubuhi, hakika nilikosa maji ya kuoga mwili mzima! Nilinunua chupa ndogo ya maji ili niweze kuoga angalau sehemu nyeti. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakwenda wapi? Wizara hii wanazo siku zile ambazo wanakwenda kutafuta pesa, wanazo siku za kujadiliana na Kamati ya Bajeti, katafuteni fedha, halafu mje mtuambie. Mheshimiwa Chenge kama Mwenyekiti, nitaiomba picha hii kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Spika akuazime, wakati mnajadili suala la maji, muwe mnaangalia nyoka wa shaba, ambaye ni akinamama, muwaonee huruma, ndugu zangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa, uniruhusu nikabidhi nyoka wa shaba ili Waheshimiwa Wabunge watakaoendelea kuchangia wawe wanatazama nyoka wa shaba. Wasipotazama adha ya akinamama kama nyoka wa shaba, akinamama hawatawarudisha humu ndani. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikae ili muda wangu uliobaki nianze kushuhudia Waheshimiwa Wabunge wanachangia kwa kutazama nyoka wa shaba. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kangi Lugola.

Baada ya matazamio hayo, Mheshimiwa Clara Mwatuka wewe ndiyo mtihani wa kwanza. (*Makof/Kicheko*)

**MHE. CLARA D. MWATUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipatia afya njema kufika siku hii ya leo na kuweza kusimama hapa kuchangia Bajeti hii ya Maji. Pia nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii. Mheshimiwa Lugola, nitaangalia, baadaye lakini. (*Vicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba nchi nzima ya Tanzania kero ya maji ni kubwa mno. Karibu kila mahali, kama kuna sehemu ambapo wanakunywa maji ya bure ni chache sana, lakini maeneo mengi maji ni ya kununua. Hata humo mijini wanamosema yanapatikana kwa urahisi, au Bajeti inapelekwa ya kutosha, napo wanunuua vile vile. Nakaa mjini pale niha kibanda changu, maji nanunuua, sasa, ni suala ambalo kila mahali linalalamikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule kwetu Mikoa ya Kusini ni mionganoni mwa maeneo ambayo yana shida sana ya maji. Kuanzia Mkoa mzima wa Mtwara, Mkoa wa Lindi na hata wa Ruvuma, maji ni shida. Kuna sehemu zingine ambazo kuna vyanzo vya maji lakini, bado havijafanyiwa kazi vilivyo ya kuweza kusambaza hata katika maeneo ambayo hakuna vyanzo karibu ili yaweze kufika. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo ningeiomba Serikali iangalie sasa maeneo yale ambayo yana vyanzo vizuri vya kudumu, basi wategeshe pale maji, yasambazwe katika maeneo yale mengine ambayo hayana maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianzia na Wilaya ya Newala, hakika Wilaya hii ni ya kuisikitikia, kama hivyo alivyosema Mheshimiwa Lugola kwamba, Mawaziri wanapendeleana, basi niombe Waziri wa Maji ampendelee ndugu yetu, Mheshimiwa Waziri kaka Mkuchika, Wilaya ya Newala anahitaji upendeleo wa hali ya juu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda Newala bahati

nzuri kwamba hivi sasa yanatumika maji ya viwandani, mkifika wageni mnapewa maji yale, lakini laiti mngekuwa mnapewa maji wanayokunyuwa wananchi wa Wilaya ya Newala, msingekunyuwa na msingeamini kama kweli maji haya wanakunyuwa watu. Kwa hiyo, ule usemi wa kwamba, Mwfrika hafi uchafu ni kweli kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Newala maji yao wanayapata kwa kutengeneza kishimo uwanjani, wakati huu wa mvua ndiyo wanachota maji pale. Sasa angalia maji na vumbi zile yanakuwa ni maji ya namna gani? Yanakuwa mazito kama *uniform* za wahudumu wetu wa ndani. Sasa hali kama ile ni ngumu! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba basi Serikali pamoja na kwamba, uwezekano wa kungoja kuletewa maji mazuri ambayo tunahitaji wayapate, basi wapelekewe dawa za kusafisha maji hayo ili yaonekane mazuri kuliko yanavyotumika, hali ni mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, wale wanaojiwezea wakachimba visima vyao na kuvijenga kwa *cement*, wanategesha hivyo hivyo maji hayo hayo ya mvua ambayo siyo mazuri, ni machafu, wengine ambaao hawana uwezo, nyumba nyingi kule kwa sababu zao la biashara kule ni mashaka, kilimo chao cha mhogo ambacho hakina soko wanashindwa kupata bati, angalau waweze kupata maji ya kutoka kwenye bati siku za mvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wanachofanya ni kukinga maji kwenye nyumba zile za nyasi, maji yanayotoka mle ni kama chai ya rangi. Sasa fikiria maji yale upewe wewe kunywa, kwa kweli huwezi kutamani. Naomba sana Waziri achukue hatua za upendeleo ili wawapatie maji wananchi wa Newala. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda Wilaya nyingine kama Masasi, kule mradi huu wa visima kumi vilipatikana, lakini visima vile havitoi maji. Nashangaa, visima viro lakini maji hakuna kwa nini, hatujui! Lakini vijana wanachimba

visima na maji yanapatikana, wanachota kwa karibu tu kwa makopo, wanafunga kamba kopo wanatumbukiza na kuchota maji. Sasa nashangaa visima vinachimbwa na mashine lakino vinakosekanaje maji? Naomba Mheshimiwa Waziri afuatilie hilo, waone kwa nini visima vile havitoi maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na michango katika vijiji kwamba, walitakiwa wachangie shilingi milioni sita au sijui tatu, kitu kama hicho, nimesahau kidogo na Serikali isaidie. Watu walikuwa wanachangia na mwisho wakulima walikuwa wanakatwa kwenye mazao kwa ajili ya maji hayo, lakini mpaka hivi sasa baadhi ya maeneo utaratibu huo haujafikia mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, sijui zile pesa kama zilikuwa zinawekwa mpaka lini sijui na ufuatilaji wake nani afuatilie, wananchi mnafahamu kwamba wengi wanashindwa kuulizia au kutafuta haki, wanaogopa maana ndiyo sera ya Watanzania, woga vijiji. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri, afuatilie hili katika vile vijiji ambavyo walichangishwa pesa zao kwa ajili ya maji na mpaka leo hawajapata. Naomba sana kwani akinamama wanalala visimani yaani ni Mkoa mzima wa Mtwara uko hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda Nanyumbu vile vile hali ni hiyo hiyo, lakini kuna mkombozi ambao ni Mto Ruvuma upo karibu. Naomba ule mto utumike, maji yasambazwe katika Wilaya zile za Mikoa yote miwili kwa maana na Ruvuma, mto huu unapita kwao, hivyo wasaidiwe ili maji yapatikane. Haiwezekani akinamama wawe daima wanakesha visimani, wakiondoka asubuhi wanawaacha watoto wao, wengine hata jinsi ya kwenda shule hawana kwa sababu hakuna hata maji ya kunawa uso. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tufanye kila linalowezekana, kwanza niiombe tu Serikali ituongezee bajeti, hiyo iliyopewa Wizara ni ndogo, haitoshi kwa tatizo liliopo nchini. Kwa hiyo, iongezewe na kila sehemu iongezwe ili

mambo haya yawe sawa. Ukweli maji ni mama, sasa inapofikia kila sehemu wanalia kwa ajili ya maji, kwa kweli hali ni mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo naomba sana hasa Newala ndugu zangu tuwahurumie, wananchi wale wanaishi siyo Tanzania hii ya leo bali ni ile ya mwaka 47. Sasa imekuwa Kusini ni kusini kweli kwa kila kitu? Naomba mtuonee huruma angalau kitu kimoja kipungue, tuseme kwamba, Kusini kwa hili aah, ni nafuu. Isiwe kila kitu ni tabu; mazao tabu, soko hakuna, mbegu za kisasa kule tunasikia tu kwa wenzetu, sasa na maji haya iwe hivyo hivyo jamani? Naomba sana tutazamwe kwa macho manne, mawili tuliyopewa na Mungu na mengine sisi tuongezee ili yawe manne. Hiki ni kilio cha Watanzania katika kila sehemu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kule hali ni ngumu, Masasi na sehemu karibu zote za Kusini tunapata maji ya kununua, vijana ndiyo mradi wao na wengine wanajenga majumba, plastiki moja sh. 1,000/=, sasa fikiria kwa matumizi ya nyumbani, familia wanatumia ndoo ngapi kwa siku? Sasa kila siku awe na pesa za kununua wakati soko la mazao ndiyo kama mnavyosikia korosho ndiyo hizo. pesa hatupati, sasa tunafanyaje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mtuonee huruma Kusini! Tupieni macho Kusini, pamoja na kwamba ni kwa muda, sasa geuza angalau kusogee kuwe kunakwenda juu kuliko kubaki Kusini, Kusini tu daima. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli nafikiri mwaka wa kuwa kila sehemu maji yanapatikana kwa urahisi, furaha itakayokuwepo kule, uchaguzi utakapofika CCM mtaokota tu, mtaokota tu kwa sababu ni kero kubwa. Kwa hiyo, watasema tumepatiwa maji basi hata Mpinzani akisimama wataona aah hakuna kitu, tunakimbilia wapi, CCM! Lakini mkiwanyima maji mnawaongeza adhabu, akinamama watasema hapana, mbona mambo yanakwenda hivi hatuipi kura.

24 APRILI, 2013

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. CLARA D. MWATUKA:** Ah! ni kengele ya ngapi hiyo?

**WABUNGE FULANI:** Ya pilii!

**MHE. CLARA D. MWATUKA:** Lah!

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Clara Mwatuka, maneno ya mtu mzima.

Mheshimiwa Laizer atafuatiwa na Mheshimiwa Mariba Chacha Nyangwine.

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie bajeti ya maji. Nizungumzie hali ya maji Wilaya ya Longido. Pamoja na sera ya Serikali kwamba, inatakiwa kila Mtanzania achote maji umbali wa mita 400, nadhani kwangu hii itakuwa ni hadithi ambayo haitatekelezwa hata siku moja. Nasema hivi kwa sababu Wilaya ya Longido ina matatizo ya maji karne na karne na hakuna sera au utaratibu uliopangwa kuondoa matatizo ya maji katika Mji wa Longido pamoja na Wilaya nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tu kusema kwamba, Mji wa Longido kila siku hapa Bungeni nasema, una matatizo kuliko Wilaya nyingine, kwa sababu Mji wa Longido ni Makao Makuu ya Wilaya na ni Wilaya ambayo wananchi wanajitahidi kujenga sana, lakini tatizo la maji limekwamisha maendeleo yote ya Longido. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Longido wanununa maji shilingi 1,500/= kwa debe. Kwa hiyo, hata maisha ya pale ni magumu kuliko maisha ya eneo lingine, maisha bora kwa kila Mtanzania ni vigumu kufikiwa na wananchi wa Longido

kwa sababu ya matatizo ya maji. Huwezi kuamini kwamba familia wanapokezana kuoga, yaani wanaoga kwa zamu, baba akloga leo, mama hawezu kuoga siku hiyo na watoto hawaogi. Kwa hiyo, sidhani kama kuna Wilaya nyingine Tanzania ambayo baba na mama wanapanga zamu ya kuoga. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali inisikilize kwa sababu nimekaa muda mrefu hapa Bungeni napiga kelele kwamba Longido wana matatizo ya maji. Naomba Mheshimiwa Waziri kama kuna safari au ziara za watendaji wa Wizara hii kwenda nje, basi hizo fedha zielekezwe Longido ili waondokane na tatizo hili la maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Longido unategemea maji ya Mlima Meru, inahitaji zaidi ya shilingi billioni sita kuleta maji kutoka Mlima Meru na kuyafikisha katika Mji wa Longido na kama ni ahadi za Rais, hata Rais amekwenda Longido na ametoa ahadi na amesema kwamba, atamwambia Mheshimiwa Waziri wa Maji, hiyo ni ahadi Mheshimiwa Rais amefikisha kwake, kwamba atekeleze, lakini bahati mbaya sikuona katika bajeti hii kama kuna mradi wowote wa Longido.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine katika Mji wa Longido, kasehemu kadogo wanashirikiana maji wananchi na mifugo. Naomba mifugo inayozunguka mji wa Longido wajengewe mabwawa ili ipunguze kasi ya wananchi Longido kung'ang'ania sehemu moja ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kijiji cha Orbomba, Ortevesi na Ranchi, kila kijiji kikipata bwawa itapunguza matatizo ya maji katika Mji wa Longido. Nashangaa sana nikiona mmeandika kwamba, Halmashauri za Vijiji au Vijiji wanapata maji kwa zaidi ya 50% ambayo Wilaya ya Longido tunapata maji kwa 15% tu. Kwa hiyo, maeneo mengi kama Glailumbwa kule hawana maji, akinamama wanakesha porini na kurudi baadaye bila hata maji, tatizo ni kubwa katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kama walivyosema wenzangu na naomba Serikali isikilize na itekeleze, tuwe na Mfuko wa Maji kama ulivyo Mfuko wa Barabara na Mfuko wa Umeme Vijiji (REA) na Mfuko huu unahitajika haraka sana kwa sababu hali ni mbaya. Jamani tukifika mwaka 2015 kama hakuna maji nchi hii sijui kitatokea nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Vijiji Kumi umefeli, tuufute kabisa Mradi wa *World Bank*, wala tusiwape tena wananchi matumaini, Serikali ichukue jukumu hilo, itafute fedha kwa ajili ya Vijiji Kumi hata visima vilivyo chimbwa ambavyo vina maji Serikali sasa ianze kutekeleza na kuwapatia wananchi maji, kwa sababu kuna baadhi ya visima ambavyo vina maji. Kwangu wamechimba visima 12 lakini visima nane havina maji na sita vina maji. Naomba hivyo visima sita ambavyo vina maji viendelezwe ili wananchi wapate maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho ni mgawo wa fedha. Kama wenzangu wanavyosema kwamba, kwa kweli kuhusu mgawo wa fedha, kila mtu anasikitika. Tunaomba mwongeze hizo fedha kwa sababu hali ni mbaya, sizungumzii fedha zilizokwenda Jimbo au Wilaya yoyote bali naomba fedha za maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani Wizara hii au Serikali imetusikiliza na Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti naomba awasikilize Wabunge amba wamesema kwamba, tunataka fedha ziongezwe katika Wizara ya Maji. Kwa hiyo, Kamati wakutane, wafikirie jambo hilo kwani ni kilio cha Wabunge wote ili fedha ziongezwe katika mradi huu, msije mkaesema kwamba tumepitisha baadaye bajeti, mkaenda kunya maza kwa sababu bajeti imepita, tunaomba fedha ziongezwe. Kesho Kamati ikae na kutafuta namna, punguzeni posho na safari za nje pia punguzeni ili fedha zote ziingie kwenye maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Lekule Laizer. Tumekusikia kwamba kuoga kwa zamu.

Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine atafuatiwa na Mheshimiwa Ahmed Shabiby.

**MHE. NYAMBARI C.M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza nianze kwa kusema kwamba, sitaunga mkono hii bajeti kamwe kwa sababu, baadhi ya Wabunge wenzangu wamesema kwamba, wananchi wao wanaoga kwa zamu, lakini kwangu hawaogi kabisa hata kidogo. Kwa hiyo, naunga mkono nyoka wa shaba. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni aibu katika nchi kama ya Tanzania ambayo tuna mito na maziwa mengi na kadhalika, lakini tunakaa tunalalamika maji, na ni aibu kwa Wabunge wenzangu tunalalamika maji, maji, maji lakini tunasema kwamba tunaunga mkono hoja. Kwa kweli nawashauri Wabunge wenzangu tusiunge mkono hoja hii. Naomba Waziri Mkuu atusikilize, leo usiku atafute fedha kama ni bilioni 200 azilete, kesho tutaunga mkono hoja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ni aibu kabisa kwamba tulalamika, tunalalamika na bado tunasema kwamba tunaunga mkono hoja. Tusiunge mkono hoja kwa sababu tunajua kabisa kwamba ndani ya Majimbo yetu kuna ahadi nyangi zilitolewa. Kwa mfano kwenye Jimbo la Tarime, Rais Mwinyi alitoa ahadi kwamba Mji wa Tarime utakuwa na neema ya maji, akaingia Mkapa, mwisho Rais Kikwete amesema mara mbili, lakini ni aibu mpaka sasa hivi hakuna utekelezaji wowote ule ambao umetekelizuka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda nchi jirani ya Kenya, maji yanamwagika yanakuja mpaka Tanzania, yaani kwa kweli ni aibu Mheshimiwa Waziri nimwambie kabisa hilo. Mwaka jana katika bajeti naomba ninukuu, mlinijibu kwamba: "Serikali imekamilisha usanifu na uandaaji wa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya mradi wa maji safi kwa Mji wa Tarime. Chanzo cha maji kwa Mji huo ni Mto Mori, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo".

Mheshimiwa Naibu Spika, unajua haiingii akilini kwamba, makabrasha yameshatengenezwa ndio mnatafuta fedha, kwa nini hizo fedha mlizochukua mkapeleka sehemu nyingine, msikumbuke kwamba kuna Tarime? Mheshimiwa Naibu Waziri alitembelea Tarime, alikwenda akaangalia na wananchi wakamweleza, sasa sijui amemshauri nini Waziri kuhusu maji ya Tarime. Mheshimiwa Waziri Mkuu alikwenda Tarime, wananchi wakamlilia na kumwambia, lakini sijui amemshauri nini Rais kuhusu maji Tarime.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli nasema ni aibu na sitaunga mkono hoja hii, hata kama kesho nitakuwa nimeondoka, nasema sitaunga mkono hoja hii kwa sababu wananchi wa Tarime...

**MBUNGE FULANI:** Hawaogi!

**MHE. NYAMBARI C.M. NYANGWINE:** Hawaogi, wanaoga siku ya nini, Blandes anasema yeye kwao wanaoga siku ya Pasaka, *Christmas* na *Eid*, kule kwangu wanaoga siku wanayonyeshewa na mvua, ni aibu. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli nasema ukweli, Mheshimiwa Waziri naomba asikilize, nimekwenda kwake nikamweleza, sitaki kwenda kumpigia magoti kwa sababu ni haki yake atekeleze. Narudia tena kwamba hakuna Waziri nitakayekwenda kumpigia magoti kwamba afanye maendeleo Tarime. Kama kuna upendeleo mnajipendelea wenyewe, kwa kweli nasema kwamba mtaalaniwa hapa duniani na mMbinguni mtalaaniwa. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mto Mara unaweza ukatatua tatizo la maji katika Mkoa wa Mara. Mto Mara unazunguka Wilaya ya Serengeti, Rorya, Tarime na Musoma na wakati huo huo tuna Ziwa Victoria, Mto Mara unapeleka maji katika Ziwa Victoria, hivi siku Wakurya wakaamua wakaziba ule Mto Mara usipeleke maji Ziwa Victoria hayo maji mtayatoa wapi ya Ziwa Victoria au Mto Simiyu na Kagera.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli utaona kabisa kuwa, hii Serikali sasa hivi haiitendei haki Kanda ya Ziwa. Kanda ya Ziwa hatutendewi haki, lazima tuseme ukweli, mmeelewa? Tunakaa tunalamika maji na mwaka jana tulisema na kulalamika kwamba, Mto Mara uko karibu *distance zero* kutoka Wilaya ya Tarime, Ziwa Victoria lipo *zero distance* kutoka Wilaya ya Musoma, Rarya na Musoma Vijiji lakini ukienda kila kitu ni kilio, kilio ni kilio. Kwa nini msiwe kama Baba wa Taifa, mbona Baba wa Taifa yeye mpaka sasa Butiama hakukuwa na maji ndiyo mmemkumbuka sasa hivi? Ninyi mnapeleka kwenu tu huko huko. Ni aibu kwa kweli na nasema hebu tutafakari upya tunapolipeleka hili Taifa letu la Tanzania.

**MBUNGE FULANI:** Safi!

**MHE. NYAMBARI C.M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba majibu ya uhakika kuhusu mgawanyo wa rasilimali katika nchi yetu, maana kwa kweli inaonekana dhahiri ukiangalia mgawanyo unavyokwenda, unapokuwa Waziri au Mbunge ukienda kujikomba kwa Waziri ndiyo Waziri anaangalia. Sasa nasema kwamba, wengine hatukuzaliwa kujikomba. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, muangalie na mtekeleze. Wananchi wa Tarime wameniambia kwamba usijikombe. Sasa sitajikomba, ila mtekeleze na kama msipotekeleza siwahitaji Tarime. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata Waziri Mkuu aliwaahidi wananchi wa Tarime, asipotekeleza nay eye simhitaji Tarime. Maana nitawaambia wananchi wa Tarime kwamba nilisema. Profesa Mwandsoya alipokuwa Waziri wa Maji aliwaahidi wananchi kabisa kwamba, upembuzi yakinifu umekamilika, maji yatakwenda, lakini mpaka sasa hivi, naona leo mmetoa bajeti mnasema kwamba, Mji wa Tarime hauna bajeti ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hakuna bajeti ya maji, hawa wananchi wa Tarime watakunywa nini, wataoga nini, watafanya nini jamani? Hebu muihurumie Tarime, au twende

Kenya, si ndiyo? Niwaambie wananchi wa Tarime waende Kenya, kwa sababu Wakurya na Wajaluo wako Kenya? Kwa kweli ukiangalia kule Kenya maji yapo kila sehemu, lakini Tarime ni aibu kabisa. Hata Mbunge wa Kenya akinitembelea kule, anashangaa kwamba kuna nini hapa? Ni nini hicho?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli, naitaka Serikali na narudia kusema, siwezi kujikomba, ni wajibu wenu mtekeleze, kama hamwezi mpishe. Nitamwandikia hata Rais barua nimwambie kwamba, kama ahadi aliyotoa haitekelezeki na Mawaziri mliokuja mkatoa ahadi hamtekelezi, kwa kweli hatutaelewana na patachimbika. (*Makofii Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kusema kwamba, Naibu Waziri allkuja Tarime na wale watu wa Tarime walimweleza tatizo lililopo Tarime na yeze mwenyewe alishuhudia. Hata kama viongozi wa Serikali walijitahidi sana kumpamba kwa kumpatia maji safi ya kununua ya kwenye chupa, Tarime maji ya kunywa ni tatizo. Ukinywa maji ya Tarime utafikiri yamechanganywa na ugoro au ni juisi. Kwa kweli ni maji machafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikwenda ofisini kwa Mheshimiwa Waziri, tukakutana akaniambia kwamba, amekumbuka Tarime, lakini nimekwenda kusoma hotuba yake anasema kabisa kwamba, miji ambayo imekuwa Halmashauri haikutengewa fedha. Sasa kama haikutengewa fedha na wakati Julai, 2012 aliahidi katika kitabu chake mwenyewe, nami nikaenda nikawaambia wananchi wa Tarime, lakini hakuna utekelezaji wowote ule, leo hii nitakwenda kuwaambiaje? Naomba kwa kweli wananchi wa Tarime hilo waliskie na walielewe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu naomba tuangalie namna ya kutumia rasilimali tulizonazo bila upendeleo kwa sehemu yoyote ile. Labda kwa sababu wengine tuna *nature* ya kutojikomba ndiyo maana hatutekelezewi. Nasema

kwamba, hatujikombi, lakini lazima kieleweke. Narudia kwa kumwambia Mheshimiwa Waziri kwamba ni lazima wajitahidi kuleta hayo maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba kuuliza, kwa nini Kanda ya Ziwa tuna mito mikubwa: Mto Kagera uko Karagwe kwa jirani yangu, Mto Simiyu, Mto Mara, ambayo ni mito mikubwa kabisa, lakini hatunufaiki nayo hata kidogo. Tuna Ziwa kubwa lakini hatunufaiki nalo hata kidogo. Wanachukua maji kutoka Ziwa Victoria wanapeleka Tabora, sawa kupeleka Tabora siyo tatizo, lakini sasa wale unaowaacha pale siyo binadamu? Au ni Wakenya? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo naomba wakae walitafakari. Nasema ukweli kwamba, nitaondoa shilingi na sitaunga mkono hoja, daima. Ahsante sana. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Asante sana, nakushukuru Mheshimiwa Chacha Mariba Nyangwine. Huyo ni Mura, anasema fita ni fita tu hata fya maji. Mheshimiwa Shabiby.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa hii nafasi. Mimi labda tu nitachangia machache sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia katika ukurasa wa 61 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri ameitaja Gairo na mwaka jana aliitaja tena Gairo. Kuna baadhi ya Wabunge wengi tu hasa ndugu yangu Ngeleja akawa ananipa hongera kwamba, sasa Gairo shida ya maji imekwisha. Lakini ni kwa vile haelewi tu. Mwaka jana sikuunga hii hoja mkono na siungi tena mpaka maji yatoke Gairo. Siyo kwamba tu naogopa sijui nyoka wa shaba, hata aje nyoka wa chuma hapa. (*Kicheko/Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi kweli nitaeleweka katika sehemu ambayo watu wanunua ndoo moja ya maji shilingi 2,000/=, halafu ninakaa hapa nasema naunga mkono hoja? Naunga mkono hoja ipi sasa? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu amesema mradi wa umefikia asilimia 86 na utakamilika mwaka 2013/2014. Mwaka jana alizungumza hivyo hivyo tu, alitaja sijui asilimia 50 au 60. Sasa toka mwaka jana mpaka mwaka huu nilichoona kilichoendelea kwenye ule mradi ni kupalilia yale matanki. Sasa kusafisha matanki nje pale kumeshafikisha tayari asilimia 36, hata mimi sielewi tunaelekea wapi kuhusu habari ya maji. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli sielewi na sitaunga hoja mkono na nitakuja na hoja binafsi sasa. Siyo kwamba wajiu zulu tu, wataalam na wao wanahuksika, kwa sababu hapa tuna kazi ya kupiga makofi, tunagombana wenyewe kwa wenyewe na wenyewe wanakaa wanashangilia pale. Wakipata vipo sho kwa kuja Dodoma, hawana chochote wanachokifanya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nitakuja na hoja binafsi tuhakishe kwamba, Wizara ya Maji wataalam wote hawapo, watafutwe wapya kwani hawana faida yoyote. (*Makofî*)

Naibu Spika, ukiangalia hapa Wabunge wengi wameshazungumza ile miradi ya Viji 10 vya *World Bank*. Jamani toka mwaka 2003 mpaka leo, kila siku mradi unatekelezwa. Kwenye Wilaya ya Kilosa, Jimbo langu la Gairo nilipata viji 10 vya Chakwale na Kibedya, mpaka leo hakuna maji. Zinaletwa fedha, ukiangalia katika ukurasa huu wa 123, Wilaya ya Kilosa imepata milioni 281, Gairo hata senti moja haijafika, fedha zote zinaishia Kilosa wanakula, na inavyoonekana kabisa wanakula pamoja na Wataalam wa Wizarani. Ndiyo maana hata ukiangalia visima vilivyo chimbwa viko wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi mnatoa fedha halafu hamwendi kuchunguza huko kwenye Wilaya kwamba, tumewapa hizi fedha za kuchimba visima kwa mgawanyo wa fedha wa kila Halmashauri, mnakwenda kusimamia, kuangalia zinafanya kazi? Hakuna! Kuna visima wanachimba hapa futi nne nne tu, maji hata ng'ombe hanywi. Halafu

watu wamekaa Wizarani huko, wana kazi ya kusema Wabunge tumewapelekeeni huko huko nyie na Madiwani mijipangie. Sasa sisi ni wataalam wa maji? Halafu unangoja Mbunge yuko hapa kule Halmashauri wanaitisha kikao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda hapa, mazungumzo ni hayo hayo tu kwamba, ninyi mmeshapitisha kwenye Halmashauri, iko wapi? Mwaka huu Wilaya ya Kilosa imepewa zaidi ya milioni 1,900, lakini lazima mjue kwamba imegawanyika katika Wilaya mbili; Wilaya ya Gairo na Kilosa. Wilaya ya Gairo kijiografia ni kame kabisa kuliko eneo lolote katika mkoa mzima wa Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa mzima wa Morogoro, Wilaya ya Gairo ndiyo iko sehemu kame kama Mkoa wa Dodoma, lakini hakuna chochote. Toka niingile katika Ubunge, sijawahi kuona hata kisima cha *hand pump* pale, ukikiona ujue nimetoa mwenyewe Mbunge. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kwenye mgao wa mwaka huu wa fedha 2013/2014, fedha za Gairo ziletwe Gairo na siyo zipitie Kilosa. Kilosa wao wabaki na kiasi fulani tu, lakini nyingi zije kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia Gairo maji hayatoki, lakini hapa tunasifiwa. Katika ukurasa wa 206, *EWURA* imetoa leseni kwa Mamlaka ya Maji Gairo. Sasa hiyo leseni inauza hewa au nini kama maji hayatoki yaani unajua vitu vingine hata havieleweki! (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimuunge mkono Mheshimiwa ole- Sendeka. Mheshimiwa Ole-Sendeka na Wabunge wengi tu wamesema kwamba, tukitaka tupate maji, lazima tuwe na Mfuko wa Maji. Nasema Serikali hajathubutu kuondoa tatizo la maji, wako watu walithubutu hapa kwenye nchi hii na wakafanikiwa. Kama Mheshimiwa Lowassa alithubutu kwenye mradi wa Ziwa Victoria. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulitumia fedha zetu za

ndani shilingi bilioni 273, lakini sasa hivi kila kitu mkopo, sijui Benki ya Dunia, sijui nani aje atoe msaada. Hivi sisi hatuwezi kujifunga mkanda kama alivyosema Mheshimiwa Ole-Sendeka hapa?

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipochangia hotuba ya Mheshimiwa Mkuu nilijaribu kutoa tu mawazo ya namna ya kupata fedha angalau tuongeze Mfuko huu. Lakini hata tukizungumza, tutaongeza Mfuko, tutapiga kelele, mapato ni yale yale. Tutaongeza bajeti ya Maji, fedha tutapunguza kwenye Wizara ya Elimu. Tuweke Mfuko kama ilivyo kwa Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Ujenzi ina Mfuko wake ambao kila lita moja ya mafuta inakatwa sh. 200/= na ndiyo maana barabara nyangi zinatengenezwa. Wizara ina Mfuko maalum. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tunasema maji ni uhai, maji ni uhai, tunajali kweli? Tunajali kama maji ni uhai kweli? Sasa tuweke Mfuko maalum kama ulivyo ule wa kwenye Wizara ya Ujenzi, Mfuko wa Barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mapendekezo yangu, kwenye simu, watumiaji wa simu tuko zaidi ya milioni 20 Tanzania. Wengi wao hapa wanaitana, mtu mzee kama Mheshimiwa Komba au Mheshimiwa Kapuya utasikia anaitwa *baby, baby, eeh*, watumiaji wengi wa simu ndiyo kauli zao hiso na hazina kodi ya aina yoyote. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hicho lazima tukubali kwamba, hapa kwenye simu...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MBUNGE FULANI:** Mwongezee muda kidogo bwana!  
(Makofi/Kicheko)

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Shabiby. Sasa mchangiaji wetu wa mwisho.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Samahani kidogo Mheshimiwa. Mchangiaji wetu wa mwisho kwa dakika chache sana, naomba radhi sana. Mheshimiwa Nimrod Mkono kwa dakika tano. Jitahidi zisizidi dakika tano.

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ndogo sana ili nami niweze kuchangia hoja hii muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kusema, siungi hoja hii kabisa, kabisa. Siungi hoja hii kwa sababu kubwa moja, waasisi wa Taifa hili katika Jimbo la Musoma Vijijiini waliweka bayana misingi bora ya kuwapatia maji wananchi na wakazi wa Musoma Vijijiini. Katika hatua hiyo walibuni miradi ya *trunk route four*, *trunk three*, kwamba itasambaza maji kutoka Ziwa Victoria kwenda Butiama mpaka Buhemba. *Trunk route three* kutoka Mto Mara kwenda Buhemba na sehemu jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahadi hiyo ya mwaka 1974 mpaka leo haijatekelezwa. Mwaka 1974 na mimi kwa miaka 12 nimekuwa Mbunge hapa, nasimama kila siku nazungumzia juu ya *trunk route four* bila mafanikio. Kwa nini sasa niunge mkono hoja hii iliyoko mbele yetu? Sioni sababu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maji yanayopatikana Butiama ni yale niliyochimba, lakini maji kutoka Mugango hakuna yanayofika pale. Mradi wa Mugango ulikuwa ukidhi mahitaji ya vijiji mbalimbali vikiwemo Kyabakari, Kwitururu, Mugango, Kiriba mpaka kufikia sehemu nyngine za karibu na Ikitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo *trunk route four* imesahaulika kabisa, mabomba yake yameng'olewa, mabomba ya kuhifadhi maji hakuna, lakini kila wakati anakuja Waziri, anapita pale anampa mkono Mama Maria, anamsalimu halafu anaondoka akisema nitaleta maji, lakini mpaka sasa hakuna maji. Kwa nini niunge mkono hoja? Watu

24 APRIL, 2013

wa Musoma Vijijini watadhani mimi ni mwehu. Mkono ninao lakini siyo wa kuunga hoja ambayo haina msingi. (*Makof/ Kicheko*)

**MBUNGE FULANI:** Namna hiyo.

**NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumzia sehemu ya Kyagata. Kyagata Mto Mara unakwenda, unatoka Kenya unaingia Ziwa Viktoria. Mto huu kila mwaka unapofurika maji yanaenea katika maeneo ya Wegero, Kongoto, Buswahili, lakini wakati wa kiangazi hakuna maji na wananchi wote wa Kyagata hawapati maji. Kwa nini niunge mkono hoja hii kama wananchi wangu wanalia miaka 12 nikiwa Mbunge wao na kwenye Chama cha Mapinduzi ambacho nakiendesha pale? Sioni kwa nini niunge mkono hoja hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mto Mara una matatizo makubwa kwa wananchi wa Musoma Vijijini. Mwezi uliopita ulifurika ukaziba hata lambo ambalo tulipewa na Wizara hii ya Maji. Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji alitembelea eneo hilo akakuta bwawa la Wegero limepasuka na maji hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, akaenda pale sehemu moja ya Mugango ambayo ndiyo chanzo cha *trunk route fourkwenda* Butiama, wananchi wanaohudumia mradi huo hawajapewa mishahara yao kwa miezi 20 sasa. Miezi 20 wafanyakazi hawajapewa mishahara, lakini Mawaziri wanakwenda pale wanaongea nao wanasema watawapa fedha, lakini hawajalipwa mpaka leo. Kwa nini niunge mkono hoja hii ili yoko mbele yako?

Mheshimiwa Spika, sina mengi ya kusema, nashukuru sana kwa kunisikiliza. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Nimrod Mkono.

Nawaona Waheshimiwa wawili wamesimama. Kwa dakika moja moja, Mheshimiwa Aliko na Mheshimiwa

Serukamba, nendeni moja kwa moja kwenye suala mnalotaka kusimamia.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nasimama kwa Kanuni ya 68(7) "Hali kadhalika Mbunge anaweza kusimama..."

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Endelea kwa ajili ya kuokoa muda.

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Ahsante sana. Kwa kuokoa muda naomba niseme hivi, mjadala ulioko mbele yetu umevuta hisia za Watanzania wengi na humu Bungeni tungetazamia kwamba, Mheshimiwa Waziri Mkuu angekuwa *ana-pay attention* kwa ajili ya jambo hili. Lakini nasikitika kwamba kuna Mbunge mwenzetu amekaa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa zaidi ya nusu saa bila kumruhusu Waziri Mkuu *ku-pay attention* katika mambo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiti chako kiliwahi kutoa msimamo na kutuonya sisi Wabunge tumuache Waziri Mkuu a- *concretate* na mijada inayoendelea Bungeni. Naomba Mwongozo wako jambo hili linaruhusiwa? (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Serukamba kwa kifupi sana.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusikiliza mjadala huu toka asubuhi unaona tatizo kubwa ni fedha. Nataka kupata Mwongozo wako, ukiangalia bajeti ya Serikali ya mwaka huu OC (*Other Charges*) zinakaribia triliioni Nne (4,000,000,000,000/=). Nataka niliombe Bunge lako na Wabunge wenzangu tufanye maamuzi, kwenye zile triliioni nne tupunguze asilimia 15 tu *prorata* kwa wote, tutapata shilingi bilioni 600. Shilingi bilioni 600 tuzipeleke kwenye miradi ya maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, toka nimeingia Bunge hili mwaka wa Nane, tunaongea matatizo ya maji. Nadhani

wakati umefika sasa tuamue tujifunge mikanda, kama ningesafiri mara tano kwenda nje ya nchi, niende mara tatu, lakini tutatue tatizo la maji kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Mwongozo wako kama inawezekana tunazo trilioni nne kwenye *Other Charges (OC) across the board*, tupunguze asilimia 15 tu. Nadhani hawawezi kushindwa kufanya kazi ili fedha itakayopatikana tuipeleke kwenye miradi ya maji. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa Waheshimiwa Wabunge nina miongozi mitatu ya kushughulika nayo kwa muda mchache sana uliobaki. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, naona unataka kusimama, karibu!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kidogo niseme hili jambo ambalo linajirudia sana juu ya Waziri Mkuu kukaa anasikiliza humu Bungeni. Kuna maelekezo kweli ya Mheshimiwa Spika, kwamba, Waziri Mkuu asiguswe, asitembelewe, asifanywe nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka tu niseme kwamba, Waziri Mkuu ni kiongozi, lakini kama mnavyojuu ni Kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni, Serikali iko hapa, siyo Waziri Mkuu. Serikali siyo huyu Pinda, Serikali ni hawa wote. Wakati mwingine kwa sababu yanayoendelea Kiti au wengine hawaijui, Waziri Mkuu anawaita hapa. Kiongozi wa shughuli za Serikali anaendesha Serikali hata hapa alipo. (*Makof!*)

Kwa hiyo, msijenge *notion* hii wananchi wakamuona huyu Waziri Mkuu siyo msikivu sana, hatii amri ya Kiti, anakaribisha watu. Yuko kazini hapa, watu wana shida zao. Nataka ieleweweke kwamba, Serikali siyo Pinda, siyo Waziri Mkuu,

huyu ni kiongozi wa shughuli za Serikali. Serikali ni sisi sote hapa na hata waliopo nje wanafanya kazi, wanatuletea majibu. (*Makofī*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, pamoja na Mwongozo wako, nataka kidogo umuonee huruma Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa sababu vinginevyo mtasema asitoke kabisa hata ndani ya Bunge, asije akatoka hapa. Sasa kama yupo hapa anatatura migogoro ya Waheshimiwa Wabunge kama jukumu lake la Kiserikali analaumiwa, akitoka huko sasa si mtamfanyia na maandamano kabisa! (*Makofī*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, ahsante, nakushukuru sana.

Sasa Mheshimiwa Saada Mkuya Salum, hapo hapo ulipo, kwa ule mwongozo wa asubuhi wa Mheshimiwa Mpina, ikiwezekana usizidishe dakika tatu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):**  
Mheshimiwa Naibu Spika, asante. Naomba kutoa maelezo kidogo kutokana na Mwongozo wa Mheshimiwa Mpina.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo nililoliona kwa Mheshimiwa Mpina ni ufahamu wake wa *recurrent expenditure vis-a-vis development expenditure*. Siku ile wakati tumejibu lile swalii alikuja hapa, nikamfahamisha kwa kadri ya uwezo wangu na nilitumaini sana kwamba, angekuwa amefahamu, lakini ndiyo hivyo hakufahamu. Labda *probably* hii sehemu aliyokuwa amekaa ilikuwa kidogo inampa shida au pengine sauti yangu by *then* ilikuwa ikimpa shida, lakini niko tayari kumpa *extra tuition*.

Mheshimiwa Naibu Spika, niko tayari kumpa *extra tuition*, kumfahamisha vizuri *what real means development and expenditure*. Anachoongea yeye ni kwamba, matumizi ya kawaida, yaani *other charges or recurrent expenditure* yanafikia 10.6 *trillion* lakini bado kuna mapato yetu ya ndani ya 9.1 *trillion*.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumwambia Mheshimiwa Mpina pamoja na Waheshimiwa Wabunge kwamba, 10.6 trillion ambayo iko kwenye bajeti *does not only*, haina maana kwamba ni mishahara, ni matumizi mengine. Ndani yake mna *a big chunk ya development expenditure.* (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka tu nimpe mfano kidogo, nilimwambia aende akafanye *analysis* aweke hesabu zake vizuri. Akienda akachambua mle ndani atakuta *expenditure* ya 1.6 trillion peke yake imekwenda kwa ajili ya *human capital investment*. Hiyo peke yake ni *development*. Yeye alisema tuna *gap* ya 1.5, lakini namwambia kuna 1.6 trillion kwa ajili ya *human capital development*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini akumbuke ndani ya hiyo *recurrent or OC* ndani yake mna Deni la Taifa. Maana yake nini? Deni la Taifa tunakopa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo, lakini ile fedha ambayo tunairejesha tunakwenda kufidia kule, *definitely that is development.* (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa muda wenyewe ni mchache na hatuna maelezo mengi, lakini kuna *components* nydingi ambazo ziko katika *recurrent expenditure* ambazo anavyoona yeye ni kwamba, sisi tunafidia kutokana na mikopo. Naomba kama hajaridhika nitaendelea kumwelimisha, kumwelimisha na kumwelimisha. *I hope one day in life* atakuwa amefahamu.

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Naibu Waziri wa Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Saada Mkuya Salum.

Miongozo iliyobakia miwili midogo, ni ya Mheshimiwa Aliko Kibona kuhusiana na Wabunge wanaokwenda kumwona Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Namshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera,

Uratibu na Bunge) amesaidia kufafanua. Lakini niongezee tu kwa kweli kwa Mheshimiwa Mbunge ambaye suala lako siyo muhimu hivyo, ni vizuri kumpa nafasi Mheshimiwa Waziri Mkuu ili apate kuwasikiliza Waheshimiwa Wabunge. Kwa wale ambao haliwezi kusubiri, basi itakuwa hivyo. Vilevile wale ambao wanakwenda kumwona kwa mambo fulani fulani, basi tuwe na *summary*. Unapokaa nusu saa unamhutubia Waziri Mkuu jambo gani? (*Makof!*)

Kama dakika 10 unaweza ukahutubia Bunge la Taifa, kwa nini usiongee na Waziri Mkuu kwa dakika tano, halafu ukamucha asikilize mambo mengine? Kwa hiyo, tunatoa wito sana kujaribu kumpa nafasi Mheshimiwa Waziri Mkuu. Lakini pale ambapo inabidi kama alivyosema Mheshimiwa Lukuvi, basi hilo liweze kuendelea.

Mheshimiwa Serukamba ametoa pendekezo, pendekezo hilo kwa kweli tunayo Kamati ya Bajeti ambayo muda wote inakutana na Serikali. Tunawaomba walitazame kama moja ya mapendekezo ambayo nina hakika wanayafanya kazi. Kwa kufuatilia kinachoendelea humu ndani, ukisikiliza upepo wa humu ndani *message* ni moja tu kwamba, jambo fulani lifanyike katika bajeti hii na wala siyo nyingine ili kuona namna gani tunatatua tatizo la maji ambalo ni kero kubwa nchini kote kwa ajili ya wananchi wetu na hasa akinamama. (*Makof!*)

Wako wachangiaji wengi ambao walikuwa wameomba kuchangia, wenginje tutaendelea kesho na uchangiaji. Msiwe na wasiwasi, wale wote ambao mliomba majina yenu yako salama kwa Makatibu hapa.

Kwa suala hili la maji ni ajabu sana, kuna baadhi ya wapiga kura wa Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakiniandia moja kwa moja wakiwaombea Wabunge wao, kwa nini Mbunge wetu hatumsikii kwenye maji, mpeni nafasi. Kwa hiyo, mjue tu ni suala ambalo linawagusa watu wengi sana.

Mwisho kabisa, baadhi ya Wabunge wengi sana

wameniandikia karatasi nyingi kweli hapa, wanasesma, aah, Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini siku tano hizi zimekuwa na utulivu mzuri, watu wamechangia kwa utulivu sana na kumekuwa na amani kubwa? Wengine wakasema kuhusu ile Kanuni ya Tano ambayo wengi huwa hawaisomi, kwa hiyo, wanakwenda kwenye vyombo vya habari wanasesma Naibu Spika ametumia Kanuni gani? Hawajasoma Kanuni ya Tano inayonipa mamlaka ya ziada kidogo.

Wabunge wengi walikuwa wanapendekeza kwa utulivu huu, adhabu iongezeke iendelee kidogo. Naomba niwakatilie, niwaombe tu kwamba, adhabu ndogo ndogo hizi ni kukumbushana tu kurudi kwenye mstari, wala hazina nia mbaya. (*Makofii Kicheko*)

Kwa kweli huu ndiyo utulivu uliokuwa kwenye Bunge la Tisa kwa wale ambao hawafahamu. Ndiyo maana Bunge la Tisa liliisifiwa sana, sana. Ni kwa sababu ya utulivu wa aina hii, kwamba kila Mbunge anachangia, anasikilizwa, ikibidi taarifa ni wakati ambao inabidi, siyo kuvurugana kwa taratibu ambazo hazina kichwa wala miguu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo hayo, naomba niwashukuruni sana kwa ushirikiano wenu. Siku ya leo imekuwa nzuri sana. Kwa hiyo, naomba kuahirisha shughuli za Bunge hadi kesho Saa Tatu asubuhi.

*(Saa 1.45 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi, Tarehe 25 Aprili, 2013 Saa Tatu Asubuhi)*